**6 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 6 Mei, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Waziri wa Uchukuzi, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kwa niaba yake Mheshimiwa Abubakari Asenga, karibu.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba kutoa pole kwa wananchi wetu wote waliokumbwa na mafuriko katika nchi nzima hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuweka Mezani Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Ahsante Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Tunaanza Maswali katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Swali la Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara Tarime Vijijini litaulizwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

Na. 242

### Kumaliza Tatizo la Matundu ya Vyoo, Viti, Meza na Madawati

**MHE. ANNE K. MALECELA K.n.y. MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kumaliza tatizo la matundu ya vyoo, viti, meza na madawati katika Halmashauri zote nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024/2025 shilingi bilioni 54 imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo 25,825, shilingi bilioni nne kwa ajili ya kununua seti za viti na meza 40,585 na shilingi bilioni 4.28 kwa ajili ya kununua madawati 47,192. Aidha, kupitia bajeti ya mwaka 2023/2024, ujenzi wa matundu ya vyoo 22,418 kwa shule za msingi na 16,795 kwa shule za sekondari unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali wa kumaliza upungufu wa matundu ya vyoo, viti, meza na madawati katika Halmashauri zote nchini ni kuhakikisha kuwa kila darasa jipya linalojengwa linawekewa madawati 15; dawati moja wanafunzi watatu kwa shule za msingi na viti 50 na meza 50 kwa shule za sekondari. Vilevile ujenzi wa madarasa mapya unaenda sambamba na ujenzi wa matundu ya vyoo kwa kuzingatia uwiano wa idadi ya madarasa yanayojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kupitia Serikali Kuu na mapato ya ndani kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Anna Kilango Malecela swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupata majibu ya Serikali, sasa naomba kuuliza maswali mawili ya

nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri ya Tarime ina mapato makubwa ya ndani na chanzo cha mapato hayo ni wananchi wenyewe: Je, Serikali iko tayari kutoa maelekezo kwa Halmashauri ya Tarime iweze kuondoa changamoto za matundu ya vyoo, viti, meza na madawati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Same inafahamu vema kwamba nimefanya jitihada kubwa kutengeneza madawati kwenye shule za msingi zaidi ya madawati 500: Je, Serikali hamwezi kuwaelekeza Halmashauri ya Wilaya ya Same ikachukua hatua nayo ya kutengeneza madawati sasa hasa katika shule za Kata za Lugulu, Mtii, Vuje na Bombo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge, ukweli ni kwamba shule ni mali ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na shule zipo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia wajibu wa kutunza na kusimamia shule hizi uko chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, tafsiri yake ni kwamba, ununuzi wa madawati, viti, ujenzi wa madarasa na miundombinu mingine ni wajibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia bajeti za maendeleo. Huo ndiyo msingi wa *D by D*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Serikali Kuu kimsingi ni miradi ya nyongeza kwa maana ni *complimentary*. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kukumbushia maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, na Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kwamba, wahakikishe wanafanya tathmini ya miundombinu na samani na kutenga kwenye bajeti za maendeleo kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maelekezo hayo ya Mheshimiwa Waziri yanaenda pia kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada binafsi za kuhakikisha kwamba ananunua madawati haya kwa ajili ya kupeleka kwenye shule zake. Jitihada hizi ni nzuri na zinafaa kuigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kukumbushia maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote zilizopo nchini kuhakikisha kwamba wanatenga fedha kwenye mapato yao ya ndani, kwenye bajeti ya maendeleo kuhakikisha kwamba wanatumia fedha hizi kwenda kununua madawati haya na pia kuendeleza miundombinu mingine kama kujenga vyoo. Hilo ni jukumu lao kwa mujibu wa *D by D*. Kwa hiyo, naomba nikumbushie hilo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mashariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, swali limechukua muda mrefu sana, tutaenda swali linalofuata. Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 243

**Ujenzi wa Barabara ya Mhanga Hadi Mgeta – Kilolo**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa barabara ya Mhanga hadi Mgeta - Kilolo utaanza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Barabara ya Mhanga - Mgeta yenye kilometa 17.0 inayounganisha maeneo ya uzalishaji katika Wilaya za Kilolo - Iringa na Kilombero - Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeanza ujenzi wa barabara hii kwa kutenga fedha kwa awamu ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023, imetoa kiasi cha shilingi 282,500,000 kujenga kilometa 13. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuchimba mifereji urefu wa meta 2,000, kalvati midomo sita pamoja na kuumba tuta la barabara kilometa 13. Kwa sasa mchakato wa kumpata Mkandarasi unaendelea na matarajio ni kuanza ujenzi mwezi huu wa Mei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Mhanga - Mgeta kila mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha ili kuifanya barabara hii kupitika kwa maendeleo ya wananchi wa Jimbo la Kilolo na maeneo jirani.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ritta Kabati swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwanza kabisa naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa kwa manufaa ya wananchi wa Kilombero na Kilolo kufungua barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, barabara hiyo inaishia Kijiji cha Itonya, je, Serikali itakuwa tayari sasa kuunganisha mtandao wa barabara hiyo katika Kijiji cha Itonya - Kimara mpaka Idete ambapo inapita barabara ya *TANROADS* ili kufungua uchumi na pia kuunganisha na reli ya *TAZARA* ili kusafirisha mazao yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa barabara nyingi sana sasa hivi katika Mkoa wetu wa Iringa zimeharibika sana kutokana na mvua kubwa; na kwa kuwa, kuna barabara ya Boma la Ng'ombe Masisiwe wananchi wameanza kuchangishana ili kuondoa sehemu korofi magari yaweze kupita kwa urahisi: Je, Serikali inawasaidiaje wananchi hao ili kuweza kutengeneza sehemu zote korofi waweze kupitisha mazao yao, akina mama wajazito na wazee?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la kwanza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kuunganisha barabara za Kitaifa na Wilaya kwa maana ya barabara za *TANROADS* na *TARURA*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali siyo tu iko tayari kuunganisha mtandao wa barabara ya Kijiji cha Itonya na Kimara, lakini ndiyo mpango wa Serikali uliopo wa kuunganisha barabara zote nchini, kwa maana ya barabara zote za vijiji ikiwemo vijiji hivi vya Itonya, Kimara na Idete, vitaunganishwa na barabara za Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, awali ya yote nawapongeza wananchi wa Boma la Ng'ombe ambao kwa jitihada binafsi wameweza kuchangia fedha kuboresha barabara iliyopo katika eneo lao. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko tayari kuunga mkono jitihada hizi za wananchi ili kuboresha barabara hii ya Boma la Ng'ombe - Masisiwe. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaifikia barabara hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeanza ujenzi wa lami kwa ajili ya kuchochea viwanda barabara ya Themi - Viwandani kwa kujenga kilometa 1.4, lakini bado kuna maeneo ya viwanda vya Lodhia, Dash, Mount Meru pamoja na *Coca Cola* hadi kwenda kwenye *World Vision* bado havina lami mpaka sasa. Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ili kuendelea kuchochea maendeleo ya viwanda nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inazingatia sana na inatambua umuhimu wa kujenga miundombinu ambayo itachochea uchumi katika nchi, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ambazo zitaunganisha wananchi kutoka kwenye mashamba yao kwenda kwenye viwanda. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya uboreshaji wa barabara hizo kwa ajili ya kuchochea uchumi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Justin Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa sasa Kata nne za Jimbo la Kilolo hazipitiki kabisa kutokana na madhara ya mvua. Kata hizo ni Masisiwe, Ukwega, Kimara na Idete. Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha upelekaji wa fedha za dharura ili Kata hizi ziweze kuunganishwa na barabara na huduma ziweze kuendelea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameeleza barabara hizi hazipitiki, namwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi hiki cha Maswali na Majibu tukae ili tuweze kufuatilia kujua mustakabali mzima wa kuleta fedha kwa ajili ya kurekebisha barabara hizi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaenda na swali linalofuata, Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula, sasa aulize swali lake.

Na. 244

**Kugawa Halmashauri ya Uyui**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, lini Halmashauri ya Wilaya ya Uyui itagawanywa na kutoa Halmashauri mpya ya Kizengi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa maeneo mapya ya utawala huzingatia Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya Sura 287 na Mamlaka za Miji Sura 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaishauri Menejimenti ya Halmashauri ya Uyui na Mkoa wa Tabora kuendelea na taratibu za maombi na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa hatua zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant Daud Protas, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, Mheshimiwa Rais alipokuja Mkoa wa Tabora tulimpelekea ombi maalumu la kuanzisha Halmashauri mpya ya Kizengi na akatoa maelekezo kwa mkoa na wilaya kuandika maombi hayo na kuyapeleka Wizarani na mkoa ulishafanya hivyo na maombi yale yameshawasilishwa kwa Katibu Mkuu, TAMISEMI. Nataka Waziri aniambie, je, hiyo barua imefika kwao au bado?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya Uyui, hasa Jimbo la Igalula katika Kata za Loya,

Tula Miswati, Mbale wanapata adha sana ya kupata huduma katika Halmashauri yetu kutoka kilometa nyingi wanatembea kufuata huduma. Hamuoni haja kama Wizara kumshauri Mheshimiwa Rais ili aweze kuitangaza Halmashauri ya Kizengi ili kuongeza huduma kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepokea kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora maombi hayo aliyoyazungumza Mheshimiwa Mbunge na inaendelea kuyafanyia uchambuzi kulingana na vigezo vilivyopo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barua hiyo ilishafika Serikalini Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kipaumbele cha Serikali kwa wakati huu kwa mujibu wa Ibara ya 9(a) (4) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi wa Mwaka 2020 ni kuimarisha Serikali za Mitaa ili ziweze kutimiza wajibu wao. Kwa mantiki hiyo Serikali kwa wakati huu imejikita katika kuimarisha maeneo ya utawala yaliyopo kwa maana ya kuajiri watumishi katika maeneo ambayo yenye upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Serikali itatengeneza au kuweka miundombinu muhimu kama majengo ya ofisi, kupeleka shule, huduma za afya, maji, barabara na umeme. Kwa hiyo, kwa wakati huu Serikali imejielekeza katika kuboresha mamlaka zilizopo tofauti na kuanzisha mamlaka mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Uyui kuendelea kuimarisha miundombinu ya huduma za kijamii na kiuchumi katika maeneo waliyonayo ili huduma ziweze kuwafikia wananchi wote karibu na maeneo yao ili kuongeza ufanisi na huduma bora zaidi kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Tunahamia Wizara inayofuata ambayo ni Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

Na. 245

**Wanufaika *TASAF* Kufuata Fedha Benki**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza: -

Je, ni kwa nini wanufaika wa *TASAF* wanalazimika kufuata fedha benki hata fedha hiyo ikiwa ni kidogo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa malipo kwa wanufaika wa *TASAF* unafanyika kwa njia kuu tatu: kwanza, kupitia akaunti ya Benki; pili, kupitia akaunti ya simu ya mkononi; na tatu, kwa malipo taslimu kupitia kwa wakala au katika kituo cha malipo. Uamuzi wa njia gani ambayo mlengwa atapenda kulipwa, unabaki kuwa wa kwake mwenyewe mlengwa ambaye anatambulika wakati wa uandikishaji wa daftari la walengwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Dkt. Charles.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali la

nyongeza. Kwa kuwa ile *database* ya watu ambao wanastahili kupata fedha za *TASAF*, iliboreshwa, je, Serikali imefikia hatua gani ya kuchakata takwimu za Sensa ya 2022 ili kuweza kujua ni wahitaji gani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na uchakataji wa taarifa za takwimu halisia juu ya mahitaji ya Watanzania wangapi ambao wanatakiwa waangaliwe katika awamu ijayo ya *TASAF*. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapokuwa tumekamilisha hatua hizo, tutawajulisha kupitia vile vikao vyetu maalumu vya *TASAF* katika ngazi yetu ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika kila sehemu ambayo watu watakuwa wanatakiwa kuingia kwenye daftari jipya la *TASAF,* basi nafasi itatolewa ili Watanzania waweze kupata fursa hiyo ya kuendelea kusaidiwa katika hatua za kupunguza umasikini.

**MWENYEKITI:** Ahsante, karibu Mheshimiwa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati mwingine wanufaika wa *TASAF* huondolewa kwenye mfumo pengine kwa kutokuelewa vigezo au kwa kuonewa. Ni kwa nini vigezo haviko dhahiri ili pale mnufaika anapoondolewa kwenye *TASAF* kusiwepo na malalamiko ya kuonekana kwamba wanaondolewa kwa sababu za kisiasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa mujibu wa taratibu za *TASAF,* katika Mkutano Mkuu wa Kijiji, Shehia au Mtaa ambapo majina ya wanufaika ndipo yanatakiwa kusemwa, pale hatua ya

kwanza inapofanyika ni kueleza sifa gani ambazo mtu anatakiwa kuwa nazo ili aingie kwenye Mfuko wa *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama inatokea mtu hajasikia zile sifa au mtu ambaye hana zile zifa na ameingizwa kwenye *TASAF*, utaratibu wa ukataji wa rufaa kwa mwananchi ambaye hajaridhishwa na uingizaji huo, zinatakiwa zifuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kipo kikao cha uchujaji wa wale watu walioingizwa kwenye Mfuko wa *TASAF*. Kwa hiyo, siyo rahisi sana Mheshimiwa Mbunge kwa mtu ambaye hana sifa za kuwa ndani ya Mfuko wa *TASAF* kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama kule chini labda wanaoneana aibu na wanashindwa kumtoa mtu fulani, nafasi kwa ajili ya kukata rufaa mpaka kwenye ngazi ya Taifa nazo zinatakiwa zifuatwe ili wale wanaoratibu katika ngazi ya Taifa waweze kushuka mpaka kwenye ngazi ya Kijiji kwa ajili ya kwenda kutafuta ushahidi wa kujiridhisha juu ya huyo mtu aliyeingizwa katika mradi huo kimakosa au kinyume cha utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunahamia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera, aulize swali lake.

Na. 246

**Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika kuwakinga Wananchi na madhara yanayoweza kutokea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera (Zanzibar), kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo kuandaa nyenzo za kisera zinazosaidia kutoa dira, kuibua mikakati na kubuni miradi inayosaidia jamii katika maeneo mbalimbali kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Hii inajumuisha Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi 2021, Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira 2022 -2032, na Mchango wa Taifa katika Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mikakati hiyo, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali nchini. Miradi hii inajumuisha upandaji miti, usambazaji wa maji safi kwa matumizi ya majumbani na mifugo, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, kuhimiza matumizi ya nishati mbadala na majiko banifu ili kupunguza kasi ya ukataji wa misitu, ujenzi wa kuta katika maeneo ya fukwe za bahari yanayokabiliwa na mmomonyoko wa ardhi, ujenzi wa matuta na mabwawa ya kudhibiti mafuriko, kuwezesha jamii kubuni miradi mbadala ya kuongeza kipato na iliyo rafiki kwa mazingira na urejeshaji wa maeneo ya ardhi yaliyoharibika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante. Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba naipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini naomba niulize maswali mawili ya ziada. Swali la kwanza, pamoja na mipango mizuri

ya Serikali kwenye hoja ya kupambana na mazingira, je, Serikali haioni sasa iko haja ya kubadilisha mkakati kwa sababu athari za mazingira zimekuwa kubwa kuliko mikakati yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa maeneo mengi ambayo Serikali imekuwa ikisema kwamba inajenga ukuta lakini bado yanaendelea kuathirika, je, Serikali iko tayari kufuatana nami kwenye Jimbo la Mwera ili wakaone athari kubwa za mazingira? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Zahor, kama alivyouliza. Kwanza tunakubaliana naye kwamba tuko tayari kuungana naye kwenda kwenye Jimbo lake ili kuangalia athari za mazingira zilizopo na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, siyo kweli kwamba athari ni kubwa ambazo zinatokea na kwamba labda mikakati yetu haiendani pengine na utatuzi wa changamoto hizo. Kwanza nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeendelea kuwa na ushirikiano mkubwa wa Kimataifa na kikanda katika kuweka mipango mikakati na madhubuti ambayo inaelezea changamoto zilizopo tunazozipata za mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hivyo, ipo mikataba ambayo kama nchi tunaitekeleza. Kwa mfano, Mkataba wa Kimataifa wa kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi na vivyo hivyo kuna Itifaki za Kyoto ambazo tumekaa na kukubaliana namna ambavyo tunaziangalia zile athari. Zaidi ya hapo, kwa ndani ya nchi hii mikakati ambayo nimeieleza, ni mipango ambayo tunaitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia mikataba ya kimataifa tuliyoiingia, tunapata usaidizi wa kifedha na usaidizi wa kitaalamu. Vilevile kwa kutumia wataalamu wetu hapa ndani, tumeendelea

kutatua changamoto hizi na ndiyo maana unaona sasa athari zilizotokea za *Global warming* zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi katika kubadilisha na kuleta mvua nyingi zilizokithiri, pepo kubwa na mafuriko ambayo yamekuwa yakisababishwa kama athari za mabadiliko ya tabianchi, Tanzania tumeendelea kuwa sehemu nzuri na salama katika rekodi za *East Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imejipanga, na tayari tunatekeleza mikataba ya kimataifa ikiwa ni pamoja na kuhudhuria mikutano ya kimataifa na kikanda. Pia ndani ya nchi kuweka mipango ambayo itasaidia kutokupata athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi, aulize swali lake.

Na. 247

**Kodi na Tozo, Fedha za Mfuko wa Jimbo – Zanzibar**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanyia kazi changamoto ya kodi na tozo kwenye fedha za Mfuko wa Jimbo kwa upande wa Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi na tozo hutozwa kwa mujibu wa sheria pindi bidhaa au huduma zinapotolewa au kununuliwa. Aidha, bidhaa na huduma zinazotolewa hukatwa kodi ya zuio la kodi *(With Holding Tax)* kwa kuzingatia Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Na. 332 chini ya kifungu cha 83 (1)(c) kwa malipo ya ada ya kwa huduma kwa ajili ya utoaji wa huduma ya kitaalamu na kifungu 83(a) malipo kwa bidhaa zinazotolewa na mkazi wa uendeshaji biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kodi hutozwa kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi inayotumika Zanzibar inayojulikana kama Sheria Zinazotolewa na Mkazi Wakati wa Undeshaji wa Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Mfuko wa Jimbo zinaendelea kuleta tija na matokeo chanya katika kuimarisha na kukuza uchumi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla na hivyo kuleta manufaa kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Omar Issa Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo kwa kweli yamekuwa ni majibu ya kufanana siku zote na wala hayaleti matumaini kwa Wabunge wote kutoka Zanzibar, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali mmekiri kwamba changamoto ni sheria na sisi ndio watunga sheria: Ni lini mtaleta Muswada hapa Bungeni ili kubadilisha sheria hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba Mfuko huu unakatwa tozo kwa sheria mbili; Sheria ya Zanzibar na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Je, hamuoni haja ya kukaa pamoja ili kuangalia ni namna gani ya kutatua changamoto hii ili iweze kukatwa tozo kwa upande mmoja tu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar Issa Kombo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwambie tu kwamba awe na matumaini kwa sababu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inafuata kabisa misingi ya Mwanafalsafa Bentham, mtaalamu wa sheria aliyesema, *"Laws should provide minimum pain and provide maximum pleasure."* Kwa msingi huo ni kwamba, sheria hizi zilizotungwa siyo Msahafu wala Biblia Takatifu. Zinaweza kubadilishwa kulingana na mahitaji yaliyopo, lakini pia kutatua changamoto ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lugha ya Kilatini wanasema, "*Ubi societas, ibi jus, ibi ius ubi societas*" kwa maana ya kwamba sheria ni zao la jamii na jamii ndiyo inayozaa sheria. Sasa Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ameleta hoja hii ndani ya Bunge na utakumbuka vizuri katika Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Waziri alijibu hapa na akaeleza kwamba suala hilo walilitolea ufafanuzi. Pia, akasema Serikali iko tayari kukaa na wataalamu kwa upande wa Zanzibar, kukaa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar; *ZRA*, *TRA* na Ofisi yetu ya Wizara ya Fedha ili kuweza kuangalia ni sehemu gani wanaweza wakarekebisha na kuhakikisha kwamba pande hizi zote wanapata nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mwisho wa siku fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ni kwa ajili ya maendeleo ya mwananchi. Pia kodi inayokatwa ni kwa ajili ya maendeleo ya mwananchi na nchi kwa ujumla. Kwa hiyo, hivi vyote kwa pamoja tutaweza kuviangalia. Nimtoe wasiwasi kwamba Serikali iko makini na tutalishughulikia ili kuweza kuhakikisha tuna-*provide maximum pleasure* na tunaondoa hizo *minimum pain,* ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante.

Waheshimiwa Wabunge tunahamia kwenye Wizara ya Nishati, swali Na. 248 ambalo lilikuwa liulizwe kwa Wizara ya Nishati, limeondolewa kwenye *Order Paper*. Tunahamia Wizara ya Maji, Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 249

**Hitaji la Maji – Kata ya Tununguo**

**MHE. HAMISI S. TALETALE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka maji Kata ya Tununguo katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Tununguo ina jumla ya wakazi 11,924 katika vijiji vinne vya Mlilingwa, Dete, Kisanga Stendi na Tununguo. Kati ya vijiji hivyo, vijiji vitatu vya Dete, Kisanga Stendi na Tununguo vinapata huduma ya maji kupitia visima sita vya pampu za mkono. Aidha, ukarabati wa Bwawa la Mlilingwa unaendelea kwa gharama ya shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Kijiji cha Mlilingwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mrefu, Serikali imeanza kufanya usanifu wa mradi mkubwa wa kutoa maji Mto Mvuha kwenda Tarafa za Ngerengere na Mvuha. Usanifu huo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024 na utekelezaji wake

kuanza katika mwaka wa fedha 2025/2026 ambapo utanufaisha vijiji 35 vya Tarafa hizo vikiwemo vijiji vinne vya Kata ya Tununguo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Hamis Shabani Tale Tale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba kuuliza kwamba, Mheshimiwa Waziri wanasema uhondo wa ngoma uingie ucheze. Naomba, kama itawezekana, Wizara ije kwenye Tarafa ya Ngerengere. Kiukweli kabisa, sisi wakazi wa Kata ya Tununguo tuna changamoto kubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kusikia kwamba kwamba tutapata visima sita, lakini hayo maji hayanyweki kabisa. Je, Serikali ni lini itaweza kutoka kwenda kwenye Tarafa nzima ya Ngerengere ili kuona hatima ya sisi Wanangerengere kupata maji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua changamoto iliyopo katika Tarafa hii ya Ngerengere. Vilevile nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa kushirikiana na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kubainisha maeneo yenye changamoto ya maji ili Serikali ikachukue hatua na wananchi waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Sekta ya Maji iko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kujionea hali ya upatikanaji wa huduma ya maji ili nasi tuingize katika mipango yetu ya muda mfupi na kati ili kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nasisitiza maswali kwa ufupi sana na majibu kwa ufupi kadri inavyowezekana. Mheshimiwa Suma Fyandomo.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, ni lini Mradi wa Maji wa kutoka Mto Kiwira kwenda Jijini Mbeya utakamilika ukizingatia Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 117, na mpaka sasa ni fedha kiasi cha shilingi bilioni 14.3 tu ndizo zilizopelekwa na hili jambo tumeanza kuongea tangu mwaka 2020? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba tunafikisha huduma ya maji katika vijiji vyote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya vijiji 12,318 Serikali tayari imeshafikisha huduma ya maji katika vijiji takribani elfu tisa mia saba na kitu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvuta subira kwa sababu Serikali tayari imeshatoa fedha kupitia Wakala wa Maji Vijijini *(RUWASA)* ambao tayari wameshapokea takribani shilingi bilioni 154. Vilevile Mamlaka za Maji Mjini wameshapokea takribani bilioni 69.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakandarasi ambao wako *site* waendelee kufanya kazi kwa weledi na maarifa na kuhakikisha kwamba wanawasilisha hati za madai ili waweze kulipwa na kuendelea na kazi ili Watanzania wapate huduma ya maji, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Mathayo David, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, mwaka 2023 Serikali iliahidi kuchimba visima 12 katika Jimbo la Same Magharibi kwenye Kata ya Ruvu, *Station*, Makanya, Mabilioni, Hedaru na Bangalala, lakini gari la Mkoa wa Kilimanjaro lilikuja likachimba visima viwili tu.

Je, hilo gari la Mkoa wa Kilimanjaro lililotolewa na Mama Samia Suluhu Hassan, litarudi lini Same ili kukamilisha visima 10 vilivyobaki ?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba Mheshimiwa Rais alitoa fedha kwa ajili ya kununua gari hizi. Shida iliyopo ni kwamba bajeti yake kidogo ilikuwa na changamoto. Sasa mwongozo umeshatolewa, kwamba magari haya yatarudi katika maeneo husika na kuendelea na uchimbaji wa visima vya maji ili wananchi wapate huduma ya maji. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mradi wa Oldonyosambu wenye vijiji takribani tisa ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli; na kwa kuwa ni mradi wenye athari kubwa kwa sababu ya *floride* na wananchi wanateseka na *floride*: Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi huo ambao sasa umechukua zaidi ya miaka minne ikitekelezwa kidogo kidogo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza miradi yote inayotokana na ahadi za Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi 2020/2025. Vilevile inaendelea kutekeleza ahadi za viongozi wa kitaifa akiwemo Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu. Kwa, hiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kuiangalia changamoto hiyo na kutafuta fedha za kutosha ili kuhakikisha kwamba mradi huo unakamilika kwa wakati, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwa kuwa Wizara ya Maji inalo jukumu la kufikisha huduma ya maji kwenye taasisi ambazo zinatoa huduma kwenye jamii: Je, Serikali itafikisha lini huduma ya maji kwenye shule ya sekondari iliyopo Kata ya Kagondo, Bukoba Mjini, shule ya msingi iliyopo Kata Kaharoro,

Shule ya Msingi Kibeta, Shule ya Msingi Rwamishenye, Shule ya Sekondari Nyanga, Kituo cha Afya Nyanga pamoja na Kituo cha Afya Ijuganyondo ili wananchi na watoto wetu wa Jimbo la Bukoba Mjini waweze kupata maji safi na salama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inatambua maji ni msingi wa uhai wa binadamu na *engine* ya maendeleo kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua changamoto ambayo Mheshimiwa Mbunge ameiongelea, kwa sababu iko ndani ya mipango ya Serikali. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, na kwa namna ambavyo anaendelea kuisemea, nasi Serikali tutaendelea kuhakikisha kwamba tunaweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba wanafunzi, vituo vya afya na taasisi nyingine zote zinapata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, Mbunge wa Kiteto sasa aulize swali lake.

Na. 250

**Kumaliza Tatizo la Maji – Kiteto**

**MHE. EDWARD O. KISAU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la maji Kiteto?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, Mbunge wa Jimbo ka Kiteto, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Kiteto ni wastani wa 64%. Katika kuboresha huduma ya maji Wilayani Kiteto na kufikia malengo ya 85%. Serikali imekamilisha utekelezaji wa miradi 11 ya Kibaya, Bwagamoyo, Majengo Mapya-Kaloleni, Sunya, Ndirgish, Mdunku, Wezamtima-Bwawani, Matui, Engongungare, Magungu-Nhati na Ostet. Vilevile utekelezaji wa miradi tisa unaendelea katika vijijini 14 vya Nchinila – Engusero, Njiapanda, Chang'ombe-Njoro, Orkine, Ilera-Esekii, Laiseri – Dongo, Kimana, Ngipa, Nasetani, Lembapuri, Esuguta, Kiperesa, Ndotoi na Enguserosidani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025 na kunufaisha wananchi wapatao 69,825 waishio kwenye vijiji hivyo na kufanya jumla ya vijiji 60 kufikiwa na huduma ya majina salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji ili kuwezesha vijiji vilivyobaki kufikiwa na huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa huu mradi wa vijiji 14 Nchinila – Engusero umechukua muda mrefu sana: Je, Serikali ina kauli gani ya kusukuma mradi huu ili umalizike na wananchi wapate maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kiteto ni kame sana, je, Serikali ina kauli gani kuhusu kutupatia kipaumbele cha mabwawa ili wananchi wa Kiteto wanufaike na maji?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, nikiri na Mheshimiwa Mbunge amekuwa mstari wa mbele kupigania mradi huu ili uweze kukamilika. Sasa kwa sababu Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ni sikivu kupitia kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nasi sekta ya maji Mheshimiwa Waziri tayari ameshaingiza kwenye mpango wa utekelezaji katika mwaka huu wa fedha, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kusoma bajeti tarehe tisa, utaona tumetenga kiasi cha shilingi bilioni 2.9 kwa ajili ya kwenda kusukuma mradi huu ili ukamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira tu, siku bajeti ya Wizara ya Maji itakapofika hapa, basi makofi yake yatasaidia kupitisha bajeti hiyo ili wananchi wa eneo lake wakapate huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; ni kweli kabisa kwamba Wilaya ya Kiteto ina changamoto ya ukame. Serikali inaendelea kufanya tafiti mbalimbali na inaendelea kujiridhisha na vyanzo vya maji ili kuhakikisha kwamba wilaya hii inapata huduma ya maji safi na salama. Kwa hiyo, kwa kuanzia ni kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri, kwamba kwenda kujenga mabwawa pamoja na malambo, ambapo mpaka sasa kuna malambo ya Dongo, huko tunaendelea na utekelezaji. Kuna Dosidosi, Bwawani, Kijungu pamoja na Lambo la Makame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba tutakapoona maji bado hayajawa toshelezi, tutaendelea kwenda kuongeza miundombinu na kuhakikisha kwamba maji yanatosha katika eneo la Kiteto, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Regina Qwaray.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Wananchi wa Kata ya Nhati bado wana changamoto

kubwa ya maji, je, ni lini Mradi wa Darakuta - Minjingu utaanza kutekelezwa?

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini. Namwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kikao hiki cha Bunge tuonane ili tuweze kupata taarifa za kina kuhusu mradi wake kwamba umefikia katika hatua gani, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mradi wa Matamba – Kinyika umeanza kujengwa mwaka 2019, lakini hadi leo umekuwa ni mradi unaosuasua, je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa mradi huu ili wananchi wa Matamba na vijiji vinavyozunguka Matamba viweze kupata maji kwa uhakika?

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Deo Sanga. Kwa kweli Wizara tunampongeza kwa sababu ya usimamizi mzuri wa miradi ndani ya jimbo lake; na katika ile miradi ya *P4R* Makete ni kati ya majimbo ambayo yamefanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba mradi huu wa Matimba – Kinyika upo katika zile hatua ambazo tunaamini wakandarasi wanasubiri fedha. Watakapo-*rise* zile *certificate,* basi watakapolipwa wataendelea na utekelezaji wake. Namwomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana ili kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunahamia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka Mbunge wa Liwale sasa aulize swali lake.

Na. 251

**Hitaji la Gari la Zimamoto – Liwale**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE K.n.y. MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kuipatia gari la Zimamoto Wilaya ya Liwale ili kukabiliana na majanga ya moto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea na jitihada za kuliimarisha na kuliboresha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha taratibu zote za mkopo wenye masharti nafuu wa thamani ya Dola za Marekani milioni 100 kutoka Taasisi ya *Abu Dhabi Export Credit Agency* iliyopo Umoja wa Falme za Kiarabu kwa ajili ya kupata vitendea kazi mbalimbali, ikiwemo upatikanaji wa magari 150 ya zimamoto na uokoaji yatakayosambazwa kwa nchi nzima, ikiwemo Wilaya ya Liwale.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Francis Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jeshi hili la Zimamoto ni la muhimu sana na limekuwa likifanya kazi kubwa sana, hasa kwenye Mkoa wetu wa Lindi, ikiwemo kudhibiti na kupambana na mafuriko yanayoendelea katika Mkoa wa Lindi. Hata hivyo, jeshi hili hawana Ofisi nzuri za kufanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Francis.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati Ofisi za Zimamoto zilizopo katika Wilaya za Mkoa wa Lindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, watumishi wa Ofisi za Zimamoto wamekuwa hawana nyumba za kuishi. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwajengea nyumba za kuishi katika Mkoa wa Lindi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Francis Ndulane kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza linalohusiana na ukarabati wa ofisi, kadiri Serikali itakavyopata fedha itatenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa Ofisi za Zimamoto na Uokoaji katika maeneo aliyotaja Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyumba za makazi ya Askari, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ni kwamba kadri Serikali itakavyopata fedha itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za askari wetu wa zimamoto na askari wengine hapa nchini, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunahamia swali linalofuata. Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, aulize swali lake.

Na. 252

**Kuboresha Sheria ya Jeshi la Magereza**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza: -

Je, lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Sheria ya kuboresha Sheria za Jeshi la Magereza ili ziendane na wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felista Njau, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Magereza inaendelea na mchakato wa maboresho ya Sheria ya Magereza sura 58 iliyorejewa mwaka 2002 ili ziweze kuendana na wakati, ambapo kwa sasa upo katika hatua ya kukusanya maoni ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Muswada wa sheria hii utawasilishwa Bungeni mara tu baada ya taratibu kukamilika, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo la wanufaika wa msamaha wa *Parole*, kwamba wakishafika uraiani wanatengwa na jamii na kuonekana bado ni wahalifu, jambo linalowafanya kufanya tena uhalifu na kurudi Magerezani.

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu ili marekebisho ya sheria yaweze kugusa jamii na jamii iweze kuelewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wapo watoto wanaozaliwa Magerezani wakiwemo na mama zao ambao watoto wale sio

watuhumiwa, lakini watoto hawa hawapati haki za msingi kwa mujibu wa Katiba kama elimu na vitu vinginevyo.

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya ya sheria yatagusa vipi watoto hawa wanaozaliwa Magerezani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Felista Njau, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa elimu ya kutosha kwa jamii nzima ili kuhakikisha kwamba wenzetu wanaotoka magerezani basi wasitengwe tena ili waendelee kuwa raia wema na kutimiza majukumu yao kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu watoto wanaozaliwa Magerezani, amedai wanakosa haki. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sheria hii itakapofanyiwa marekebisho itapata maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kama vile jamii nzima, viongozi wa dini pamoja na Maafisa wa Magereza pamoja na Wizara nyingine za kisekta ili kuhakikisha kwamba tunatunga sheria mahususi kwa ajili ya ku-cover watoto wetu wanaozaliwa katika Magereza. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mafupi na yanayoeleweka moja kwa moja.

Tunahamia swali linalofuata, Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, aulize swali lake.

Na. 253

**Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Polisi Igurubi - Igunga**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Polisi Tarafa ya Igurubi - Igunga utakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kituo cha Polisi Igurubi ulianza mwaka 2018 kwa kushirikisha nguvu za wananchi na ulisimama mwaka 2020 baada ya kukosa fedha. Tathmini kwa ajili ya kumaliza ujenzi ili kuunga mkono jitihada za wananchi imeshafanyika ambapo kiasi cha fedha shilingi 53,000,000 zinahitajika. Fedha hizo zinatarajiwa kutengwa kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2024/2025, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, karibu.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, kwanza nianze kuishukuru Serikali kwa kuamua kukamilisha kituo hiki ambacho kiko Tarafa ya Igurubi kitakachozihudumia Kata za Kinungu, Igurubi, Mwaitunduru, Mwamashiga, Kinig'inila, Mwamashimba na Mwamakona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nauliza kwamba, kwa kuwa Serikali yetu imeamua inapojenga vituo inatoa na vitendea kazi, je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na kituo hiki kitakapokamilika, watatupatia vitendea kazi kwa ajili ya doria ?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali imeshatoa pikipiki kama 105 kama vitendea kazi nchi nzima na bado tuna mpango wa kutoa pikipiki kwa awamu ili kuhakikisha kwamba kata zote ambazo tunajenga ofisi za Polisi pia zinapata pikipiki ili kurahisisha utendaji kazi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa tunahamia Wizara ya Afya. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, aulize swali lake.

Na. 254

**Hitaji la Mochwari Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Katavi**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga jengo la kuhifadhia Maiti Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Katavi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024 Serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 12.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa jengo la kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi utaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 na kukamilishwa mwaka wa fedha

2024/2025. Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Katavi wanapata shida sana, ndugu zao wanapofariki pale kwenye hospitali ya mkoa ambapo inawalazimu wasafirishe maiti kilometa tatu kupeleka hospitali ya rufaa. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, je, ni lini Serikali itatoa fedha za ujenzi tu wa ile mochwari kwa sababu ujenzi wake ni shilingi milioni 500? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Hospitali ya Mkoa wa Katavi haina *ambulance*, ina *ambulance* moja na kwa afua za udaktari huwezi kubeba maiti kwenye *ambulance*…

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itatupatia *ambulance* kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anafuatilia masuala mbalimbali ya afya kwenye Mkoa wa Katavi, lakini nimwambie moja kuhusiana na suala la kumalizika mochwari. Nimhakikishie kwamba kabla ya mwezi wa Kumi mwakani, mochwari yao hii itakuwa imekamilika. Kwa sasa tuendelee kutumia mochwari ya hospitali ya wilaya ambayo ilikuwa inatumika kabla ya hospitali ya mkoa wakati tunaendelea kutatua hili la kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama shilingi bilioni 12.9 zimeletwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, shilingi milioni 300 ni fedha ndogo sana katika Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali lake la pili linalohusiana na suala la *ambulance*, ninyi mnajua kwamba Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amenunua *ambulance* nyingi na Wabunge wengi ni mashahidi kwamba majimbo mengi wakati huu yamepata takribani *ambulance* mbili mbili. Nataka kumhakikishia pia kwamba hospitali yao itaongezewa *ambulance* ya pili ili waweze kufanya shughuli kama ambavyo alitamani kufanya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hospitali ya Wilaya ya Chemba tuna jengo la *mortuary,* lakini hatuna majokofu, ni lini Serikali itapeleka majokofu ili kutoa huduma kwa wananchi wanaotumia hospitali hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge, nikimaliza kujibu maswali hapa, aje tuwapigie *MSD* mara moja mimi na yeye ili tuweze kumpa *exactly* tarehe ngapi hizo *fridge* za *mortuary* zinaweza zikafika kwenye Wilaya yake ya Chemba.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunahamia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini, aulize swali lake.

Na. 255

**Mkakati wa Kukomesha Mapenzi ya Jinsia Moja**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukomesha mapenzi ya jinsia moja nchini pamoja na ukatili dhidi ya watoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara za kisekta inaratibu utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na tatizo la mmomonyoko wa maadili na ukatili dhidi ya watoto. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kusimamia utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto pamoja na kuanzisha na kuimarisha madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto katika shule za msingi, sekondari na vyuo; na

(ii) Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) pamoja na Mpango wa Taifa wa Kuwekeza katika Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe (NAIHA). Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma na kuongeza afua za malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto pamoja na kuimarisha taasisi za familia kwa lengo la kupunguza au kumaliza kabisa changamoto ya mmomonyoko wa maadili nchini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuku kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nashukuru kwa majibu hayo, japo naamini kwamba Mheshimiwa Waziri ama Serikali itakubaliana nami kwamba tatizo hili la mmomonyoko wa maadili nchini ni kubwa kuliko hatua ambazo tunachukua. Sasa naomba kuuliza maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi za kuhakikisha tunachukua hatua dhidi ya watu wanaojihusisha na masuala haya ya mapenzi ya jinsia moja pamoja na mashirika ama watu wanao-*support* ama wanaosaidia kuenea kwa jambo hili hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Sasa Serikali ina mpango gani wa kuleta Muswada hapa Bungeni ili tuweze kutunga sheria ya kudhibiti masuala ya mapenzi ya jinsia moja hapa nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja ni kosa la jinai kwa Kifungu Na. 154 cha Sheria, na Kanuni za Adhabu Sura ya 16 inatambua mtu yeyote ambaye atapatikana na hatia ya kosa hilo ataadhibiwa kifungo cha miaka 30. Ikithibitika na mtendewa aliridhia kufanyiwa kitendo, basi atahusika na kosa hilo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, sheria na kanuni na adhabu zipo. Kinachotakiwa ni kufanyiwa marekebisho. Bunge la Kumi na Mbili, Mkutano wa Kumi na Moja, Kikao cha Sita aliagiza Serikali kushirikiana na Tume ya Sheria kuhakikisha kwamba tunafanya utafiti kwa kushirikiana na Tume ya Sheria ambayo mabadiliko yatakayofanyika yafikishwe katika Bunge lako Tukufu. Tume inaendelea na kazi hiyo, na mara baada ya kumalizika, Muswada huo utaletwa Bungeni ili kujadiliwa na kupitishwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, Serikali ina mkakati gani wa kushirikiana na taasisi za kidini na wataalam ili kuwasaidia wale walioathirika na mapenzi ya jinsia moja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ina malezi, makuzi na utamaduni wa Mtanzania. Kwa hiyo, Serikali kwa kushirikiana na vyombo vya dini tunahakikisha kwamba tunatoa elimu ambayo itawasaidia wananchi ili kujikinga na vitendo hivyo vya jinsia moja na kuondoa mmomonyoko wa maadili ili nchi yetu iendelee kuwa salama, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na kukithiri kwa ukatili dhidi ya watoto hasa kubakwa na kulawitiwa, na sababu mojawapo ni watuhumiwa wanapewa dhamana na hivyo kuharibu ushahidi kabisa. Ni kwa nini Serikali isiwanyime watuhumiwa hawa dhamana kama inavyofanya kwa wale wa *armed robbery*? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo lipo, tunajua kwamba...

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Naibu Waziri, naonaMwanashria Mkuu wa Serikali amesimama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Bila kuathiri majibu ya maswali yanayoendelea kutolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kwanza nimpongeze kwa majibu ambayo ameyatoa kwa maswali haya ya mwisho ambayo yamekuwa na mlengo wa ukiukwaji wa sheria ambazo zinahusu *morality,* yaani ukiukwaji wa haki kwa watu wanaotendewa kwa makosa ya kujamiiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tulipenda kuomba Bunge hili Tukufu lielewe kwamba makosa yote yanatungwa na yanakuwa ni

makosa ya jinai yanapotungwa na Bunge hili. Kama alivyosema Naibu Waziri, baada ya maswali kuwa mengi sana kwenye Bunge hili kuhusiana na nini kifanyike, mwaka 2023 Bunge lilitoa maelekezo kwa Serikali kwamba, ifanye utafiti wa kina kupitia *Law Reform Commission,* ambapo kazi hii inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa swali la Mheshimiwa Esther Matiko, yote ambayo yanaendelea, yanahusisha jamii yetu na makundi mbalimbali, hivyo, hakuna tofauti yoyote kwa sababu uhalifu wowote unapofanyika, mtoa taarifa anatakiwa atoe taarifa yake kwa mujibu wa Kifungu cha Saba cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, na baada ya taarifa ya jinai kutolewa, basi upelelezi unaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la dhamana linashughulikiwa kwa mujibu wa kifungu cha 148 cha Sheria yetu ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai. Inapokuja sasa kwamba kuna mazingira ya kupinga dhamana, mwendesha mashtaka ambaye ndiye anaiwakilisha Jamhuri, anawasilisha pingamizi kwa mujibu wa sheria na linasikilizwa. Wapo wengi ambao hawapewi dhamana kwa sababu ya vitendo walivyovifanya ambavyo viko kinyume na kustahili wao kupewa dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, dhamana ni haki ya Kikatiba na ni haki kwa mujibu wa sheria isipokuwa kwa makosa ambayo Kifungu cha 148(5) imezuia makosa hayo yasidhaminike. Kwa hiyo, kwa makosa yote yanayodhaminika, dhamana hupingwa kuendana na mazingira ambayo nayasema na hulazimika Mahakama yenye dhamana ipewe hoja na ifanye maamuzi. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani kwa sehemu yako umehitimisha, nakushukuru sana.

Tunahamia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 256

**Vyuo Vikuu Kushirikiana na Halmashauri Nchini**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani kuhakikisha kila Chuo Kikuu na Vyuo Vishiriki vinashirikiana na halmashauri ili kuwezesha vyuo hivyo kutekeleza umahiri wao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki hushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji katika shughuli mbalimbali kama vile kuendesha semina, warsha na huduma za ugani katika maeneo mbalimbali kulingana na ubobezi wa chuo kikuu husika *(outreach activities)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hufanya tafiti ambazo matokeo yake hutumika kutatua changamoto mbalimbali za jamii katika halmashauri husika. Pia kumekuwa na utaratibu wa wanafunzi kutoka vyuo vikuu kufanya mafunzo kwa vitendo katika taasisi zilizopo chini ya halmashauri kwa lengo la kutoa huduma kwa jamii pamoja na kupata uzoefu wa kazi wanazozisomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vikuu vitaendelea kushirikiana kwa karibu na halmashauri zote katika kutoa huduma kwa jamii na kutatua changamoto zinazoikabili jamii. Aidha, naomba mamlaka zote za Serikali za Mitaa kuendelea kutoa fursa kwa taasisi za elimu ya juu kutumia rasilimali zilizopo kuwezesha kutoa mafunzo. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Thea.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili utekelezaji mahiri uonekane kiuhalisia Serikali inaonaje sasa kuvielekeza vyuo

kuwa na jiji au halmashauri za kuzilea kama wafanyavyo wenzetu kule Japan, China na Indonesia.?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, wanafunzi wanapata shida sana unapokuja wakati wa kwenda *field* kupokelewa katika taasisi au idara mbalimbali. Je, Serikali ina mpango gani sasa kutoa mwongozo kwa idara na taasisi hasa za Serikali kupokea wanafunzi wa kufanya tafiti zao *freely* bila vikwazo vyovyote? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hakuna utaratibu wa vyuo vikuu kulea halmashauri au majiji katika nchi yetu. Utaratibu uliopo ni kwamba halmashauri hizi ziko huru kupata huduma katika vyuo vikuu au vyuo vikuu vishiriki kwa kadiri ya chuo kikuu kilivyokuwa na wabobezi katika eneo fulani. Sasa kwa vile Mheshimiwa Mbunge ametoa ushauri hapa tuweze kuangalia jambo hili, basi ushauri wake tumeupokea na tunaenda kuufanyia tathmini kuweza kuangalia namna gani vyuo vyetu vinaweza vikashirikiana na halmashauri hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la pili kuhusiana na suala la mwongozo, tunaomba nalo tulipokee. Tutakwenda kukaa na halmashauri zetu pamoja na taasisi nyingine ili kuweza kuona namna bora ya wanafunzi wetu wanapokwenda kufanya tafiti zao katika maeneo mbalimbali ya taasisi hizi nchini wasiweze kupata usumbufu wa aina yoyote, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tumehitimisha kipindi chetu cha Maswali na Majibu kwa Serikali. Sasa nitumie fursa hii kuwatangaza wageni ambao tunao Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza, tunao wageni walioko Jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Makame

Mbarawa, Mbunge na Waziri wa Uchukuzi, kwanza tunaye Profesa Godius Walter Kahyarara - Katibu Mkuu; Dkt. Ally Possi - Naibu Katibu Mkuu; Mheshimiwa Balozi Ernest Jumbe Mangu - Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari; Mheshimiwa Jaji Mshibe Ali Bakari - Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa *TMA;* Bwana Ally Amani Karavina - Mwenyekiti wa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na Dkt. Mwamin Tulli - Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi la Chuo cha Bahari Dar es Salaam *(DMI)*. *(Makofi)*

Wengine ni Bwana Juma Hassan Fimbo - Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA);* Meja Jenerali Mstaafu John Julius Mbung'o - Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Huduma za Meli; Kepteni Mussa Hamza Mandia - Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* na Dkt. Khamis Hassan Mwinyimvua - Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA)*. *(Makofi)*

Vilevile yupo Profesa Ulingeta Obadia Mbamba ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi la Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT)*; Profesa Ame Ahmed Ame ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA);* Profesa Neema Munisi Mori ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)* na Bwana Agustus Emmanuel Fungo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *LATRA – CCC*. *(Makofi)*

Wengine ni Mhandisi Ladislaus Matindi ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa *ATCL;* yupo Bwana Masanja K. Kadogosa ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa *TRC;* yupo Bwana Plusduce Mbossa - Mkurugenzi wa *TPA;* Mhandisi Bruno T. Chingandu - Mkurugenzi Mtendaji *TAZARA;* Dkt. Ladislaus Chang'a, yeye ni Mkurugenzi Mkuu *TMA;* yupo *CPA* Habibu Suluo - Mkurugenzi Mkuu *LATRA;* Bwana Mussa F. Mbura - Mkurugenzi Mkuu *TAA* na Bwana Hamza S. Johari, yeye ni Mkurugenzi Mkuu *TCAA*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunaye Bwana Mohamed M. Salum - Mkurugenzi Mkuu *TASAC;* Bwana Erick Benedict Hamisi, yeye ni Mkurugenzi Mkuu *MSCL;* tunaye Kepteni Budodi Budodi, yeye ni Afisa

Mtendaji Mkuu *TGFA;* yupo Profesa Prosper Mgaya, yeye ni Mkuu wa Chuo cha *NIT* na Dkt. Tumaini S. Gurumo, Mkuu wa Chuo cha *DMI*. Hao ndiyo wageni wa Mheshimiwa Waziri Profesa Makame Mbarawa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo naomba pia niwatangaze wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi, Mbunge ambao ni ndugu zake kutoka Lushoto, Mkoa wa Tanga, wasiamame na ahsante. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Arusha, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni 66 wa Mheshimiwa Venant Daud ambao ni Viongozi wa Jumuiya za CCM kutoka Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora, ahsanteni na karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni 90 wa Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum wa Kata, kutoka Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, kwanza ni wanafunzi 93 na walimu saba kutoka Shule ya Awali na Msingi *Brother Martin* ya Jijini Dodoma. Kama wapo wasimame, ahsante na karibuni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 50 na walimu saba wa Shule ya Awali na Msingi Gloria ya Ihumwa, Jijini Dodoma, wasimame, ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 13 kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania *(TIA)* Tawi la Mwanza, wasimame, ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hapo tumemaliza matangazo yetu kwa sasa. Kama yatajitokeza mengine tutayatangaza wakati ukifika.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**MWENYEKITI:** Hoja za Serikali, Wizara ya Uchukuzi, sasa namwita Waziri wa Uchukuzi awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia kukutana hapa leo tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kuwa, tarehe 30 mwezi Agosti, mwaka jana 2023, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliunda Wizara ya Uchukuzi baada ya kugawanywa kwa iliyokuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Tangu kuundwa kwake, Wizara ya Uchukuzi imeendelea kutekeleza kazi zake kulingana na Hati ya Mgawanyo wa Majukumu iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Uchukuzi. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Rais na Bunge lako Tukufu kuwa, nitaendelea kutekeleza

majukumu yangu kwa uaminifu mkubwa ili kuliletea Taifa letu maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, naomba kutoa hotuba yangu ya kwanza ya Wizara ya Uchukuzi ambayo imejikita katika masuala ya usimamizi na uwezeshaji wa maendeleo ya miundombinu ya uchukuzi. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Ujenzi baada ya iliyokuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kugawanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, niruhusu nitumie fursa hii kuungana na Bunge lako Tukufu katika kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu na kutimiza miaka mitatu katika uongozi wake mahiri ulioleta mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi nyingine, Mheshimiwa Rais ameendelea kuweka mkazo na kipaumbele katika kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za uchukuzi ikiwemo, ujenzi wa *Standard Gauge Railway*, uboreshaji wa bandari, ukarabati na ujenzi wa meli, uendelezaji wa viwanja vya ndege, ununuzi wa mitambo ya kuongozea ndege, ununuzi wa ndege, ununuzi wa rada za hali ya hewa na ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika vyuo vinavyosimamiwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, kwa namna anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utendaji na kuongoza nchi yetu, kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa letu kwa ujumla. Ni dhahiri kuwa, utendaji wake umeleta chachu kubwa katika utendaji wa Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa uongozi wake

makini. Kwa hakika kazi anazozifanya katika utekelezaji wa majukumu yake ndani na nje ya Bunge zimekuwa na ufanisi mkubwa katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika nafasi hiyo. Kwa hakika Naibu Waziri Mkuu ameonesha umakini mkubwa katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi mkubwa na pia kwa heshima kubwa. Nampongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Tunaomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema ya kutekeleza majukumu yake ya kitaifa na kimataifa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu yake katika kumsaidia Mheshimiwa Spika kuliongoza Bunge letu. Vilevile natumia fursa hii kumpongeza Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Giga, kwa kuendelea kuaminiwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Mwenyekiti wa Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nakupongeza wewe Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kwa kuteuliwa kushika nyadhifa ya Uenyekiti wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Mheshimiwa David Kihenzile, Mbunge, na Mheshimiwa Daniel Sillo, Mbunge, waliokuwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri wa Wizara za Uchukuzi na Mambo ya Ndani ya Nchi, mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa naomba kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Sambamba na viongozi hao wa Kamati, ninawashukuru Wajumbe wote wa Kamati. Kamati hii imeendelea kutoa maelekezo na ushauri wenye tija kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa simanzi kubwa nachukua fursa hii kutoa pole nyingi kwa Bunge lako Tukufu na Taifa kwa ujumla kufuatia kifo cha Hayati Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Awamu ya Pili, kilichotokea tarehe 29 Februari, mwaka 2024, na kifo cha Hayati Mheshimiwa Edward Lowassa, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Awamu ya Nne, kilichotokea tarehe 10 Februari, mwaka 2024. Hakika tunaendelea kujifunza kutokana na utumishi wao katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kufuatia kifo cha Hayati Mheshimiwa Francis Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kilichotokea tarehe 1 Julai, 2023 na kifo cha Hayati Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani kilichotokea tarehe 8 Aprili, mwaka huu. Tunaendelea kuthamini na kuenzi michango yao katika Bunge hili na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza watoa hoja wote waliowasilisha hotuba zao kabla yangu. Kipekee namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake ambayo imetoa Hali ya Utekelezaji wa Ujumla katika Utendaji wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na kuonesha dira na mwelekeo wa Taifa letu kwa mwaka wa fedha 2024/2025 katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba uniruhusu nitoe Taarifa ya Mapitio ya

Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2023/2024, sekta ya uchukuzi imeendelea kutoa mchango mkubwa wa ukuaji wa uchumi kwa Taifa kwa kuwa, ni sekta wezeshi katika kuchagiza ukuaji wa sekta nyingine za uzalishaji zikiwemo sekta za kilimo, madini, utalii, viwanda na biashara. Mathalan, katika mwaka 2022 sekta ya uchukuzi ilikua kwa 3.8% na kuchangia katika pato la Taifa kwa 6.7%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sekta hii ni ya tatu kwa kuchangia fedha za kigeni kupitia mauzo ya huduma *(Trade in Services)*. Katika kipindi cha miaka mitatu, mchango wa sekta hii katika fedha za kigeni umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka dola za Marekani bilioni 1.6 Mwaka 2022 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 2.4 mwaka 2024, sawa na ongezeko la 50% kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Uchukuzi, Fungu 52, iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 2.089, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 118.215 ni za matumizi ya kawaida ya Wizara na taasisi zake na shilingi trilioni 1.971 ni za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Mwezi Machi, mwaka 2024, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi trilioni 1.827 sawa na 87.48% ya bajeti yote ya Wizara iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, shilingi bilioni 71.125 ni fedha za matumizi ya kawaida ambazo ni sawa na 60.16% ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa. Shilingi trilioni 1.756 ni fedha za miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na 89.12% ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa. Baada ya kupokea fedha hizo, Wizara ya Uchukuzi iliendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Udhibiti wa Usafiri wa Anga. Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA)* imeendelea kutoa huduma ya udhibiti wa usafiri wa anga nchini. Hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu *TCAA* ilifanya uchunguzi na kusajili ndege 15 ambazo zilipewa vyeti vya ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, jumla ya ndege mbili ziliondolewa kwenye daftari la usajili baada ya kumalizika kwa mikataba ya ukodishaji. Ndege nyingine 91 zilikaguliwa na kupewa vyeti vya ubora ili kuendelea kutoa huduma hapa nchini. Ukaguzi huo umewezesha daftari la usajili wa ndege kuwa na jumla ya ndege 419.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza wigo wa soko la usafiri wa anga nchini, Serikali kupitia *TCAA* iliendelea kusaini mikataba mipya na kupitia mikataba iliyopo ya usafiri wa anga, *(Bilateral Air Services Agreements – BASA)*, baina ya Tanzania na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2024, Serikali ilifanikiwa kusaini Hati za Makubaliano tano za nchi za Poland, Suriname, Algeria, Jamhuri ya Czech na Ivory Coast. Makubaliano hayo yameifanya Tanzania kuwa na mikataba ya *BASA* na nchi 85 ikilinganishwa na nchi 80 iliyokuwa imeingiwa hadi kufikia mwaka wa fedha 2022/2023. Mikataba ya *BASA* imewezesha mashirika 25 ya ndege za kimataifa kutoa huduma nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCAA* pia iliratibu shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo ambapo hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu abiria waliosafiri kwa kutumia usafiri wa anga wameongezeka hadi kufikia abiria 5,080,920 ikilinganishwa na abiria 4,105,375 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2022/2023, ambayo ni sawa na ongezeko la 23.76%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mizigo iliyosafirishwa imeongezeka hadi kufikia tani 27,532 ikilinganishwa na tani 23,070.3 katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/2023 sawa na ongezeko la 19.33%. Utendaji wa *TCAA* umeoneshwa kwenye kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 14 hadi 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa usafiri wa ardhini unaojumuisha usafiri kwa njia ya barabara, usafiri wa reli na usafiri kwa njia ya waya unatekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA)*. Katika kudhibiti mwendo wa mabasi ya masafa marefu na treni, Serikali kupitia *LATRA* imeendelea kufuatilia mwenendo wa mabasi na vichwa vya treni kupitia Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Vyombo *(Vehicle Tracking System)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, mwaka 2024, mabasi 10,270 yanayotoa huduma za usafiri wa masafa marefu na vichwa vya treni 20 vimeunganishwa katika mfumo huo. Matumizi ya mfumo huo yamepunguza ajali zinazotakana na mwendokasi na kuongeza ufanisi wa vyombo vinavyodhibitiwa ambapo kwa mwaka 2022/2023 ajali zilipungua hadi kufikia ajali 166 za mabasi ya masafa marefu ikilinganishwa na ajali 179 zilizotokea mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kuwa, tarehe 28 Juni, mwaka 2023, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitangaza hapa Bungeni uamuzi wa Serikali wa kuondoa zuio la mabasi ya abiria kusafiri nyakati za usiku lililowekwa mwaka 1994. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi na *LATRA* ilifanya maandalizi na kuanza kutoa ratiba za mabasi kusafiri nyakati za usiku kuanzia tarehe 1 Oktoba, mwaka 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, mwaka 2024 jumla ya ratiba za mabasi 798 zimetolewa kwa ajili ya safari za usiku. Ni dhahiri kuwa…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu, Mheshimiwa Esther Matiko.

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utaniruhusu, imekuwa ni kawaida sasa hivi Mawaziri wanasoma, wanaenda mpaka dakika 10, 15, Wabunge hatuna ripoti husika. Wakimaliza tu kusoma sisi tunatakiwa tuanze kuchangia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaposimama kuhusu utaratibu, utaratibu lazima uwe umeelekezwa na Kanuni. Mheshimiwa Matiko tutafanya rejea ya Kanuni, lakini nasisitiza Waheshimiwa Mawaziri na Serikali mjitahidi kuhakikisha kwamba, taarifa zenu zinakuwa zimeingia kwenye vishkwambi vya Wabunge wakati mnasoma taarifa hizi Bungeni ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kufuatilia.

Mheshimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeonesha dhamiri ya kweli ya kuifungua nchi kiuchumi. Utendaji wa *LATRA* umeoneshwa katika kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 23 hadi ukurasa 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa usafiri wa majini, Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania, *(TASAC)*, imeendelea kutoa huduma za udhibiti wa huduma ya bandari, usafiri wa majini Tanzania Bara na kutoa huduma mahsusi ya biashara ya meli kwa bidhaa mahsusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usimamizi wa watoa huduma zinazodhibitiwa, Serikali kupitia *TASAC* imeendelea kutoa leseni na vyeti vya usajili kwa watoa huduma waliokidhi vigezo. Hadi kufikia mwezi Machi, mwaka 2024 jumla ya watoa huduma 1,722 walisajiliwa na kupewa leseni ikilinganishwa na jumla ya watoa huduma 1,498 katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/2023 sawa na ongezeko la 14.95%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TASAC* katika kipindi cha kuanzia Julai, mwaka 2023 hadi Machi, mwaka 2024, imeendelea kurasimisha Bandari Bubu za Tanzania Bara. Katika kutekeleza jukumu hilo, bandari bubu 99 zimekaguliwa na kufanyiwa tathmini ya kina na Serikali kupitia *TASAC* kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za Serikali, bandari 45 zilirasimishwa. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa Serikali inaimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ya bandari ili kuboresha utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TASAC* imeendelea kuratibu shughuli za ufuatiliaji na uokoaji kupitia Vituo vya Ufuatiliaji na Uokoaji Majini vilivyopo Dar es Salaam na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha usalama wa usafiri katika Ziwa Victoria, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda chini ya utaratibu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, zimeendelea kutekeleza mradi wa kikanda wa kuboresha mawasiliano na uchukuzi katika Ziwa Victoria wenye lengo la kuimarisha huduma za utafutaji na uokoaji katika ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, mwaka 2024 ujenzi wa kituo kikuu cha kikanda cha uratibu wa masuala ya utafutaji na uokoaji katika Ziwa Victoria umefikia 26%. Aidha, ujenzi wa vituo vidogo vitatu vya uokoaji na ufuatiliaji unaendelea vizuri. Utendaji kazi wa *TASAC* umeoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 32 hadi 44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imeendelea na utoaji wa huduma na kuratibu shughuli za hali ya hewa nchini. *TMA* imeendelea kutoa utabiri wa kila siku, wa siku kumi na ule wa muda mrefu pamoja na tahadhari ya matukio ya hali mbaya ya hewa ili kuhakikisha usalama wa watu na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TMA* imekamilisha ufungaji wa rada za hali ya hewa katika mikoa ya Kigoma na Mbeya na kufikisha jumla ya rada tano za hali ya hewa hapa nchini. Aidha,

utengenezaji wa rada mbili nyingine unaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, mwaka 2024 na zitafungwa katika Mikoa ya Kilimanjaro na Dodoma. Utendaji kazi wa *TMA* umeoneshwa katika kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 44 hadi 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* imeendelea kusimamia na kutoa huduma zote za kibandari katika Bandari zote za Tanzania Bara. Hadi mwezi Machi, mwaka 2024, *TPA* ilihudumia tani milioni 20.72 ya shehena ya mizigo ikilinganishwa na tani milioni 14.56 katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/2023, sawa na ongezeko la 42.31%. Aidha, kwa upande wa makasha, *TPA* ilihudumia makasha 805,167 ikilinganishwa na makasha 686,609 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la 16.92%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hilo la shehena ya mizigo na makasha limetokana na mikakati mbalimbali inayoendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Serikali kupitia *TPA* imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa bandari nchini pamoja na Bandari Kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *TPA* imeendelea na juhudi mbalimbali za kuboresha huduma zake ikiwa ni pamoja na kufungua ofisi nje ya nchi, kutafuta masoko na kufanya ununuzi wa vifaa na mitambo kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma katika bandari zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, *TPA* imeendelea kutekeleza kazi mbalimbali ambapo uchimbaji wa kina umefikia mita 15.5 na upanuzi wa lango la kuingilia meli ambalo kwa sasa lina upana wa mita 200. Kwa sasa, Bandari ya Dar es Salaam ina uwezo wa kupokea meli kubwa zenye urefu wa mita 305. Aidha, upembuzi yakinifu na uboreshaji wa gati namba nane mpaka 11 na ujenzi wa gati namba 12 mpaka 15 bado unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, mkataba wa kuendeleza miundombinu ya kupokelea mafuta *(Single Receiving Terminal)* unaohusisha ujenzi wa matenki 15 ya mafuta pamoja na miundombinu yake yenye uwezo wa kuhifadhi kiasi cha mita za ujazo 420,000 umesainiwa tarehe 26 Februari, mwaka 2024 na maandalizi ya kuanza ujenzi yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi imeendelea kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwa baadhi ya maeneo ya bandari kwa kuingia ubia na kampuni binafsi katika kuendeleza na kuendesha shughuli za bandari kuanzia gati namba nne mpaka saba. Kwa sasa hatua mbalimbali zikiwemo za makabidhiano na *mobilization* zinaendelea ili kuruhusu utekelezaji rasmi kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea na utaratibu wa kumpata mwekezaji mwingine atakayekuwa na jukumu la kufanya shughuli za uendeshaji wa kuanzia gati namba nane hadi 11. Lengo ni kuongeza tija katika utendaji wa bandari yetu. Utendaji wa kazi wa *TPA*, umeoneshwa katika kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 51 hadi 59. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia na kuendeleza miundombinu ya reli iliyopo ya *Meter Gauge Railway* yenye urefu wa kilometa 2,706 na kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kutumia reli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, shirika limeendelea na ujenzi wa Reli ya kisasa ya *Standard Gauge Railway* ya ushoroba wa kati kwa awamu zote mbili, ambapo awamu ya kwanza ina jumla ya kilometa 1,219 na awamu ya pili ina jumla ya kilometa 1,590. Hivyo kuifanya reli mpya ya *SGR* inayojengwa kuwa na mtandao wenye jumla ya kilometa 2,809 ambazo ni zaidi ya kilometa 103 ikilinganishwa na Reli ya *MGR* ambayo ilijengwa wakati wa mkoloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hiyo, Serikali itaendelea na ujenzi wa reli ya *SGR* kwa maeneo mengine ya ushoroba wa kusini na wa kaskazini kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali iliahidi kuendelea na ujenzi wa reli ya *SGR* kwa awamu zote mbili. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia mwezi Machi, mwaka 2024, ujenzi wa kipande cha kutoka Dar es Salaam – Morogoro umefikia 98.93%; kipande cha kutoka Morogoro – Makutupora umefikia 99.61%; kipande cha kutoka Mwanza – Isaka umefikia 56.21%; kipande cha Makutupora – Tabora umefikia 14.22%; na kipande cha kutoka Tabora – Isaka umefikia 5.72%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa awamu ya pili, kipande cha kutoka Tabora – Kigoma, umefikia 1.81% na ujenzi wa kipande cha Uvinza – Musongati – Gitega (Burundi) umeanza ambapo hatua ya ununuzi wa mshauri elekezi na mkandarasi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuanza uendeshaji wa treni katika reli ya *SGR* kwa kipande cha Dar es Salaam – Dodoma, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kupitia *TRC* inaendelea na majaribio ya miundombinu ya reli kwa ajili ya kuanza utoaji wa huduma hiyo rasmi ifikapo mwezi Julai, mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, majaribio hayo yanafanyika kwa lengo la kukidhi matakwa ya usalama kabla ya kuanza uendeshaji. Utendaji kazi wa *TRC* umeoneshwa katika kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 60 hadi 76. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA)* inamilikiwa na Serikali mbili za Tanzania na Zambia kwa hisa za 50% kwa 50%. Katika kuendeleza huduma ya reli katika nchi hizo mbili, *TAZARA* imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa huduma kusafirisha abiria na mizigo, kulinda na kuimarisha

miundombinu ya reli yenye urefu wa jumla ya kilometa 2,153 na maeneo yote yaliyopo ndani ya ukanda wa reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu, *TAZARA* ilisafirisha jumla ya tani za mizigo 251,264 ikilinganishwa na tani 235,071 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/2023 sawa na ongezeko la 6.89%. Ongezeko hili limechangiwa na ushirikishwaji wa sekta binafsi ya Kampuni ya *Calabash Freight Limited* na *African Inland Container Depot*. Utaratibu huu umeiingizia *TAZARA* mapato ya shilingi bilioni 8.91 kutokana na kampuni hizo kulipia tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, treni za abiria zinazofanya safari kati ya Dar es Salaam – *New Kapiri Mposhi*, Zambia na ile inayosafiri kati ya Stesheni ya Kidatu na Makambako, zilisafirisha jumla ya abiria 672,006. Aidha, Treni ya Jijini Dar es Salaam inayofanya safari zake kati ya Stesheni ya *TAZARA* hadi Stesheni ya Mwakanga – Pugu Jijini Dar es Salaam ilisafirisha abiria 1,582,833 ikilinganishwa na abiria 1,447,738 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/2023 sawa na ongezeko la 9.33%. Utendaji kazi wa *TAZARA* umeoneshwa katika kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 76 hadi 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* imeendelea kutoa huduma za usafiri na usafirishaji katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu, *MSCL* ilisafirisha abiria 198,080 ikilinganishwa na abiria 170,137 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/2023 sawa na ongezeko la 16.42%. Kwa upande wa mizigo, *MSCL* ilisafirisha tani 33,288.44 ikilinganishwa na tani 18,909 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/2023 sawa na ongezeko la 76.05%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili limetokana na kukamilika kwa ukarabati na kuanza kazi kwa meli ya *MV* Umoja ambayo ilianza kutoa huduma mwezi Oktoba, mwaka 2024 katika Ziwa Victoria kati ya Bandari ya Mwanza Kusini na Bandari za *Port Bell* na Jinja nchini

Uganda. Aidha, ujenzi wa Meli ya *MV* Mwanza Hapa Kazi Tu umekamilika kwa 95% na tayari meli hiyo imefanyiwa majaribio ziwani ya mifumo na mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *MSCL*, ilisaini mkataba wa ujenzi wa meli mpya ya kubebea mizigo ya tani 3,000 katika Ziwa Victoria. Pia ilisaini mikataba miwili ya ujenzi wa meli ya mizigo ya tani 3,500 na ujenzi wa kiwanda cha kujengea meli katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kiwanda hiki ni hatua muhimu ya kujivunia kwa Taifa letu kwa kuwa ni mara ya kwanza kujengwa kiwanda cha aina hii hapa nchini ambapo kwa miaka ya nyuma meli nyingi zilikuwa zinajengwa au zinatengenezwa nje ya nchi. Vilevile mradi wa ukarabati wa *MV* Liemba, tayari umesainiwa. Utendaji kazi wa *MSCL* umeoneshwa katika kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 81 hadi 86.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* ina jukumu la kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege 58 vya Serikali vilivyopo Tanzania Bara. Hadi kufikia mwezi Machi, mwaka 2024, *TAA* ilihudumia jumla ya abiria 3,202,573 ikiwa ni sawa na ongezeko la 8.58% ikilinganishwa na abiria 2,949,508 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa, hadi kufikia Machi mwaka 2024, *TAA* ilikamilisha ujenzi wa uzio wa usalama wenye urefu wa kilometa 7.2 na ufungaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na ufungaji wa mfumo wa kamera za usalama *(CCTV Camera)* katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere umekamilika kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutambua umuhimu wa kuwa na viwanja vya ndege venye ubora, *TAA* imeendelea na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha ambapo ujenzi wa jengo jipya la abiria umekamilika kwa 98%. Majengo mapya ya abiria katika Viwanja vya Ndege vya Kahama na Kilwa Masoko yamekamilika, wakati ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mpanda, umekamilika kwa 97%. Aidha, usanifu wa kina wa jengo la mnara wa kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Bukoba, umekamilika na taratibu za ununuzi wa mkandarasi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2023, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa jukumu la ujenzi la viwanja vya ndege litarejeshwa rasmi *TAA* kwa utaratibu maalumu ambao hautaathiri miradi iliyokuwa imeanza kutekelezwa na *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa jukumu hilo sasa limerejeshwa na linatekelezwa na *TAA* kwa miradi mipya na miradi iliyokuwa chini ya 40% ya utekelezaji wake. Baada ya uamuzi huo, *TAA* imeendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege vya Moshi, Lindi, Mtwara na *JNIA* jengo la pili la abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za Serikali za kukuza fursa za ajira na uhaulishaji wa teknolojia *(technological transfer)* kwa wazawa, Serikali kupitia *TAA* imewezesha uwekezaji wa kiwanda cha uunganishaji na utengenezaji ndege ndogo katika Kiwanja cha Ndege cha Morogoro kupitia Kampuni ya *Airplane Africa Limited*. Kampuni hiyo inafanya kazi ya kuunganisha na kutengeneza ndege za kubebea abiria wawili ambazo ni aina ya *Skyleader*. Kwa sasa kiwanda hicho ni cha kipekee Afrika Mashariki ambapo kina matawi katika nchi za Urusi, Jumuiya ya Czech, Ujerumani na China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro *(KIA)*; katika Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2023/2024, niliahidi kuwa Serikali itaendelea na taratibu za kurejesha shughuli za uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha

Kimataifa cha Kilimanjaro kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* kutoka *KADCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu rasmi Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekamilisha urejeshwaji wa Kiwanja cha *KIA* kwa *TAA* kutoka *KADCO* na kiwanja hicho kwa sasa kinaendeshwa na *TAA*. Utendaji kazi wa *TAA* umeoneshwa katika Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 86 hadi 98. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za usafiri wa anga, Serikali imeendelea kuboresha utendaji wa Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL)* kwa kununua ndege mpya na kuboresha miundombinu wezeshi ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na majengo na karakana. Hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu, Serikali imekamilisha malipo ya ndege tatu, ndege mbili za *Boeing 737-9 Max*, tayari zilishawasili nchini na zinafanya kazi. Ndege moja ya *Boeing 787-8 Dreamliner* itawasili mwishoni mwa mwezi huu. Kuwasili kwa ndege hizi kutaifanya *Air Tanzania* kuwa na jumla ya ndege 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuongeza wigo wa huduma zake, *ATCL* imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa anga katika vituo 24 ambapo vituo 13 ni vya ndani na vituo 11 ni vya nje ya nchi. Vituo vya ndani ya nchi ni Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kilimanjaro, Kigoma, Songwe, Mpanda, Mwanza, Songea, Tabora na Zanzibar. Vituo vya nje ya nchi ni Bujumbura, Dubai, Entebbe, Hahaya, Guangzhou, Harare, Lubumbashi, Lusaka, Mumbai, Nairobi na Ndola huko Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa *ATCL* umeongeza utendaji wa *ATCL* ambapo hadi kufika mwezi Machi mwaka 2024, *ATCL* ilisafirisha abiria 850,660 ikilinganishwa na abiria 826,594 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/2023 sawa na ongezeko la 2.9%. Vilevile *ATCL* iliweza kusafirisha jumla ya tani 5,034.2 za mizigo ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na tani 2,680.9 katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/2023 sawa na ongezeko la 87.78%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hilo limetokana na kuanza kufanya kazi kwa ndege ya mizigo ya aina ya *Boeing* 767-300F yenye uwezo wa kubeba tani 54. Utendaji kazi wa *ATCL* umeainishwa katika kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 98 hadi 107. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya mafunzo ya sekta; katika kutekeleza azma ya Serikali ya kujenga uwezo na kutumia wataalamu wa ndani pamoja na kupunguza gharama za kusomesha wataalamu nje ya nchi, Serikali kupitia vyuo vya kisekta vinavyosimamiwa na Wizara ya Uchukuzi, imeendelea kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali za mafunzo ya usafiri wa anga, usafiri wa ardhini na usafiri majini, kwa lengo la kuzalisha wataalamu wanaotoa huduma katika sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa Vyuo vya Mafunzo vya Sekta umeonyeshwa katika kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 107 hadi 122.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta ya uchukuzi, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba miradi ya maendeleo ya sekta ya uchukuzi ni miongoni mwa miradi ambayo katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea kutekelezwa bila kusuasua na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ya kimkakati inayojumuisha miradi ya reli, viwanja vya ndege, uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania, ujenzi na uboreshaji wa bandari, ujenzi na ukarabati wa meli katika Maziwa Makuu, ufungaji wa rada za hali ya hewa na uboreshaji wa vyuo vya mafunzo vya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muhtasari, yapo mafanikio mengi na makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita. Mafanikio hayo ni pamoja na

kuongeza wigo wa reli ya *SGR* kwa kuifanya kuwa ya kikanda, ambapo Serikali hii imeweza kuanza mikakati ya kuifikisha reli ya *SGR* nje ya mipaka ya nchi; kuendelea kuboresha kwa kasi huduma za meli, ambapo baadhi ya meli zimeanza kujengwa na kukarabatiwa; kutekeleza kwa vitendo Mpango wa Uboreshaji wa Huduma za Bandari Nchini kwa Serikali ya Awamu ya Sita kuendelea kushirikisha sekta binafsi; kuanzishwa kwa mafunzo ya urubani nchini kwa mara ya kwanza tangu kupata uhuru na kubaini; na kutekeleza mikakati iliyoondoa foleni ya malori katika mpaka wa Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita yaliyomo ya mwaka wa fedha 2023/2024 yameoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 132 hadi 146.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Uchukuzi imekabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizo na mikakati ya kuzitatua imeoneshwa katika kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia ukurasa wa 147 hadi 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, hususan bajeti ya miradi ya maendeleo ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati inayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Uchukuzi – Fungu 52 imetengewa jumla ya shilingi 2,729,676,417,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 114,744,476,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 2,614,931,941,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotengwa zinajumuisha shilingi 86,661,930,000 kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 28,082,546,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Vilevile, fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa zinazojumuisha shilingi 2,524,369,202,000 ni fedha za ndani na shilingi 90,562,739,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ifuatayo itatekelezwa: Miradi ya ukarabati na ujenzi wa viwanja vya ndege nchini; mradi wa uboreshaji wa usalama wa usafiri katika Ziwa Victoria; mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam; mradi wa ujenzi wa reli ya *SGR;* mradi wa ukarabati wa reli ya *MGR;* mradi wa ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga; mradi wa ukarabati wa reli ya *TAZARA;* mradi wa ununuzi wa vifaa na miundombinu ya hali ya hewa; mradi wa uboreshaji ya Kampuni ya Ndege Tanzania; mradi wa ujenzi na ukarabati wa meli katika Maziwa Makuu ikiwemo MV Liemba na MV Mwongozo; mradi wa ununuzi wa mitambo ya mawasiliano ya ndege; mradi wa uboreshaji wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika vyuo vya *DMI na NIT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina na kazi zinazofanyika katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kila mradi wa maendeleo na fedha zilizotengwa yameainishwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 153 hadi 173. Kazi nyingine zitakazotekelezwa na Wizara kupitia mapato ya ndani ya taasisi zilizo chini yake zimeainishwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 173 hadi 209.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024. Ufanisi huu ulitokana na mchango mkubwa na ushirikiano mkubwa wa wadau mbalimbali. Ili Wizara iendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kuishauri Serikali ipasavyo katika masuala mbalimbali hususan yanayogusa maendeleo ya wananchi moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nawaomba wananchi na wadau wengine kuendelea kushirikiana na Serikali katika kulinda miundombinu ya usafiri na usafirishaji ambayo Serikali imekuwa ikitumia kiasi kikubwa cha fedha kuijenga na kuikarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza na kutambua mchango unaotolewa na viongozi wenzangu katika kutekeleza majukumu ya Wizara, nikianza

na Naibu Waziri, Mheshimiwa David Kihenzile, Katibu Mkuu, Prof. Kahyarara na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Possi. Pia, kipekee napenda kuishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa jitihada kubwa wanazozifanya katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kutumia fursa hii kwa niaba ya Wizara kutoa shukurani za dhati na kuwatambua wadau wote wa Wizara ambao wamechangia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kwa namna ya kipekee niruhusu niwatambue wafuatao: Shirika la Kimataifa la Usalama, Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga; Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini, Shirika la Hali ya Hewa Duniani; Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Japani *(JAICA),* na Korea Kusini *(KOICA),*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengine ni Ujerumani *(KfW), Foreign Common Wealth and Development Office (U.K),* Shirika la Maendeleo la Ufaransa, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Shirika la Maendeleo la Marekani, *Trade Mark Africa,* Sekretarieti ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Nchi za Urusi, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Japani, India, China, Denmark, Korea Kusini, Ufaransa, Ubeligiji, Ujerumani na Uturuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengine ni Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *NSSF* na *PSSSF,* Taasisi za Kifedha za *CRDB, NMB, AZANIA BANK, NBC,* na *TCB* na Asasi mbalimbali za kiraia, Sekta binafsi pamoja na wadau wengine wengi ambao sikuwataja hapa kutokana na uwingi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee niruhusu nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti na kwa Bunge zima kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muhtasari wa maombi ya fedha ya Wizara ya Uchukuzi katika mwaka wa fedha 2024/2025 naomba

kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,729,676,417,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 114,744,476,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 2,614,931,941,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha majedwali mbalimbali yenye taarifa na takwimu kwa ajili ya kutoa uelewa zaidi kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kuhusu kazi zinazotekelezwa na Wizara. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya hotuba hii. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara *www.uchukuzi.go.tz*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA UCHUKUZI MHESHIMIWA PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A: UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/24 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/25.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kwanza kabisa naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi, kwa kutujalia afya njema, usalama na amani katika Taifa letu na kutuwezesha kukutana tena siku hii ya leo. Ninamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze vyema katika kujadili Hotuba hii ya Wizara ya Uchukuzi na Bajeti ya Serikali kwa ujumla ili tuweze kuendelea kuwahudumia Watanzania.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** utakumbuka kuwa, tarehe 30 Agosti, 2023 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliunda Wizara ya Uchukuzi baada ya kugawanywa kwa iliyokuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Tangu kuundwa kwake, Wizara ya Uchukuzi imeendelea kutekeleza kazi zake kulingana na Hati ya Mgawanyo wa Majukumu iliyotolewa. Kwa heshima kubwa, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Uchukuzi. Ninaomba kumhakikishia Mhe. Rais na Bunge lako Tukufu kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uwezo na uaminifu mkubwa ili kuliletea Taifa letu maendeleo. Kwa muktadha huo, naomba kutoa Hotuba yangu ya kwanza ya Wizara ya Uchukuzi ambayo imejikita katika masuala ya usimamizi na uwezeshaji wa maendeleo ya miundombinu, huduma za uchukuzi na hali ya hewa kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Ujenzi baada ya iliyokuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kugawanywa.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee, niruhusu nitumie fursa hii kuungana na Bunge lako Tukufu katika kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu na kutimiza miaka mitatu (3) katika uongozi wake mahiri ulioleta mafanikio makubwa. Pamoja na juhudi nyingine, Mheshimiwa Rais ameendelea kuweka mkazo na kipaumbele katika kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za uchukuzi ikiwemo: ujenzi wa reli ya *Standard Gauge Railway* (SGR); uboreshaji wa bandari; ukarabati na ujenzi wa meli; ujenzi wa boti za utafutaji na uokoaji katika Maziwa Makuu; uendelezaji wa viwanja vya ndege; ununuzi wa mitambo ya kuongozea ndege; ununuzi wa ndege; ununuzi wa rada za hali ya hewa; uendelezaji wa miundombinu; na ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika vyuo vinavyosimamiwa na Wizara.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla miradi hiyo imeendelea kutekelezwa kwa kasi kubwa na hivyo kuchochea ukuaji wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Vilevile, kutokana na umahiri wake katika utendaji, tunu za nchi yetu za Amani, Umoja

wa Kitaifa na Diplomasia ya Uchumi vimeendelea kuimarika na kuifanya nchi yetu kuwa mfano kwa Mataifa mengine.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango kwa namna anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utendaji na kuongoza nchi yetu kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa kwa ujumla. Ni dhahiri kuwa, utendaji wake umeleta chachu kubwa katika utendaji wa Serikali ya Awamu ya Sita.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), kwa uongozi wake makini. Kwa hakika kazi anazozifanya katika utekelezaji wa majukumu yake ndani na nje ya Bunge zimekuwa na ufanisi mkubwa katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Aidha, sote ni mashuhuda kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa kiungo muhimu kati ya Bunge na Serikali.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** pia nimpongeze Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.) kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika nafasi hiyo. Kwa hakika Naibu Waziri Mkuu ameonesha umakini mkubwa katika kutekeleza majukumu yake.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi mkubwa na pia kwa heshima kubwa nakupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), nafasi ambayo ni heshima kubwa kwako na kwa nchi yetu. Tunakuombea Mungu aendelee kukupa afya njema ya kutekeleza majukumu yako ya kitaifa na kimataifa kwa ufanisi.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, nimpongeze Naibu Spika Mheshimiwa

Mussa Azzan Zungu (Mb.), kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu yake katika kumsaidia Spika kuliongoza Bunge. Vilevile, nitumie fursa hii kumpongeza Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), kwa kuendelea kuaminiwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Mwenyekiti wa Bunge letu.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile nawapongeza Mheshimiwa **Dkt. Joseph Kizito Mhagama**, Mbunge wa Jimbo la Madaba na Mheshimiwa **Deodatus Philip Mwanyika**, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa kuteuliwa kushika nyadhifa za uenyekiti wa Bunge hili. Pia niwapongeze Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mb.) na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.) waliokuwa Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri wa Wizara za: Uchukuzi na Mambo ya Ndani ya Nchi, mtawalia.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa naomba kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso (Mb.) na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Anne Kilango Malecela (Mb.). Sambamba na viongozi hao wa Kamati, niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kamati hii imeendelea kutoa maelekezo na ushauri wenye tija kwa Wizara. Nikiri kuwa, Kamati hii imekuwa chachu ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa Wizara. Napenda pia kuishukuru Kamati kwa uchambuzi makini iliyoufanya kwenye Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/24 na Mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25. Maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa umeiwezesha Wizara kukamilisha maandalizi ya Mpango wa makadirio ya mapato na matumizi tunaouwasilisha leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa simanzi kubwa nichukue fursa hii kutoa pole nyingi kwa Bunge lako Tukufu na Taifa kwa ujumla kufuatia kifo cha Hayati **Ali Hassan Mwinyi**, aliyekuwa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Pili kilichotokea

tarehe 29 Februari, 2024 na kifo cha Hayati **Edward Ngoyai Lowassa,** aliyekuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Nne kilichotokea tarehe 10 Februari, 2024. Hakika tutaendelea kujifunza kutokana na utumishi wao katika kulitumikia Taifa. Aidha, nitoe pole kwa Bunge lako Tukufu kufuatia kifo cha **Francis Leonard Mtega** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kupitia Chama cha Mapinduzi kilichotokea tarehe 1 Julai, 2023 na kifo cha **Ahmed Yahya Abdulwakil** aliyekuwa Mbunge Jimbo la Kwahani kupitia Chama cha Mapinduzi kilichotokea tarehe 8 Aprili, 2024. Tutaendelea kuthamini na kuenzi michango yao katika Bunge hili na Taifa kwa ujumla.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwapongeza watoa hoja wote waliowasilisha hotuba zao kabla yangu. Kipekee nimshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imetoa hali ya utekelezaji wa ujumla katika utendaji wa Serikali kwa mwaka 2023/24 pamoja na kuonesha dira na mwelekeo wa Taifa letu kwa mwaka 2024/25 katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Uchukuzi.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa uniruhusu nitoe taarifa ya mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/24 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25.

## B: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

16. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uchukuzi imeendelea kutoa mchango mkubwa wa ukuaji wa Uchumi kwa Taifa kwa kuwa ni sekta wezeshi katika kuchagiza ukuaji wa sekta nyingine za uzalishaji zikiwemo sekta za kilimo, madini, utalii, viwanda na biashara. Mathalan, katika mwaka 2022 Sekta ya Uchukuzi ilikua kwa asilimia 3.80 na kuchangia katika Pato la Taifa kwa asilimia 6.70. Hivyo,

utendaji wa sekta hii una mchango mkubwa katika kuwezesha utendaji wa sekta nyingine. Sekta hii ni ya tatu kwa kuchangia fedha za kigeni kupitia mauzo ya huduma (Trade in Services). Kwa mujibu wa Taarifa za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kipindi cha kuishia mwezi Februari, 2024, Sekta ya Uchukuzi ilichangia mauzo ya kiasi cha Dola za Marekani bilioni 2.4 ya fedha za kigeni ikiwa nyuma ya mauzo ya dhahabu na biashara za utalii. Pia katika utalii, mchango wa usafirishaji ni mkubwa na umejumuishwa katika mapato hayo (Travel and Tourism), hususan watalii wanaofika nchini kupitia usafiri wa anga pamoja na usafirishaji wa ndani kutoka eneo moja kwenda eneo jingine. Aidha, katika kipindi cha miaka mitatu, mchango wa sekta hii katika fedha za kigeni umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka Dola za Marekani bilioni 1.6 mwaka 2022 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 2.4 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 50 katika kipindi hicho.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mchango wa fedha za kigeni, Sekta ya Uchukuzi imekuwa na mchango mkubwa katika uchumi ikiwemo: mchango mkubwa katika ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi nyingine, hususan inayotokana na mafuta ya petrol na dizeli; Ajira kwa mamilioni ya Watanzania walioajiriwa au kujiajiri katika biashara za bodaboda, bajaji, taxi, malori ya mizigo, uendeshaji wa bandari, reli na ndege; Ufungamanishaji wa uchumi kwani sekta zote zinategemea huduma ya usafirishaji katika kuunganishwa kwa namna tofauti; na Urahisishaji biashara ndani ya nchi, nchi za jirani na biashara za kimataifa.

18. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Uchukuzi (Fungu 62) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,089,245,508,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 118,215,599,000** ni za Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Taasisi zake na **Shilingi 1,971,029,909,000** ni za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi 1,827,759,579,008.65 sawa na asilimia 87.48 ya bajeti yote ya Wizara iliyoidhinishwa.

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya Shilingi 118,215,599,000 zilizoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Shilingi 89,291,108,000 ni fedha za Mishahara na Shilingi 28,924,491,000 ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC) kwa ajili ya Wizara na Taasisi zake. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya Shilingi 71,125,937,092.65 sawa na asilimia 60.17 ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa zilikuwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo zilizotolewa, Shilingi 56,024,111,119.74 zilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na Shilingi 15,101,825,972.91 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) ya Wizara na Taasisi.

**Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Uchukuzi ilitengewa jumla ya Shilingi 1,971,029,909,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,863,764,800,000 ni fedha za ndani na Shilingi 107,265,109,000 ni fedha za nje. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya Shilingi 1,756,633,641,916 sawa na asilimia 89.12 ya bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa zilitolewa.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea fedha hizo, Wizara ya Uchukuzi ilitekeleza shughuli mbalimbali za utoaji wa huduma za uchukuzi pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kielelezo na kimkakati ambayo pindi itakapokamilika itaimarisha huduma za uchukuzi nchini kwa kuongeza usalama; uhakika na kuleta unafuu wa gharama katika huduma kwa Watanzania na wadau wengine wakiwemo wa nchi zinazotumia bandari zetu.

**Udhibiti wa huduma za Usafiri wa Anga**

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imeendelea kutoa huduma za udhibiti wa usafiri wa anga, viwanja vya ndege, masuala ya kiusalama na kiuchumi katika huduma za usafiri wa anga pamoja na kutoa huduma za

uongozaji ndege katika viwanja 15 vya Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza, Bukoba, Arusha, Pemba, Tabora, Kigoma, Dodoma, Iringa, Songwe, Mtwara, Tanga, Songea na Kilimanjaro. Aidha, TCAA imeendelea kudhibiti viwanja vya ndege vinavyomilikiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) pamoja na Sekta Binafsi.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kudhibiti usafiri wa anga nchini tuliahidi kuendelea kusimamia ubora wa huduma za usafiri wa anga kulingana na viwango vya kimataifa. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia TCAA imeendelea kuhakikisha usalama wa usafiri wa anga kwa kutoa vyeti vya ubora kwa ndege zinazotoa huduma nchini ambapo hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya ndege 15 zilisajiliwa na kufanyiwa ukaguzi na kupewa vyeti vya ubora (Certificate of Airworthiness). Aidha, jumla ya ndege mbili (2) ziliondolewa kwenye daftari la usajili baada ya kumalizika kwa mikataba ya ukodishaji. Ndege nyingine 91 zilikaguliwa na kupewa vyeti vya ubora ili kuendelea kutoa huduma nchini. Ukaguzi huo umewezesha daftari la usajili wa ndege kuwa na jumla ya ndege 419.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** TCAA imeendelea kutoa huduma za uongozaji ndege zinazoruka na kupita katika anga la juu katika nchi ya Burundi. Anga la juu la Burundi limeendelea kukasimishwa kwa Tanzania na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO). Kupitia TCAA, nchi yetu imeendelea kuaminika katika usimamizi wa masuala ya anga kimataifa kutokana na ubora wa huduma zake inazoendelea kuzitoa. Vilevile, kutokana na ufanisi huo, Tanzania kupitia TCAA imeendelea kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uratibu wa Usafiri wa Anga Barani Afrika (The African Flight Procedure Programme - AFPP) kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2022/23 – 2024/25. Aidha, baada ya muhula huo kuisha nchi yetu kulingana na vigezo inaweza kutetea nafasi yake. Kamati hiyo ina jukumu la kujadili uendelezaji wa miundombinu ya njia za ndege angani. Kupitia nafasi hiyo, nchi yetu imeendelea kujijengea umahiri katika usafiri wa anga kimataifa.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza wigo wa soko la usafiri wa anga nchini kwa kuvutia mashirika ya ndege ya kimataifa kutoa huduma za usafiri wa anga pamoja na kuimarisha ushindani katika utoaji wa huduma, Serikali kupitia TCAA imeendelea kusaini mikataba mipya na kupitia mikataba iliyopo ya usafiri wa Anga (Bilateral Air Services Agreements - BASA) baina ya Tanzania na nchi nyingine. Hadi kufikia Machi 2024, Serikali ilifanya majadiliano ya mikataba ya usafiri wa Anga na nchi 11 katika Mkutano wa Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAN2023) uliofanyika mwezi Disemba 2023 jijini Riyadh, Saudi Arabia na kufanikiwa kusaini Hati za Makubaliano tano (5) za nchi za Poland, Suriname, Algeria, Jamhuri ya Czech na Ivory Coast. Makubaliano hayo yaliyosainiwa yanaifanya Tanzania kuwa na Mikataba ya BASA na nchi 85 ikilinganishwa na nchi 80 iliyokuwa imeingiwa hadi kufikia mwaka wa fedha 2022/23. Mikataba ya BASA imewezesha mashirika 25 ya ndege za kimataifa kutoa huduma nchini.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, TCAA iliratibu shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo ambapo hadi kufikia Machi, 2024 abiria waliosafiri kwa kutumia usafiri wa anga wameongezeka hadi abiria 5,080,920 ikilinganishwa na abiria 4,105,375 waliotumia usafiri wa anga katika kipindi kama hicho cha mwaka 2022/23, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 23.76. Kati ya abiria hao waliosafirishwa, abiria 2,769,192 walisafiri ndani ya nchi na abiria 2,311,728 walisafiri kimataifa. Ongezeko hilo limetokana na kuendelea kuimarika kwa biashara ya usafiri wa anga nchini kutokana na ongezeko la watalii pamoja na kuimarika kwa biashara ya usafiri wa anga duniani.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mizigo iliyosafirishwa kupitia usafiri wa anga iliongezeka hadi kufikia tani 27,532 ikilinganishwa na tani 23,070.3 za mizigo zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 19.33. Ongezeko la mizigo iliyosafirishwa linatokana na jitihada za Serikali kuendelea kuboresha huduma za usafiri wa anga ikiwa ni pamoja ununuzi wa ndege ya mizigo ambayo ilianza kutoa huduma mwezi Juni, 2023.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** TCAA imeendelea kuongoza ndege za mashirika ya ndani na kimataifa ambapo hadi kufikia Machi, 2024 miruko ya safari za ndege ilifikia 205,968 ikilinganishwa na miruko 109,308 iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 88.43. Ongezeko hilo limetokana na juhudi za Serikali zinazoendelea kuchukuliwa zikiwemo za: ununuzi wa ndege mpya; mikakati ya kujitangaza zaidi kimataifa; na kuendelea kuingia makubaliano ya usafiri wa anga na nchi mbalimbali.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na miongozo ya udhibiti na usalama wa usafiri wa anga inayotolewa kitaifa na kimataifa inayosimamiwa na TCAA, uwezo wa uokoaji na udhibiti wa majanga ya ajali umeimarika nchini. Hadi kufikia Machi, 2024 ilitokea ajali ya ndege moja (1) ya EMB120 ya kampuni ya Unity Air katika kiwanja cha Ndege cha Mikumi National Park na watu wote 33 waliokuwa ndani ya ndege hiyo waliokolewa. Aidha, matukio mengine mawili (2) yanayohusisha kampuni ya Unity Air yalitokea katika viwanja vya ndege vya Mikumi na Seronera ambapo katika matukio hayo yote watu wote waliokuwemo ndani ya ndege waliokolewa.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usalama wa usafiri wa anga, katika hotuba yangu ya mwaka jana tuliahidi kuendelea kutekeleza mradi wa ununuzi wa mitambo na vifaa vya kuongozea ndege (VHF). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imeendelea kuboresha mawasiliano ya sauti baina ya Mwongoza Ndege na Rubani ambapo ufungaji wa mitambo ya mawasiliano ya sauti unaendelea kufanyika katika viwanja vya ndege 13 ambavyo ni Pemba, Abeid Amani Karume International Airport (AAKIA), Kilimanjaro (KIA), Tanga, Dodoma, Arusha, Tabora, Kigoma, Mtwara, Iringa, Mwanza, Songea na Songwe. Utekelezaji huu umefikia asilimia 80.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, ufungaji wa mitambo umeendelea kwenye vituo 18 (VHF relay stations) kwa ajili ya mawasiliano ya anga la juu ambavyo ni Gairo (Morogoro),

Matogoro (Songea), Michakaini (Pemba), Nambunga (Newala-Mtwara), Lolkisale (Arusha), Kwenjugo (Handeni - Tanga), Mwaseni (Rufiji - Pwani), Kitulo (Njombe), Kaluwe (Mbeya), Mwisi (Igunga - Tabora), Kasulu (Kigoma), Nyamanyama (Biharamulo - Kagera), Ndisso - Sitalike (Katavi), Muganza (Butiama - Mara), Mugumu (Serengeti), Oldean Malanja (Ngorongoro - Arusha), Lubuli (Dodoma) na Ngoli (Dodoma). Utekelezaji wake umefikia asilimia 80.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuboresha utoaji wa huduma za usafiri wa anga, Wizara kupitia TCAA imeanza taratibu za kuanza uboreshaji wa Chuo cha Usafiri wa Anga. Chuo hiki kimesajiliwa kimataifa na kutambuliwa na ICAO kwa ajili ya kutoa mafunzo ya usalama wa anga. Kwa sasa Upembuzi Yakinifu umekamilika na Mshauri Elekezi amepatikana. Chuo hiki kikikamilika kitakuwa cha kwanza kwa ukubwa na cha kisasa katika nchi za Afrika Mashariki. Chuo hiki pamoja na manufaa mengine, kitawezesha kuongeza fedha za kigeni kutokana na malipo ya ada za washiriki kutoka nje ya nchi; kuongeza mapato ya Serikali; na kuendelea kuitangaza Tanzania kimtaifa.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2024 TCAA ilitekeleza kazi nyingine kama ifuatavyo:-

i. Kukamilisha ufungaji wa mitambo ya kutoa taarifa za hali ya hewa kwa njia ya mfumo wa sauti ya radio (D-ATIS system) katika viwanja vya ndege vya Kilimanjaro na Arusha;

ii. Kuhakiki na kuboresha michoro inayoonesha taratibu za utuaji wa ndege (GNSS procedures) kwa kutumia vifaa vya mawasiliano vya angani (Satellite) na vya ardhini katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere (JNIA), KIA na Arusha;

iii. Kukamilisha matengenezo kinga (Preventive Maintenance) ya mitambo ya kuongozea ndege katika vituo 10 vya mawasiliano vya Lilungu, Gairo, Nyanshana, Lolkisale, Changarawe, Kaluwe, Matogoro, Mnyusi, Kasulu na Kazehill pamoja na viwanja 14 vya ndege vya JNIA, Abeid Amani

Karume cha Zanzibar (AAKIA), Kilimanjaro, Mwanza, Dodoma, Songea, Pemba, Mtwara, Kigoma, Tabora, Tanga, Arusha, Iringa na Songwe;

iv. Kukamilisha matengenezo kinga katika mtambo wa kufundishia waongoza ndege wa Chuo cha Usafiri wa Anga *(3D Tower Simulator and Radar Simulator);*

v. Kukamilisha uchoraji wa ramani ya kuonyesha njia ya ndege ndani ya Kiwanja *(Aerodrome ground movement charts)* katika viwanja vya ndege vya KIA na Mtwara; na

vi. Kukamilisha ukarabati wa mnara wa kuongozea ndege *(Control Tower)* katika Kiwanja cha Ndege cha Mtwara.

**Udhibiti wa Usafiri Ardhini**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** udhibiti wa Usafiri Ardhini unaojumuisha usafiri kwa njia ya barabara, usafiri wa reli, na usafiri kwa njia ya waya unatekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA). LATRA inadhibiti utoaji wa huduma za usafiri kibiashara kwa njia ya barabara ikijumuisha usafiri wa Umma kwa mabasi ya masafa marefu na yale ya mijini; magari ya mizigo; na usafiri wa kukodi wa abiria ikiwemo teksi za kawaida, teksi mtandao, pikipiki za magurudumu matatu (maarufu kwa jina la bajaji), na pikipiki za magurudumu mawili (maarufu kwa jina la bodaboda). Vilevile, LATRA inadhibiti huduma za usafiri wa reli na miundombinu yake pamoja na usafiri kwa njia ya waya.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, LATRA inatoa, inahuisha na kufuta leseni za usafirishaji; kudhibiti viwango vya tozo za huduma; kufuatilia mwenendo wa utendaji kazi wa sekta zinazodhibitiwa kwa kuangalia viwango vya uwekezaji, gharama za upatikanaji na ufanisi wa huduma; kusajili na kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wa vyombo vya usafiri; kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na vyombo vinavyodhibitiwa; kutoa elimu kwa umma; na kusuluhisha migogoro itokanayo na watoa huduma za usafiri ardhini.

## Ufuatiliaji mwenendo wa Mabasi ya Masafa Marefu na Treni

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kudhibiti mwenendo wa mabasi ya masafa marefu na treni, Serikali kupitia LATRA imeendelea kufuatilia mwenendo wa mabasi na vichwa vya treni kupitia Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Vyombo (Vehicle Tracking System – VTS). Hadi kufikia Machi, 2024 mabasi 10,270 yanayotoa huduma ya usafiri wa masafa marefu na vichwa vya treni 20 (TAZARA - 18 na TRC - 2) vimeunganishwa katika mfumo huo. Matumizi ya mfumo huo yamepunguza ajali zitokanazo na mwendokasi na kuongeza ufanisi wa vyombo vinavyodhibitiwa ambapo kwa mwaka 2022/23 ajali zilipungua hadi kufikia ajali 166 za mabasi ya masafa marefu ikilinganishwa na ajali 179 zilizotokea mwaka 2021/22, sawa na punguzo la asimilia 7.26 za ajali za mabasi. Aidha, mpango wa Serikali ni kuendelea kuimarisha udhibiti kwa kuyaunganisha magari ya mizigo na mabasi ya masafa mafupi kwenye mfumo wa VTS.

37. ***Mheshimiwa Spika***, utakumbuka kuwa, tarehe 28 Juni, 2023, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitangaza hapa Bungeni uamuzi wa Serikali kuondoa zuio la mabasi ya abiria kusafiri nyakati za usiku lililowekwa mwaka 1994. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi na LATRA ilifanya maandalizi na kuanza kutoa ratiba za mabasi kusafiri nyakati za usiku kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2023. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya ratiba za mabasi 798 zimetolewa kwa ajili ya safari za usiku. Kwa ujumla usafiri wa saa 24 unaungwa mkono na watanzania wengi hususan wafanyabiashara na watumiaji wengine wa huduma hiyo.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** hakika hatua hii imeleta manufaa mengi yakiwemo ya kutumia nyakati za usiku katika safari na hivyo kupata muda wa nyakati za mchana kutumika katika shughuli zingine za kiuchumi na kijamii. Aidha, hatua hiyo imepunguza msongamano wa mabasi barabarani tofauti na ilivyokuwa awali ambapo mabasi mengi yalikuwa yanaanza safari kwa pamoja. Ni dhahiri kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe.

Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeonesha dhamira ya kweli ya kuifungua nchi kiuchumi.

39. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha kunakuwa na usalama katika safari zinazofanyika nyakati za usiku kwa mabasi ya masafa marefu, Serikali imeweka utaratibu unaofuatwa na wamiliki pamoja na madereva wa mabasi wanaosafirisha abiria nyakati za usiku ikiwemo utaratibu wa mabasi ya masafa marefu zaidi ya saa nane (8) kuwa na madereva wawili (2). Sambamba na hilo, Serikali kupitia LATRA na Jeshi la Polisi imeimarisha udhibiti na usalama kwa mabasi hayo ikiwemo kuimarisha ufuatiliaji wa safari za mabasi wakati wote kupitia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Mabasi (VTS). Katika kuboresha usimamizi wa VTS, Serikali imeandaa na kutangaza Kanuni za Matumizi ya VTS ya mwaka 2024 ambazo zilianza kutumika mwezi Januari, 2024.

**Udhibiti wa madereva na wahudumu wengine wa vyombo vinavyodhibitiwa.**

40. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia LATRA imeendelea kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wengine wa vyombo vinavyodhibitiwa na LATRA ili kuboresha ufanisi na usalama. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya madereva 7,867 walisajiliwa ili kuweza kuthibitishwa baada ya kufanya mtihani maalumu wa kudhibitisha umahiri wa madereva. Aidha, jumla ya madereva 3,082 walifanya mtihani, kati yao madereva 1,441 walithibitishwa. Kati ya madereva waliothibishwa, madereva 1,190 wamesajiliwa kwenye mfumo wa kufuatilia mwenendo wa mabasi (VTS) na kupatiwa vitufe maalumu vya utambulisho (i-buttons) kinachowezesha kutambua madereva wanaoendesha magari ya abiria wakati wote wa safari. Hata hivyo, kufuatia matukio ya ajali yaliyoanza kujitokeza wakati wa mchana na kubainika kuwa sababu za ajali hizo ni uchovu wa madereva kwa safari za usiku, LATRA imeanza kuhakikisha madereva wanaosafiri mchana pia wanatumia i-buttons.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** LATRA inaendelea kuboresha mfumo huu ili utumike kuthibitisha madereva wa treni kwa ajili ya kuimarisha usalama wa huduma za usafiri wa treni. Halikadhalika, Serikali kupitia LATRA imeendelea kuboresha Mfumo wa TEHAMA unaojulikana kama *Railway and Road Information Managemet System* (RRIMS) unaotumiwa na watoa huduma kuwasilisha maombi ya leseni za usafirishaji pamoja na majukumu ya kiudhibiti.

**Matumizi ya tiketi za kielektroniki**

42. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali iliahidi katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2023/24 kufanya maboresho katika mfumo wa tiketi za kielektroniki (e-ticketing system) ili kuwawezesha abiria kuchagua na kukata tiketi mahali popote bila kufika vituoni. Nitumie nafasi hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa, mfumo wa tiketi za kielektroniki umeboreshwa ambapo watoa huduma wengi wamewawezesha abiria kukata tiketi kwa njia ya mtandao akiwa mahali popote bila kufika kituoni. Mfumo huo umesaidia kupunguza kero kwa abiria zinazotokana na 'wapiga debe' na pia wamiliki wa mabasi wanaweza kudhibiti mapato yao na kujua idadi ya abiria waliosafirishwa. Aidha, mfumo huo unamwezesha abiria kukata tiketi mwenyewe kwa kuchagua kampuni ya usafirishaji, daraja la basi, namba ya kiti na kulipia kisha kupata tiketi ya kielektroniki. Hata hivyo, ili kuboresha usimamizi wa tiketi za kielektroniki Serikali imeandaa na kutangaza Kanuni za Matumizi ya Tiketi za Kielektroniki za mwaka 2024 zilizoanza kutumika mwezi Januari, 2024.

**Udhibiti wa viwango vya nauli na utoaji wa leseni**

43. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia LATRA imeendelea kudhibiti viwango vya nauli za huduma zinazodhibitiwa ambapo viwango vya nauli za abiria kwa mabasi ya masafa marefu na mijini vilifanyiwa mapitio. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa viwango vya nauli vinakuwa shindani na havimuumizi mwananchi. Vilevile, LATRA iko katika hatua za mwisho za kuidhinisha nauli za abiria kwa treni ya kisasa ya SGR ambazo zitatumika pindi treni ya

kisasa itakapoanza kutoa huduma.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha udhibiti wa huduma za usafiri nchini hasa ikizingatiwa kuwa vyombo vinavyotoa huduma katika usafiri kwa njia ya barabara vimeongezeka. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya leseni 240,341 za usafirishaji zilitolewa ikilinganishwa na leseni 210,059 zilitolewa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 14.42. Kati ya leseni hizo, leseni 36,149 zilitolewa kwa magari ya abiria sawa na asilimia 15.04 ya leseni zote na leseni 142,604 zilitolewa kwa magari ya mizigo sawa na asilimia 59.33 ya leseni zote. Pia, leseni 61,588 zilitolewa kwa vyombo vya kukodi sawa na asilimia 25.63 ya leseni zote.

**Udhibiti wa Usafiri Majini**

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) imeendelea kusimamia ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri majini katika eneo la Tanzania Bara; udhibiti wa huduma za bandari na watoa huduma za usafirishaji; kutoa huduma ya biashara ya meli kwa bidhaa mahsusi; na kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za usafiri majini.

**Udhibiti wa Watoa Huduma za Usafirishaji Majini**

46. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu usimamizi wa watoa huduma zinazodhibitiwa, Serikali kupitia TASAC imeendelea kutoa leseni/vyeti vya usajili kwa watoa huduma waliokidhi vigezo vya kutoa huduma zinazodhibitiwa na kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni hizo kwa mujibu wa sheria na kanuni ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya watoa huduma 1,722 zinazodhibitiwa walisajiliwa na kupewa leseni ikilinganishwa na jumla ya watoa huduma 1,498 zinazodhibitiwa waliosajiliwa na kupewa leseni katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 14.95. Aidha, TASAC ilifanya ufuatiliaji kwa watoa huduma hao,

ambapo, uzingatiwaji wa viwango vya utendaji vya watoa huduma hao kulingana na kanuni za utoaji wa huduma hizo ulifikia asilimia 90.50 ikilinganishwa na asilimia 89 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/23. Ufanisi huu ulifikiwa kutokana na juhudi zinazofanyika na Serikali kupitia TASAC zikiwemo za kufanya ufuatiliaji na tathmini mara kwa mara.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TASAC katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024 imeendelea kurasimisha bandari bubu za Tanzania Bara. Katika kutekeleza jukumu hilo, bandari bubu 99 zilikaguliwa na kufanyiwa tathmini ya kina na Serikali kupitia TASAC kwa kushirikisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tazania (TPA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ambapo bandari 45 zilirasimishwa. Urasimishaji huo ulifanyika kupitia Tangazo la Serikali (GN) 855/2023 na 60/2024 na lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa Serikali inaimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ya bandari ili kuboresha utoaji wa huduma.

**Usimamizi wa utoaji wa Mafunzo ya Bahari**

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia utekelezaji wa miongozo ya kimataifa, Serikali kupitia TASAC imeendelea kutekeleza majukumu kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa utoaji wa Vyeti vya Mabaharia kwa Utaratibu wa Kimataifa (International Convention on Standards of Training, Certification and Watch-keeping (STCW) for Seafarers of 1978 as amended). Hadi kufikia Machi 2024, TASAC ilitoa jumla ya vyeti 10,571. Kati ya vyeti hivyo, vyeti vya umahiri (Certificates of Proficiency - COP) vilikuwa 9,818, kitabu cha kumbukumbu za kazi kwa baharia (Continuous Discharge Certificates – CDC) vilikuwa 619 na vyeti vya umahiri kwa maofisa wa meli (Certificates of Competency - COC) vilikuwa 134.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, Serikali kupitia TASAC, inaendelea na hatua za mwisho za kukamilisha mfumo wa utoaji wa vyeti vya kielektroniki kwa mabaharia (Maritime Administration

Management System – Seafarers' module). Mfumo huo utasaidia kutoa vyeti vinavyoendana na matakwa ya sasa ya Shirika la Bahari Duniani (IMO) na Shirika la Kazi Duniani (ILO), kupunguza muda wa utoaji wa vyeti na kuondoa uwezekano wa kughushi vyeti na hatimaye kufanya mabaharia wetu waweze kutambulika na kukubalika kimataifa, hususan katika masuala ya ajira.

**Usalama wa Vyombo vya Usafiri Majini**

50. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu shughuli za utafutaji na uokoaji, Serikali kupitia TASAC imeendelea kuratibu shughuli hizo kupitia Vituo vya Utafutaji na Uokoaji Majini vilivyopo Dar es Salaam na Mwanza (Maritime Rescue and Coordination Centre – MRCC). Kutokana na udhibiti ambao umekuwa ukifanyika, matukio ya ajali katika usafiri majini yamekuwa yakipungua. Mathalan, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, jumla ya watu 40 walipata ajali, ambapo kati yao watu 39 walikolewa na mtu mmoja (1) alipoteza maisha. Aidha, hakukutokea ajali yoyote iliyohusisha vyombo vya majini vyenye ujazo wa tani 50 na zaidi. Ili kudhibiti na kupunguza ajali zitokanazo na usafiri majini, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati kwa lengo la kupunguza ajali za vyombo vidogo vya usafiri majini ikiwemo kuendelea kutoa elimu kuhusu usalama wa usafiri majini na taarifa za hali ya hewa kwa wadau wa usafiri majini kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

51. ***Mheshimiwa Spika****,* vilevile, TASAC imeendelea kufanya kaguzi za usalama kwa meli kubwa zenye ujazo wa tani 50 na kuendelea za ndani na za kimataifa zinazofanya shughuli katika maeneo ya Tanzania (Port and Flag State Inspection) na vyombo vidogo vyenye ujazo wa chini ya tani 50 ili kuhakikisha kuwa ni salama na zinaendeshwa na mabaharia wenye sifa katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Mwanza, Kigoma, Kagera, Mara, Mbeya, Pwani, Lindi, Rukwa, Geita, Dodoma na Morogoro. Kutokana na kaguzi hizo, vyeti vya ubora vilitolewa kwa vyombo vilivyothibitika kukidhi vigezo vya kiusalama na vyombo vilivyobainika kuwa na

kasoro, hatua stahiki zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na kusimamisha vyombo husika kutoa huduma. Hadi kufikia Machi, 2024, TASAC ilifanya kaguzi 227 za meli kubwa zenye ujazo wa tani 50 na kuendelea na kaguzi 8,410 za vyombo vidogo vyenye ujazo wa chini ya tani 50 ikilinganishwa na kaguzi 171 za meli kubwa zenye ujazo wa tani 50 na kuendelea na kaguzi 5,634 za vyombo vidogo vyenye ujazo wa chini ya tani 50 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23. Kutokana na kaguzi hizo vyombo vidogo 8,081 vilikidhi matakwa ya kiusalama na hivyo kupewa vyeti vya ubora ikiwa ni sawa na asilimia 96.08 ya vyombo vyote vidogo vilivyokaguliwa. Aidha, vyombo vidogo 329 havikukidhi vigezo kutokana na kukosekana kwa vifaa vya zimamoto, vifaa vya kuongoza vyombo na mawasiliano.

52. ***Mheshimiwa Spika****,* Serikali kupitia TASAC ilifanya kaguzi za ulinzi kwenye maeneo nane (8) ya bandari kwa kuzingatia miongozo ya kimataifa ya ulinzi wa usafiri majini (International Ship and Port Facility Security – ISPS Code). Maeneo hayo ni katika Bandari ya Dar es Salaam eneo la mizigo ya kichele (General Cargo), Gati la Mafuta la Kurasini (Kurasini Oil Jetty – KOJ), Gati la Mafuta Nje ya Bandari ya Dar es Salaam (Single Bouy Mooring – SBM), Kitengo cha Makasha, Bandari ya Kilwa, Bandari ya Tanga, Bandari ya Mtwara na Bandari ya Malindi. Maeneo haya ya bandari yalikidhi viwango na vigezo vya ISPS Code.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha usalama wa usafiri katika Ziwa Victoria, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda chini ya uratibu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria zimeendelea kutekeleza Mradi wa Kikanda wa Kuboresha Mawasiliano na Uchukuzi Katika Ziwa Victoria wenye lengo la kuimarisha huduma za utafutaji na uokoaji pindi inapotokea ajali katika Ziwa hilo. Hadi kufikia Machi, 2024 ujenzi wa Kituo Kikuu cha Kikanda cha Uratibu wa Masuala ya Utafutaji na Uokoaji katika Ziwa Victoria (Regional Maritime Rescue Coordination Centre - RMRCC) kinachojengwa Ilemela Jijini Mwanza umefikia asilimia 26. Aidha, ujenzi wa vituo vidogo vitatu (3) vya utafutaji na uokoaji

(Search and Rescue - SARs) katika Ziwa Victoria kwenye eneo la Kanyala - Sengerema umefikia asilimia 20, Nansio - Ukerewe umefikia asilimia 20, na Musoma Mjini umefikia asilimia 25.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza miongozo yake ikiwemo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 ambayo katika Ibara 59(c) pamoja na mambo mengine, imeelekeza Serikali kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kujenga boti kwa ajili ya kuwezesha shughuli za utafutaji na uokoaji. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali kupitia TASAC imesaini mkataba na Kampuni ya *LOCA Muhendislik Gemi Makine Plastik ve GIDA SAN TIC LTD STI* kwa ajili ya ujenzi wa Boti Maalum (Ambulance Boat). Boti hiyo ya kisasa ambayo itajengwa katika Ziwa Victoria tofauti na boti nyingine, ina sifa za ziada zikiwemo za kuwa na vifaa vya kisasa vya uokoaji na kutolea huduma za dharura za afya; na vifaa vya matibabu ndani yake. Sambamba na hilo, hatua za kupata mzabuni kwa ajili ya ununuzi wa boti nyingine mbili (2) za utafutaji na uokoaji katika Ziwa Victoria zinaendelea.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mawasiliano katika Ziwa Victoria, TASAC imeandaa hati ya makubaliano baina yake na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) pamoja na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa ajili ya ujenzi wa minara mitatu (3) ya mawasiliano ya simu. Minara hiyo inatarajiwa kuongeza upatikanaji wa mawasiliano ya simu na vyombo vya usafiri majini katika Ziwa Victoria. Aidha, ufungaji wa mfumo wa upatikanaji wa taarifa za hali ya hewa katika Ziwa Victoria (weather buoy forecast system) unaendelea ambapo vifaa vya mfumo huo vimewasili nchini na kazi za mradi zinaendelea kutekelezwa. Kazi hii inafanyika kwa kushirikiana na TMA ambayo ni Taasisi inayosimamia mfumo huo.

**Uwakala wa Forodha kwa Shehena za Kipekee**

56. ***Mheshimiwa Spika****,* katika kutekeleza jukumu la kipekee la ugomboaji wa shehena, TASAC imeendelea kutoa huduma za Uwakala wa Forodha kwa Shehena za Kipekee (exclusive

mandate) kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415 na marekebisho yaliyofanyika kupitia Sheria ya Fedha Na. 5 ya mwaka 2022 iliyoanza kutumika tarehe 1 Julai, 2022. Shehena zinazohudumiwa na TASAC ni silaha na vilipuzi; makinikia; kemikali zitumikazo kwenye kampuni za uchimbaji madini; nyara za Serikali; na wanyama hai kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Uhifadhi wa Wanyama Pori, Sura 283.

57. ***Mheshimiwa Spika***, kazi nyingine zilizotekelezwa na Serikali kupitia TASAC ni pamoja na: -

i. Kuimarisha na kujenga mifumo ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na mfumo wa utoaji wa vyeti vya kielektroniki kwa mabaharia (Maritime Administration Management System - MAMS) mifumo ya ukusanyaji wa mapato na mifumo ya matumizi ambapo Mfumo wa Mapato (TASAC Revenue Gateway) na Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE) ilianza kutumika;

ii. Kuwajengea uwezo watumishi kwa kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na udhibiti, huduma za meli kibiashara na huduma saidizi ili kuongeza weledi na kuboresha utendaji kazi kunakoendana na mabadiliko ya teknolojia. Hadi kufikia Machi, 2024 watumishi zaidi ya 70 walihudhuria mafunzo ya kujengewa uwezo;

iii. Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma zinazodhibitiwa ambapo jumla ya vipindi 60 vya elimu vilitolewa kwa umma kupitia redio, televisheni, magazeti, vipeperushi, maonesho, mikutano ya wadau na mitandao ya kijamii; na

iv. Kutoa elimu kwa Watumishi 248 kuhusiana na masuala mtambuka ikiwemo suala la UKIMWI, magonjwa yasiyoambukiza na rushwa.

58. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kuchukua nafasi hii kutoa pole kwa

Wananchi na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na pia kwa familia zilizopoteza wapendwa wao kufuatia kuzama kwa meli ya MV. Maman Benita katika eneo la Kabimba nchini DRC siku ya tarehe 6 Aprili, 2024. Kwa taarifa tulizopokea ni kuwa, meli hiyo imesajiliwa chini ya bendera ya DRC na inamilikiwa na kampuni ya Kikongo, iitwayo Établissement Manimani na imekuwa ikifanya safari zake kati ya bandari ya Kigoma kwa upande wa Tanzania na bandari ya Kalemie kwa upande wa DRC. Kwa kuwa meli ni ya DRC na pia imezama kwenye maji ya eneo la DRC, Serikali kupitia TASAC itashirikiana na DRC mara uchunguzi utakapoanza ili kujua chanzo cha ajali hiyo. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Serikali za nchi jirani itaendelea kushirikiana zaidi katika kusimamia masuala ya usalama wa vyombo vya majini ili kuepusha kutokea kwa ajali zitokanazo na vyombo hivyo.

**Huduma za Hali ya Hewa**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea na utoaji wa huduma, kudhibiti na kuratibu shughuli za hali ya hewa nchini. Majukumu mengine ni pamoja na kutoa utabiri wa hali ya hewa na tahadhari za hali mbaya ya hewa, kupima na kufuatilia mifumo ya hali ya hewa na kutafiti kisayansi mabadiliko ya hali ya hewa nchini, kubadilishana taarifa za hali ya hewa katika mtandao wa mawasiliano wa dunia kulingana na makubaliano ya Kimataifa na kuiwakilisha Tanzania katika masuala ya hali ya hewa Kikanda na Kimataifa.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TMA imeendelea kutoa huduma za utabiri wa kila siku, siku kumi na ule wa muda mrefu pamoja na tahadhari ya matukio ya hali mbaya ya hewa ili kuhakikisha usalama wa watu na mali zao ambapo usahihi wa utabiri umefikia asilimia 86 ambao ni juu ya asilimia 70 ya kiwango cha usahihi kinachokubalika na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO). TMA ilifanyiwa ukaguzi wa kimataifa kuanzia tarehe 22 - 27 Januari 2024, na kuendelea kukidhi vigezo vya kumiliki cheti cha ubora (ISO 9001: 2015).

61. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 Ibara ya 59(j) na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III 2021/22-2025/26), Serikali iliahidi kuendelea kuimarisha miundombinu na huduma za hali ya hewa ikiwemo ununuzi wa rada. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia TMA imekamilisha ufungaji wa rada za hali ya hewa katika mikoa ya Kigoma na Mbeya na kufikisha jumla ya rada tano (5) za hali ya hewa nchini. Aidha, utengenezaji wa rada nyingine mbili (2) unaendelea kiwandani nchini Marekani na inatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2024. Rada hizo zitafungwa katika mikoa ya Kilimanjaro na Dodoma na hivyo kukamilisha lengo la muda mrefu la kuwa na rada saba (7) za hali ya hewa nchini. Sambamba na hilo, Serikali imeingia mkataba wa kuboresha rada za hali ya hewa zilizofungwa katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza ili kuendana na teknolojia ya kisasa ya rada za hali ya hewa.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma za hali ya hewa kwa sekta ya usafiri wa anga, Serikali ilikamilisha ufungaji wa mitambo mitano (5) ya kutoa huduma za hali ya hewa katika viwanja vya ndege vya Songwe, Zanzibar, Mtwara, Arusha na Songea. Taratibu za ufungaji wa mitambo mitatu (3) ya kupima hali ya hewa katika viwanja vya ndege vya Musoma, Iringa na Mpanda zinaendelea.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Serikali imekamilisha ununuzi wa seti 28 za mitambo ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe (Automatic Weather Stations) ambapo mitambo mitatu (3) imefungwa katika vituo vya hali ya hewa vilivyopo katika viwanja vya ndege vya Mtwara, Songea na Arusha na mitambo 25 inaendelea na maandalizi ya kufungwa katika mikoa ya Morogoro, Iringa, Njombe, Tanga, Dodoma, Singida, Kilimanjaro, Katavi, Shinyanga, Kagera, Geita, Simiyu, Kaskazini Unguja, Mara na Mwanza.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na kujenga uwezo kwa watumishi, Serikali kupitia TMA imeendelea na

ujenzi wa jengo la ofisi ya Kanda ya Mashariki na Kituo cha Tahadhari ya Matukio ya Tsunami ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 39. Vilevile, watumishi 74 wanaendelea na mafunzo ndani na nje ya nchi katika ngazi mbalimbali za elimu.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** TMA imeendelea kufanya tafiti mbalimbali za masuala ya hali ya hewa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi ambapo jumla ya tafiti nne (4) zilichapishwa katika majarida ya kimataifa ya kisayansi. Idadi hii inafanya tafiti zilizochapishwa na majarida ya kimataifa kuwa nane (8) ndani ya kipindi cha miaka miwili (2) kuanzia mwaka 2022/23 hadi 2023/24. Tafiti hizo ni kuhusu tathmini ya matukio ya hali mbaya ya hewa katika Bahari ya Hindi; tathmini ya ongezeko la joto kwa kipindi kati ya mwaka 1982 hadi 2022; tathmini ya hali ya mvua katika vituo vya hali ya hewa nchini; na tathmini ya mabadiliko ya mvua na athari zake katika kilimo kwa nchi za Afrika Mashariki. Lengo kuu la tafiti hizo ni kuboresha utoaji wa huduma za hali ya hewa nchini.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TMA imeendelea kutoa huduma za hali ya hewa kwa watumiaji wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu kupitia ofisi zake tisa (9) zilizopo katika bandari za Malindi - Unguja, Mkoani - Pemba, Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Ziwa Victoria katika Bandari ya Mwanza, Ziwa Tanganyika katika Bandari za Kigoma na Karema na Ziwa Nyasa katika Bandari ya Itungi na hivyo kuendelea kuchagiza shughuli za Uchumi wa Buluu. Aidha, wadau wa Uchumi wa Buluu ambao wameendelea kupatiwa huduma za hali ya hewa ni pamoja na watumiaji wa vyombo vya usafiri na usafirishaji, Watafiti na wachimbaji wa Mafuta na gesi, Mamlaka za bandari, Wavuvi, Wakulima wa mwani na matango bahari, wafugaji samaki na Vikundi vya usimamizi wa maeneo ya bahari na fukwe.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umahiri katika utoaji wa huduma za hali ya hewa, mwaka 2019 Shirika la Hali ya Hewa Duniani liliichagua Tanzania kupitia TMA kuendesha kituo cha kanda cha kutoa mwongozo wa utabiri wa hali mbaya ya hewa (Regional Specialized Meteorological Centre) kwa nchi zilizopo katika

ukanda wa Ziwa Victoria. Kituo hicho kipo Dar es Salaam na kinahudumia nchi tano (5) ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, na Burundi. Sambamba na hilo, TMA iliteuliwa kutekeleza jukumu la kufuatilia ubora wa takwimu za hali ya hewa (data) zinazopimwa katika vituo vya hali ya hewa vya nchi sita (6) vya ukanda wa Afrika Mashariki ikujumuisha nchi ya Sudan Kusini. Majukumu haya ambayo TMA imeendelea kuyatekeleza kwa ufanisi na kuzidi kuitangaza nchi yetu kimataifa.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa, Tanzania kupitia TMA ilifanya vizuri na kuchaguliwa katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa linalosimamia sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa (Intergovernmental Panel on Climate Change-IPCC). Hii ni fursa kwa Tanzania kuweza kushiriki katika Maamuzi ya Kimataifa kuhusu hali ya hewa pamoja na kupata usaidizi wa vifaa na utaalam.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa umma wa Watanzania unapata taarifa sahihi za hali ya hewa, TMA imeongeza wigo wa kuhabarisha umma kwa kusaini mikataba ya utangazaji wa taarifa za hali ya hewa na Redio tano (5) za jamii ambazo ni Jambo FM (Shinyanga), Harvest FM (Pwani), Inland FM (Mwanza), Revival FM (Manyara) na CGFM (Tabora) na kuwa na jumla ya vyombo vya habari 108 vinavyohusisha redio 80, Televisheni 17, magazeti matatu (3) na Televisheni Mtandao (Online TV nane (8).

**Huduma za Bandari**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imeendelea kusimamia Bandari za Mwambao wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu kwa kuendeleza miundombinu na utoaji wa huduma za kibandari; kuweka taratibu na viwango kwa watoa huduma za bandari nchini; kusimamia na kudhibiti huduma za bandari, kulinda mazingira na usalama wa bandari kwa viwango vinavyokubalika; na kuweka mazingira mazuri yatakayovutia uwekezaji katika sekta ya bandari. Aidha, TPA imeendelea kutangaza bandari kimasoko kwa kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa shughuli za kibandari.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 TPA ilihudumia tani milioni 20.72 ya shehena ikilinganishwa na tani milioni 14.56 ya shehena ya mizigo iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 42.31. Aidha, kwa upande wa uhudumiaji wa makasha, TPA ilihudumia makasha 805,167 ikilinganishwa na makasha 688,609 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 16.92. Ongezeko hilo la shehena ya mizigo na makasha limetokana na mikakati mbalimbali inayoendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPA inaendelea kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 ambayo katika Ibara ya 59b(i-vi) imesisitiza kuendelea na uboreshaji na uimarishaji wa miundombinu na utoaji wa huduma za bandari nchini. Katika kufanyia kazi maelekezo hayo, TPA imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa bandari nchini katika bandari za ukanda wa mwambao wa Bahari ya Hindi, Maziwa Makuu na Bandari Kavu. Aidha, TPA imeendelea na juhudi mbalimbali za kuboresha huduma zake ikiwa ni pamoja na kufungua ofisi nje ya nchi; kutafuta masoko; na kufanya ununuzi wa vifaa na mitambo kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma katika bandari nchini.

73. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, TPA imeendelea kutekeleza kazi mbalimbali ambapo uchimbaji wa kina umefikia mita 15.5 na upanuzi wa lango la kuingia na kugeuzia meli umefikia upana wa mita 200. Kwa sasa, Bandari ina uwezo wa kupokea meli kubwa zenye urefu wa mita 305. Aidha, upembuzi yakinifu wa kuboresha Gati Na. 8 – 11 na ujenzi wa Gati Na. 12 - 15 bado unaendelea kwa ajili ya kuhudumia meli na shehena. Vilevile, mkataba wa kuendeleza miundombinu ya kupokelea mafuta (Single Receiving Terminal - SRT) unaohusisha ujenzi wa matenki 15 ya mafuta (tank farms) pamoja na miundombinu yake, yenye uwezo wa kuhifadhi kiasi cha mita za ujazo 420,000

umesainiwa tarehe 26 Februari, 2024 na maandalizi ya kuanza ujenzi yanaendelea.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** uboreshaji wa Bandari ya Tanga katika awamu ya pili umekamilika kwa asilimia 100, ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na: kuboresha magati 2 yenye jumla ya urefu wa mita 450; uboreshaji wa eneo la kuhifadhia Makasha lenye ukubwa wa mita za mraba 6,400 na uwezo wa kuhudumia makasha 1,020 TEUs; na ununuzi wa jumla ya mitambo 16 ambayo ni *Forklift (4), Crane (3), Container spreaders (4), Terminal Tractors (2) Front end loader (1), Empty handlers stacking (1)* na *Grabs (1)* kwa ajili ya kuhudumia shehena.

75. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TPA imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Kisiwa Mgao ambayo ni maalum kwa ajili ya kuhudumia shehena ya mzigo mchafu (dirty cargo) kama vile makaa ya mawe na saruji. Kazi ya Upembuzi Yakinifu imekamilika mwezi Februari, 2024 ambapo kwa sasa taratibu za ununuzi wa Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi zinaendelea. Lengo la hatua hii ni kuiwezesha bandari ya Mtwara iendelee kutoa huduma kwa ufanisi katika mizigo mingine tofauti na mizigo michafu.

76. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu Bandari ya Bagamoyo, Serikali imekamilisha zoezi la kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi lenye ukubwa wa hekta 887. Kwa sasa mradi huo upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa kuhuisha Upembuzi Yakinifu. Ujenzi wa Bandari hiyo ni wa kimkakati kwa kuwa itachochea shughuli za viwanda na biashara katika eneo la Ukanda Maalum wa Kiuchumi (Special Economic Zone).

**Huduma za kibandari katika Bandari Kavu ya Kwala**

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Bandari Kavu ya Kwala, utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya zege yenye urefu wa kilometa 15.5 kutoka barabara kuu ya Morogoro hadi Bandari Kavu ya Kwala umekamilika na ujenzi wa yadi ya sakafu ngumu (pavement) yenye ukubwa wa

hekta tano (5) kwa ajili ya kuhifadhi shehena unaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 96. Bandari Kavu hii imeanza kutoa huduma za kibandari kwa kutoa makasha kutoka bandari ya Dar es salaam na kwenda Kwala kwa kutumia njia ya reli.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPA imeendelea kuboresha bandari zilizopo katika Ziwa Victoria ambapo uboreshaji wa Bandari ya Bukoba umefikia asilimia 47 na Bandari ya Kemondo umefikia asilimia 52. Aidha, uboreshaji wa Bandari ya Mwanza North umefikia asilimia 40 na kwa upande wa uboreshaji wa Bandari ya Mwanza South utaanza baada ya kukamilika kwa baadhi ya miundombinu ya Bandari ya Mwanza North ili kutoathiri shughuli za kibandari katika mkoa huo. Maboresho haya yatawezesha kuhudumia meli kubwa kama vile MV. Mwanza Hapa Kazi tu katika Ziwa Victoria.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendelea kuongeza wigo wa huduma zake za kibandari kwa kujenga bandari katika maziwa makuu nchini. Katika kutekeleza nia hiyo, Serikali inaendelea na ujenzi wa Bandari katika Ziwa Tanganyika ambapo mradi wa ujenzi wa Bandari za Kibirizi unaohusisha ujenzi wa gati, uongezaji wa kina, maghala ya mizigo, jengo la abiria na ofisi mbili (2); na bandari ya Ujiji unaohusisha ujenzi wa gati, jengo la abiria, jengo la kuhifadhi mizigo, ujenzi wa uzio na kuongeza kina. Ujenzi wa Bandari hizi umefikia asilimia 98.60.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, mkataba wa uboreshaji wa Bandari ya Mbamba Bay katika Ziwa Nyasa umesainiwa tarehe 11 Januari, 2024 na kuanza utekelezaji mwezi huo. Kazi zinazofanyika kwa sasa ni pamoja na maandalizi ya awali ya mradi (mobilisation) yanayojumuisha ukusanyaji wa vifaa, mitambo pamoja na usanifu wa mradi. Ujenzi wa Bandari hii utaongeza fursa za ajira katika Ushoroba wa Kusini mwa nchi kwa kuunganisha nchi za Malawi na Zambia.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Ofisi za TPA zilizo nje ya nchi imeendelea kufanya jitihada kubwa za kimasoko katika

kujitangaza na kutafuta fursa zaidi za kibiashara kwa nchi jirani zinazotumia Bandari za Tanzania zikiwemo nchi za Rwanda, Burundi, Uganda, Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Zimbabwe ambapo kutokana na jitihada hizo shehena ya mizigo iliyosafirishwa kwenda nchi jirani imeongezeka hadi kufikia tani 8,871,438 kwa mwaka 2023 kutoka tani 8,239,112 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 7.67.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPA imeendelea kuratibu ununuzi wa vifaa na mitambo kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma katika Bandari nchini. Hadi kufikia Machi 2024, TPA imefanikiwa kununua na kupokea vifaa na mitambo 121 sawa na asilimia 53.78 ya lengo la kununua mitambo na vifaa 225. Ununuzi wa mitambo hii umeongeza ufanisi katika kutoa huduma bandarini.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wa TPA ambapo watumishi 2,288 walihudhuria mafunzo kati ya watumishi 2,749 waliopangwa kuhudhuria mafunzo sawa na asilimia 83.23 ya lengo. Kati ya hao, watumishi 1,646 walishiriki mafunzo ya vikundi, watumishi 486 walishiriki mafunzo ya kitaaluma (professional), watumishi 57 walishiriki mafunzo ya muda mfupi kwa mtu mmoja mmoja na watumishi 99 walishiriki mafunzo ya muda mrefu.

**Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika Shughuli za Uendelezaji na Uendeshaji wa Bandari**

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi imeendelea kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwa baadhi ya maeneo ya bandari kwa kuingia ubia na Kampuni Binafsi katika kuendeleza na kuendesha shughuli za bandari kuanzia Gati Na. 4 hadi 7. Kwa sasa hatua mbalimbali zikiwemo za makabidhiano na *mobilization* zinaendelea ili kuruhusu utekelezaji rasmi kuanza. Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za kumpata mwekezaji mwingine atakayekuwa na jukumu la kufanya shughuli za uendeshaji kuanzia Gati Namba 8 hadi 11. Lengo ni kuongeza tija katika utendaji wa bandari zetu ili

kuziwezesha zichangie zaidi katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu na maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

**Huduma za Usafiri wa Reli**

**Shirika la Reli Tanzania (TRC)**

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma ya uchukuzi kwa njia ya reli, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia na kuendeleza miundombinu ya reli iliyopo ya *Meter Gauge Railway* (MGR) yenye urefu wa kilometa 2,706 na kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kutumia reli ya Kati na reli ya Kaskazini. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa Reli ya Kisasa ya *Standard Gauge Railway* (SGR) kwa awamu zote mbili ambapo awamu ya kwanza ina jumla ya kilometa za njia kuu 1,219 na awamu ya pili ina jumla ya kilometa 1,590 na hivyo kufanya reli mpya ya SGR inayojengwa kuwa na mtandao wenye jumla ya kilometa 2,809 ambazo ni zaidi ya kilometa 103 ikilinganishwa na reli ya MGR ambayo ilijengwa wakati wa Mkoloni. Pamoja na hatua hiyo, Serikali itaendelea na ujenzi wa reli ya SGR kwa maeneo mengine ya Ushoroba wa Kusini na wa Kaskazini kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** TRC imeendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo na abiria kupitia njia ya reli iliyopo ya MGR ambapo hadi kufikia Machi 2024, tani 240,439 za mizigo zimesafirishwa ikilinganishwa na tani 310,881 zilizosafirishwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2022/23 sawa na upungufu tani 70,442 za mizigo. Kwa upande wa abiria, hadi kufikia Machi, 2024, abiria wa masafa marefu 320,514 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 380,012 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/23 sawa na upungufu wa abiria 59,498. Upungufu huu umetokana na kufungwa kwa njia ya reli kwa zaidi ya miezi miwili (2) kufuatia mvua kubwa zilizonyesha kuanzia mwezi Novemba, 2023 na kuharibu miundombinu ya reli katika maeneo ya Ruvu - Mruazi Junction; Kilosa - Gulwe; Kaliua – Mpanda; na Njia ya reli ya Tanga - Arusha.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma ya usafiri wa reli Jijini Dar es Salaam imeendelea kutolewa na TRC kutoka Stesheni ya Kamata kwenda Ubungo na Pugu. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya abiria 2,236,423 wamesafirishwa ikilinganishwa na abiria 1,813,835 waliosafirishwa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 23.29. Idadi ya abiria waliosafirishwa imeongezeka kutokana na mikakati ya Serikali ya kuboresha huduma kwa wananchi kwa kuongeza idadi ya safari (routes) kutoka sita (6) hadi nane (8) kwa siku kulingana na mahitaji yaliyopo.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 Ibara ya 58(e)(ii) na Ibara ya 59(d), Serikali iliahidi kuendelea na ujenzi wa reli ya SGR kwa awamu zote mbili. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa reli ya SGR katika awamu ya kwanza. Hadi kufikia Machi 2024, ujenzi wa reli ya SGR katika awamu ya kwanza ya kutoka Dar es Salaam – Mwanza yenye urefu kilometa 1,219 za njia kuu umeendelea kutekelezwa katika vipande vyote vitano (5).

89. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa kipande cha kwanza cha kutoka Dar es Salaam – Morogoro (km 300) utekelezaji wake umefikia asilimia 98.93 na kazi zinazoendelea ni pamoja na: ujenzi wa njia kuelekea bandarini (port link) (asilimia 76.12); ujenzi wa uzio (asilimia 99.01); ujenzi wa vivuko vya juu vitatu (3) vya Vingunguti, Airport na Njia Panda ya Segerea (asilimia 99.36); ujenzi wa mifumo ya ishara, mawasiliano na umeme (asilimia 99.92); na majaribio ya uendeshaji katika kipande hiki yanaendelea.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa kipande cha pili cha kutoka Morogoro – Makutupora (km 422) umefikia asilimia 96.61 na kazi zinazoendelea ziko katika hatua mbalimbali ambazo ni pamoja na ujenzi wa vivuko vya juu (asilimia 98.52); ujenzi wa stesheni (asilimia 98.27); ujenzi wa uzio (asilimia 86.02); na majaribio ya miundombinu ya njia na mifumo ya uendeshaji yanaendelea.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa kipande cha tatu cha kutoka Makutupora – Tabora (km 368) umefikia asilimia 14.22 na kazi zinazoendelea ni pamoja na: usanifu wa kina ambao umefikia asilimia 54.98; ujenzi wa kambi; ukataji wa miinuko na ujazaji mabonde; na utwaaji wa ardhi. Aidha, utekelezaji wa kipande cha nne cha kutoka Tabora – Isaka (km 165) umefikia asilimia 5.74 ambapo kazi zinazoendelea ni pamoja na usanifu wa kina; utafiti wa udongo na miamba; ujenzi wa kambi; machimbo ya kokoto; na utwaaji wa ardhi.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa kipande cha tano cha kutoka Mwanza – Isaka (km 341) umefikia asilimia 56.21 na kazi zinazoendelea ni usanifu wa kina; ujenzi wa tuta; majengo ya stesheni; madaraja na vivuko vya binadamu na wanyama; utandikaji wa reli; ujenzi wa mifumo ya mawasiliano; na umeme pamoja na utwaaji wa ardhi.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza azma ya Serikali ya kuifungua nchi kikanda na kimataifa, Wizara imeazimia kutekeleza miradi ya kimkakati kwa lengo la kuifanya Tanzania iweze kuendelea kuhudumia zaidi masoko ya mizigo kwa nchi jirani. Katika kuendeleza hatua hiyo, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya SGR kwa awamu ya pili ambapo ujenzi wa reli ya SGR kutoka Tabora – Kigoma (Km 506) umeanza na utekelezaji wake umefikia asilimia 1.81. Kazi zinazoendelea ni pamoja na utwaaji wa ardhi; ujenzi wa kambi; usanifu pamoja na usafirishaji wa mitambo na vitendea kazi.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka uliopita nililiarifu Bunge lako kuwa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Burundi zilikubaliana kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha kutoka Uvinza – Musongati – Gitega (km 282). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeridhia kutoa mkopo wenye masharti nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa reli hiyo. Mafanikio haya ni matokeo ya juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa

Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha mahusiano ya kimataifa na diplomasia ya kiuchumi. Utekelezaji wa kipande hiki umeanza; ambapo hatua za ununuzi wa Mshauri Elekezi na Mkandarasi zinaendelea. Kukamilika kwa reli hii kutafungua nchi ya Tanzania kikanda kwa kuwezesha na kurahisisha ufanyaji biashara kati ya nchi hizo.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwa ni pamoja na wawekezaji kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na binafsi (PPP) kwa ajili ya ujenzi wa reli ya SGR kwa maeneo yaliyobaki yanayojumuisha reli ya SGR ya kutoka Kaliua – Mpanda – Karema (km 321); Isaka – Rusumo – Rwanda (km 371); Mtwara – Mbambabay na matawi ya Liganga na Mchuchuma (km 1,000); Tanga – Arusha – Musoma (km 1,028); Reli ya Jiji la Dar es Salaam (km 166); na Reli ya Jiji la Dodoma (km 107).

96. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuchagiza ukuaji wa uchumi wa nchi kupitia usafirishaji kwa njia ya reli sambamba na utekelezaji wa maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati akihutubia Taifa mwezi Disemba, 2023 ya kuanza uendeshaji wa treni katika reli ya SGR kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kupitia TRC inaendelea na majaribio ya miundombinu ya reli; mifumo ya ishara, mawasiliano na umeme; na vitendea kazi kwa ajili ya kuanza utoaji wa huduma hiyo ifikapo mwezi Julai, 2024. Aidha, majaribio haya yanafanyika kwa lengo la kukidhi takwa la usalama kabla ya kuanza uendeshaji.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** reli hiyo itakuwa na uwezo wa kupitisha treni za abiria kwa mwendo kasi wa kilometa 160 kwa saa na za mizigo kwa mwendokasi wa kilometa 120 kwa saa. Ni wazi kuwa utekelezaji wa mradi huu umetumia fedha nyingi za maendeleo ikiwemo mikopo ambayo itahitaji marejesho. Uzoefu unaonesha kuwa kwa kiwango kikubwa biashara ya reli inategemea uwepo wa mizigo ya kutosha ili kuwa na fedha za uendeshaji. Kwa

mantiki hiyo, Serikali imeanza kufanya maandalizi ili kufanya usafirishaji katika reli hiyo kuwa wa kibiashara pamoja na kuzingatia utoaji wa huduma kwa jamii.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na maandalizi mengine, Wizara imeendelea kuchukua mikakati mbalimbali ya kuifanya reli ya SGR kujiendesha kibiashara ikiwa ni pamoja na: kufanya utafiti wa viwango vya nauli na tozo za mizigo na viwango vya gharama zitakazotumika katika utaratibu wa kushirikisha Sekta Binafsi (Open Access); na kushawishi wadau wa ndani na nje kupitia mikutano mbalimbali ili washiriki katika kutoa huduma ya kusafirisha kupitia miundombinu ya reli.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** mikakati mengine inayoendelea kutekelezwa na Serikali ni pamoja na:-

i. Kufungamanisha mtandao wa reli na bandari zilizopo katika Bahari ya Hindi, Maziwa Makuu na Bandari Kavu ambapo ujenzi wa reli kuelekea Bandari ya Dar es Salaam umefikia asilimia 76.12;

ii. Kuhamasisha shughuli za uchumi na uzalishaji zitakazofungamanishwa katika mfumo wa usafirishaji ikiwa ni pamoja na ushoroba wa kijani unaozalisha matunda na mbogamboga na ushoroba wa njano unaozalisha madini;

iii. Kuingia makubaliano na wafanyabiashara wakubwa wanaosafirisha mizigo kwenda nchi jirani;

iv. Kuhakikisha kuwa mifumo ya reli ya kati inaendeshwa kibiashara kwa kufungamanisha na reli ya TAZARA; na

v. Kuchochea ushiriki wa sekta binafsi katika mnyororo wa usafirishaji, uzalishaji na masoko.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika kutambua na kuimarisha matumizi ya reli

iliyopo kwa sasa ya MGR, kwa kuwa reli hii ipo katika maeneo ya kimkakati ikiunganisha bandari za bahari za Dar es Salaam na ile ya Tanga pamoja na Bandari Kavu za Kwala na Isaka. Katika maungio ya Tabora reli hii inaunganisha nchi zinazozunguka Ziwa Tanganyika na kwa upande wa kanda ya ziwa, reli hii inaingia nchini Uganda kupitia meli maalum za kubeba mabehewa ikiwemo MV. Umoja kupitia Ziwa Victoria.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na mikakati hiyo, Serikali imeanza kubuni namna bora ya kufungamanisha reli iliyopo ya MGR, reli ya TAZARA pamoja na reli ya SGR ili kuwezesha kutumia fursa ya utajiri mkubwa wa mtandao wa reli unaounganisha sehemu kubwa ya nchi. Hatua hii itaimarisha muunganiko wa reli ya kati na reli ya TAZARA kupitia kiungio cha Kidatu. Kwa kuzingatia umuhimu wa reli hii na ukweli kuwa reli inawezesha kuunganisha mzigo kutoka mikoa ya Songwe, Mbeya, Iringa, Morogoro na kuwezesha muingiliano kuelekea maziwa makuu. Hii ni fursa ya soko kwa kuunganisha nchi za EAC, SADC na COMESA na hatimaye reli ya mwendo kasi. Aidha, Serikali imeanza kutathmini upatikanaji wa maeneo ambayo yatatumika wakati wa kufaulisha mizigo (Trans-shipment) kwa ajili ya kuleta urahisi wa kufanya biashara hususan usafirishaji wa mizigo katika reli hizo. Lengo la Serikali ni kuifungua nchi na kurahisisha shughuli za biashara ndani na nje ya nchi.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2023/24 nilieleza kuwa Serikali kupitia TRC itaendelea na taratibu za ununuzi wa vichwa vya treni, mabehewa na mitambo itakayotumika kutoa huduma ya usafiri kwenye reli ya SGR. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia Machi 2024, mabehewa 65 ya abiria kati ya 89 yamewasili nchini na mabehewa 24 ya abiria yaliyosalia yanatarajiwa kuwasili kwa nyakati tofauti kuanzia mwezi Juni, 2024; Utengenezaji wa vichwa vya treni vya umeme 17 umefikia asilimia 83 na tayari vichwa vya treni vya umeme tisa (9) vimepokelewa na kuanza majaribio na vichwa nane (8) vilivyosalia vinatarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwezi Mei, 2024; na utengenezaji wa seti 10 za treni (Electric Multiple

Unit – EMU) kwa ajili ya treni ya abiria umefikia asilimia 70 ambapo seti ya kwanza imewasili nchini tarehe 26 Machi, 2024. Aidha, hatua za utengenezaji wa mabehewa 1,430 ya mizigo zinaendelea baada ya uzalishaji wa mabehewa ya mfano (prototype) kukamilika na kukaguliwa na wataalam kutoka TRC.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa lengo la kuhakikisha ushiriki wa sekta binafsi katika usafirishaji kwa njia ya reli, Serikali kupitia TRC imekamilisha marekebisho ya Sheria ya Reli Na. 10 ya mwaka 2017 (Sura ya 170) kuweka utaratibu kwa watoa huduma binafsi kutumia njia ya reli kutoa huduma ya usafirishaji kwa kutumia vichwa vya treni na mabehewa yao (open access). Aidha, ili kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa mizigo itakayosafirishwa kupitia reli ya MGR na SGR, Serikali imebuni mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuhamasisha upatikanaji wa mizigo na watoa huduma (operators) ambapo miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kufanya Jukwaa la Wadau wa Uwekezaji na Biashara katika Reli lililofanyika tarehe 5 – 6 Machi, 2024 jijini Mwanza na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 300 kwa lengo la kunadi fursa zilizopo za usafirishaji kwa kutumia miundombinu iliyopo ya reli ya MGR na reli ya SGR pindi ujenzi wake utakapokamilika.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na uendelezaji wa ujenzi wa reli ya SGR, reli ya MGR iliyopo imeendelea kusafirisha mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kuelekea nchi jirani. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kukarabati reli ya MGR katika maeneo mbalimbali nchini ili kuwezesha kusafirisha shehena ya mizigo na abiria katika kipindi chote cha mwaka. Sambamba na hilo, Serikali kupitia TRC inaendelea kutekeleza mradi wa ukarabati wa miundombinu ya njia ya reli kutoka Dar es Salaam hadi Isaka awamu ya pili (Tanzania Intermodal Rail Project-TIRP II) unaohusisha ukarabati wa njia ya reli, ujenzi wa madaraja, makalvati, na ujenzi wa vituo vya kuhudumia mizigo vya Ilala na Isaka. Mikataba ya usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa vipande hivyo ilisainiwa tarehe 17 Novemba, 2023 na kuanza

utekelezaji tarehe 15 Desemba, 2023 ambapo kazi inatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi sita (6).

105. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zinazoendelea kutekelezwa na TRC kwenye ukarabati wa miundombinu ya reli iliyopo ya MGR ni pamoja na: -

i. Uboreshaji wa mifumo ya ishara, mawasiliano na umeme katika njia ya reli iliyopo ya Meter Gauge ambapo maboresho ya umeme yamekamilika kwa njia nzima na maboresho ya ishara na mawasiliano yanaendelea katika maeneo ya Tabora-Mwanza;

ii. Ununuzi wa vipuri kwa ajili ya ukarabati wa mabehewa 600 ya mizigo na 37 ya abiria yatakayotumika kutoa huduma katika njia ya reli iliyopo. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya mabehewa 285 ya mizigo na 28 ya abiria yamekarabatiwa na yameanza kutoa huduma;

iii. Uundwaji wa vichwa vya treni 9 (64XX - 7 na 88U-2). Lengo la mradi huu ni kuongeza vitendea kazi kwa kukarabati vichwa viwili (2) vya njia kuu aina ya 88U na vichwa saba (7) vya sogeza aina ya 64XX. Kazi ya uundwaji wa vichwa vya treni inaendelea katika karakana ya reli ya Morogoro na utekelezaji umefikia asilimia 63;

iv. Ukarabati wa njia ya reli ya MGR ya Kaliua-Mpanda (km 210) ambapo kazi inaendelea na imefikia asilimia 11;

v. Ukarabati wa njia ya MGR ya Tabora- Kigoma (km 411). Mkataba wa ukarabati ulisainiwa tarehe 23 Juni, 2023 kati ya TRC na kampuni ya CCECC. Maandalizi ya awali kwa ajili ya ukarabati wa njia yanaendelea;

vi. Kuendelea na ujenzi wa njia ya reli yenye urefu wa kilometa 6.2 na daraja katika eneo la Godegode –Gulwe. Hadi kufikia Machi, 2024 kazi imefikia kwa asilimia 32.87;

vii. Ukarabati wa njia ya reli ya MGR ya Ruvu Junction –Mruazi Junction (km 188). Mkataba wa ununuzi wa vifaa vya matengenezo (reli, mataruma na vifungashio) ulisainiwa na malipo ya awali (Advance payment) yamefanyika na hatua za ufunguzi wa barua ya dhamana (Letter of Credit) zinaendelea; na

viii. Uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA ikiwemo ufungaji wa kamera za CCTV kwa ajili ya ulinzi na usalama katika maeneo ya stesheni na mfumo wa kielektroniki wa ukataji tiketi (e-ticketing).

**Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) inamilikiwa na Serikali mbili za Tanzania na Zambia kwa hisa za asilimia 50 kwa 50. Katika kuendeleza huduma za reli kati ya nchi hizo mbili, TAZARA imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa huduma za kusafirisha abiria na mizigo kwa njia ya reli ya TAZARA kati ya Dar es Salaam, Tanzania na New Kapiri Mposhi, Zambia pamoja na kulinda na kuimarisha miundombinu ya reli yenye urefu wa jumla ya kilometa 2,153, ambapo kilometa 1,860 ni za njia kuu, kilometa 293 ni njia za reli zilizoko stesheni na zile za michepuko, pamoja na maeneo yote yaliyo ndani ya ukanda wa reli (mita 50 pande zote kutoka katikati ya reli).

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024, Mamlaka ya reli ya TAZARA ilisafirisha jumla ya tani za mizigo 251,264 ikilinganishwa na tani 235,071 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 6.89. Ongezeko hilo limechangiwa na ushirikishaji wa sekta binafsi kwenye usafirishaji wa mizigo sambamba na kukamilika kwa ukarabati wa Daraja la Mto Chambeshi ambalo lilifungwa kwa mwaka mmoja kuanzia Septemba 2021 hadi Oktoba 2022. Aidha, katika tani hizo zilizosafirishwa Kampuni binafsi mbili (2) za Ms Calabash Freight Limited kutoka Zambia na Ms African Inland

Container Depot (AFICD) kutoka Tanzania zilisafirisha jumla ya mizigo ya tani 136,082 ikilinganishwa na mizigo ya tani 82,576 iliyosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 64.80. Utaratibu huu umeiingizia TAZARA mapato ya Shilingi bilioni 8.91 kutokana na Kampuni hizo kulipia tozo (Access Fee).

108. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kutekeleza Mpango wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 59(f), ambao unaelekeza Serikali kuboresha huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Reli ya TAZARA, Mwezi Machi 2024 TAZARA iliingia mkataba na Kampuni binafsi ya Bravo Group Ltd kwa ajili ya kusafirisha mizigo kwa kutumia njia ya reli ya TAZARA na kulipia tozo ya njia (Access Fee). Hatua hii inafanya idadi ya Kampuni binafsi zilizoingia mikataba na TAZARA kufikia Kampuni tatu (3).

109. ***Mheshimiwa Spika***, treni za abiria zinazofanya safari kati ya Dar es Salaam - Tanzania na New Kapiri Mposhi – Zambia na ile ya Udzungwa inayosafiri kati ya stesheni za Kidatu na Makambako, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi, 2024 zilisafirisha jumla ya abiria 672,006 ikilinganishwa na abiria 712,428 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na upungufu wa abiria 40,422. Upungufu huu unatokana na uhaba wa mabehewa na mvua kubwa zilizonyesha katika kipindi cha mwezi Disemba, 2023 hadi Machi, 2024 zilizosababisha kuharibika kwa miundombinu ya reli na hivyo kutopitika kwa njia husika.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, Treni ya Jijini Dar es Salaam inayofanya safari zake kati ya Stesheni ya TAZARA hadi Stesheni ya Mwakanga - Pugu jijini Dar es Salaam ilisafirisha abiria 1,582,833 ikilinganishwa na abiria 1,447,738 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 9.33. Pia, treni ya Udzungwa inayofanya safari zake kuanzia Kidatu, Morogoro hadi Makambako, Njombe ilisafirisha abiria 225,657 ikilinganishwa na abiria 274,880 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na upungufu wa abiria 49,223. Upungufu huu wa abiria waliosafirishwa unatokana na mvua kubwa

zilizonyesha na kusababisha kuharibika kwa miundombinu ya reli na hivyo kutopitika kwa njia husika.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuimarisha reli ya TAZARA ili iendelee kutoa huduma kwa ufanisi, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya reli hiyo na kufanya ununuzi wa vifaa. Hadi kufikia Machi 2024, ukarabati wa maeneo korofi umefanyika na malipo ya awali ya Shilingi bilioni 4.1 yamefanyika kwa ajili ya ununuzi wa *Tamping Machine* moja (1) ambayo ni maalum kwa kushindilia kokoto na kunyoosha reli.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa muda mrefu reli ya TAZARA imekuwa na changamoto mbalimbali za kiutendaji ambazo zinafifisha juhudi za kuifanya reli hiyo itoe mchango uliokusudiwa katika usafirishaji. Serikali zote mbili za Tanzania na Zambia ziko kwenye mazungumzo na Serikali ya China kupitia kampuni binafsi kutoka nchi hiyo, ili kuangalia namna bora ya kuboresha na kuondoa mapungufu yanayoikabili kutoa huduma kwa ufanisi. Lengo la Serikali hizo mbili ni kuingia makubaliano katika uendeshaji wa TAZARA kwa utaratibu maalum wa ukodishaji (Concession). Mazungumzo hayo yatakamilika kabla ya mwishoni mwa mwezi Mei, 2024.

**Huduma za Usafirishaji Baharini**

113. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa huduma za uchukuzi katika Bahari, Kampuni ya Meli ya China na Tanzania (SINOTASHIP) imeendelea kutoa huduma za uchukuzi wa masafa marefu baharini kwa kutumia meli yake moja yenye uwezo wa kubeba jumla ya tani 57,000 kwa wakati mmoja. Kampuni hii inamilikiwa kwa uwiano wa asilimia 50:50 kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Januari, 2023 hadi Disemba 2023, SINOTASHIP ilisafirisha jumla ya tani 619,870 za shehena ya mizigo ikilinganishwa na jumla ya tani 610,774 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2022 sawa na ongezeko

la asilimia 1.49. Pia, kampuni iliendelea kutoa huduma ya uwakala wa meli ambapo jumla ya makasha 73,500 yalihudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na makasha 63,529 yaliyohudumiwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 15.69. Ongezeko hilo linatokana na kuimarishwa kwa mikakati ya kutafuta mizigo inayosafirishwa nje ya nchi kwa bei shindani.

**Huduma za Uchukuzi katika Maziwa Makuu**

115. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imeendelea kutoa huduma za usafiri na usafirishaji katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa ndani na nje ya nchi zikiwemo nchi jirani za Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo - DRC, Zambia, Malawi na Msumbiji. Kampuni hii inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 MSCL ilisafirisha abiria 198,080 ikilinganishwa na abiria 170,137 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 16.42. Kwa upande wa mizigo, MSCL ilisafirisha tani 33,288.44 ikilinganishwa na tani 18,909 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 76.05. Ongezeko hili limetokana na kukamilika kwa ukarabati na kuanza kazi kwa meli ya MV. Umoja ambayo ilianza kutoa huduma mwezi Oktoba, 2023. Aidha, MSCL iliendelea kuimarisha uwezo wa kiutendaji ambapo watumishi wapya 83 waliajiriwa.

117. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha utoaji wa huduma za usafiri katika maziwa makuu, Serikali kupitia Mpango wa Taifa wa Maendeleo (FYDP III) ukurasa wa 203 kipengele cha 20 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 katika Ibara ya 59(c) iliahidi kuboresha huduma za usafiri katika maziwa makuu kwa kujenga na kukarabati meli. Napenda nitumie fursa hii kulitaarifu bunge lako tukufu kuwa, Serikali kupitia MSCL imeendelea kukamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa meli mpya na kukarabati meli

zilizopo katika Ziwa Victoria na Tanganyika ili kuimarisha usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo.

118. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi, 2024, Serikali kupitia MSCL imekamilisha ukarabati wa Meli ya MV. Umoja ambayo ilizinduliwa tarehe 17 Novemba, 2023, meli hii kwa sasa hufanya biashara ya kusafirisha mizigo katika Ziwa Victoria kati ya Bandari ya Mwanza Kusini na Bandari za Port bell na Jinja za nchini Uganda. Meli hii ina uwezo wa kubeba tani 1,200 au mabehewa 22 ya reli ya *MGR* sawa na treni nzima kuingia ndani ya meli tofauti na mabehewa 19 kabla ya ukarabati. Aidha, ujenzi wa Meli ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu umekamilika kwa asilimia 95 na tayari meli hiyo imefanyiwa majaribio ya mifumo na mitambo kati ya tarehe 25 na 27 Machi, 2024.

119. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile tarehe 11 Oktoba, 2023 Serikali kupitia MSCL ilisaini Mkataba wa Ujenzi wa meli mpya ya kubeba mzigo wa tani 3,000 katika Ziwa Victoria. Pia, Serikali imesaini mikataba ya ukarabati wa meli mbili (2) zilizopo katika Ziwa Victoria ambazo ni meli ya uokozi ya MT. Ukerewe na meli ya kubeba shehena ya mafuta ya MT. Nyangumi yenye uwezo wa kusafirisha shehena ya mafuta ya lita 410,000. Kwa sasa taratibu za utekelezaji zinaendelea, lengo ni kukamilisha ujenzi na ukarabati wa meli kulingana na mikataba hiyo ndani ya miaka miwili (2) tangu utekelezaji wake kuanza.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Ziwa Tanganyika, Serikali imeendelea na ukarabati wa meli ya MT. Sangara ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 92. Pia, Serikali imesaini mikataba miwili (2) ambayo ni ya ujenzi wa kiwanda cha kujengea meli katika Ziwa hilo chenye uwezo wa kubeba meli yenye uzito wa tani 5,000 na ujenzi wa meli ya kubeba mizigo tani 3,500. Ujenzi wa kiwanda hiki ni hatua muhimu ya kujivunia kwa Taifa letu kwa kuwa ni mara ya kwanza kujenga kiwanda cha aina hii hapa nchini ambapo kwa miaka ya nyuma meli nyingi zilikuwa hazijengwi nchini badala yake zilikuwa zinatengenezwa nje ya nchi na kuletwa nchini kwa ajili ya kuunganishwa, suala

ambalo lilikuwa linachangia kuongeza gharama; kukosesha fursa ya kujenga ujuzi nchini; na kukosesha ajira kwa Watanzania.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ukarabati katika Ziwa Tanganyika, Serikali imesaini mkataba wa ukarabati wa meli ya MV. Liemba inayotegemewa na wananchi wa mwambao wa Ziwa Tanganyika katika kusafirisha abiria na mizigo. Meli hii itakuwa na uwezo wa kusafirisha abiria 600 na tani 200 za mizigo, ambapo kwa sasa maandalizi ya kufanya ukarabati huo yanaendelea.

**Huduma za Viwanja vya Ndege**

122. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) imeendelea kutoa huduma kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa inayohusiana na Usafiri wa Anga. Mamlaka hii ina jukumu la kuendesha, kusimamia, kuboresha na kuendeleza Viwanja vya Ndege 58 vya Serikali vilivyopo Tanzania Bara. Aidha, TAA inalo jukumu la kutoa huduma bora zenye ufanisi na salama pamoja na vifaa wezeshi kwa ajili ya usafirishaji wa abiria na mizigo katika viwanja vya ndege inavyovisimamia. Hadi kufikia Machi 2024, TAA ilihudumia jumla ya abiria 3,202,573 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 8.58 ikilinganishwa na abiria 2,949,508 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha huduma kwa abiria, ndege na mizigo zinaendelea kutolewa kwa ufanisi, Serikali kupitia TAA imeendelea kuimarisha huduma za ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege nchini kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa. Hadi kufikia Machi 2024, TAA ilikamilisha ujenzi wa uzio wa usalama wenye urefu wa kilometa 7.2 na ufungaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege (AGL) katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma. Ufungaji wa taa za kuongozea ndege umewezesha kutolewa kwa huduma za usafiri wa ndege kwa saa 24 kila siku. Aidha, ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na ufungaji wa mfumo wa kamera za usalama (CCTV) katika

Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere umekamilika kwa asilimia 100.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 Ibara ya 59(h) imeelekeza Serikali kuendelea kuboresha huduma za usafiri wa anga nchini. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Serikali imeendelea kuzingatia miongozo ya kimataifa ya uendeshaji wa viwanja vya ndege, ambayo utekelezaji wake umekuwa ukipimwa kulingana na vigezo vilivyowekwa kimataifa kupitia Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO). Kupitia ukaguzi wa mwisho wa Ulinzi (security audit) uliofanywa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) mwishoni mwezi Mei, 2023 ambapo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere - JNIA ni miongoni mwa viwanja vilivyokaguliwa; nchi ilifanikiwa kupata ufaulu wa asilimia 86.70 na kuwa nchi ya nne barani Afrika kwa ubora. Kwa sasa TAA inaendelea na maandalizi ya ukaguzi wa usalama (safety) katika Kiwanja cha Ndege cha JNIA unaotarajiwa kufanywa na ICAO mnamo mwezi Juni, 2024. Haya yote yanafanyika kwa lengo la kuhakikisha shughuli za ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege nchini zinakidhi viwango na matakwa ya usafiri wa anga duniani.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hayo, TAA imeandaa programu za ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege 21 vya Lake Manyara, Arusha, Mwanza, Iringa, Mafia, Lindi, Mpanda, Tanga, Tabora, Songea, Songwe, Kigoma, Bukoba, Dodoma, Shinyanga, Kilwa Masoko, Musoma, Kahama, Mtwara, Geita na Nachingwea. Aidha, katika kupima utayari wa kukabiliana na majanga viwanjani, TAA imefanya mazoezi ya kujipima na dharura ya uokozi (emergency drills) katika viwanja vya ndege vya Mtwara, Lake Manyara na Bukoba. Pia, TAA imehuisha leseni za uendeshaji wa viwanja vya ndege vya Bukoba, Arusha na Dodoma ili kuhakikisha viwanja hivyo vinakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za zimamoto viwanjani zimeendelea

kutolewa kwa kuhakikisha kunakuwepo na madawa ya kuzima moto, vifaa mbalimbali vya uokoaji pamoja na kufanyika kwa matengenezo ya mitambo ya zimamoto katika viwanja vya ndege vinavyomilikiwa na Serikali. TAA imekamilisha taratibu za ununuzi wa mtambo mmoja (1) wa zimamoto na uokoaji kwa ajili ya Kiwanja cha Ndege cha Arusha ambapo kwa sasa mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi ya utengenezaji wa mtambo huo. Aidha, katika kuendelea kuboresha utoaji wa huduma hiyo katika viwanja vingine, uundwaji wa mitambo miwili mipya ya zimamoto kwa ajili ya viwanja vya ndege vya JNIA na Dodoma unaendelea ambapo hadi mwishoni mwa mwezi Machi, 2024 kazi hiyo ilikuwa imefikia asilimia 97 na itakamilika mwezi Juni, 2024.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa kuwa na viwanja vya ndege vyenye ubora, Serikali imeendelea kuboresha huduma za usafiri wa anga kwa kuendeleza na kukarabati viwanja vya ndege nchini. Hadi kufikia Machi 2024, Serikali kupitia TAA imeendelea na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha ambapo ujenzi wa jengo jipya la abiria pamoja na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA umekamilika kwa asilimia 98. Baadhi ya kazi zilizosalia ni pamoja na usimikaji wa mfumo wa kuhudumia mizigo ya abiria na mfumo wa viyoyozi ambazo zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2024. Aidha, Mkandarasi anayehusika na ufungaji wa taa za kuongozea ndege (AGL) katika kiwanja hiki tayari amekabidhiwa eneo la mradi na anaendelea na maandalizi ya awali (mobilization).

128. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha ujenzi wa majengo mapya ya abiria katika viwanja vya ndege vya Kahama na Kilwa Masoko na ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mpanda umekamilika kwa asilimia 97. Aidha, Usanifu wa Kina wa Jengo la Mnara wa Kuongozea Ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Bukoba umekamilika na taratibu za ununuzi wa Mkandarasi zinaendelea. Pia, ukarabati na upanuzi wa barabara ya kuingia kiwanjani (Access Road) na njia ya watembea kwa miguu (Pedestrian Walkway) kwa kiwango cha lami pamoja na

ufungaji wa mfumo na mitambo mipya ya umeme katika Kiwanja cha Ndege Dodoma vimekamilika.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Hotuba yangu ya bajeti ya mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa, jukumu la ujenzi wa viwanja vya ndege liliamriwa rasmi kurejeshwa TAA kwa utaratibu maalum wa kutoathiri miradi iliyokuwa imeanza kutekelezwa na TANROADS. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa jukumu hilo sasa limeendelea kutekelezwa na TAA kwa miradi mipya na miradi iliyorejeshwa ikiwa chini ya asilimia 40 ya utekelezaji. Baada ya uamuzi huo, Wizara kupitia TAA imeendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Moshi, Lindi, Mtwara, Mwanza na JNIA (Jengo la Pili la Abiria – TB II). Aidha, TANROADS imeendelea na ujenzi wa viwanja vilivyokuwa vimeanza kujengwa chini ya ufadhili wa wadau wa maendeleo na vilivyokuwa vimefikia zaidi ya asilimia 40 ya utekelezaji chini ya fedha za Serikali wakati uamuzi huo unafanyika. Viwanja hivyo ni pamoja na: Msalato, Tabora, Shinyanga, Sumbawanga, Iringa, Musoma, Kigoma, Lake Manyara na Tanga.

130. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege inayosimamiwa na TAA, hadi kufikia Machi 2024, ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi umefikia asilimia 55. Pia, kazi ya ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Lindi zipo katika hatua za ununuzi wa Mkandarasi ambapo tathmini za zabuni zinaendelea na kuhusu usanifu na ujenzi wa jengo la abiria, Kituo cha Zimamoto, Kituo cha Hali ya Hewa na Mnara wa kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Mtwara, taratibu za manunuzi zimekamilika na Mkataba umesainiwa tarehe 29 Aprili, 2024. Aidha, kwa upande wa mradi wa uboreshaji na upanuzi wa Jengo la Pili la Abiria – JNIA usanifu wa awali umefikia asilimia 98.

131. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha TAA inaendana na kasi ya ukuaji wa shughuli za usafiri wa anga nchini unaosababisha mahitaji ya upanuzi na ujenzi wa viwanja vipya, Serikali imeendelea na

juhudi za utwaaji, upimaji na upatikanaji wa Hati Miliki katika viwanja vya ndege mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 TAA imefanikiwa kupata Hati Miliki saba (7) za viwanja vya ndege vya Songea, Kasulu, Uvinza, Kibondo, Mbeya, Loliondo na Mombo na hivyo kupelekea Mamlaka kuwa na jumla ya Hati Miliki 30. Aidha, taratibu za upatikanaji wa Hati Miliki za Viwanja vya Ndege vya Mwanza, Mtwara, Msalato, Masasi, Liuli na Mbamba Bay zipo hatua za mwisho za upatikanaji wake.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea na jitihada za kuboresha huduma na kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo na vyanzo vingine visivyohusiana na ndege (Non Aeronautical Revenue), Serikali kupitia TAA imeendelea kuimarisha mifumo ya maegesho ya magari ambapo kazi za usimikaji mifumo ya kielektroniki ya maegesho ya magari katika Viwanja vya Ndege vya Dodoma na Mwanza zimekamilika. Aidha, TAA inaendelea kukamilisha taratibu za kupata wawekezaji kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa watu mashuhuri katika viwanja vya ndege vya Dodoma na Arusha.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za Serikali za kukuza fursa za ajira na uhaulishaji wa teknolojia (technological transfer) kwa wazawa, Serikali kupitia TAA imewezesha uwekezaji wa kiwanda cha uunganishaji na utengenezaji wa ndege ndogo katika Kiwanja cha Ndege cha Morogoro kupitia Kampuni ya *Airplane Africa Limited*. Kampuni hiyo inayomilikiwa na wawekezaji kutoka Jamhuri ya Czech inafanya kazi ya kuunganisha na kutengeneza ndege za kubeba abiria wawili (2) ambazo ni aina ya "Skyleader". Kwa sasa kiwanda hicho ni cha pekee Afrika Mashariki ambapo kina matawi katika nchi za Urusi, Jamhuri ya Czech, Ujerumani na China. Uwekezaji huu pamoja na manufaa mengine, utawezesha kukuza ujuzi na kuongezeka kwa mapato ya Serikali kutokana na kodi mbalimbali zitakazolipwa.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendana na kasi ya ukuaji wa sekta ya anga na uimarishaji wa utoaji huduma katika Viwanja vya Ndege, TAA imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa

watumishi wake ambapo katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024, jumla ya watumishi 738 kutoka katika kada mbalimbali zikiwemo zimamoto na uokoaji, uendeshaji, ulinzi na usalama waliweza kupatiwa mafunzo ya muda mfupi ili kuboresha utendaji kazi wao.

**Huduma katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA)**

135. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba yangu ya bajeti kwa mwaka 2023/24 niliahidi kuwa Serikali inaendelea na taratibu za kurejesha shughuli za uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) kutoka KADCO. Napenda kulitaarifu rasmi Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekamilisha urejeshwaji wa Kiwanja cha KIA kwa TAA kutoka KADCO.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) kilitoa huduma za usafiri wa anga kwa mashirika ya ndege ya ndani na kimataifa yenye ratiba maalum za safari na mashirika ya ndege ya kimataifa yasiyokuwa na ratiba maalum. Mashirika hayo ya ndege yaliwezesha Kiwanja cha KIA kuhudumia miruko ya ndege 17,089 sawa na ongezeko la asilimia 7.64 ikilinganishwa na miruko ya ndege 15,876 iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/23.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro umeendelea kuimarika kutokana na jitihada za Serikali katika kukitangaza kiwanja hicho kimataifa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya abiria 828,867 walihudumiwa kupitia Kiwanja hicho sawa na ongezeko la asilimia 8.72 ikilinganishwa na abiria 762,407 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/23. Aidha, jumla ya tani 4,961.25 za mizigo zimehudumiwa katika Kiwanja cha KIA sawa na ongezeko la asilimia 44.78 ikilinganishwa na tani 3,426.65 za mizigo iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa

fedha 2022/23.

138. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kushughulikia mgogoro kati ya kiwanja cha KIA na wananchi. Hadi kufikia Machi, 2024 Serikali imekamilisha kulipa fidia kwa wananchi 1,631 kati ya 1,712 waliopaswa kulipwa ambayo ni sawa na asilimia 95.27. Wananchi 81 wanaendelea kulipwa kadri wanavyowasilisha taarifa zao za kibenki. Tayari alama za kudumu za mipaka kuzunguka eneo lote la kiwanja cha KIA zimewekwa ili kuzuia uvamizi unaoweza kutokea hapo baadaye.

**Huduma za Usafiri wa Anga**

139. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) imeendelea kufanya biashara ya usafiri wa anga kwa kusafirisha abiria na mizigo ndani na nje ya Tanzania ili kuinua uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi. Aidha, ATCL imeanza hatua kwa hatua kujihudumia katika baadhi ya maeneo ikiwa ni pamoja na matengenezo ya ndege, utoaji wa huduma uwanjani (ground handling services) kwa kituo cha Dodoma na huduma ndani ya ndege pamoja na kutoa huduma ya mafunzo kwa wahudumu wa ndani ya ndege kupitia Chuo chake kijulikanacho kama ATCL Training Centre.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) katika sehemu ya 5.7 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 Ibara ya 59(i) ilidhamiria kuendelea kufufua Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege ili kuimarisha ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Nichukue fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imeendelea kuboresha utendaji wa ATCL kwa kununua ndege mpya na kuboresha miundombinu wezeshi ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na majengo na karakana. Uboreshaji wa ATCL unalenga kuongeza ufanisi wa utendaji ili kuweza kuhudumia soko la ndani na nje ya nchi la kusafirisha mizigo na abiria; na kuchagiza shughuli za utalii, kilimo ikiwa ni pamoja na kusafirisha mazao yanayoharibika haraka (perishable goods) na

madini. Ununuzi wa ndege na uboreshaji wa miundombinu umelenga kuipunguzia ATCL gharama za uendeshaji na kuifanya iwe shindani katika soko la usafiri wa anga duniani.

141. ***Mheshimiwa Spika,*** uboreshaji wa ATCL umeongeza utendaji wa ATCL ambapo hadi kufikia Machi, 2024, ATCL imeendelea kutoa na kuboresha huduma za usafiri wa anga kwa kusafirisha abiria na mizigo ndani na nje ya Tanzania. Kwa takwimu zilizopo, ATCL ilisafirisha abiria 850,660 ikilinganishwa na abiria 826,594 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 2.91. Kati ya abiria waliosafirishwa, abiria 650,221 walikuwa ni wa ndani ya nchi na abiria 200,439 walikuwa ni wa nje ya nchi.

142. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi 2024, ATCL iliweza kusafirisha jumla ya tani 5,034.2 za mizigo ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na tani 2,680.9 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 87.78. Ongezeko hilo limetokana na kuanza kufanya kazi kwa ndege ya mizigo aina ya Boeing 767-300F yenye uwezo wa kubeba tani 54 ambayo husafirisha mizigo kati ya Dar es Salaam na vituo vya Nairobi na Dubai mara moja (1) kwa wiki, pamoja na vituo vingine ambavyo wateja wenye mizigo hukodi vikiwemo vya Mumbai (India), Eldoret (Kenya), Mombasa (Kenya), Bujumbura (Burundi), Kinshasa (Kongo DRC), Bangui (Cetral Afrika), N'Djamena (Chad), Entebbe (Uganda), na Lusaka (Zambia). Ndege hii imesafirisha tani 2,084.7 za mizigo sawa na asilimia 41.41 ya mizigo iliyosafirishwa katika kipindi tajwa.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuongeza wigo wa huduma zake, ATCL imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa anga katika vituo 24 ambapo vituo 13 ni vya ndani ya nchi na vituo 11 ni vya nje ya nchi. Vituo vya ndani ya nchi ni Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kilimanjaro, Kigoma, Songwe, Mpanda, Mwanza, Songea, Tabora na Zanzibar. Vituo vya nje ya nchi ni Bujumbura, Dubai, Entebbe, Hahaya, Guangzhou, Harare,

Lubumbashi, Lusaka, Mumbai, Nairobi na Ndola.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu usimamizi na ununuzi wa ndege, kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi kufikia Machi 2024, Serikali ilikamilisha malipo ya ndege tatu (3) ambazo ni Boeing 737-9 Max mbili (2) na Boeing 787-8 Dreamliner moja (1). Ndege mbili aina ya Boeing 737-9 Max tayari zimewasili nchini ambapo ndege moja (1) ilipokelewa tarehe 3 Oktoba, 2023 na nyingine tarehe 26 Machi, 2024. Aidha, ndege moja (1) ya Boeing 787-8 Dreamliner iliyosalia inatarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwezi Mei, 2024. Kuwasili kwa ndege hiyo kutaifanya ATCL kuwa na jumla ya ndege 16. Ndege hizo zitasaidia ATCL kuendelea kupanua mtandao wake wa safari za ndani na nje ya nchi ili kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za uchumi kama utalii, madini, biashara, kilimo, mifugo na uvuvi.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, ATCL ilinunua vifaa na vipuri kwa ajili ya kuwezesha kufanya matengenezo makubwa na madogo ya ndege aina zote yaliyoruhusiwa katika karakana zilizopo katika kiwanja cha JNIA na KIA. Aidha, ukarabati wa miundombinu katika Karakana ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro - KIA (KIMAFA) na JNIA unaendelea. Pia, ukarabati wa nyumba 38 zilizopo KIA unaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 47. Ukarabati wa nyumba hizi ni muhimu kwa ajili ya matumizi ya watumishi wa ATCL wataokuwa wakitoa huduma katika kituo cha KIA. Kituo cha KIA ni kituo muhimu kwa ajili ya utalii hivyo ATCL itafanya kituo hicho kuwa kitovu kidogo (sub hub) kadri utoaji wa huduma unavyokuwa.

146. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeiwezesha ATCL kuanza ujenzi wa Karakana mpya yenye uwezo wa kuhudumia Ndege kubwa na kuifanya JNIA kitovu cha safari za ATCL, ujenzi wa Ofisi za ATCL - Dodoma ili kuhakikisha utoaji huduma Makao Makuu ya Nchi unakuwa wa haraka, na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mizigo katika viwanja vya Ndege vya JNIA, KIA na Songwe ili kukuza biashara ya usafirishaji wa mizigo pamoja na ubora wa bidhaa zinazosafirishwa ambapo mchakato wa kumpata mkandarasi

upo katika hatua za mwisho na hivyo ujenzi wa miundombinu tajwa unatarajiwa kuanza robo ya nne ya mwaka huu 2023/24.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na ulipaji wa madeni ya zamani ya ATCL. Kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza katika hotuba yake wakati wa kuahirisha Mkutano wa 11 wa Bunge la 12 tarehe 28 Juni 2023 kuwa Taasisi zilipe madeni katika Mifuko ya Pensheni, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Shilingi bilioni 18.58 zimelipwa kwa wastaafu ikiwa ni sehemu ya madeni yaliyorithiwa na ATCL kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa Mpango wa Ufufuaji. Hadi sasa madeni kiasi cha Shilingi bilioni 148.95 sawa na asilimia 64 tayari yamelipwa na kubakia kiasi cha Shilingi bilioni 82 sawa na asilimia 36. Serikali itaendelea na ulipaji wa madeni haya ili kuweka vizuri mizania ya vitabu vya hesabu za Kampuni na kuimarisha imani miongoni mwa wadau wa ATCL.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia ATCL imeendelea kuajiri watumishi ambapo hadi kufikia Machi 2024, ATCL ilikuwa na watumishi 792 ikilinganishwa na watumishi 689 waliokuwepo katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/23. Idadi ya watumishi walioongezeka hadi mwezi Machi, 2024 inajumuisha marubani ambao kwa sasa wamefikia 117 ikilinganishwa na marubani 108, wahandisi na mafundi ndege wamefikia 178 ikilinganishwa na 139 na watumishi wengine wamefika 497 ikilinganishwa na 442 waliokuwepo katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2022/23.

149. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, ATCL imeendelea kujenga uwezo wa ndani wa watumishi wake ambapo watumishi 765 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na watumishi nane (8) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu. Kati ya watumishi hao, watumishi watatu (3) wamehitimu shahada ya uzamili katika uongozi na usimamizi wa shughuli za usafiri wa anga (Global Executive MBA Aerospace Management) katika Chuo cha Toulouse Ufaransa. Aidha, watumishi wengine wanne (4) wanaendelea na mafunzo ya aina hiyo hiyo katika chuo hicho.

Vilevile, mtumishi mmoja (1) kati ya hao watumishi nane (8) anaendelea na mafunzo ya shahada ya uzamili katika eneo la sheria za usafiri wa anga kwenye chuo kikuu cha Sharijah katika Falme za Kiarabu (UAE).

150. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile ATCL imeendelea kujenga uwezo wa chuo chake cha mafunzo cha masuala ya usafiri wa anga. Chuo hicho kina uwezo wa kuzalisha takribani wahudumu wa ndani ya ndege 120 kwa mwaka. Chuo hicho pia kinasaidia utoaji wa mafunzo mbalimbali kwa watumishi ikiwemo kuwaandaa marubani wanaotakiwa kufanya mafunzo ya nadharia na vitendo ya *type rating* ya ndege nje ya nchi.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa huduma, ATCL imeendelea kubuni na kutoa huduma rafiki kwa wateja wake zikiwemo ATCL Mobile App ambayo ilizinduliwa Disemba, 2023; huduma ya kulipia kidogo kidogo (Kibubu); na huduma ya kuwatambua wasafiri wa mara kwa mara na kuwapa motisha (Loyalty Program). Wateja wa ATCL wanaweza kupata huduma ya tiketi pamoja na huduma nyingine katika Ofisi za ATCL Makao Makuu Dar es Salaam na mikoani, Ofisi za GSA katika vituo vya nje, kupiga simu ya huduma kwa wateja namba **+255 748 773900**, tovuti ya ATCL ***www.airtanzania.co.tz***, na mawakala mbalimbali. Kutokana na kuendelea kuboresha huduma, ATCL imefanikiwa kuchukua Tuzo ya *Africa Most Preferred Domestic Airline of the year 2023* na Tuzo ya *Most Preferred International Airline of the Year 2023* iliyotolewa na *Consumer Choice Awards* mwezi Novemba, 2023.

## B. 1: VYUO VYA MAFUNZO YA KISEKTA

152. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza azma ya Serikali ya kujenga uwezo na kutumia wataalam wa ndani pamoja na kupunguza gharama za kusomesha wataalam nje ya nchi, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 Ibara ya 59(i) iliahidi kuboresha na kuvijengea uwezo vyuo vya mafunzo vya kisekta. Serikali kupitia vyuo vya kisekta vinavyosimamiwa na Wizara ya Uchukuzi,

imeendelea kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali za usafiri na usafirishaji ikiwemo mafunzo ya usafiri wa anga, usafiri ardhini na usafiri majini kwa lengo la kuwa na wataalam wanaotoa huduma katika Sekta ya Uchukuzi. Utekelezaji wa majukumu ya vyuo vya kisekta kwa mwaka wa fedha 2023/24 unajumuisha Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Chuo cha Usafiri wa Anga, Chuo cha Bandari, Chuo cha Hali ya Hewa na Chuo cha Reli.

**Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)**

153. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) imeendelea kutoa mafunzo, kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na kuandaa machapisho kwa lengo la kujenga uwezo wa wataalam katika njia zote za usafirishaji ambazo ni barabara, anga, reli, maji na usafirishaji kwa njia ya bomba.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa masomo 2023/24, Chuo cha NIT kimeendelea kutoa mafunzo ya kozi ndefu 55 ikilinganishwa na kozi 51 zilizotolewa katika mwaka wa masomo 2022/23 sawa na ongezeko la kozi nne (4). Ongezeko hili limetokana na uhitaji mkubwa wa wataalam ili kuendeleza miradi mikubwa ya kitaifa inayotekelezwa na Serikali. Kwa sasa, Chuo, kina wanafunzi wa kozi ndefu 16,131 ikilinganishwa na wanafunzi 14,920 kwa mwaka wa masomo 2022/23 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 8.12. Ongezeko hili linatokana na Chuo kuendesha kozi za kimkakati zinazoendana na miradi mikubwa ya kitaifa inayotekelezwa na Serikali. Aidha, jumla ya wanafunzi 3,884 walihitimu mafunzo ya kozi za muda mrefu ikilinganishwa na wanafunzi 2,772 waliohitimu katika mwaka wa masomo 2021/22 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 40.11.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2024, jumla ya washiriki 3,679 waliohudhuria mafunzo ya kozi za muda mfupi za Menejimenti ya Usafirishaji na Uchukuzi; Ukaguzi wa Magari; na ueledi wa Madereva ikilinganishwa na washiriki 1,760 waliohudhuria kozi za muda mfupi katika kipindi kama hicho katika mwaka wa

masomo 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 109.03. Ongezeko hili linatokana na utekelezaji wa sheria za uendeshaji wa vyombo vya moto ya kuwataka madereva kupata mafunzo kabla ya uhuishwaji wa leseni.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 Ibara ya 59(i) iliahidi kukiwezesha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kutoa elimu kwa wataalam wa kada ya usafiri wa anga. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imekamilisha ununuzi wa Ndege mbili (2) za injini moja (1) za mafunzo ya urubani na taratibu za kuanza Mafunzo ya Urubani katika Chuo hicho zinaendelea ambapo mafunzo yanatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Septemba, 2024. Hivyo, kuanza kutolewa mafunzo haya hapa nchini kutapunguza gharama na kuongeza wigo na fursa kwa Watanzania kusomea mafunzo ya Urubani.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia NIT imeendelea kutekeleza mradi wa kuboresha miundombinu na vifaa vya kufundishia ambapo ujenzi wa Kituo cha Raslimali Mafunzo (Maktaba) umefikia asilimia 75; uundwaji wa Ndege moja (1) yenye injini mbili (2) kwa ajili ya kufundishia Marubani unaendelea kiwandani nchini Marekani na unatarajiwa kukamilika mwezi Machi 2025. Aidha, zoezi la kukamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya uanzishwaji wa Kituo Atamizi cha Mafunzo (Incubation Centre) ya wataalam mahiri wa Usafiri Majini Mkoani Lindi lipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha NIT kupitia Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirishaji kilichoanzishwa chini ya Mradi wa *East Africa Skills for Transformation and Regional Intergration Project* (EASTRIP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kimeendelea kutekeleza kazi za mradi kama ifuatavyo:-

i. Ujenzi wa majengo matano (5) yanayojengwa katika Kampasi ya Mabibo – Dar es Salaam ambayo yana madarasa 11, maabara 16, karakana tano (5), mabweni ya wanafunzi

mawili (2) na ofisi za watumishi 13, ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 75;

ii. Ujenzi wa majengo matatu (3) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) ambayo ni Karakana ya Matengenezo ya Ndege (Aviation Hangar), Bweni la wanafunzi 20 wa Urubani na nyumba za watumishi 10 upo katika hatua ya ununuzi wa mkandarasi; na

iii. Ununuzi wa Vifaa vya mafunzo ya Urubani na Uhandisi Matengenezo ya Ndege ikiwemo *Flight Simulators* mbili (2), *Workshop, Multimedia and Computer Based equipment* umefikia asilimia 60.

159. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Chuo cha NIT kupitia Kituo cha Kikanda cha Umahiri cha Mafunzo ya Usalama Barabarani kilichoanzishwa kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kimeendelea kutekeleza kazi zake kama ifuatavyo:-

i. Ufungaji wa vifaa vya TEHAMA ikiwemo *Camera with ZOOM, Digital Television*, *CCTV Cameras*, *WiFi AP and Teleconferencing System* kwa ajili ya mafunzo ya usalama barabarani upo kwenye hatua za mwisho;

ii. Kukamilisha uandaaji miongozo 16 ya kufundishia ambao umesaidia kuboresha utoaji wa mafunzo katika Chuo cha NIT;

iii. Mafunzo ya kozi ya Ukaguzi wa Usalama Barabarani yamefanyika kwa washiriki 180 katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini katika mkoa wa Njombe (23), Kanda ya Kati - Dodoma (26), Kanda ya Ziwa - Mwanza (58) na Zanzibar (73); na

iv. Taarifa ya awali (Inception report) kwa ajili ya uandaaji wa mitaala na miongozo ya kuwajengea uwezo watumishi katika kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi katika masuala ya usalama barabarani imeandaliwa na kukamilika.

160. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuboresha utoaji wa huduma ya elimu na mafunzo kwa ufanisi zaidi, Chuo cha NIT kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi katika mafunzo ya muda mrefu ambapo jumla ya watumishi 78 wanaendelea na mafunzo hayo. Kati ya watumishi hao; 41 wanasoma Shahada ya Uzamivu, 26 Shahada ya Uzamili, watano (5) mafunzo ya Urubani (Integrated Commercial Pilot License Course - ICPL) na watumishi sita (6) mafunzo ya Leseni ya Matengenezo ya Ndege (Basic Aircraft Maintenance Technician License).

**Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)**

161. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha elimu na mafunzo ya bahari nchini, Serikali kupitia Chuo cha Bahari Dar es Salaam (*DMI)* imeendelea kutoa mafunzo, kufanya tafiti, kutoa huduma ya ushauri wa kitaalam na kuandaa machapisho ili kuandaa na kuzalisha wataalam wa sekta ya Bahari katika maeneo ya uhandisi wa meli, usanifu wa meli, unahodha wa meli, usafirishaji baharini na uhandisi wa mafuta na gesi baharini. Aidha, Chuo kimeendelea kutoa kozi za Umahiri (*Certificates of Competency*) katika elimu na mafunzo ya bahari.

162. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa masomo 2023/24, Chuo kilitoa mafunzo ya kozi ndefu 51 zikiwemo kozi 10 za maafisa wa vyombo vya majini (Certificate of competency). Aidha, Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi wa kozi ndefu 5,177 ikilinganishwa na wanafunzi 3,505 waliodahiliwa katika mwaka wa masomo 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 47.70. Ongezeko hilo limetokana na uelewa wa jamii kuhusu kozi zinazotolewa na Chuo hicho.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imeendelea kusimamia tasnia ya ubaharia, ambapo katika Mwaka wa Masomo 2023/24, Mabaharia 4,303 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi ya kozi za Umahiri katika elimu na mafunzo ya Bahari ikilinganishwa na Mabaharia 3,100 waliohudhuria mafunzo ya muda mfupi katika kipindi kama hicho Mwaka wa Masomo 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 38.81. Ongezeko hilo linatokana na uhamasishaji na ufuatiliaji wa tasnia hii uliofanyika kupitia usimamizi

wa Chuo cha DMI.

164. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza mikakati ya kujenga uwezo wa Chuo kutoa mafunzo, katika mwaka wa masomo 2023/24 hadi kufikia Machi, 2024 idadi ya watumishi wa Chuo cha DMI iliongezeka kutoka 119 kwa mwaka wa masomo wa 2022/23 hadi 160 kwa mwaka wa masomo wa 2023/24 sawa na ongezeko la watumishi 41. Aidha, Ikama ya Chuo ni kuwa na watumishi 266 ili kukidhi mahitaji ya Chuo. Kati ya watumishi hao 160, watumishi 74 ni wanataaluma (Academic Staff) na watumishi 86 ni wa kada ya uendeshaji. Ongezeko hilo la watumishi 41 limetokana na kuajiri watumishi 18 na watumishi 23 waliohamia katika Chuo hicho cha DMI.

165. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2024, Serikali kupitia Chuo cha Bahari Dar es Salaam imeendelea kuwajengea uwezo watumishi katika mafunzo ya muda mrefu, ambapo watumishi 22 wanaendelea na mafunzo hayo. Kati ya watumishi hao, saba (7) wanasoma Shahada ya Uzamivu; 12 wanasoma Shahada ya Uzamili; mmoja (1) anasoma Shahada ya kwanza; mmoja (1) anasoma Stashahada; na mmoja (1) anahudhuria mafunzo ya vitendo melini.

166. ***Mheshimiwa Spika,*** utakumbuka kuwa katika Hotuba ya bajeti yangu iliyopita, Serikali iliahidi kuendelea kuboresha miundombinu na vifaa vya kufundishia katika vyuo vyake vya kisekta kikiwemo Chuo cha Bahari Dar es Salaam. Naomba kutoa taarifa kuwa hadi kufikia Machi 2024, Serikali imetimiza ahadi hiyo kwa kununua mtambo maalum wa kufundishia kwa vitendo (full mission crane simulator). Tayari mtambo huo umeanza kutumika kutoa mafunzo kwa vitendo na umeongeza ubora na umahiri katika utoaji wa mafunzo ya kutumia mitambo maalum ya kuhudumia mizigo kwenye meli na vyombo vingine vya usafiri majini.

**Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC)**

167. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Chuo cha Usafiri wa Anga kilichopo Dar es Salaam (Civil Aviation Training Centre -CATC)

imeendelea kutoa mafunzo katika kozi mbalimbali za usafiri wa anga ambazo ni pamoja na: uongozaji ndege; uendeshaji wa mitambo ya kuongozea ndege na mawasiliano; mawasiliano ya taarifa za anga; usalama wa anga na upekuzi; usimamizi na uandaaji wa safari za ndege; urushaji wa ndege zisizokuwa na rubani (Drones); na usimamizi wa viwanja vya ndege.

168. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2024, Chuo cha CATC kilitoa mafunzo ya kozi 96 ambazo zilikuwa na washiriki 1,523 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 60.82 ikilinganishwa na washiriki 947 waliopewa mafunzo katika kipindi kama hicho mwaka wa masomo 2022/23. Kati ya washiriki hao, Washiriki 121 walitoka nje ya nchi (wanaume 102 na wanawake 19) na 1,402 (wanaume 958 na wanawake 444) walikuwa washiriki wa ndani ya nchi. Aidha, idadi ya nchi zinazoleta washiriki imeongezeka kutoka nchi 12 hadi kufikia nchi 16. Washiriki hao walitoka nchi za Uganda, Botswana, Namibia, Eswatini, Burundi, Rwanda, Somalia, Nigeria, Liberia, Sierra Leone, Guinea Conakry, Kenya, Sudan Kusini, Afrika Kusini na Zambia.

169. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Chuo hicho kwa kushirikiana na Chuo cha Concordia cha Canada kilitoa mafunzo ya menejimenti ya usalama wa anga (ICAO Professional Management Course) kwa washiriki 20 waliotoka Bara la Afrika na Asia (India) kuanzia tarehe 6 Julai, 2023 hadi 9 Oktoba, 2023. Kozi hii inaendeshwa mara moja tu kwa mwaka duniani kote. Pia, Chuo cha CATC kimeanzisha kozi mpya sita (6) kulingana na uhitaji katika soko.

**Chuo cha Bandari**

170. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Bandari kinatoa mafunzo, tafiti na ushauri wa kitaalam katika tasnia ya Usafirishaji kwa njia ya Bahari na Maziwa nchini. Chuo hiki kinatoa mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Usimamizi wa Wakala wa Forodha na Usafirishaji wa Mizigo; Mipango ya Usafiri wa Majini na Nchi Kavu; Usimamizi wa Operesheni za Meli na Bandari; Usimamizi wa Vifaa vya Bandari na Matengenezo, Usimamizi wa

Moto na Usalama. Mafunzo ya muda mfupi yanayotolewa na chuo ni pamoja na mafunzo maalum ya kuandaa mizigo kwa kutumia mashine mbalimbali.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Chuo hiki kilidahili jumla ya wanafunzi 1,025 wa mafunzo ya muda mrefu ikilinganishwa na wanafunzi 937 waliodahiliwa katika mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 9.39. Kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi, Chuo kilidahili jumla ya washiriki 1,717 kati ya hao, washiriki 864 walitoka katika sekta binafsi, washiriki 415 ni kutoka Taasisi mbalimbali na washiriki 438 ni kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania. Aidha, Chuo kimeandaa mitaala 15 inayohusiana na taaluma ya uhudumiaji shehena na miundombinu ya mafuta na gesi na mitaala mingine mipya sita (6) ya *Standards of Training Certification and Watch Keeping for Seafarers 1978 as amended* (STCW 1978) inayolenga kutoa mafunzo kwa Watumishi wa TPA na wadau wanaohusika na shughuli za usafiri majini kwa kutoa mafunzo ya huduma ya kwanza, uzimaji moto na usalama na uokoaji.

**Chuo cha Hali ya Hewa**

172. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa kilichopo Kigoma, imeendelea kutoa mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya awali na Diploma, ambapo jumla ya wanafunzi 40 walidahiliwa katika mwaka wa fedha 2023/24. Kati ya wanafunzi hao, Wanafunzi 19 ni ngazi ya Diploma (NTA Level 6), Wanafunzi 12 ni ngazi ya kati (NTA Level 5) na wanafunzi 9 ni ngazi ya Cheti (NTA Level 4). Aidha, Serikali imeendelea kukiboresha Chuo hicho ili kuimarisha utoaji wa mafunzo na wigo wa udahili wakiwemo wanafunzi kutoka nchi jirani.

**Chuo cha Reli**

173. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha Reli imeendelea kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi katika usafiri wa njia ya reli ili kuleta tija katika Shirika la Reli Tanzania (TRC) na

wadau wengine husika katika usafiri wa kwa njia ya reli. Chuo kina kampasi mbili (2) ya Tabora (Kampasi kuu) na Morogoro ambazo zinatoa mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Usafirishaji kwa njia ya Reli; Matengenezo ya mabehewa; Matengenezo ya miundombinu ya Reli; na Fundi Sanifu wa Mifumo ya Umeme kwenye Vichwa vya Treni.

174. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 466 ikilinganishwa na wanafunzi 381 waliodahiliwa katika mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 22.31. Ongezeko hili limetokana na kuanzishwa kwa kozi mpya ya stashahada ya matengenezo ya miundombinu ya Reli na matengenezo ya mabehewa katika kampasi ya Morogoro.

**B. 2:MASUALA MTAMBUKA**

**Rasilimaliwatu na Maendeleo ya Watumishi**

175. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Wizara inakuwa na rasilimaliwatu endelevu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuajiri Watumishi wa kada mbalimbali ambapo hadi kufikia Machi, 2024 watumishi 31 waliajiriwa. Sambamba na hilo, Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ili waweze kuongeza ujuzi na kuleta tija katika Utumishi wa Umma. Halikadhalika, katika kipindi hicho watumishi 136 wa Idara na Vitengo vya Wizara walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya Nchi, ambapo Watumishi 125 walipata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 11 walipata mafunzo ya muda mrefu.

176. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza azma ya Serikali kupitia mwongozo wa kufanya mazoezi mahala pa kazi, Wizara imeendelea kutekeleza mwongozo huo unaolenga kuimarisha Afya za Watumishi kwa kuandaa na kushiriki michezo mbalimbali ikiwemo bonanza na SHIMIWI. Michezo hiyo imekuwa chachu ya

kuhamasisha watumishi kufanya mazoezi ya viungo, kuimarisha afya na kupunguza hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukizwa. Vilevile, katika kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kuzuia na kudhibiti UKIMWI na magonjwa yanayoambukiza, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe; vifaa vya kujikinga na maambukizi; na semina na mafunzo mbalimbali juu ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza.

177. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kupambana na Kuzuia Rushwa wa Miaka Mitano (NACSAP 2021/22 - 2025/26) kwa kuendelea kutoa mafunzo ya maadili kwa watumishi kwa ajili ya kuzuia vitendo vya rushwa kupitia semina mbalimbali ili kuongeza uwajibikaji na uadilifu kwa watumishi. Aidha, katika kuhakikisha ubora na ufanisi wa utoaji huduma, Wizara inatekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Client Service Charter) ambao unalenga kuhabarisha umma na wateja juu ya huduma na viwango vinavyotolewa.

**B. 3: MASUALA MENGINE YALIYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

**Maboresho ya Sera, Sheria na Kanuni za Kisekta**

178. ***Mheshimiwa Spika,*** kisera masuala ya uchukuzi yameendelea kuongozwa kwa muda mrefu na Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003. Hata hivyo, kutokana na mtazamo wa Serikali na maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, Wizara ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Sera hiyo ili kuona mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha utekelezaji, hatua ya kuzitatua na kama sera hiyo inakidhi mahitaji ya sasa. Tathmini imekamilika mwishoni mwa mwezi Agosti, 2023. Pamoja na masuala mengine, tathmini hiyo imebaini kuwa kuna umuhimu wa kufanya mapitio ya sera husika kwa kuandaa sera ya sasa kulingana na mahitaji na maoni ya wadau. Baada ya hatua hiyo, Serikali imeanza maandalizi ya kuhuisha Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003 kwa hatua za awali ambapo kwa sasa ipo katika hatua za ununuzi wa Mtaalam Elekezi atakayeshirikiana na Wizara katika kuhuisha sera

husika.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendana na mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika utendaji wa Sekta ya Uchukuzi, Wizara imeendelea kufanya mapitio ya sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha utendaji wa Sekta. Kutokana na hali hiyo, Wizara imefanya marekebisho ya Sheria ya Reli Na. 10 ya mwaka 2017, Sura ya 170 kwa lengo la kuongeza wigo wa ushiriki wa Sekta Binafsi katika utoaji wa huduma za usafiri na kwa njia ya reli nchini. Marekebisho ya Sheria hii yaliidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Juni, 2023. Sheria hii sasa inawezesha Sekta Binafsi kushiriki katika utoaji wa huduma za usafirishaji wa mizigo na abiria kwa kutumia njia ya reli kwa kulipa tozo (access fee). Kupitia sheria hii Sekta Binafsi itaweza kununua vichwa vya treni na mabehewa na kusafirisha mizigo na abiria. Kwa sasa Wizara imekamilisha Kanuni zinazoainisha utaratibu utakaotumika kutekeleza suala hili. Utaratibu huo utaongeza ushindani baina ya watoa huduma na kasi ya utoaji wa shehena bandarini.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Zambia zimeendelea kushirikiana katika kufanya marekebisho ya Sheria ya TAZARA ya mwaka 1995 ili kuiwezesha TAZARA kujiendesha kwa tija zaidi. Juhudi mbalimbali zimeendelea kufanyika ili kuruhusu marekebisho ya sheria hiyo ikiwemo ziara ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoifanya nchini Zambia tarehe 25 Oktoba, 2023 ambapo katika kuhutubia Bunge la Zambia pamoja na mambo mengine, alisisitiza umuhimu wa wabunge wa Zambia kuunga mkono marekebisho hayo na kupitisha marekebisho ya Sheria ya TAZARA. Kwa sasa marekebisho yanaendelea, na lengo la Serikali zote mbili ni kuhakikisha marekebisho hayo yanakamilika ndani ya mwaka 2024.

181. ***Mheshimiwa Spika***, kwa lengo la kuboresha utendaji wa sekta na kuendana na mabadiliko, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake,

imeandaa Kanuni mpya na kufanya marekebisho katika kanuni mbalimbali za Sekta ya Uchukuzi. Miongoni mwa kanuni hizo ni: Kanuni za Uchunguzi wa Afya za Mabaharia, 2023 (The Merchant Shipping (Medical Examinations) Regulations, 2023; Kanuni za Ulinzi wa Mizigo na Usalama wa Huduma za Vituo vya Bandari (The Tanzania Shipping Agencies (Cargo Security and Safety of Terminal Operations) Regulations, 2023); Kanuni za Usajili wa Wasafirishaji, 2023 (The Tanzania Shipping Agencies (Shippers Registration) Regulations, 2023); Marekebisho ya Kanuni za Bandari Kavu, 2024 (The Tanzania Shipping Agencies (Dry Port) (Amendment), Regulations, 2024); Marekebisho ya Kanuni za Biashara za Meli, 2024 (The Tanzania Shipping Agencies (Shipping Business) (Amendment), Regulations, 2024); Kanuni za Matumizi ya Miundombinu ya Reli kwa Watoa Huduma Binafsi, 2024 (The Railways (Open Access) Regulations, 2024; Kanuni za Utoaji wa Vyeti, Leseni na Usajili wa Viwanja vya Ndege, 2023 (The Civil Aviation (Certification, Licensing and Registration of Aerodrome) Regulations, 2023) na Kanuni za Uwezeshaji wa Usafiri wa Anga (The Civil Aviation (Facilitation of Air Transport) Regulations, 2023).

182. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa lengo la kuimarisha ushirikiano baina ya nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) katika masuala ya usafiri wa anga hasa usalama, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi iliwasilisha hapa Bungeni mapendekezo ya kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya Mwaka 2009 (The Constitution of the African Civil Aviation Commission – AFCAC Constitution, 2009). Katiba hiyo iliridhiwa na Bunge lako Tukufu tarehe 30 Agosti, 2023 kupitia Azimio Na. 05/2023. Utekelezaji wa Katiba hiyo utaziwezesha Mamlaka za Usafiri wa Anga katika nchi wanachama wa AU kuwa na utaratibu wa kujadili na kupanga hatua zote zinazohitajika katika utekelezaji wa shughuli za usafiri wa anga yakiwemo masuala ya usalama wa anga.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na upungufu wa kisheria uliopo katika usimamizi, uendelezaji na uendeshaji wa viwanja vya ndege Tanzania Bara, Wizara iliwasilisha Serikalini mapendekezo ya kutungwa kwa sheria mahsusi kwa ajili ya suala hili. Baada ya

majadiliano ya kina ndani ya Serikali kwa taratibu zilizopo, mapendekezo ya kutungwa kwa sheria hiyo yaliridhiwa. Kwa sasa taratibu zinakamilishwa ili muswada huo uwasilishwe katika Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine, itasaidia na kuwezesha kuimarisha usimamizi wa huduma zitolewazo katika viwanja vya ndege nchini na kuchangia katika kuimarisha usalama wa usafiri wa anga.

**Ufuatiliaji na Tathmini**

184. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Uchukuzi imekuwa na utaratibu wa kufanya tathmini ya utendaji wake kila mwaka kwa kuendesha mkutano mahsusi wa mapitio wa shughuli zote za kisekta (Joint Transport Sector Review Meeting – JTSR). Katika mikutano hiyo wadau muhimu wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Wanazuoni na wadau kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali hushiriki na kufanya majadiliano kwa pamoja kuhusu kazi zote zilizofanyika kwa mwaka husika. Mkutano huo kwa mwaka 2023 ulifanyika tarehe 5 hadi 8 Disemba, 2023 na ulihudhuriwa na wadau zaidi ya 300. Pamoja na mambo mengine, mkutano huo hupitia masuala ya kisera, kiutendaji na kufanya mapitio ya utekelezaji wa maazimio ya mikutano iliyopita. Kupitia mikutano hiyo, Wizara imeweza kujipima kiutendaji kwa kujadili changamoto zinazoikabili Sekta ya Uchukuzi na kuweka mikakati ya kutatua changamoto hizo. Vilevile, Wizara imekuwa na utaratibu wa kufanya tathmini ya kiutendaji kwa Taasisi zake kupitia mikataba inayosainiwa baina ya Wizara na Taasisi hizo. Tathmini hiyo hufanyika katika masuala ya mbalimbali yakiwemo ya ufanisi katika ukusanyaji wa mapato; utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kimkakati; na utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha husika.

**Mifumo ya TEHAMA**

185. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuongeza ufanisi

na kutoa huduma kwa wakati. Vilevile, Tovuti ya Wizara imeboreshwa ili kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanapata taarifa mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Uchukuzi kwa wakati. Kufuatia kuimarika kwa mifumo ya TEHAMA, Wizara imepunguza matumizi ya shajala na hivyo kupunguza gharama za kudurufu nyaraka mbalimbali katika utendaji wa Wizara.

## B. 4: MAFANIKIO YA MIAKA MITATU (3) YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA UCHUKUZI

186. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na maelezo niliyoyatoa kuhusu utendaji wa Wizara kwa mwaka 2023/24, naomba kwa muhtasari niainishe baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Uchukuzi katika kipindi cha miaka mitatu (3) ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba miradi ya maendeleo ya sekta ya uchukuzi ni miongoni mwa miradi nchini ambayo katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutekelezwa bila kusuasua na kwa ufanisi mkubwa. Katika kipindi hicho, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ya maendeleo inayojumuisha: miradi ya reli; viwanja vya ndege; uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania; ujenzi na uboreshaji wa bandari; ujenzi na ukarabati wa meli katika maziwa makuu; ufungaji wa rada za hali ya hewa; na uboreshaji wa vyuo vya mafunzo vya kisekta. Utekelezaji wa miradi hiyo umechochea sekta nyingine za kiuchumi na kijamii katika kuwaletea wananchi maendeleo. Serikali imepata mafanikio mbalimbali katika kipindi cha Awamu ya Sita kama ambavyo nitaelezea kwa muhtasari.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni *kuendeleza Ujenzi wa Reli ya SGR kwa Kasi:* Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendeleza ujenzi wa reli ya kisasa kutoka **kilometa 722** zilizokuwa zinajengwa mwaka 2021 wakati anaingia madarakani hadi kufikia **kilometa 2,102** zinazojengwa mwaka huu wa 2024.

Hatua hii imewezekana baada ya Serikali yake kufanikisha kupatikana kwa fedha za kuendelea na kuanza ujenzi wa reli ya SGR kwa vipande vya: Makutupora hadi Tabora (km 368); Tabora hadi Isaka (km 165); Tabora hadi Kigoma (km 506); na Isaka hadi Mwanza (km 341). Kazi ya ujenzi katika vipande hivyo inaendelea na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

189. ***Mheshimiwa Spika,*** *kuongeza wigo wa Reli ya SGR kwa kuifanya kuwa ya kikanda***:** pamoja na uendelezaji wa reli hiyo, jambo kubwa ni kwamba Serikali hii imeweza kuanza mikakati ya kuifikisha reli ya SGR nje ya mipaka ya nchi kupitia ujenzi wa kipande cha Uvinza - Gitega ambacho ni mchepuo wa njia ya reli ya Tabora – Kigoma. Kutokana na ujenzi wa reli hii kuhudumia nchi zaidi ya moja umeifanya reli hii kuwa ya kikanda kwa kuhudumia nchi za Afrika Mashariki zikiwemo DRC, Rwanda, na Burundi. Aidha, katika kuhakikisha kuwa Sekta binafsi inashiriki kwa ufasaha katika uendeshaji wa reli nchini, Serikali imefanya marekebisho ya Sheria Na. 10 ya reli ya mwaka 2017 ili kushirikisha sekta hiyo kwenye uendeshaji na utoaji huduma za usafirishaji kupitia miundombinu ya reli. Lengo la ushirikishaji sekta binafsi ni kuwezesha Serikali kuhudumia shehena nyingi ikiwemo kuongeza ufanisi na ushindani utakaomwezesha mwananchi kupata Huduma ya uhakika, nafuu na bora zaidi.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** *kuendelea kuimarisha kimkakati Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL):* Katika kuimarisha usafiri wa anga nchini, ni jambo la kujivunia kuwa, Serikali imeweza kuongeza uwezo wa ATCL kwa kuinunulia ndege mpya 15 tangu kuanza kwa utekelezaji wa Mpango wa Ufufuaji mwaka 2016. Ununuzi wa ndege hizo umeifanya ATCL kuwa na jumla ya ndege 16 ikijumuisha ndege yake ya zamani ya Dash 8Q300. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, zimenunuliwa jumla ya ndege saba (7) kati ya ndege 15 mpya zilizonunuliwa tangu kuanza kwa ufufuaji wa ATCL. Aidha, ndege sita (6) kati ya hizo saba (7) zimewasili na ndege moja (1) inatarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwezi Mei, 2024. Kutokana na hatua hizo, ATCL imeweza kuongeza mtandao wa safari zake za

kutoa huduma hadi kufikia jumla ya vituo 24 vya ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na vituo 19 vilivyokuwepo mwaka 2021. Vilevile, abiria wameongezeka hadi kufikia abiria 1,070,734 mwaka 2023 ikilinganishwa na abiria 537,155 waliosafirishwa mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 99.33. Aidha, uboreshaji huo wa usafiri wa anga umechochea ukuaji wa kiuchumi katika sekta nyingine zikiwemo Utalii na Biashara.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** *kuendelea kuboresha kwa kasi huduma za meli:* Tangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, yafuatayo yamefanyika katika kuboresha utoaji wa huduma za meli nchini:-

i. Kuendelea kwa ufanisi na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu ambao hadi Machi, 2024 umefikia asilimia 95 kutoka asilimia 40 ya mwaka 2021 na mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2024;

ii. Kuanzishwa kwa miradi miwili ya ukarabati wa meli ambayo ni: Ukarabati wa meli ya kubeba mabehewa ya MV. Umoja ambao ulianza kutekelezwa mwezi Novemba, 2021 na kukamilika mwezi Septemba, 2023; na Ukarabati wa meli ya kubeba shehena ya mafuta katika Ziwa Tanganyika iitwayo MT. Sangara ambao hadi kufikia Machi, 2024 umefikia asilimia 92 ya utekelezaji wake; na

iii. Kusainiwa kwa mikataba ya miradi mipya sita (6) mwishoni mwa mwaka 2023 yenye thamani ya Shilingi bilioni 674.32. Miradi hiyo ipo katika hatua za awali za utekelezaji na inahusu ujenzi wa: kiwanda cha kujengea meli (shipyard) katika Ziwa Tanganyika; meli kubwa ya kubeba mizigo (RoRo & Wagon ferry) yenye uwezo wa kubeba tani 3,500 za mizigo; na meli nyingine ya kubeba shehena ya mizigo (RoRo & Wagon ferry) katika Ziwa Victoria yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mizigo. Pia, kuna miradi ya ukarabati wa meli ya MV. Liemba

iliyoko Ziwa Tanganyika pamoja na ukarabati wa meli za MT. Ukerewe na MT. Nyangumi zilizoko Ziwa Victoria.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** *kutekeleza kwa vitendo mipango ya uboreshaji wa bandari nchini:* Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuboresha utendaji wa bandari nchini. Pamoja na manufaa mengine, usafirishaji mizigo bandarini umeongezeka kutoka tani milioni 17.69 mwaka 2020/21 hadi kufikia tani milioni 24.89 mwaka 2022/23. Pamoja na mafanikio hayo, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi imeendelea kushirikisha sekta binafsi kwa kuingia ubia na Kampuni ya DP World katika kuendeleza na kuendesha baadhi ya maeneo ya Bandari ya Dar es Salaam. Kwa sasa hatua mbalimbali zikiwemo za makabidhiano na *mobilization* zinaendelea ili kuruhusu utekelezaji rasmi kuanza. Lengo ni Tanzania kuwa kitovu cha usafirishaji wa shehena na kuongeza tija katika utendaji wa bandari zetu ili kuziwezesha zichangie zaidi katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu na maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** *kufungua fursa zaidi katika Viwanja vya Ndege na nchi kushamiri Kimataifa katika usafiri wa anga:* Kwa upande wa usafiri wa anga, chini ya uongozi wa Awamu ya Sita, Serikali imeweza kushamiri kimataifa kutokana na kaguzi zilizofanyika. Mathalan, kupitia ukaguzi wa mwisho wa Ulinzi (security audit) uliofanywa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) mwishoni mwezi Mei, 2023 ambapo Viwanja vya Ndege vya Kimataifa vya Julius Nyerere - JNIA na Abeid Amani Karume vilikaguliwa, nchi yetu ilifanikiwa kupata ufaulu wa asilimia 86.70 na kuwa nchi ya nne (4) barani Afrika kwa ubora.

194. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imefungua fursa mbalimbali kwa: kuanzishwa kwa kiwanda cha kuunganisha na kutengeneza ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Morogoro; na kuboresha viwanja mbalimbali vya ndege nchini ikiwa ni pamoja na kuviwekea taa za kuongozea ndege ili kutoa huduma kwa saa 24.

195. ***Mheshimiwa Spika,*** *kuboresha Vyuo chini ya Wizara:* Pamoja na shughuli hizo, Serikali ya Awamu ya Sita imeendeleza vyuo vilivyo chini ya Wizara ambavyo ni Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam (DMI) kwa kuvinunulia vifaa vya kisasa vya kufundishia vikiwemo ndege za mafunzo kwa NIT na *Full Mission Crane Simulator* kwa Chuo cha DMI. Katika Awamu hii, vyuo hivi vimeendelea kuboreshwa ili kuweza kutoa mafunzo kwa ufanisi zaidi. Mathalan, Chuo cha NIT hadi Machi 2024, kinatoa mafunzo ya kozi ndefu 55 ikilinganishwa na kozi 33 zilizotolewa katika Mwaka wa Masomo 2021/22 ikiwa ni ongezeko la kozi 22. Kwa sasa, Chuo kina wanafunzi wa kozi ndefu 16,131 ikilinganishwa na wanafunzi 12,942 katika Mwaka wa Masomo 2021/22 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 3,189.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** *kuweka historia ya kuanzisha Mafunzo ya urubani nchini kwa mara ya kwanza:* Kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa ikitumia fedha nyingi kusomesha marubani nje ya nchi, hali iliyofanya kuwepo na uchache mkubwa wa marubani na hivyo kuwaajiri kwa gharama kubwa. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, chini ya Uongozi Mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kitaanza rasmi kutoa mafunzo ya urubani ifikapo mwezi Septemba, 2024. Kwa sasa, Chuo kinaendelea kukamilisha taratibu mbalimbali za kuanza mafunzo hayo zikiwemo za kupata ithibati ya kuendesha mafunzo husika.

197. ***Mheshimiwa Spika,*** *kuondoa foleni ya Malori katika Mpaka wa Tunduma:* Kufuatia ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Rais aliyofanya Nchini Zambia tarehe 23-25 Oktoba, 2023 pamoja na mambo mengine, Marais wa nchi hizo mbili waliagiza kuchukuliwa hatua za haraka za kuondosha msongamano wa malori katika Mpaka wa Tunduma/Nakonde ikiwemo kuhuisha mifumo ya forodha kusomana. Katika kulitekeleza agizo hilo, Serikali kwa kuhusisha wadau mbalimbali imefanikiwa kuondoa foleni katika Mpaka wa Tunduma, hatua iliyoleta ufanisi mkubwa wa kibiashara. Kituo cha Forodha cha Tunduma huvusha mizigo kutoka Tanzania kwenda Zambia, DRC na Zimbabwe ambapo inakadiriwa

Mpaka huo unavusha zaidi ya magari ya mizigo kwa wastani wa malori 1,200 kwa siku. Kituo hicho cha forodha kilikuwa na changamoto ya foleni ambapo malori yalikuwa yakitumia muda mrefu kuvuka Mpaka huo kutokana na mifumo ya vibali kutosomana. Sambamba na hilo, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu na mifumo ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi na ushindani wa Bandari ya Dar es Salaam katika kupunguza muda wa safari za malori yanayovuka Mpaka wa Tunduma.

198. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio hayo ya miaka mitatu (3), Wizara pia imepata mafanikio katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024 kama ifuatavyo:-

i. Kupokelewa kwa vichwa tisa (9) vya treni vya umeme na mabehewa 65 ya abiria kwa ajili ya uendeshaji wa reli ya SGR, vichwa vya treni tayari vimeanza majaribio;

ii. Kukamilika ukarabati wa mabehewa 285 ya mizigo kati ya mabehewa 600 na mabehewa 28 ya abiria kati ya mabehewa 37 na tayari yameanza kutoa huduma, hatua hii inasaidia kuboresha huduma za usafirishaji wa mizigo kwa njia ya reli iliyopo ya MGR;

iii. Kuendelea kwa ukarabati wa njia ya reli iliyopo ya MGR wa kipande cha Tabora – Kigoma (km 411) ambapo maandalizi ya kuanza ukarabati wa kipande hiki yanaendelea na ukarabati wa kipande cha Kaliua – Mpanda (km 210) umefikia asilimia 11;

iv. Wizara kupitia TPA imeendelea na jukumu la kuitangaza bandari kimasoko, kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika uendeshaji wa shughuli za bandari. Kupitia juhudi hizo, hadi kufikia Machi, 2024 TPA ilitoa huduma za bandari kwa kuhudumia jumla ya tani milioni 20.72 za shehena ya mizigo ikilinganishwa na tani milioni 14.56 ya shehena ya mizigo iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 42.31;

v. TASAC imeendelea kufanya kaguzi za usalama kwa meli kubwa zenye ujazo wa tani 50 na zaidi na vyombo vidogo vyenye ujazo wa shehena chini ya tani 50 ili kuhakikisha kuwa ni salama na zinaendeshwa na mabaharia wenye sifa katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Mwanza, Kigoma, Kagera, Mara, Mbeya, Pwani, Lindi, Tanga, Kigoma, Rukwa, Geita, Dodoma na Morogoro. Kutokana na kaguzi hizo, vyeti vya ubora vilitolewa kwa vyombo vilivyothibitika kukidhi matakwa ya kiusalama na vyombo vilivyobainika kuwa na kasoro, maelekezo yalitolewa ikiwa ni pamoja na kuvisimamisha vyombo husika kutoa huduma;

vi. Kuendelea na ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uratibu wa Masuala ya Utafutaji na Uokozi katika Ziwa Victoria (Maritime Rescue Cordination Centre – MRCC - Mwanza) ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 26. Kituo hicho kitaimarisha usalama wa usafirishaji, usalama wa watu na vyombo vya usafiri katika Ziwa Victoria;

vii. TCAA ilihuisha Daftari la Usajili wa Ndege na kufikia Ndege 419 zikijumuisha Ndege 15 zilizosajiliwa katika kipindi husika na kuondoa ndege mbili (2) baada ya kumalizika kwa mikataba ya ukodishaji;

viii. Kukamilisha ujenzi wa uzio kwa ajili ya usalama katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma wenye urefu wa kilometa 7.2 na ufungaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege ambapo kwa sasa kiwanja kina uwezo wa kuhudumia ndege kwa saa 24;

ix. Kukamilika kwa usanifu wa kina wa mnara wa kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Bukoba;

x. Kuanza kutoa huduma kwa ndege ya mizigo aina ya Boeing 767-300F ambapo kumechochea biashara nchini;

xi. Kuendelea kusimamia kwa ufanisi masuala ya hali ya hewa nchini na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kukamilisha ufungaji wa rada mbili (2) za hali ya hewa katika Mikoa ya Kigoma na Mbeya;

xii. Kukamilika ufungaji wa Mtambo Maalum wa kisasa (Full Mission Crane Simulator) wa kufundishia kwa vitendo kuhudumia mizigo kwenye meli na vyombo vingine vya usafirishaji na umeongeza thamani ya elimu inayotolewa katika Chuo cha DMI;

xiii. Serikali kupitia LATRA na Jeshi la Polisi imeendelea kuimarisha udhibiti ili kuimarisha usalama kwa mabasi yanayosafiri usiku kwa kuendelea kufanya ufuatiliaji wa safari za mabasi wakati wote kupitia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Mabasi (VTS). Pamoja na manufaa mengine, kuruhusu mabasi kusafiri usiku kumeleta chachu mpya katika kufanya biashara na kupongezwa na wadau wengi kutokana na kuokoa muda wa kusafiri, hususan kwa safari za mikoani;

xiv. Serikali imeridhia kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania ya mwaka 2023. Taratibu zinakamilishwa ili kuwasilisha muswada husika Bungeni; na

xv. Serikali iliendelea kusimamia viwanja vyake, kikiwemo Kiwanja cha KIA ambapo kiwanja hicho kilifikia miruko ya ndege 15,088 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 6.50 ikilinganishwa na miruko ya ndege 14,167 iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/23.

## B. 5: CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUZITATUA

199. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2023/24, Wizara ya Uchukuzi inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo na mikakati ya kuzitatua ni: -

### i. Mabadiliko ya tabianchi

Mabadiliko ya tabianchi (Climate Change) yanayosababisha mifumo ya hali ya hewa kubadilika mara kwa mara na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya uchukuzi kutokana na mafuriko hususan miundombinu ya reli.

**Mkakati**

Kuendelea kuimarisha huduma za hali ya hewa ikiwemo kufunga Rada za hali ya hewa na kuongeza mtandao wa vituo vya hali ya hewa ili kuongeza usahihi wa utoaji wa tahadhari ya matukio ya hali mbaya ya hewa; na kufanya tafiti mbalimbali zitakazosaidia kubaini athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwa ajili ya usanifu wa miundombinu stahiki.

**ii. Mdororo wa uchumi wa Dunia**

Mdororo wa uchumi wa Dunia unaoathiri shughuli za usafiri na usafirishaji nchini.

**Mkakati**

Kuendelea kuchukua tahadhari za athari za mdororo wa uchumi wa dunia kwa kuweka mikakati ya kukabiliana nazo pindi zinapotokea ili kutoleta madhara zaidi katika huduma za usafiri na usafirishaji.

**iii. Mfumuko wa bei ya mafuta (Petroli na Dizeli) na mitambo**

Kumekuwepo na mfumuko wa bei ya mafuta (Petroli na Dizeli) na mitambo inayotumika katika vyombo vya usafiri na usafirishaji nchini na hivyo kuathiri shughuli za uendeshaji na utoaji wa huduma vikiwemo kupanda kwa viwango vya nauli nchini.

**Mkakati**

Kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati ya gesi asilia (CNG na LNG) katika vyombo vya usafiri nchini ili kupunguza matumizi ya mafuta (Petroli na Dizeli).

**iv. Mahitaji Makubwa ya Fedha za Utekelezaji wa Miradi**

Miradi mingi ya uchukuzi kuhitaji fedha nyingi (capital intensive) katika utekelezaji wake. Mathalan, Mradi wa SGR utagharimu takriban Shilingi trilioni 23 hadi kukamilika kwake.

**Mkakati**

Kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kutekeleza baadhi ya miradi inayohitaji uwekezaji mkubwa na hivyo kupunguza gharama kwa Serikali.

**v. Uchache wa wataalam wa kada maalum, hususan marubani na wahandisi ndege**

Sekta ya Uchukuzi inakabiliwa na uchache wa wataalam katika nyanja mbalimbali za usafiri na usafirishaji, zikiwemo usafiri kwa njia ya anga na majini.

**Mkakati**

Wizara kupitia Vyuo vyake vya Kisekta kuendelea kuwezesha uzalishaji wa wataalam wa kada maalum katika usafiri wa majini na anga wakiwemo mabaharia, marubani na wahandisi ndege kupitia Vyuo vyake vya DMI na NIT.

**vi. Uvamizi na uharibifu kwa miundombinu ya usafiri**

Uvamizi na uharibifu kwa miundombinu ya usafiri ikiwemo reli hususan mataruma, vifungio na madaraja ya reli.

**Mkakati**

Kuendelea kushirikiana na vyombo vya dola pamoja na jamii inayozunguka kutoa elimu ya athari za uvamizi, uharibifu na hujuma za miundombinu ya usafiri ikiwemo miundombinu ya reli ili kujenga uwezo wa jamii inayozunguka miundombinu kuwa walinzi wa miundombinu.

## C: MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

200. ***Mheshimiwa Spika,*** Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2024/25, hususan bajeti ya miradi ya maendeleo ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati inayoendelea yenye lengo la kuhakikisha kuwa huduma za uchukuzi nchini zinakuwa zenye usalama; uhakika na gharama nafuu.

201. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Uchukuzi (Fungu 62) imetengewa jumla ya **Shilingi 2,729,676,417,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 114,744,476,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,614,931,941,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotengwa zinajumuisha **Shilingi 86,661,930,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 28,082,546,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Vilevile, Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotengwa zinajumuisha **Shilingi 2,524,369,202,000** fedha za ndani na **Shilingi 90,562,739,000** fedha za nje.

**Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2024/25**

202. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/25 inajumuisha miradi ya Wizara inayoendelea ikiwemo miradi ya kielelezo ya ujenzi wa reli ya SGR na ufufuaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL). Aidha, miradi ya kimkakati inajumuisha miradi ya kuziwezesha Taasisi kiutendaji; miundombinu ya viwanja vya ndege; miundombinu ya bandari; ukarabati wa reli iliyopo; ujenzi na ukarabati wa meli;

ununuzi wa rada za hali ya hewa; ununuzi wa boti za uokoaji; ununuzi wa mitambo ya mawasiliano baina ya waongoza ndege na marubani; na miundombinu na vifaa vya kufundishia.

**Mradi wa Kuwezesha Taasisi (Institutional Support)**

203. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 32.33** fedha za ndani. Kazi zitakazotekelezwa ni:-

i. Uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria JNIA;

ii. Ulipaji fidia kwa maeneo ya viwanja vya ndege;

iii. Ununuzi wa Mshauri Elekezi wa ujenzi wa kituo cha mafunzo ya usalama katika uchimbaji wa mafuta na gesi baharini;

iv. Kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kituo cha mafunzo ya usalama katika uchimbaji wa mafuta na gesi baharini; ununuzi wa Mshauri Elekezi kwa ajili ya kusimamia ujenzi wa miundombinu ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam katika eneo la Kimbiji Wilayani Kigamboni, Dar es Salaam; na

v. Kusimamia ujenzi wa miundombinu ya Chuo cha Bahari katika eneo la Kimbiji Wilayani Kigamboni, Dar es Salaam.

**Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha**

204. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 5.08** fedha za ndani kwa ajili ya ufungaji wa Mfumo wa Taa za Kuongozea Ndege; ujenzi wa Karakana ya Matengenezo ya Ndege ya Kilimo Anga; na ujenzi wa tabaka la juu la lami la barabara ya kuruka na kutua ndege**.**

**Mradi wa Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa**

205. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu

umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 21.09** fedha za ndani kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Lindi; ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi; ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Singida; Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Kiwanja cha Ndege cha Njombe kwa Daraja 4E; na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kiwanja kipya cha Ndege cha Serengeti. Aidha, Kiwanja cha Ndege cha Serengeti kitajengwa kwa kuzingatia mazingira (ecosystem) na kujulikana kama *Green International Airport* na kitafungamanisha Sekta ya Utalii na kuchagiza shughuli za utalii kwa kuwa kiunganishi na viwanja vya ndege vya kimataifa nchini.

**Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

206. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 15.00** fedha za ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa kazi mbalimbali katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ukiwemo Ujenzi wa Jengo la Abiria na miundombinu yake.

**Mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba**

207. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 3.46** fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la kuongozea ndege na usimikaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege; na kuanza zoezi la utwaaji ardhi katika eneo la Omukajunguti kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja kipya cha Ndege cha Mkoa wa Kagera.

**Mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

208. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 7.30** fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria, jengo la kuongozea ndege, kituo cha zimamoto na kituo cha hali ya hewa.

**Mradi wa Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro – KIA**

209. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu ambao utatekelezwa kupitia TAA umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 50.00** fedha za ndani kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa njia ya kuruka na kutua ndege pamoja na mfumo wa taa za kuongozea ndege; kujenga jengo la wageni mashuhuri; kujenga jengo la watendaji na watoa huduma KIA; kukarabati jengo la abiria la sasa; na kukarabati jengo la kuhifadhia mizigo.

**Mradi wa Uboreshaji na Upanuzi wa Jengo la Pili la Abiria JNIA**

210. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 6.60** fedha za ndani kwa ajili ya Uboreshaji na Upanuzi wa Jengo la Pili la Abiria; uboreshaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege; na ujenzi wa eneo maalum la usalama kwenye barabara ya kuruka na kutua ndege.

**Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Usafiri katika Ziwa Victoria (Multinational Lake Victoria Maritime Communications and Transport - MLVMCT Project).**

211. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 1.78** fedha za nje kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kukamilisha ujenzi wa vituo 3 vya utafutaji na uokoaji (Nansio – Ukerewe, Musoma Mjini, Kanyala – Sengerema);

ii. Ununuzi wa boti tatu (3) za utafutaji na uokoaji;

iii. Kuwezesha utekelezaji wa kazi za mradi kupitia Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi (PIU);

iv. Kuwezesha gharama za uendeshaji wa Taasisi Tendaji (National Executing Agency - NEA) wakati wa Utekelezaji na Ufuatiliaji wa kazi za mradi;

v. Kuwezesha Kaguzi za ndani, Kaguzi Maalum na Kaguzi za nje za mradi; na

vi. Kuwezesha ujenzi wa vichanja vya wanawake kwa ajili ya kukaushia Samaki (Katete – Chato, Magarini - Muleba, Kibarastoo – Bunda na Bukima – Musoma).

**Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam (DMGP)**

212. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 51.10** fedha za nje kwa ajili ya uboreshaji na usimamizi wa Gati Na. 8 –11; upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Gati Na. 12 -15; ufungaji wa Mfumo wa Umeme na uboreshwaji wa eneo la kuhudumia shehena katika Gati Na. 1 – 7; maboresho ya Gati la Malindi; na kufanya ukaguzi wa kitaalam wa mradi wa DMGP.

**Mfuko wa Reli (Railway Infrastructure Fund)**

213. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2024/25, Mfuko wa Reli *(Railway Infrastructure Fund)* unatarajia kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 294.80** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea na ukarabati na matengenezo ya njia ya reli iliyopo ya Meter Gauge Railway (MGR);

ii. Kuendelea na ununuzi na ukarabati wa vitendea kazi vitakavyotumika kutoa huduma katika njia ya reli ya MGR;

iii. Kuendelea na uboreshaji wa mifumo ya ishara, mawasiliano na umeme katika njia ya reli ya MGR;

iv. Kuendelea na uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA;

v. Kuendelea na uwekaji wa uzio na alama katika maeneo ya reli; na

vi. Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ukarabati reli ya MGR kipande cha Kilosa – Kidatu (km 108).

**Mradi wa Ujenzi wa Reli ya SGR**

214. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 1,511.00** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kukamilisha ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (Km 300);

ii. Kukamilisha ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Morogoro - Makutupora (Km 422);

iii. Kuendelea na ujenzi wa njia ya reli ya SGR kwa kipande cha Makutupora – Tabora (Km 368);

iv. Kuendelea na ujenzi wa njia ya reli ya SGR kwa kipande cha Tabora - Isaka (Km 165);

v. Kuendelea na ujenzi wa njia ya reli ya SGR kwa kipande cha Mwanza-Isaka (Km 341);

vi. Kuendelea na ujenzi wa njia ya reli ya SGR kwa kipande cha Tabora - Kigoma (Km 506);

vii. Kuanza ujenzi wa njia ya reli ya SGR kwa kipande cha Uvinza-Musongati (Km 156.6);

viii. Kuendelea na ununuzi wa vitendea kazi (Vichwa vya treni, mabehewa, mitambo na mashine za matengenezo ya njia);

ix. Kuendelea kuwezesha mafunzo ya wataalam wa usimamizi na uendeshaji wa reli ya SGR;

x. Kugharamia uendeshaji wa awali wa reli ya SGR kutoka Dar es Salaam - Dodoma; na

xi. Kuendelea kubuni na kutekeleza mikakati ya kuzalisha na kutafuta mizigo kwa ajili ya reli ya SGR.

**Mradi wa Ukarabati wa Reli ya MGR - Tanzania Intermodal Rail Project – TIRP II**

215. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 17.23** fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea na ukarabati wa njia ya reli ya MGR kipande cha Dar es Salaam-Tabora (Km 257.4);

ii. Kuendelea na ukarabati wa njia ya reli ya MGR kipande cha Tabora – Isaka (Km 135);

iii. Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya reli ya Kilosa-Mikumi (Km 108) na Tanga – Arusha (Km 626);

iv. Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya reli ya Kilosa-Gulwe-Igandu; na

v. Kuwezesha huduma za ushauri (Consultancy) na wataalam katika utekelezaji wa mradi.

**Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga**

216. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 23.20** fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Utawala; ujenzi wa jengo moja (1) lenye sakafu (4) (madarasa) pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufundishia; ujenzi wa jengo la hosteli; ujenzi wa ukumbi wa mikutano na mgahawa wa chakula; na kufanya utafiti ili kubaini fursa na changamoto katika usafiri wa anga nchini.

**Mradi wa Ukarabati wa Reli ya TAZARA pamoja na Maeneo Mahsusi Kibiashara**

217. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 13.69** fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zifuatazo:-

i. Kukamilisha ununuzi wa Tamping Machine;

ii. Kununua vipuri vya injini 15 za njia kuu;

iii. Kununua vipuri na kukarabati injini moja (1) ya kupangia mabehewa (shunting engine);

iv. Kukarabati mabehewa 100 ya mizigo na mabehewa 30 ya abiria; na

v. Kununua mzani wa kupimia mabehewa ya mizigo katika Mpaka wa Tunduma na kujenga njia mbili (2) za reli katika Stesheni ya Tunduma.

**Mradi wa Rada, Vifaa na Miundombinu ya Hali ya Hewa**

218. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 15.00** fedha za ndani. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kukamilisha malipo ya uundaji wa Rada zitakazofungwa Dodoma na Kilimanjaro pamoja na ujenzi wa miundombinu ya Rada hizo;

ii. Ununuzi wa vifaa vya hali ya hewa pamoja na mitambo ya mawasiliano;

iii. Kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi ya Kanda ya Mashariki pamoja na Kituo cha Tahadhari ya Matukio ya Tsunami;

iv. Kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya TMA Jijini Dodoma;

v. Ujenzi wa kituo kimoja cha hali ya hewa kilimo;

vi. Ukarabati wa vituo viwili (2) vya hali ya hewa;

vii. Kukamilisha malipo pamoja na ufungaji wa vifaa vya uangazi katika Bahari ya Hindi vitakavyofungwa Zanzibar, Dar es Salaam na Bagamoyo; na

viii. Kuboresha mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato.

**Mradi wa Ufufuaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)**

219. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 324.50** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali zikiwemo:-

i. Kuwezesha malipo ya ununuzi wa ndege tatu (3) mpya ambazo ni: ndege moja (1) ya masafa ya kati, moja (1) ya masafa mafupi na moja (1) ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 23;

ii. Ununuzi wa injini moja (1) ya ziada kwa ajili ya ndege aina ya Boeing 737- 9 Max;

iii. Kuwezesha malipo ya gharama za awali za uendeshaji wa ndege ndogo moja (1) aina ya Dash 8 Q400;

iv. Ukarabati wa Karakana za JNIA na KIMAFA;

v. Ujenzi wa karakana mpya ya ndege JNIA;

vi. Ukarabati wa Ofisi za ATCL zilizoko Terminal I;

vii. Ujenzi wa Jengo la Ofisi za ATCL Dodoma;

viii. Kukamilisha ukarabati wa nyumba 38 zilizoko KIA;

ix. Kufanya ukarabati wa nyumba za ATCL zilizoko Johannesburg na Lusaka;

x. Kujenga jengo la kuhifadhi mizigo katika uwanja wa JNIA, KIA na Mbeya; na

xi. Kujenga jengo la kuhifadhi vipuri, huduma za ndani ya ndege na mafunzo.

**Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu**

220. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 190.00** fedha za ndani. Fedha hizi ni kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ambayo inajumuisha:-

i. Kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,500 katika Ziwa Tanganyika;

ii. Kuanza ujenzi wa meli mpya ya abiria 600 na mizigo tani 400 katika Ziwa Tanganyika;

iii. Kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 katika Ziwa Victoria;

iv. Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya ya mizigo katika Bahari ya Hindi; na

v. Kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha kujengea meli chenye uwezo wa kuhimili meli zenye uzito wa tani 5,000 katika Ziwa Tanganyika.

221. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ukarabati wa meli zilizopo katika Maziwa Makuu kupitia mradi huo, Serikali kupitia MSCL itakamilisha ukarabati wa meli ya MT. Sangara na kuendelea na ukarabati

wa meli za MV. Liemba na MV. Mwongozo zilizopo katika Ziwa Tanganyika; ukarabati wa meli ya MT. Ukerewe na MT. Nyangumi zilizopo katika Ziwa Victoria. Aidha, Serikali kupitia MSCL itafanya ununuzi wa wahandisi washauri kwa ajili ya kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa meli; maboresho ya mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato; kugharamia mahitaji ya awali ya uendeshaji kwa meli za MV. Mwanza na MT. Sangara (Start up cost); ununuzi wa boti za uokozi nne (4) katika Maziwa Makuu kutokana na matakwa ya kiusalama na miongozo ya kimataifa ya usafirishaji wa abiria na mizigo, ambayo inaelekeza watoa huduma kwa njia ya maji ikiwemo MSCL kuwa na boti hizo. Pia, MSCL itafanya Upembuzi Yakinifu wa miradi na kuwezesha kufanya utafiti wa maendeleo ya biashara; ununuzi wa mabehewa 44 ya kusafirishia mizigo na uboreshaji wa miundombinu ya meli ikiwemo *floating Docks* na *Slipways* katika Bandari za Mwanza.

**Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Mawasiliano ya Ndege (VHF Navigation Aids)**

222. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 2** fedha za ndani kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa mitambo ya uongozaji ndege (Doppler Very High Frequency Omnidirectional Radio Range (DVOR)/Distance Measuring Equipmet (DME).

**Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu na Ununuzi wa Vifaa vya Kufundishia - Infrastructure Development and Training Equipment (NIT)**

223. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 9.30** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea na ujenzi wa Jengo la Kituo cha Rasilimali Mafunzo (Maktaba) katika Kampasi ya Mabibo - Dar es Salaam;

ii. Ujenzi wa Kituo Atamizi cha Mafunzo ya wataalam Mahiri wa Usafiri Majini Mkoani Lindi;

iii. Ununuzi wa Ndege mbili (2) zenye injini moja (1) kwa ajili ya Mafunzo ya Urubani (Awamu ya Kwanza);

iv. Ununuzi wa kifaa Maalum cha kufundishia wahudumu wa ndani ya ndege namna bora ya kufunga na kufungua mlango wa ndege (Door Trainer for Boeing B787-800); na

v. Ununuzi wa mafuta ya ndege na vilainishi kwa ajili ya ndege za mafunzo na matengenezo ya ndege za mafunzo ya urubani.

**Mradi wa East African Skills for Transformation and Regional Intergration Project (EASTRIP)**

224. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, mradi huu umetengewa bajeti ya jumla ya **Shilingi bilioni 20.44** fedha za nje kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa kazi zifuatazo:-

i. Kuanza ujenzi wa miundombinu ya Kituo cha Umahiri katika Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirishaji katika kampasi ya KIA (karakana ya matengenezo ya ndege, nyumba ya wakufunzi na hosteli za wanafunzi wa urubani);

ii. Kukamilisha ujenzi wa majengo matano (5) ya Kituo cha Umahiri katika Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirishaji katika Kampasi ya Mabibo - Dar es salaam;

iii. Ununuzi wa samani kwa ajili ya majengo matano (5) katika Kampasi ya Mabibo-Dar es Salaam pamoja na Majengo matatu (3) yatakayojengwa katika Kampasi ya KIA;

iv. Ununuzi wa vifaa vya kisasa vya mafunzo ya urubani na uhandisi wa matengenezo ya ndege, *multimedia* na TEHAMA kwa ajili ya maabara, madarasa na ofisi katika Kampasi za Mabibo – Dar es salaam na KIA - Kilimanjaro;

v. Utoaji wa huduma (Outreach) kwa wadau wa Sekta ya Uchukuzi pamoja na taasisi zingine zisizonufaika na mradi moja kwa moja; na

vi. Kuandaa na kuhuisha mitaala pamoja na miongozo ya kufundishia ili kukidhi mahitaji ya soko na miradi ya kimkakati ya Serikali katika sekta ya uchukuzi na usafirishaji.

**Kazi nyingine zitakazotekelezwa kupitia Mapato ya Ndani ya Taasisi kwa mwaka 2024/25**

225. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi zilizo chini ya Wizara pia zitatekeleza shughuli mbalimbali kwa kutumia mapato ya ndani ya Taasisi hizo katika kuboresha huduma za Sekta ya Uchukuzi.

**Udhibiti wa Usafiri wa Anga**

226. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 98.70** kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani vitokanavyo na huduma za udhibiti na uongozaji ndege katika anga la Tanzania. Fedha hizo zitatumika kutekeleza kazi kama ifuatavyo: -

i. Kuendelea kuboresha huduma za uongozaji ndege kwa kuboresha mitambo ya uongozaji ndege katika viwanja na vituo vyenye mitambo hiyo;

ii. Kuimarisha udhibiti wa sekta kwa kuendelea kufanya mapitio ya kanuni ili kuhakikisha anga letu linaendelea kuwa salama;

iii. Kuboresha mifumo ya kielektroniki ili kuimarisha na kuleta ufanisi katika shughuli za udhibiti na ukusanyaji wa mapato; na

iv. Kufanya tafiti ili kubaini fursa za uwekezaji kwenye sekta ya usafiri wa Anga ili kuvutia mashirika ya kimataifa ya usafiri wa anga.

**Udhibiti wa Usafiri Ardhini**

227. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) katika mwaka wa fedha 2024/25 itakusanya jumla ya **Shilingi bilioni 43.89** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani ili kudhibiti huduma za usafiri ardhini katika sekta ndogo za reli, barabara na waya. Fedha hizo zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea kutoa na kusimamia masharti ya leseni kwa watoa huduma wanaodhibitiwa;

ii. Kufanya ukaguzi wa miundombinu pamoja na mitambo ya reli ili kuhakiki usalama pamoja na ubora wake;

iii. Kufanya ukaguzi wa mitambo ya reli kabla na baada ya kuingia nchini ili kuhakiki na kuthibitisha usalama na ubora wake kwa ajili ya matumizi;

iv. Kufanya uchunguzi wa ajali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kubaini vyanzo vya ajali na kuchukua hatua madhubuti ili kuzuia ajali hizo kujirudia;

v. Kufuatilia uzingatiaji wa utunzaji mazingira kwa vyombo vya usafiri vya kibiashara wakati vikiwa safarini pamoja na watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa;

vi. Kuendelea kufanya tafiti mbalimbali kwa lengo la kusaidia ukuaji wa sekta na kufanya maamuzi sahihi ya kiudhibiti;

vii. Kukuza matumizi ya TEHAMA katika kusimamia huduma zinazodhibitiwa na huduma zitolewazo na Mamlaka ili kuongeza ufanisi, uwazi na urahisi wa upatikanaji wa huduma;

viii. Kufuatilia upatikanaji wa huduma bora na salama kwa wananchi pamoja na kuimarisha ushindani wa utoaji huduma za usafiri wa ardhini;

ix. Kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma na masuala ya udhibiti wa usafiri ardhini;

x. Kuwajengea uwezo watumishi ili waweze kukuza weledi na ujuzi wa kutekeleza majukumu ya Mamlaka kwa ufanisi na kwa kuwajali wateja;

xi. Kuendelea kushirikisha wadau wa huduma za usafiri ardhini, hususan sekta binafsi kwa lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji na utoaji huduma kwa watumiaji;

xii. Kuandaa kanuni za udhibiti usafiri kwa njia ya waya na kuweka mazingira ya kuvutia wawekezaji katika usafiri huo (Cable Cars Transport) hususan katika maeneo yenye vivutio vya utalii; na

xiii. Kuendelea kushirikiana na Taasisi za kikanda na Kimataifa katika masuala ya usafiri ardhini.

**Huduma za Usafiri kwa Njia ya Reli**

228. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) inatarajia kukusanya **Shilingi bilioni 118.89** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani kwa kusafirisha tani za mizigo 523,358, abiria 514,867 wa masafa marefu, abiria 2,315,551 wa masafa mafupi jijini Dar es Salaam kwa kutumia reli ya MGR na abiria 1,990,656 kwa kutumia reli ya SGR. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kuendelea kukarabati na kuimarisha miundombinu ya reli, majengo ya karakana, stesheni na kambi za watumishi;

ii. Kuhakikisha usalama wa huduma za usafiri wa treni kwa kufunga mifumo mbalimbali ikiwemo mfumo wa ufuatiliaji mizigo (cargo tracking system);

iii. Kuhakikisha ulinzi wa mizigo ya wateja kuanzia sehemu ya kupakia hadi kituo cha mwisho;

iv. Kuendelea kutoa huduma za usafiri kwa njia ya reli jijini Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza msongamano; na

v. Kujenga uwezo wa rasilimaliwatu kupitia mafunzo na ajira.

229. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mwaka wa fedha 2024/25 itaanza kutekeleza mkakati wa kuhakikisha SGR inaanza kufanya kazi na kujiendesha kibiashara. Lengo la Serikali ni kutoendelea kutumia Ruzuku kuendesha reli ya SGR mara baada ya kukamilika. Ili kufikia azma hiyo, Serikali itachukua hatua mbalimbali zikiwemo: -

i. Kufungamanisha Reli zote Tatu za MGR, TAZARA na SGR kupitia Kidatu *Transhipment* ambapo reli zote hizo zitawasiliana kwa kuweka Gantry Crane Storage Facilities pamoja na kuimarisha reli ya Morogoro, Kilosa hadi Kidatu kilometa 108. Uunganishaji huu utawezesha usafirishaji wa mizigo kutoka Kusini mwa Afrika mpaka mikoa yote ya Tanzania pamoja na nchi Jirani; na

ii. Kufungamanisha Bandari Kavu za Kwala, Isaka, Bandari za Mwanza na Kigoma na hatimaye Bandari za Dar es Salaam na Tanga kwa kuunganishwa na MGR na SGR. Njia hii pamoja na manufaa mengine itaongeza wigo wa matumizi ya Reli kwa mizigo ya ndani pamoja na inayotoka na kuingia nchini.

230. ***Mheshimiwa Spika,*** tofauti na ilivyozoeleka nchi yetu imekuwa ikitegemea mizigo inayoletwa kutoka nje ya nchi. Ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na upatikanaji wa mizigo ndani ya nchi, Serikali

kupitia Wizara itatekeleza Mkakati wa kuchochea upatikanaji wa mizigo kwa kuhamasisha Shoroba za Kiuchumi kandokando na sehemu zinazofikika na huduma za miundombinu ya Usafirishaji (Transport and Logistics Economic Corridors). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Taasisi ya Ushoroba wa Kati (Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency - CCTTFA), Mfuko wa Chakula Duniani (WFP), na Watumiaji wakubwa wa Bandari za Tanzania wa ndani na nje wamebaini Shoroba kubwa tatu (3) ambazo zitaweza kuchochea upatikanaji wa mizigo ndani ya nchi.

231. ***Mheshimiwa Spika,*** Shoroba zilizobainishwa kuwezesha upatikanaji ni Ushoroba wa Baridi (Cold Chain) ambao utahamasisha mizigo ya nyama, samaki, matunda, mboga na maua; Ushoroba wa Njano (Yellow Chain) kwa ajili ya mizigo ya madini; na Ushoroba wa Kichele (General Cargo Chain) ambao utahusisha mizigo mingine, hususan mizigo mikubwa (bulk cargo) pamoja na mizigo ya Viwandani na Kilimo ikiwemo pembejeo. Utekelezaji wa Mkakati huu utawezesha kupatikana kwa mizigo mingi ndani ya nchi na kuwezesha TRC kuingia makubaliano na makampuni makubwa na wateja wa muda mrefu. Aidha, hatua hii itawezesha TRC pia kuendelea kuratibu usafirishaji kwa kutumia wabia wa sekta binafsi kupitia utaratibu wa *Open Access*.

232. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia TAZARA inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 111.11** kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na: -

i. Kusafirisha tani 350,000 za mizigo;

ii. Kusafirisha abiria 500,000 kwa upande wa safari ndefu na abiria 300,000 kwa treni ya Udzungwa inayosafiri kati ya Kidatu na Makambako (km 365) na abiria 2,600,000 wa treni ya Dar es Salaam (*commuter train*);

iii. Kufanya matengenezo kinga ya injini 12, mabehewa 783 ya mizigo na 54 ya abiria;

iv. Kuendelea kukarabati na kuimarisha miundombinu ya reli hususan maeneo yaliyowekewa ukomo wa mwendokasi ili kuleta ufanisi katika utendaji; na

v. Kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa tiketi mtandao ili kuleta ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na nauli za abiria na mizigo.

**Udhibiti wa Usafiri Majini**

233. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 82.85** kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kutoa leseni kwa watoa huduma zinazodhibitiwa na kusimamia masharti ya leseni;

ii. Kudhibiti nauli na tozo mbalimbali za usafiri majini kwa kuzingatia Sheria na Kanuni ili kuhakikisha kuwa tozo hizo zinaendana na gharama za uzalishaji na pia zinaleta ushindani katika soko;

iii. Kufanya ukaguzi wa meli za nje zinazokuja katika bandari za Tanzania Bara na meli zilizosajiliwa nchini ili kuhakikisha vyombo hivyo vinazingatia viwango vya ubora, usalama na utunzaji wa mazingira;

iv. Kuongeza vifaa na kuratibu kazi za utafutaji na uokoaji sambamba na mazoezi ya utafutaji na uokoaji majini;

v. Kuimarisha mifumo ya utoaji wa Vyeti vya Mabaharia;

vi. Kuweka mifumo thabiti ya kukabiliana na uchafuzi wa mazingira majini utokanao na meli;

vii. Kuimarisha uratibu wa shughuli za kukabiliana na matukio ya meli kuvujisha mafuta baharini;

viii. Kutoa elimu na uelewa wa masuala yanayohusu usalama, ulinzi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira utokanao na meli;

ix. Kuendelea kutoa huduma za uwakala wa forodha zinazojumuisha ugomboaji na uondoshaji wa bidhaa mahsusi, ambazo ni silaha na vilipuzi, makinikia, wanyama hai kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Wanyamapori, nyara za Serikali na kemikali zinazotumiwa na kampuni za madini;

x. Kuendelea kuimarisha mifumo ya mapato na matumizi kwa kukuza matumizi ya TEHAMA katika kudhibiti huduma za usafiri na biashara ya usafirishaji majini;

xi. Kuendelea kuandaa kanuni na nyenzo za utendaji zitoazo mwongozo kuhusu udhibiti huduma za usafiri majini, usalama na ulinzi kwa vyombo vya usafiri majini na uchafuzi baharini kutoka katika meli;

xii. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa kuhusu Usafirishaji majini inayoratibiwa na Shirika la Bahari Duniani (International Maritime Organization);

xiii. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na shughuli za udhibiti ili kuendelea kukidhi haja na kukabiliana na changamoto za kupanuka kwa maeneo ya udhibiti na mabadiliko ya teknolojia; na

xiv. Kuendelela kutoa huduma na elimu kwa Watumishi kuhusiana na masuala mtambuka kama vile UKIMWI na rushwa na elimu kwa umma kuhusu sekta zinazodhibitiwa

na Shirika kwa kupitia njia mbalimbali kama vile redio, runinga, magazeti, vipeperushi, mikutano ya wadau, maonesho na mitandao ya kijamii.

**Huduma za Bandari**

234. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) itakusanya jumla ya **Shilingi bilioni 1,837.78** kutoka katika vyanzo vya ndani vya mapato vitokanavyo na huduma za kibandari. TPA itatekeleza kazi mbalimbali zikiwemo:-

i. Kuhudumia jumla ya meli 5,909 zenye ukubwa (Gross Registered Tonnage – GRT) wa milioni 45.507. Kati ya hizo, meli 1,268 ni za Kimataifa (Deep Sea) zenye ukubwa wa (GRT) milioni 40.713, meli 1,175 ni za mwambao (coastal) zenye ukubwa wa (GRT) milioni 2.479 na meli 3,466 zenye ukubwa wa (GRT) milioni 2.315 zitahudumiwa katika Bandari za Maziwa Makuu; na

ii. Kuhudumia Shehena ya tani milioni 29.321 ikijumuisha tani za shehena ya makasha (TEUs) 1,262,416 zitakazohudumiwa bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

235. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi itakayotekelezwa na Serikali kwa kutumia fedha zitokanazo na vyanzo vya mapato ya TPA kwa mwaka wa fedha 2024/25 inajumuisha bandari zilizopo katika Bahari ya Hindi, Maziwa Makuu na Bandari Kavu.

236. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam. Lengo la mradi huu ni kuwezesha Bandari ya Dar es Salaam kuhudumia meli kubwa (Post Panamax 1) zenye shehena kubwa na hivyo kuwezesha meli za makasha za kizazi cha tatu kuhudumiwa kwa urahisi. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kuendelea na ujenzi wa matenki 15 ya kupokelea mafuta (Single Receiving Terminal – SRT);

ii. Kuanza ujenzi wa gati nyongeza la mita 500 kutoka gati la kushushia magari (RORO) kuelekea Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI);

iii. Kuendelea na ujenzi wa kituo cha kisasa cha kuhudumia shehena itakayochukuliwa na reli ya TAZARA, MGR na SGR ndani ya Bandari;

iv. Ujenzi wa eneo la kuhudumia na kuhifadhia shehena eneo la Kurasini;

v. Kufanya upembuzi yakinifu katika Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kupata maeneo ya ziada ya kuhudumia shehena; na

vi. Serikali itaendelea na upembuzi yakinifu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mbegani – Bagamoyo na kuanza maandalizi ya kujenga miundombinu wezeshi (barabara, reli na umeme).

237. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa kuboresha Bandari ya Tanga. Lengo la mradi huu ni kuwezesha Bandari ya Tanga kuhudumia meli kubwa za mzigo wa mafuta. Kupitia mradi huu, Serikali itaendelea na shughuli mbalimbali zikiwemo:-

i. Ujenzi wa gati na miundombinu ya kupokelea na kusafirisha mafuta katika eneo la Raskazone – Tanga; na

ii. Ujenzi wa gati la kuhudumia makasha na abiria na kupanua lango la kuingilia meli.

238. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Mtwara. Lengo la mradi huu ni kuwezesha Bandari ya Mtwara kuhudumia meli mbalimbali zikiwemo za mzigo mchafu (dirty cargo). Serikali kupitia mradi huu, itaendelea na shughuli za ujenzi wa bandari kwa ajili ya kuhudumia shehena ya mzigo mchafu ambao unaweza kuchafua mazingira. Mizigo hiyo ni pamoja na makaa

ya mawe na saruji katika eneo la Kisiwa Mgao. Aidha, TPA itaendelea na ukarabati wa maeneo ya kuhudumia shehena na miundombinu ya barabara zinazoingia bandarini.

239. ***Mheshimiwa Spika,*** ukamilishaji ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala, Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi wa yadi na sakafu ngumu (pavement) yenye ukubwa wa hekta tano (5); na kuanza awamu ya pili ya uboreshaji na uendelezaji wa eneo la kuhudumia shehena, majengo ya ofisi, karakana na maghala ya kuhifadhia shehena katika eneo la Kwala.

240. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu Bandari za Maziwa Makuu, Serikali itaendelea na uboreshaji wa bandari zilizopo katika Ziwa Victoria ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa Bandari za Bukoba, Kemondo Bay, Mwanza North na Mwanza South ili kuwezesha meli ya kisasa inayojengwa na Serikali kutia nanga na kutoa huduma. Aidha, kwa upande wa bandari zilizopo katika Ziwa Tanganyika kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na uboreshaji wa Bandari ya Kigoma kwa kujenga barabara za kiungo, *Cargo Shed,* ujenzi wa jengo la abiria *(Passenger Wharf and Lounge)*. Kwa Bandari ya Ujiji, ujenzi wa barabara ya kiungo (access road) inatarajiwa kujengwa.

241. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuboresha bandari za Ndumbi na Mbambabay katika Ziwa Nyasa ambapo kazi zitakazotekelezwa ni kuendelea na uboreshaji wa Bandari ya Ndumbi kwa kujenga barabara unganishi; na kuendelea na uboreshaji wa Bandari ya Mbambabay ili kuwezesha kuhudumia meli na shehena za kwenda nchi jirani zikiwemo za Malawi na Zambia.

242. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuboresha huduma za bandari nchini, Serikali itaendelea na uboreshaji na ununuzi wa mitambo na vifaa mbalimbali vitakavyotumika katika bandari nchini kwa ajili ya kuwezesha kuongoza meli na kuhudumia shehena bandarini.

243. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara inatambua umuhimu mkubwa wa huduma za bandari katika Uchumi wa nchi yetu. Hii

ni pamoja na ukweli kwamba bandari inachangia asilimia 98 ya huduma ya usafiri kwa biashara ya nje na asilimia zaidi ya 40 katika mapato ya kodi. Aidha, ni ukweli kwamba uimarishaji wa huduma za bandari kwa kuongeza miundombinu kama gati na vifaa vya kisasa ndiyo njia sahihi na ya haraka katika kuongeza mchango wa uchumi. Katika kuhakikisha kuwa bandari nchini zinaendelea kuchangia ipasavyo, Serikali imepanga kuongeza zaidi uwezo wa bandari zetu, hususan bandari ya Dar es Salaam. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuongeza idadi ya magati na vifaa vya kisasa ili kuwezesha upakuaji wa meli katika saa 24 badala ya siku Tano (5). Ili kutimiza lengo hilo, Serikali itatekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo:-

i. Kuimarisha huduma za bandari kavu ili ziweze kutoa huduma zote za kibandari zikiwemo huduma za upokeaji na ukamilishaji nyaraka za utumaji na upokeaji mizigo, nyaraka za kodi na kukidhi matakwa ya usafirishaji mizigo ndani na nje ya nchi. Hii ni pamoja na kuongeza bandari kavu kwenye maeneo ya kimkakati na kuunganisha maeneo mengine ya kibiashara;

ii. Kuanzisha na kuimarisha maeneo ya kiunganishi ya bandari na Reli kwa ajili ya kuongeza nafasi ndani ya bandari (Evacuation Points) ambazo zitakuwa na miundombinu ya Reli zinazosogeza mizigo ikiwemo bandari Kavu ya Kwala; na

iii. Uhamasishaji wa uwekezaji wa sekta binafsi kutoka ndani na nje ya nchi katika miundombinu na uendeshaji wa bandari Kavu nchini.

**Huduma za Usafiri Baharini**

244. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2024/25, Serikali kupitia Kampuni inayomilikiwa kwa Ubia kati ya Tanzania na China (SINOTASHIP), imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 19.70** kutokana na vyanzo vya mapato vya ndani ikiwa ni pamoja na huduma ya usafirishaji wa mizigo katika masafa marefu kwa njia ya

bahari na huduma ya uwakala wa meli. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo;

ii. Kuendelea kushawishi makampuni ya meli ili kuongeza idadi ya meli na mizigo itakayoingia katika bandari nchini. Jitihada hizo zitawezesha kuongezeka kwa idadi ya makasha kutoka makasha 73,500 mwaka 2023 hadi kufikia makasha 80,000 mwaka 2024; na

iii. Kushirikiana na Taasisi za fedha nje na ndani ya nchi ili kufanikisha kupata fedha kwa ajili ya kununua meli ya kubeba mizigo (general cargo vessel) itakayofanya safari kati ya China na Tanzania.

**Huduma za Usafiri katika Maziwa Makuu**

245. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) itakusanya jumla ya **Shilingi bilioni 17.65** kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani kwa kusafirisha abiria na mizigo katika Maziwa Makuu. Kazi zitakazotekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani ni pamoja na:-

i. Kuendelea kusafirisha abiria na mizigo katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa;

ii. Uboreshaji miundombinu ya meli ikiwemo chelezo (Shipyard, floating Docks na Slipways) katika bandari za Mwanza na Kigoma;

iii. Kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ofisi za makao makuu na matawi;

iv. Kuwezesha shughuli za kiutawala na uendeshaji wa ofisi ya makao makuu ya Kampuni na matawi yake ya Mwanza, Kigoma na Kyela;

v. Kuendeleza watumishi kwa kuwajengea uwezo wa umahiri na ujuzi kazini; na

vi. Ununuzi wa vitendea kazi vya ofisi na matengenezo ya magari na mitambo inayowesha utekelezaji wa majukumu ya Kampuni.

**Huduma za Viwanja vya Ndege**

246. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) imeweka lengo la kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi bilioni 161.18** kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani vya TAA. Kazi zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/25 ni pamoja na: -

i. Kuendelea kuhudumia viwanja vya ndege vya Serikali nchini kwa kufanya matengenezo ya miundombinu na kusimamia shughuli za uendeshaji;

ii. Ununuzi wa mashine za kisasa za ukaguzi wa abiria na mizigo katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere na Songwe;

iii. Uboreshaji wa Jengo la Mizigo katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza;

iv. Kufunga Mifumo ya kuhudumia Abiria katika Viwanja vya Ndege vya Mwanza, Bukoba, Arusha, Songwe na Dodoma;

v. Kuratibu upimaji na upatikanaji wa Hati Miliki katika Viwanja vya Ndege mbalimbali ikiwemo Mwanza, Kigoma, Tabora, Mafia, Manyoni, Kongwa na Kondoa; na

vi. Kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuwaongezea ujuzi na weledi katika utendaji wao wa kazi katika Viwanja vya Ndege.

247. ***Mheshimiwa Spika,*** mkakati wa Serikali katika kuendeleza

viwanja vya ndege nchini utakuwa ni kuimarisha viwanja vya ndege kwa ajili ya kutoa huduma katika maeneo mbalimbali kwa ufanisi zaidi. Huduma zitakazoendelea kuboreshwa ni pamoja na: Usafirishaji Abiria (Passenger Services); usafirishaji wa mizigo (Freight Services); na kuvutia uwekezaji mwingine (Non-Aeronautical Business Development) katika viwanja husika. Kimsingi, viwanja vingi vimekuwa na mchango mdogo na hivyo mikakati hii inalenga kuongeza ufanisi pamoja na viwanja hivyo kutumika kuchochea uchumi. Ili kufikia lengo hilo, Serikali ina mkakati wa kuongeza matumizi ya viwanja vyote (Airports Installed Capacity Utilization), hususan kuhakikisha kuwa viwanja vyote vinatumika angalau si chini ya asilimia 80 ya uwezo wake na kwa shughuli nyingine angalau kwa asilimia 40 ya mapato ya viwanja vya ndege (Non-Aeronautical Revenue) yanayotokana na shughuli nyingine zitakazowekezwa katika viwanja vya ndege husika. Ili kuwezesha utekelezaji huu, hatua zifuatazo zitatekelezwa:

i. Kuhakikisha umiliki wa viwanja vya ndege unaimarishwa ikiwemo upatikanaji wa hati, kuondoa wavamizi katika viwanja na kuvutia uwekezaji mahiri wa kibiashara;

ii. Kuimarisha miundombinu ya viwanja, hususan majengo ya abiria na mizigo na kuhamasisha mizigo maalum kama uwekezaji wa kilimo cha maua katika maeneo yaliyotengwa kando ya viwanja na uvutiaji wasafiri katika makundi kama utalii na uunganishaji wa ndege;

iii. Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji wa huduma mbalimbali pamoja na uendeshaji katika viwanja vya ndege nchini; na

iv. Kuhamasisha na kuimarisha matangazo ya kuvutia wateja na watumiaji wapya wa viwanja vya ndege ikiwemo ndege za masafa marefu na ya kati ili kuongeza matumizi ya viwanja vyetu katika kuhudumia wateja wa ndani na nchi zinazotuzunguka.

**Huduma katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro – KIA**

248. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia TAA itaendelea kukisimamia Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro ambapo kupitia Kiwanja hicho jumla ya **Shilingi bilioni 40.46** zitakusanywa kutokana na huduma mbalimbali zitolewazo katika kiwanja hicho. Kazi zitakazotekelezwa na TAA kupitia Kiwanja hicho ni pamoja na:-

i. Kuendelea kuboresha huduma za abiria katika kiwanja cha KIA;

ii. Ujenzi wa uzio wa kiwanja kwa awamu ya pili na ujenzi wa karakana ya masuala ya ufundi;

iii. Ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa 33kv kutoka KIA Lodge kuelekea katika eneo la kituo cha umeme Namba 6 (PC6);

iv. Usanifu na kufanya matengenezo ya mfumo wa usimamizi wa shughuli za kutua na maegesho ya ndege, mizigo pamoja na mafuta ya ndege;

v. Ununuzi wa mashine ya x-ray (Small tunnel) *with Metal detectors, STP and OTP* pamoja na mashine ya X-ray (Large tunnel) *with Metal detectors, STP and OTP;*

vi. Ufungaji wa mfumo wa kamera za ulinzi awamu ya pili utakaopitia maeneo ya Tower, Cargo, Gate 6 & Parking bay kuelekea KIMAFA; na

vii. Kuendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika uwekezaji katika kilimo cha maua na mbogamboga katika eneo lililotengwa katika eneo la kiwanja.

**Huduma za Usafiri wa Anga**

249. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali

kupitia ATCL imeweka lengo la kukusanya jumla ya mapato ya **Shilingi bilioni 717.97** kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani. Mapato hayo yanatokana na huduma za kusafirisha abiria na mizigo ndani na nje ya nchi kwa kutumia ndege zilizonunuliwa. Kazi zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/25 ni pamoja na:-

i. Kufanya safari katika vituo 27 ndani na nje ya Tanzania, vikijumuisha vituo 14 vya ndani ya nchi, ambavyo ni Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Mpanda, Pemba, Songea, Tabora na Zanzibar; vituo 9 vya kikanda vikiwemo Bujumbura, Entebbe, Hahaya, Harare, Johannesburg, Lubumbashi, Lusaka, Nairobi na Ndola; na vituo vinne (4) vya kimataifa ambavyo ni Dubai, Guangzhou, London, na Mumbai;

ii. Kusafirisha mizigo kwa ratiba maalum kwa kutumia ndege ya mizigo aina ya Boeing 767-300F katika vituo vya Dubai (Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu), Guangzhou (China), Mumbai (India), na Nairobi (Kenya). Pia, ATCL itaendelea kusafirisha mizigo kwa safari zisizo na ratiba maalum kwa kuzingatia mahitaji ya soko;

iii. Kutoa mafunzo kwa marubani na wahandisi wa ndege pamoja na kuajiri na kuwapandisha madaraja marubani ambao wako kwenye hatua mbalimbali za mafunzo maalum (type rating and initial training) kwa aina mbalimbali za ndege;

iv. Kufanya matengenezo ya ndege kwa ratiba maalum pamoja na matengenezo mengine yatakayohitajika; na

v. Kutangaza shughuli za ATCL na kugharamia mifumo ya mauzo na uendeshaji pamoja na michango mbalimbali ya kisheria.

## Huduma za Hali ya Hewa

250. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 15.98** kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na mapato yatokanayo na tozo za huduma za hali ya hewa, hususan zitumiwazo katika usafiri wa anga na majini. Kazi zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/25 ni kama ifuatavyo:-

i. Kuboresha huduma za hali ya hewa kwa sekta mbalimbali zikiwemo: sekta za nishati, madini, rasilimali maji, usafiri, kilimo, utalii na ujenzi;

ii. Kuendelea kuimarisha udhibiti na usimamizi wa ubora wa huduma za hali ya hewa zinazotolewa kwa sekta ya usafiri wa anga na shughuli zinazofanyika majini kulingana na vigezo vilivyopo;

iii. Kufanya tafiti za hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi;

iv. Kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kutumia huduma zinazotolewa na TMA;

v. Kudhibiti na kuratibu huduma za hali ya hewa zinazotolewa nchini kwa kuhakikisha taratibu na matakwa ya kisheria yanafuatwa katika utoaji wa huduma hizo;

vi. Kuendesha na kuimarisha mtandao wa vituo vya hali ya hewa hapa nchini kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa takwimu za hali ya hewa; na

vii. Kuboresha matumizi ya TEHAMA kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na uendeshaji wa shughuli za hali ya hewa hapa nchini.

## C. 1: VYUO VYA MAFUNZO VYA KISEKTA

251. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwa na rasilimali yenye ujuzi wa kutosha na kupunguza gharama za kusomesha wataalam nje ya nchi, Serikali kupitia Wizara itaendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 kama ilivyobainishwa katika Ibara ya 59(i) kwa kuboresha na kuvijengea uwezo vyuo vya mafunzo vya kisekta. Vyuo hivyo vya kisekta vinajumuisha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam, Chuo cha Usafiri wa Anga, Chuo cha Bandari, Chuo cha Hali ya Hewa na Chuo cha Reli.

### Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

252. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia Chuo cha NIT imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 27.50** kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani yatokanayo na utoaji wa mafunzo, utafiti na ushauri wa kitaalam. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na: -

i. Kuongeza udahili wa wanafunzi wa kozi ndefu kutoka wanafunzi 16,131 hadi wanafunzi 18,320;

ii. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kupitia ziara za kitaaluma, mafunzo ya muda mrefu na mfupi, mafunzo ya vitendo na kubadilishana wakufunzi na vyuo vya nje ya nchi;

iii. Ujenzi wa Jengo la kuweka vifaa Maalum kikiwemo kifaa cha kufundishia wahudumu wa ndani ya ndege *(Full Motion Mock-up)* na ukarabati wa barabara za ndani katika Kampasi ya Mabibo-Dar es Salaam;

iv. Ununuzi wa samani, *Generator*, vifaa vya TEHAMA na vya kuzimia moto kwa ajili ya majengo mapya ya Chuo; na

v. Kuendelea kutekeleza majukumu ya Kituo cha Kikanda cha

Umahiri cha Mafunzo ya Usalama Barabarani kwa fedha za Serikali na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

**Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)**

253. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Chuo cha Bahari Dar es Salaam kitakusanya **Shilingi bilioni 16.35** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ya ndani. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kuanza taratibu za ujenzi wa Kampasi za Chuo katika wilaya ya Kigamboni (Kimbiji) na Lindi (Kikwetu);

ii. Kuongeza vifaa vya kufundishia vikiwemo vifaa vya mafunzo ya uongozaji meli (navigation equipment);

iii. Kuanzisha maabara ya mekatroniki (Mechatronic laboratory);

iv. Kuboresha tafiti na utoaji machapisho hususan katika maeneo yanayolenga ukuaji wa uchumi wa buluu;

v. Kujenga mifumo ya TEHAMA (DMI help desk and Inventory Management system) na kuongeza upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA; na

vi. Kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

254. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Uchukuzi kupitia Chuo cha Bahari Dar es Salaam itakuwa mwenyeji wa Kongamano kubwa la Kimataifa la Uchumi wa Buluu litakalofanyika mwezi Julai, 2024. Kongamano hili litajadili mchango wa sekta za uchumi wa buluu ikiwemo Sekta ya Uchukuzi katika ukuaji wa uchumi wa nchi na kuchochea uwekezaji. Kongamano litahusisha zaidi ya washiriki 300 kutoka nchi mbalimbali ambayo ni fursa kwa nchi kujitangaza.

## Chuo cha Usafiri wa Anga

255. ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali kupitia TCAA katika mwaka wa fedha 2024/25 itaendelea kutoa mafunzo katika kozi mbalimbali zinazohusiana na masuala ya usafiri wa anga kupitia Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC). Chuo hiki kinatarajia kudahili wanafunzi 2,500 na kuandaa kozi mpya nne (4).

## Chuo cha Bandari

256. ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali kupitia TPA katika mwaka wa fedha 2024/25 itaendelea kutoa mafunzo katika kozi mbalimbali zinazohusiana na kuhudumia mizigo katika bandari nchini kupitia Chuo cha Bandari. Aidha, Chuo hiki kinatarajia kudahili wanafunzi 1,175.

## Chuo cha Reli

257. ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali kupitia TRC katika mwaka wa fedha 2024/25 itaendelea kutoa mafunzo ya reli katika kampasi zote za Tabora na Morogoro. Aidha, Chuo kinatarajia kudahili wanafunzi 796 kwa mwaka 2024/25.

## Chuo cha Hali ya Hewa

258. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) itaendelea kutoa mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya awali na Diploma kupitia Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa kilichopo Kigoma ikiwemo udahili wa wanafunzi kutoka nje ya nchi. Aidha, Chuo kitakamilisha ununuzi wa eneo lenye ukubwa wa ekari 38 lililopo Nyamoli, Kigoma kwa ajili ya upanuzi wa shughuli za Chuo; ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kufundishia pamoja na usanifu wa mabweni na jengo la utawala.

## C. 2: MASUALA MTAMBUKA

259. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara na Taasisi zake itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Miaka Mitano (5) kuanzia 2021/22 hadi 2025/26. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kutoa mafunzo yanayohusu maadili na kuzuia vitendo vya rushwa kupitia semina na vikao mbalimbali vya wafanyakazi. Hivyo, natoa rai kwa Watumishi na Wananchi kwa ujumla kuendelea kutoa taarifa katika vyombo husika pale wanapohisi vitendo vya rushwa.

260. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa Watumishi ili kujikinga na maambukizi mapya ya VVU ikiwemo kuhimiza upimaji wa hiari wa VVU na magonjwa mengine yasiyoambukiza; na ushiriki wa watumishi kwenye mazoezi ya viungo kupitia bonanza na SHIMIWI kama njia mojawapo ya kuimarisha afya na uhusiano baina ya watumishi katika mahala pa kazi.

261. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo Watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na weledi katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Vilevile, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo katika kutumia Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma na Taasisi (PEPMIS na PIPMIS). Lengo la mfumo huu ni kuhakikisha kuwa kila mtumishi anawajibika kutekeleza majukumu yake ya kila siku na kufanya tathmini ya utendaji kazi ili kuimarisha uwajibikaji na kufikia malengo ya Taifa kwa ujumla.

## C. 3: MASUALA MENGINE YATAYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA 2024/25

### Maboresho ya Sera, Sheria na Kanuni za Kisekta

262. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuendelea kuboresha utendaji katika utoaji

wa huduma za uchukuzi, Wizara itaendelea kuandaa na kufanya mapitio ya miongozi yake zikiwemo Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali. Pamoja na hatua nyingine, Wizara itaendelea kuhuisha Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003. Vilevile, Wizara itaendelea kufanya mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali ili kuendana na mahitaji ya sasa.

**Ufuatiliaji na Tathmini**

263. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Uchukuzi ni miongoni mwa Wizara ndani ya Serikali zinazotekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati. Katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara itaendelea kuimarisha ufuatiliaji na tathmini kwa ajili ya kuhakikisha kuwa miradi hiyo inatekelezwa ipasavyo na kwa wakati. Pamoja na miradi hiyo, Wizara itafuatilia kwa ukaribu utendaji wa Taasisi zilizo chini yake ili ziwe na ufanisi katika kutoa huduma stahiki kwa Watanzania.

**Kuongeza Upatikanaji wa Fedha za Kigeni**

264. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25, Wizara ya Uchukuzi na Taasisi zake itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni nchini na kupunguza matumizi ya fedha hizo. Kupitia mikakati hiyo, katika kipindi hicho Wizara inatarajia kukusanya fedha za kigeni takriban Dola za Marekani milioni 762.41 kutokana na shughuli zake. Mikakati itakayotekelezwa ni pamoja na: -

i. Kuendelea kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji na uendelezaji wa shughuli za Uchukuzi zikiwemo za bandari nchini;

ii. Kuimarisha uunganishaji wa njia ya reli na barabara katika maeneo mbalimbali ikiwemo bandari ya Kwala ili kuwezesha nchi jirani zilizopewa maeneo kuwekeza na kuanza kutumia bandari kavu ya Kwala;

iii. Kujenga miundombinu wezeshi kwa ajili ya kupokelea na kuhifadhi mafuta yanayoagizwa na nchi jirani na kutunza bidhaa zinazoharibika haraka zikiwemo bidhaa za kilimo na mifugo;

iv. Kuendelea kutekeleza mikakati ya kukuza soko la usafirishaji wa mizigo nje ya nchi kupitia ATCL kwa kujitangaza ndani na nje ya nchi;

v. Kuboresha viwanja vya ndege ili viweze kuhudumia ndege kwa saa 24 kwa kuweka miundombinu mbalimbali ikiwemo kuweka taa za kuongozea ndege katika viwanja husika;

vi. Kuboresha miundombinu ya reli iliyopo na kukamilisha ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR;

vii. Kukarabati na kujenga meli katika Maziwa Makuu na kuwezesha kuhudumia nchi jirani zinazozunguka Maziwa Makuu hayo;

viii. Kukamilisha ukarabati wa karakana za Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro - KIA (KIMAFA) na JNIA ili matengenezo madogo ya ndege yafanyike ndani ya nchi na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni;

ix. Kuanza mafunzo ya urubani ndani ya nchi ambapo kupitia Chuo cha NIT, Serikali imenunua ndege za mafunzo hayo na taratibu za kuanza mafunzo husika ndani ya nchi zinaendelea kukamilishwa; na

x. Kuendelea kuboresha miundombinu na vifaa vya kufundishia katika vyuo vya mafunzo vya kisekta ili kuwavutia wanafunzi wa kigeni kuja nchini kwa wingi zaidi.

## D: SHUKRANI

265. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake

kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24. Ufanisi huo ulipatikana kutokana na ushirikiano wa wadau mbalimbali ndani na nje ya Wizara wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi na Wananchi kwa ujumla. Ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote waliotoa michango mbalimbali ikiwemo rasilimali fedha, ushauri, na nguvu kazi na wale walioshiriki moja kwa moja katika utendaji wa shughuli mbalimbali za uchukuzi. Shukrani za kipekee ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao ambayo imesaidia katika kuimarisha utendaji wa Wizara katika kutoa huduma kwa wananchi.

266. ***Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara iendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu, niwaombe Waheshimiwa Wabunge muendelee kuishauri Serikali ipasavyo katika masuala mbalimbali hususan yanayogusa maendeleo ya wananchi moja kwa moja. Pia, niwaombe wananchi na wadau wengine kuendelea kutoa michango yao ya hali na mali pamoja na kuendelea kushirikiana na Serikali katika kulinda miundombinu ya usafiri na usafirishaji ambayo Serikali imekuwa ikitumia kiasi kikubwa cha fedha za Umma kuijenga na kuikarabati.

267. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza na kutambua mchango unaotolewa na viongozi wenzangu katika kunisaidia kutekeleza majukumu ya Wizara, nikianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa **David Mwakiposa Kihenzile** (Mb.); Katibu Mkuu, **Prof. Godius Walter Kahyarara** na Naibu Katibu Mkuu **Dkt. Ally Saleh Possi**. Pia, kipekee napenda kuishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa jitihada zao katika utekelezaji wa Majukumu ya Wizara.

268. ***Mheshimiwa Spika,*** Pia, naomba kutumia fursa hii kwa niaba ya Wizara kutoa shukrani zangu za dhati na kuwatambua wadau wote wa Wizara ikiwa ni pamoja na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia kwa hali na mali katika utekelezaji wa

Programu, Miradi na Mipango mbalimbali ya Wizara. Kwa namna ya kipekee niruhusu niwatambue wafuatao: Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO); Shirika la Kimataifa la Usafiri Majini (IMO); Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Benki ya Dunia (WB); Japan (JICA); Korea Kusini (KOICA); Ujerumani (KfW); Foreign Commonwealth and Development Office (FCDO); Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD); Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU); Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB); Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID); Trade Mark Africa; Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki – EAC; Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika - SADC; Nchi za Urusi; Umoja wa Falme za Kiarabu-UAE; Uingereza; Marekani; Uholanzi; Japan; India; China; Denmark; Korea Kusini; Ufaransa; Ubelgiji; Ujerumani na Uturuki; Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PSSSF; Taasisi za fedha za CRDB, NMB, AZANIA BANK, NBC na TCB na Asasi mbalimbali za kiraia; Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine wengi ambao sikuwataja hapa kutokana na uwingi wao.

269. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee niruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika na kwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

## E: MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UCHUKUZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2024/25

270. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,729,676,417,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 114,744,476,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,614,931,941,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

271. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na Hotuba hii, nimeambatisha Jedwali la Muhtasari wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/25 ikionesha kiasi cha fedha kilichotengwa kwa kila mradi pamoja na majedwali mbalimbali yenye taarifa na takwimu kwa ajili ya kutoa uelewa

zaidi kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kuhusu kazi zinazotekelezwa na Wizara. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya hotuba yangu. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (**www.uchukuzi.go.tz**).

272. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili muhimu, tangazo la kwanza, alisimama Mheshimiwa Esther Matiko kwa Kanuni ya 75(1) ya kutaka taarifa zinazosomwa hapa Mezani ziwe zimeshaingia kwenye vishikwambi vya Wabunge ili kuwawezesha Wabunge kufuatilia hotuba. Katika majibu yangu niliielekeza Serikali iwasilishe hizo taarifa kwa wakati, lakini nimepata taarifa hapa kwamba Serikali ilishawasilisha taarifa hizi kwa Bunge na ilikuwa ni wajibu wa Bunge kuhakikisha kwamba inaweka taarifa hizi kwenye vishikwambi vya Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, naomba niweke huo msisitizo kwamba Bunge tuhakikishe kwamba tunatekeleza huo wajibu kwa wakati ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kufuatilia hotuba zinazosomwa hapa mbele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo la pili nimepewa taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo Bungeni, hivyo, atakayekaimu nafasi ya Waziri Mkuu Bungeni kwa siku ya leo ni Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumshukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa Daniel Sillo ambaye amepambana kushikilia nafasi hiyo mpaka sasa wakati anakuja Mheshimiwa Waziri Deogratius Ndejembi. Pia, Mwanasheria Mkuu wa Serikali hayupo Bungeni na nafasi hiyo kwa sasa inashikiliwa na Mheshimiwa Ridhiwan Kikwete, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, na sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ili aweze kufanya wasilisho lake. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Fungu Na. 62 – Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo la Februari, 2023, na imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya kwanza ni utangulizi na inaeleza kuhusu msingi na muundo na taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majumu yake.

(ii) Sehemu ya pili inaeleza kuhusu uchambuzi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iii) Sehemu ya tatu ni uchambuzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iv) Sehemu ya nne ni maoni ya mapendekezo ya Kamati; na

(v) Mwisho ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matokeo ya uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kwa kuzingatia msingi wa uchambuzi, Kamati ilichambua taarifa za utekelezaji wa Fungu 62 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) katika uchambuzi huo. Kamati ilijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Mwenendo wa makusanyo ya maduhuli;

(ii) Upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida; na

(iii) Utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwenendo wa upatikanaji wa fedha, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi ilitengewa bajeti ya jumla ya shilingi 2,089,245,508,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 118,215,599,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 1,971,029,909,000 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imepokea shilingi 1,820,698,515,147.48 sawa na wastani wa 87.15% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizotolewa, shilingi 56,968,628,462.72 zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 1,763,729,886,684.76 ni fedha za bajeti ya maendeleo kama ambavyo kielelezo Na. 1 kinafafanua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha katika Bajeti ya Fungu 62 hususan katika mradi wa maendeleo. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ambayo ni 48.19% kwa sababu unaathiri shughuli za kila siku za Wizara pamoja na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Serikali ikaweka kipaumbele cha kutoa fedha za matumizi ya kawaida kwa uwiano unaostahili ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa kila siku wa Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake ziliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 3,064,641,847,131 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Februari, 2024, makusanyo yalikuwa ni shilingi 1,697,912,693,717.31 sawa na asilimia 55.40 ya malengo waliyojiwekea. Mchanganuo wa mwenendo wa makusanyo unafafanuliwa katika Kielelezo Na. 2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wastani, mwenendo wa makusanyo ya Fungu 62 katika mwaka wa fedha 2023/2024 ni wa kuridhisha. Kamati inazipongeza taasisi ambazo zilikusanya vizuri na inaishauri Serikali kuendelea kufanya mapitio ya mara kwa mara ili kubaini uwezo wa kila taasisi kukusanya kulingana na vyanzo vya mapato vilivyopo. Kwa upande mwingine, Kamati haikuridhishwa na taasisi ambazo makusanyo yake yalikuwa chini ya asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hadi kufikia Februari, 2024, Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* lilikusanya asilimia 25.76 ya makadirio waliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kamati ilitaarifiwa kwamba, Shirika la Reli lilikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ziliathiri mwenendo wa makusanyo ikiwemo changamoto ya kuharibika kwa miundombinu ya reli nchini kutokana na mvua kubwa zilizonyesha katika maeneo mbalimbali hapa nchini, hivyo kuathiri makusanyo yatokanayo na usafirishaji wa abiria na mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, wakati wote kunakuwa na fungu maalumu linalotosheleza kukabiliana na uharibifu unaoweza kujitokeza katika miundombinu ya reli. Uwepo wa fungu hilo uende sambamba na kuwa na mkakati endelevu wa kukabiliana na dharura za uharibifu wa miundombinu ya reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Uchukuzi ilitengewa jumla ya shilingi 118,215,599,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2024 jumla ya fedha za matumizi ya kawaida zilizokuwa zimetolewa ni shilingi 56,968,628,462.72 sawa na 48.19% ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa kama ambavyo Kielelezo Na. 3 kinafafanua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya jambo mahsusi lililobainiwa na Kamati katika mwenendo wa mapokezi ya fedha za Matumizi ya Kawaida, ni kwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA)* kutopewa fedha kabisa. Kamati inatambua kwamba *(TCAA)* inajitegemea kiuendeshaji. Kwa muktadha huo, mishahara pamoja na matumizi mengine hulipwa kutoka katika vyanzo vyake. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilitenga shilingi 10,929,320,000 kama sehemu ya utekelezaji wa uendelezaji wa Chuo cha Usafiri wa Anga na hadi kufikia Februari, 2024 hakuna fedha iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitaarifiwa kwamba, sababu za kutotolewa kwa fedha hizo ni *TCAA* kutokuwa na mkataba wa uendelezaji wa chuo husika. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaharakisha michakato yote muhimu ili fedha za matumizi ya kawaida zitolewe kwa wakati kutekeleza malengo yaliyokusudiwa kabla ya mwaka wa fedha 2023/2024 kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Uchukuzi ilitengewa jumla shilingi 1,971,029,909,000 ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,863,764,800,000 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi 107,265,109,000 zilikuwa ni fedha za nje. Mwenendo wa mapokezi ya fedha za maendeleo unafafanuliwa katika Kielelezo Na. 4 kwa muhtasari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa mapokezi ya fedha za maendeleo. Pia Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1), Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kati ya tarehe 12 na 17 Machi, 2024 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Simiyu na Mwanza. Katika ziara hiyo, Kamati ilifanya tathmini ya baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *SGR* Kipande cha Tatu unahusisha ujenzi wa reli kutoka Makutupora - Singida hadi Tabora yenye urefu wa kilometa 368. Mradi ulianza kutekelezwa tarehe 8 Machi, 2022 kwa lengo la kukamilika tarehe 07 Januari, 2026 kwa thamani ya dola za Kimarekani 1,923,693,000 ambazo ni sawa na shilingi 4,809,237,500,000 za Kitanzania. Hadi kufikia Machi, 2024, Serikali ilikuwa imefanya malipo kwa Mkandarasi ya jumla ya dola za Kimarekani 476,726,122.08 sawa na shilingi 1,191,815,305,200 za Kitanzania, sawa na 24.78%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati inatembelea kukagua mradi wa maendeleo, utekelezaji wake ulikuwa ni 14% tu, ambayo kwa maoni ya Kamati, hayaakisi kiwango cha fedha kilichotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa mradi unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo: -

(a) Serikali kuchelewa kufanya malipo kwa mshauri sanifu, ambapo imesababisha kukwama kwa kazi za usanifu na ujenzi;

(b) Mkandarasi kuchelewa kununua malighafi na vifaa vya ujenzi kwa sababu ya kushindwa kukamilika kwa wakati kwa baadhi ya kazi kama vile ujenzi wa makambi na madaraja;

(c) Mkandarasi kulundika madeni ya wasambazaji wa vifaa na huduma, na

(d) Serikali kutolipa fedha za fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yalitwaliwa kupisha mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya utekelezaji wa mradi kwa kuzingatia mtaji ambao tayari Serikali imeuweka, uwezo wa Mkandarasi kukamilisha mradi kwa ubora unaotakiwa pamoja na athari ambazo zinaweza kujitokeza iwapo mradi huo utachelewa kukamilika. Tathmini hiyo itoe mapendekezo ya haraka ambayo yatawezesha mradi huo kukamilika ili kutoa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kikanda cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji Majini ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Kimataifa wa Mawasiliano na Uchukuzi katika Ziwa Victoria, unaotekelezwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* katika eneo la Ilemela, Jijini Mwanza. Mradi unatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, mradi ulitengewa jumla ya shilingi 4,769,673,000 kwa ajili ya usanifu na ujenzi uliopangwa kukamilika ifikapo Novemba, 2024. Hadi kufikia Machi, 2024 fedha iliyolipwa kutekeleza mradi ilikuwa shilingi 953,934,600 sawa na 20% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapokezi yasiyoridhisha ya fedha kwa mradi kwa sehemu kubwa yameathiri utekelezaji wa mradi ambapo hadi Kamati inafikia uwandani kwa ajili ya ukaguzi, ujenzi wa mradi ulikuwa 10% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kwa kuibua mradi ambao utasaidia kuboresha usalama wa raia katika usafiri wa maji kwenye Ziwa Victoria. Hata hivyo, kwa kuzingatia kuchelewa kwa mradi huu, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mradi huo ili ukamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa Bandari ya Mwanza Kaskazini, katika Ziwa Victoria, mradi huu unahusisha ujenzi

wa upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya Bandari ya Mwanza Kaskazini *(North Port),* katika Ziwa Victoria unaotekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)*. Mradi una thamani ya shilingi 18,606,443,416.66 na ulianza kutekelezwa tarehe 3 Mei, 2023 kwa lengo la kukamilika tarehe 2 Novemba, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi kwa kuwa maendeleo ya mradi huo yalikuwa ni 30% ukilinganisha na matarajio ya 46% kulingana na mpango wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zilizosababisha kusuasua kwa mradi. Moja ya changamoto hizo ni kuwepo kwa shughuli za ujenzi unaoingilia huduma za kila siku zitolewazo kwenye eneo la bandari. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina ili kubuni namna bora za kutekeleza mradi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi 4295 - ujenzi na ukarabati wa meli katika Ziwa Victoria. Mradi unahusisha ujenzi wa meli mpya ya *MV Mwanza Hapa Kazi Tu,* ujenzi wa meli ya kubeba mizigo, ukarabati wa Meli ya *MT Ukerewe*, na ukarabati wa Meli ya *MT Nyangumi*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za utekelezaji wa mradi huo ni jumla ya Dola za Kimarekani 49,322,365.40, sawa na shilingi 123,305,913,500. Hadi wakati Kamati inafanya ziara ya ukaguzi, mkandarasi alikuwa ameshalipwa 90.87% ya gharama zote za mradi wa maendeleeo ya ujenzi kwa 93%. Inatarajiwa kwamba, mradi utakamilika ifikapo tarehe 31 Mei, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya Mradi wa *MV Mwanza Hapa Kazi Tu*, meli ambayo itahudumia wananchi walio wengi katika Ukanda wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ni kuhusu Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi Fungu 66 - Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Muundo wa Bajeti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Uchukuzi - Fungu 62 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,729,676,417,000 ambapo kati ya fedha inayoombwa, shilingi 114,744,476,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 2,614,931,941,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa wastani wa 30.65% ukilinganisha na bajeti ya shilingi 2,089,245,508,000 iliyotengwa kwa mwaka wa fedha unaoishia. Kielelezo Na. 5 kinafafanua kwa muhtsari, ulinganisho kati ya bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 na bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezo la bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kutokana na Serikali kuongeza shilingi 643,902,032,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo, kama ambavyo Kielelezo Na. 5 kilivyoonesha, bajeti ya matumizi ya kawaida mwaka wa fedha 2024/2025 imepungua kwa 2.93% ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya makusanyo ya maduhuli, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa kukusanya maduhuli ya shilingi 3,310,021,435,500 ambayo ni ongezeko la shilingi 245,379,588,369 ikilinganishwa na malengo ya kukusanya shilingi 3,064,641,847,131 katika mwaka wa fedha unaoisha. Ongezeko hilo ni wastani wa 8.01% na mchanganuo huo unapatikana katika Kielelezo Na. 6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa ujumla hususan taasisi ambazo zimeongeza wigo wa makadirio ya makusanyo yake. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba, baadhi ya taasisi zimekadiria kukusanya maduhuli pungufu ukilinganisha na makadirio waliyojiwekea katika mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* ambalo makadirio ya makusanyo yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yamepungua kwa 4.97%. Kamati ina maoni kwamba, *TRC* ifanye tathmini upya ya uwezo wake wa kukusanya maduhuli, hasa kwa kuongeza huduma za usafirishaji wa abiria, mizigo na uendeshaji wenye ufanisi wa *SGR* kipande cha Dar es Salaam – Dodoma. Makusanyo yanaweza kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu 62 linaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 114,744,476,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 86,661,930,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 28,082,546,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2024/2025 imepungua kwa shilingi 3,471,123,000 sawa na 2.94% ukilinganisha na shilingi 118,215,599,000 iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 kama ambavyo Kielelezo Na. 7 kinaonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza fedha za matumizi ya kawaida kwa namna inayoakisi kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu 62 Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,614,931,941,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,524,369,202,000 ni fedha za ndani, sawa na 96.54% na shilingi 90,562,739,000 ni fedha za nje, sawa na 3.46% ya bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa wastani wa 32.67% ukilinganisha na bajeti ya shilingi 1,971,029,909,000 katika mwaka wa fedha 2023/2024. Ongezeko hilo linajionyesha katika Kielelezo Na. 8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ongezeko la jumla la bajeti ya maendeleo, Kamati imebaini kwamba bajeti ya fedha za ndani imeongezeka kwa 35.44%, wakati bajeti ya fedha za nje kutekeleza miradi hiyo, imepungua kwa 15.57%. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kubajeti utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutenga zaidi fedha za ndani na kupunguza utegemezi wa bajeti ya fedha kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ambapo ufanisi mkubwa umeendelea kutoa fedha za kutekeleza majukumu mbalimbali ya Fungu 62 Wizara ya Uchukuzi, hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitatu, Kamati imeshuhudia sehemu kubwa ya Bajeti ya Sekta ya Uchukuzi ikitolewa kwa kiwango kinachoridhisha. Aidha, Kamati imebaini kwamba, miradi yote ya kimkakati ambayo ilianza kutekelezwa katika Serikali ya Awamu ya Tano, Serikali ya Awamu ya Sita imeitekeleza kwa ufanisi mkubwa. Kwa mfano, zaidi ya 70% ya uendelezaji wa mradi wa *SGR* umefanyika katika Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, na kwa kuthamini mtaji wa fedha za maendeleo unaotokana na kodi za wananchi, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

(a) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika utendaji kazi utakaochochea kuboresha huduma za Sekta ya Usafirishaji nchini, kwa kuwa Sekta hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi;

(b) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika kukusanya maduhuli kutokana na vyanzo vilivyopo, na kubaini vyanzo vipya ambavyo vitaongeza wigo wa makusanyo hayo. Sambamba na hilo, Serikali ihakikishe kwamba, huduma zitolewazo na taasisi zake zitakuwa bora ili kukidhi matarajio ya wadau muhimu katika sekta ya uchukuzi ambao wanachangia mapato; na

(c) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu na kuwepo kwa thamani ya fedha *(value for money)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoni mahususi, Kamati inapongeza hatua ambayo imefikiwa na Serikali kwa treni ya umeme kufanya majaribio kwa mafanikio kusafirisha abiria kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma katika Reli ya Kisasa ya *SGR*. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba huduma rasmi za usafiri wa treni katika Reli ya *SGR* kati ya Dar es Salaam na Dodoma zinaanza haraka ili kutoa huduma kwa wananchi na kuongeza pato la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maboresho ya uendeshaji wa Bandari nchini, Kamati inatambua marekebisho ya sheria yaliyofanyika 2017 katika Sheria ya Bandari Sura Na. 166, ili kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* ikusanye mapato ya *wharfage* katika bandari na kupelekwa katika akaunti maalumu iliyofunguliwa katika Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)*. Mabadiliko hayo, yameweka utaratibu unaoitaka *TPA* kuwasilisha maombi ya fedha hizo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya uendeshaji kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya Serikali, ili kuboresha utendaji wa *TPA*, Kamati inashauri kwamba, Sheria ya Bandari ifanyiwe tena marekebisho ili kwamba mapato yatokanayo na *wharfage* yakusanywe na kubaki *TPA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba, mapato yatokanayo na *wharfage* yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021. Inatarajiwa kwamba ifikapo mwaka wa fedha 2026/2027, mapato hayo yatakuwa shilingi trilioni 1.4. Kati ya mwaka wa fedha 2023/2024, makadirio ya makusanyo yalikuwa ni shilingi bilioni 592 na inakadiriwa kwamba mapato hayo yataongezeka kufikia shilingi bilioni 792.489 kati ya mwaka wa fedha 2024/2025, kama ambavyo Kielelezo Na. 9 kinaonyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Kamati katika jambo hili yamejengwa katika msingi kwamba, Mamlaka ya Bandari ni moja kati ya nyenzo kuu za makusanyo ya Serikali *(revenue facilitator)*. Kwa utafiti mdogo ambao Kamati imeufanya, imebaini kwamba katika mwaka wa fedha 2022/2023, makusanyo ya *TRA* yalikuwa jumla ya shilingi trilioni 22.611. Kati ya fedha hizo, makusanyo ya ushuru wa forodha, ambao kwa sehemu kubwa unachangiwa na huduma zitolewazo na bandari, yalikuwa ni shilingi trilioni 9.354 sawa na 41% ya makusanyo yote. Kielelezo Na. 10 kinafafanua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utafiti huo, mchango wa bandari ni dhahiri na Kamati inaamini kwamba, iwapo *TPA* itakusanya *wharfage* kwa mujibu wa sheria, Mamlaka hiyo itakuwa na uwezo wa kuendeleza miundombinu ya bandari ikiwemo ujenzi wa gati mpya ambazo zinaweza kupunguza msongamano wa shehena zilizopo na meli ambazo zipo kwenye eneo la bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kuongezeka kwa shehena katika bandari zetu, usafirishaji wa mizigo kwa njia ya reli na barabara utaongezeka na hatimaye kukuza uchumi wa nchi na kuifanya *TRA* iwe na makusanyo makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa ujenzi wa meli katika Ziwa Tanganyika, katika Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilibaini kwamba, suala la usafiri wa maji katika Ziwa Tanganyika bado halijapatiwa ufumbuzi pamoja na kwamba bajeti ilitengwa kwa ajili ya mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Kamati ilitaarifiwa kwamba hatua za awali za kumpata mkandarasi zimekamilika, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka ili kuhakikisha kwamba Mradi wa Usafiri wa Meli katika Ziwa Tanganyika unaanza mara moja. Aidha, Serikali iongeze fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025 ili kuhakikisha kwamba mradi huo unakamilika na kuanza kutoa huduma za usafiri katika Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Ndege *(ATCL)*, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kununua ndege za abiria na ndege za mizigo. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati inaishauri Serikali kubuni njia bora zaidi zitakazoongeza ufanisi wa uendeshaji wa *ATCL* ili Shirika hilo liboreshe huduma zake kwa wasafiri, kujiendesha, kuzalisha faida na hatimaye kuongeza pato la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo ilielezwa hapo awali, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* kwa kufikia malengo ya makusanyo waliyojiwekea. Hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba, Mamlaka hiyo ina uwezo wa kuongeza vyanzo vyake vya mapato na kutoa huduma bora zaidi kwa abiria na mizigo iwapo tu, watawezeshwa kisheria kubakiza fedha itokanayo na tozo ya huduma kwa ajili ya abiria *(Passenger Service Charges)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha ilikuwa ikiipatia *TAA* fedha zitokanazo na tozo ya huduma abiria kwa mfumo wa *retention*. Hata hivyo, mnamo mwaka 2017, Serikali ilifuta utaratibu wa *retention* kwa taasisi za Umma kupitia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, Kifungu 58. Kielelezo Na. 11 kinafafanua tofauti ya makusanyo na marejesho ya tozo hiyo kati ya mwaka wa fedha 2013/2014 na 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali iwasilishe marekebisho ya sheria yatakayoweka utaratibu wa kisheria, kubakiza kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* walau 40% ya fedha zitokanazo na kodi ya huduma za wasafiri ili kuipunguzia taasisi hiyo utegemezi kwa kutegemea Serikali Kuu na kuiwezesha kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa Bajeti ya *TASAC* hususan katika miradi ya maendeleo Kamati haikuridhishwa na mipango ya utekelezaji wa Mradi wa Usalama wa Usafiri Majini wa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kuisimamia *TASAC* ili fedha za maendeleo zilizopangwa kwa

mwaka wa fedha 2024/2025 zitekeleze shughuli halisi zinazogusa usalama wa usafiri majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli hizi ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya uokozi, huduma za dharura na ujenzi wa vituo vya uratibu wa shughuli za uokozi katika maeneo ambayo itakuwa rahisi kutoa msaada wa haraka iwapo ajali zitatokea katika eneo lolote ndani ya maziwa na bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maboresho ya miundombinu – Kiwanja cha Ndege cha Bukoba, Kamati inatambua kwamba, Serikali kupitia *TAA* na *TCIA* iko katika hatua ya kujenga mnara wa kuongoza ndege *(Control Tower)* pamoja na kuweka taa ili kuwarahisishia marubani kuona njia ya ndege ya *runway* kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti tayari kulikuwa na mapendekezo ndani ya Serikali ya kujenga uwanja mpya katika eneo la Omukajunguti, ingawa bado Serikali inasisitiza kwamba uwanja unaotumika sasa bado ni salama na unaweza kuendelea kutumika iwapo miundombinu itaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina na kuliarifu Bunge lako mpango wa kudumu wa kutatua changamoto za usalama wa ndege katika uwanja wa Bukoba, Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninamshukuru Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, na Wenyeviti wa Bunge kwa kusaidia kuendesha vikao vya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati kabisa ninawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zilizo chini yake. Maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Kwa sababu ya muda, naomba majina yao yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, Mbunge kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati, akisaidiwa na Naibu Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile. Aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi Prof. Godius Kahyalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, ninawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, ninaomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 62 - Wizara ya Uchukuzi, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

6 MEI, 2024

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA FUNGU 62 - WIZARA YA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 na imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

a) **Sehemu ya Kwanza** ni Utangulizi na inaeleza kuhusu Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeza majukumu yake;

b) **Sehemu ya Pili** inaeleza kuhusu Uchambuzi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

c) **Sehemu ya Tatu** ni Uchambuzi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

d) **Sehemu ya Nne** ni Maoni na Mapendekezo yaKamati; na

e) **Sehemu ya Tano** ni Hitimisho.

1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Majukumu yake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti mbalimbali yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilifanya yafuatayo: -

a) Kupokea na kufanya uchambuzi wa Randama ya Wizara (Kanuni ya 115 (1));

b) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 (Kanuni ya 117 (1));

c) Kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na

d) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA FUNGU 62 - WIZARA YA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

2.1 Msingi na Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inalipa Bunge madaraka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti. Kwa muktadha huo, Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni

za Kudumu za Bunge imeweka masharti kwa Kamati za Kisekta kufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi za Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia msingi wa uchambuzi, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Fungu 62 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2).

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

a) Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli
b) Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida
c) Utekelezaji wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

2.2 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi** ilitengewa bajeti ya jumla ya **Sh. 2,089,245,508,000**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 118,215,599,000** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 1,971,029,909,000** zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imepokea **Sh. 1,820,698,515,147.48** sawa na wastani wa **asilimia 87.15** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Sh. 56,968,628,462.72** zilikuwa ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Sh. 1,763,729,886,684.76** ni fedha za bajeti ya maendeleo kama ambavyo **Kielelezo Na. 1** kinafafanua.

**KIELELEZO NA. 1 – MWENENDO WA UPATIKANAJI WA FEDHA WA FUNGU 62 KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

| MAPOKEZI | BAJETI YA MWAKA 2023/2024 (TZS) | MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 (TZS) | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | 118,215,599,000 | 56,968,628,462.72 | 48.19% |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | 1,971,029,909,000 | 1,763,729,886,684.76 | 89.48% |
| **JUMLA** | **2,089,245,508,000** | **1,820,698,515,147.48** | **87.15%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 62 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha katika Bajeti ya Fungu 62 hususan katika Miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ambayo ni **asilimia 48.19** kwa sababu unaathiri shughuli za kila siku za Wizara pamoja na taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika**, ni vema Serikali ikaweka kipaumbele cha kutoa fedha za matumizi ya kawaida kwa uwiano unaostahili ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa kila siku wa Wizara na taasisi zake.

2.3 **Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake ziliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. 3,064,641,847,131** kutoka katika vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Februari, 2024, makusanyo yalikuwa ni **Sh. 1,697,912,693,717.31** sawa na **asilimia 55.40** ya malengo waliyojiwekea. Mchanganuo wa mwenendo wa makusanyo unafafanuliwa katika **Kielelezo Na. 2**.

**KIELELEZO NA. 2 – MWENENDO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

| CHANZO | MALENGO BAJETI YA 2023/2024 | MAKUSANYO KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | % |
|---|---|---|---|
| KADCO | 34,814,424,120 | 27,237,967,569.16 | 78.24% |
| SINOTASHIP | 18,546,269,583 | 13,625,676,682 | 73.47% |
| TAA | 142,002,931,143 | 103,714,282,582.32 | 73.04% |
| TCAA | 92,000,000,000 | 66,055,801,114.17 | 71.80% |
| DMI | 14,883,538,644 | 10,408,432,693 | 69.93% |
| TASAC | 76,000,000,000 | 46,881,415,000 | 61.69% |
| ATCL | 482,205,391,833 | 282,199,943,399.97 | 58.52% |
| LATRA | 40,100,000,000 | 22,753,660,000 | 56.74% |
| TPA | 1,858,000,000,000 | 1,020,998,189,000 | 54.95% |
| NIT | 25,500,000,000 | 12,886,186,874 | 50.53% |
| TMA | 18,164,798,745 | 7,317,026,900 | 40.28% |
| TAZARA | 120,000,000,000 | 46,055,425,801.94 | 38.38% |
| MSCL | 17,306,085,200 | 5,543,042,653.88 | 32.03% |
| TRC | 125,118,407,863 | 32,235,643,446.87 | 25.76% |
| **JUMLA** | **3,064,641,847,131** | **1,697,912,693,717.31** | **55.40%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 62 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, kwa wastani, mwenendo wa makusanyo ya **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni wa kuridhisha. Taasisi nne (4) chini ya Fungu hilo zimefanya vizuri kwa kukusanya zaidi ya asilimia 70 kufikia Februari, 2024, taasisi sita (6) zilikusanya kati ya asilimia 50 hadi 70, wakati taasisi nne (4) zilikusanya chini ya asilimia 50.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inazipongeza taasisi ambazo zilikusanya vizuri na na inaishauri Serikali kuendelea kufanya mapitio ya mara kwa mara ili kubaini uwezo wa kila taasisi kukusanya kulingana na vyanzo vya mapato vilivyopo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Kamati haikuridhishwa na taasisi ambazo makusanyo yake yalikuwa chini ya asilimia 50. Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zilizosababisha makusanyo ya taasisi hizo kuwa hafifu. Kwa mfano, hadi kufikia Februari, 2024, Shirika la Reli Tanzania (TRC) lilikusanya **asilimia 25.76** ya makadirio waliyojiwekea katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kamati ilitaarifiwa kwamba, Shirika la Reli lilikabiliwa na changamoto zifuatazo ambazo ziliathiri mwenendo wa makusanyo:-

a) Kuharibika kwa miundombinu ya reli nchini kutokana na mvua kubwa zilizonyesha katika maeneo mbalimbali nchini hivyo kuathiri makusanyo yatokanayo na usafirishaji wa abiria na mizigo; na

b) Kutoanza kwa safari za treni katika reli mpya ya SGR kwa kipande cha Dar es Salaam – Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua juhudi za Serikali za kuhakikisha changamoto zilizoainishwa hapo juu zinatatuliwa kwa haraka. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serika kuhakikisha kwamba, wakati wote kunakuwa na fungu maalum linalotosheleza kukabiliana na uharibifu unaoweza kujitokeza katika miundombinu ya reli. Uwepo wa fungu hilo uende sambamba na kuwa na mkakati endelevu wa kukabiliana na dharura za uharibifu wa miundombinu ya reli *(emergency and contingency strategy for rehabilitation of railways infrastructures*).

**Mheshimiwa Spika,** Mkakati huo pamoja na fungu tajwa vitasaidia Serikali kukarabati miundombinu ya reli kwa haraka zaidi pale inapoharibika ili kuendelea kutoa huduma za usafirishaji wa mizigo na abiria na hivyo kuendelea kukusanya mapato. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, Shirika la Reli linaanza

mara moja safari za treni kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma katika Reli Mpya ya SGR ili kuongeza makusanyo ya mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaishauri Serikali kuandaa Moduli ya Kiuchumi na Kifedha kubainisha mtiririko wa mapato na matumizi ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa miaka ijayo. Moduli hiyo italiwezesha Shirika kuwa na maoteo yenye uhakika wa makusanyo na matumizi bora ya fedha za umma katika uendeshaji wa Shirika kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), mgao wa makusanyo yalikuwa ni **asilimia 38.38** ya makadirio waliyojiwekea kufikia Februari, 2024. Kamati imebaini kwamba, makusanyo hayo hafifu yamesababishwa na changamoto mbalimbali za kiuendeshaji, ambapo utatuzi wa changamoto hizo upo katika hatua mbalimbali kwa kuhusisha nchi yetu na Zambia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na Serikali ya Zambia, kuhakikisha kwamba inaboresha uendeshaji wa TAZARA ili kuimarisha makusanyo ya taasisi.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilikusanya **asilimia 40.28** ya malengo waliyojiwekea. Kamati ilibaini kwamba, makusanyo hafifu ya TMA yalisababishwa na kutokuwepo kwa makadirio yenye uhalisia kutokana na taasisi hiyo kutarajia vyanzo vipya vya mapato ambavyo havikuanza kufanya kazi.

**Mheshimiwa Spika**, huduma ya hali ya hewa ni muhimu katika mustakabali wa sekta mbalimbali nchini ikiwemo ujenzi, kilimo, uvuvi, viwanda, maji, usafiri, usafirishaji, mifugo, shughuli za biashara n.k. Iwapo huduma hii itapewa kipaumbele katika kuwezesha kukusanya kutoka sekta mbalimbali, itawezesha TMA kuimarisha miundombinu ya utabiri wa hali ya hewa na hatimaye kuongeza ufanisi na weledi wa wafanyakazi katika kutoa matokeo bora na sahihi zaidi ya masuala ya hali ya hewa.

2.4 Utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Uchukuzi ilitengewa jumla ya **Sh. 118,215,599,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizo zinajumuisha **Sh. 89,291,108,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi (PE) wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake na **Sh. 28,924,491,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari 2024, jumla ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizokuwa zimetolewa ni **Sh. 56,968,628,462.72** sawa na **asilimia 48.19** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo**, Sh. 45,870,961,503.33** zilkuwa ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi (P.E.) na **Sh. 11,097,666,959.39** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C.) kama ambavyo Kielelezo Na. 3 kinafafanua.

**KIELELEZO NA. 3 – MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KUFIKIA FEBRUARI, 2024**

| CHANZO | BAJETI YA MWAKA 2023/2024 | MAPOKEZI YA FEDHA KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | % |
|---|---|---|---|
| Wizara | 12,558,871,900 | 5,487,547,939.44 | 43.69% |
| TCAA | 10,929,320,000 | 0.00 | 0% |
| TMA | 12,875,744,276 | 6,873,959,982.80 | 53.39% |
| MSCL | 4,169,964,487 | 371,819,719.98 | 8.92% |
| TAA | 30,619,351,950 | 14,993,379,714.36 | 48.97% |
| ATCL | 3,886,680,000 | 2,591,120,040 | 66.67% |
| TRC | 12,922,957,000 | 8,615,304,432 | 66.67% |
| TAZARA | 14,983,217,000 | 9,988,812,000 | 66.67% |
| NIT | 10,611,880,387 | 5,815,364,448.83 | 54.80% |
| DMI | 4,657,612,000 | 2,231,320,185.31 | 47.91% |
| **JUMLA KUU** | **118,215,599,000** | **56,968,628,462.72** | **48.19%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 62 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya jambo mahsusi lililobainiwa na Kamati katika mwenendo wa mapokezi ya fedha za Matumizi ya Kawaida, ni kwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) kutopokea fedha kabisa. Kamati inatambua kwamba, TCAA inajitegema kiuendeshaji na kwa muktadha huo, Mishahara pamoja na Matumizi Mengineyo hulipwa kutoka katika vyanzo vyake. Hata hivyo, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilitenga **Sh. 10,929,320,000** kama sehemu ya utekelezaji wa uendelezaji wa Chuo cha Usafiri wa Anga na hadi kufikia Februari, 2024 hakuna fedha iliyotolewa. Kamati ilitaarifiwa kwamba, sababu za kutotolewa kwa fedha hiyo ni TCAA kutokuwa na Mkataba wa Uendelezaji wa Chuo husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, inaharakisha michakato yote muhimu ili fedha za matumizi ya kawaida zinatolewa kwa wakati kutekeleza malengo yaliyokusudiwa kabla ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 kuisha.

2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Uchukuzi ilitengewa jumla ya **Sh. 1,971,029,909,000** ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 1,863,764,800,000** zilikuwa ni fedha za ndani, na **Sh. 107,265,109,000** zilikuwa ni fedha za nje. Mwenendo wa Mapokezi ya Fedha za Maendeleo unafafanuliwa katika Kielelezo Na. 4 kwa muhtasari.

**KIELELEZO NA. 4 - MWENENDO WA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MAENDELEO BAJETI YA 2023/2024**

| CHANZO | BAJETI YA MWAKA 2023/2024 (TZS) | MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 (TZS) | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA NDANI** | 1,863,764,800,000 | 1,671,982,467,124.76 | 89.71% |
| **FEDHA ZA NJE** | 107,265,109,000 | 91,747,419,560 | 85.53% |
| **JUMLA** | **1,971,029,909,000** | **1,763,729,886,684.76** | **89.48%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 62 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa mapokezi ya Fedha za Maendeleo na inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya sekta ya uchukuzi.

2.6 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1), Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kati ya tarehe 12 – 17 Machi, 2024 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Simiyu na Mwanza. Katika ziara hiyo, Kamati ilifanya tathmini ya baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Tathmini iliyofanyika ilijumuisha uchambuzi wa mapokezi ya fedha, hali ya utekelezaji wa miradi husika pamoja na changamoto za utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

### 2.6.1 **Mradi Na. 4281 Ujenzi wa SGR Kipande cha Tatu (Makutupora - Tabora)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa SGR **Kipande cha Tatu** unahusisha ujenzi wa reli kutoka Makutupora, Singida hadi Tabora yenye urefu wa **kilometa 368**. Mkandarasi wa Mradi ni Kampuni ya Yapi Merkezi kutoka Uturuki. Mradi ulianza kutekelezwa tarehe 8 Machi, 2022 kwa lengo la kukamilika tarehe 07 Januari, 2026 kwa thamani ya **Dola za Kimarekani 1,923,695,000** (**Sh. 4,809,237,500,000**).[1] Hadi kufikia Machi, 2024, Serikali ilikuwa imefanya malipo kwa Mkandarasi ya jumla ya **Dola za Kimarekani 476,726,122.08** (**Sh. 1,191,815,305,200**) sawa na **asilimia 24.78.**

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati inatembelea ili kukagua Mradi Mwezi Machi, 2024, maendeleo ya utekelezaji wake yalikuwa ni **asilimia 14** tu ambayo kwa maoni ya Kamati, hayaakisi kiwango cha fedha kilichotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kwamba, Mradi unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo: -

a) Serikali kuchelewa kufanya malipo kwa mshauri sanifu *(design consultant)* ambapo imesababisha kukwama kwa kazi za usanifu na ujenzi kwa Kipande cha III;

b) Mkandarasi kuchelewa kununua malighafi na vifaa vya ujenzi na kusababisha kushindwa kukamilika kwa wakati kwa baadhi ya kazi mfano ujenzi wa makambi na madaraja;

c) Mkandarsasi kulundika madeni ya wasambazaji wa vifaa na huduma *(suppliers)*; na

d) Serikali kutolipa fedha za fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yalitwaliwa kupisha Mradi.

[1] USD 1= TZS 2,500

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali, kuharakisha mchakato wa malipo kwa kwa mshauri sanifu *(design consultant)* na kulipa fidia kwa wananchi wote ambao maeneo yao yamechukuliwa kupisha Mradi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Kamati ilihoji iwapo kuna hatua zozote zilizochukuliwa kuunusuru Mradi kwa kuzingatia changamoto za kiuchumi ambazo Mkandarasi anazipitia. Serikali ilitoa maelezo kwamba imechukua hatua mbalimbali zikiwemo zifuatazo: -

a) Kutoa taarifa *(notice)* mbalimbali za Kimkataba kuhusu kudai haki *(claims)* za ucheleweshaji wa utekelezazaji wa Mradi;

b) Serikali imesaini hati ya makubaliano na Mkandarasi ili kwamba fedha inayokuja, Shirika la Reli (TRC) liamue kwamba fedha hiyo itumike kulipa kwanza wakandarasi wa ndani *(suppliers and subcontractors)*;

c) Kutumia fedha ya zuio *(retention)*, ambayo ni ya Mkandarasi, inayokatwa katika hati za malipo *(certificate)* kama *bank guarantee* ili fedha hiyo pia itumike kulipa madeni; na

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mradi huu kwa kuzingatia mtaji ambao tayari Serikali imeuweka, uwezo wa Mkandarasi kukamilisha Mradi kwa ubora unaotakiwa pamoja na athari ambazo zinaweza kujitokeza iwapo mradi huo utachelewa kukamilika. Tathmini hiyo itoe mapendekezo ya haraka ambayo yatawezesha mradi huo kukamilika ili kuokoa Fedha za Serikali.

### 2.6.2 **Mradi Na. 4281 Ujenzi wa SGR Kipande cha Tano (Isaka - Mwanza)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Ujenzi wa SGR Kipande Tano, unahusisha ujenzi wa reli kutoka Isaka (Shinyanga) hadi Mwanza, chenye urefu wa

kilometa 341. Mradi ulianza kutekelezwa tarehe 15 Mei, 2021 kwa lengo la kukamilika ifikapo tarehe 14 Mei, 2024 kwa thamani ya **Dola za Kimarekani 1,326,077,288.76** (**Sh. 3,315,193,221,900**). Mkandarasi wa Mradi ni Kampuni ya CCECC kutoka China.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2024 wakati Kamati inatembelea Mradi, Serikali ilikuwa imeshafanya malipo kwa Mkandarasi ya jumla ya **Dola za Kimarekani 537,511,387.73** (**Sh. 1,343,778,469,325**) sawa na **asilimia 40.53** ya gharama za Mradi. Aidha, maendeleo ya mradi huo yalikuwa yamefikia **asilimia 54.01**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina mashaka kuhusu muda uliobaki kukamilsha Mradi husika kufikia Mei, 2024 ukilinganisha na asilimia iliyobaki ya ujenzi. Serikali ilitaarifu Kamati kwamba, wana matumaini kuwa Mkandarasi atakamilisha ujenzi kwa sababu kazi iliyobaki sio kubwa ukilinganisha na kazi iliyofanyika tayari.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto ya malalamiko ya baadhi ya wananchi kutolipwa fedha za fidia kutokana na kutwaliwa kwa maeneo yao kupisha Mradi. Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha kwamba wananchi waliopisha Mradi, wanalipwa fidia stahiki kwa mujibu wa Sheria za Nchi.

### 2.6.3 **Mradi Na. 4290 – Rada, Mitambo na Miundombinu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), Mwanza**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Rada katika Eneo la Kiseke, Mkoa wa Mwanza ni Mradi wa pili kutekelezwa baada ya Mradi wa Rada ya Dar es Salaam katika mfululizo wa Rada 7 zilizopangwa kutekelezwa kwenye malengo ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu umetumia kiasi cha **Shillingi Bilioni 4.353**. Gharama hizo zinajumuisha ununuzi, na ufungwaji wa mtambo wa Rada, miundombinu ya majengo, barabara yenye urefu wa kilometa 1.1 kuelekea kwenye kilima cha Ngitiri, Kiseke,

Wilaya ya Ilemela pamoja na gharama za kuweka njia ya umeme mkubwa 11KV pamoja na ufungaji wa transfoma katika kituo cha RADA.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara ya ukaguzi wa Mradi huu, Kamati ilijionea na kupata maelezo kutoka Serikalini kwamba, Rada iliyofungwa Eneo la Kiseke ina uwezo wa kufuatilia matukio ya hali ya hewa katika eneo la nusu kipenyo cha kilometa 450 kutoka eneo ilipofungwa. Hivyo basi, ukanda Ziwa Victoria ikijumuisha mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara iko katika uangalizi wa hali ya hewa kupitia Rada hiyo. Aidha, Serikali ilibainisha kwamba, Rada hiyo inaendana na mabadiliko ya teknolojia katika kutoa taarifa sahihi za utabiri wa hali ya hewa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudi za Serikali katika kuboresha Sekta ya Hali ya Hewa nchini.

### 2.6.4 **Mradi Na. 4201 – Ujenzi wa Kituo cha Kikanda cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji Majini (MRCC)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kikanda cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji Majini *(Maritime Rescue Coordination Centre - MRCC)* ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Kimataifa wa Mawasiliano na Uchukuzi katika Ziwa Victoria (Multinational Lake Victoria Maritime Communications and Transport Project - MLVMCTP) unaotekelezwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) katika Eneo la Ilemela, Jijini Mwanza. Mradi unatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uganda. Mkandarasi wa Mradi ni CK Asscociates Co. Ltd akishirikiana na Oubuntu Consulting Co. Ltd.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mradi ulitengewa jumla ya **Sh. 4,769,673,000** kwa ajili ya usanifu na ujenzi uliopangwa kukamilika ifikapo Novemba, 2024. Hadi kufikia Machi, 2024 fedha iliyolipwa kutekeleza mradi ilikuwa **Sh. 953,934,600** sawa na **asilimia 20** tu.

**Mheshimiwa Spika**, mapokezi yasiyoridhisha ya fedha za mradi, kwa sehemu kubwa yameathiri utekelezaji wa Mradi ambapo hadi Kamati inafika uwandani kwa ajili ya ukaguzi, ujenzi wa mradi ulikuwa ni **asilimia 10** tu.

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la Mradi ni kuimarisha usalama wa usafiri majini katika Ziwa Victoria, hasa kutokana na matukio mbalimbali ya ajali zilizotokea majini. Kamati imebaini kwamba, katika kipindi cha miaka mitano kwa upande wa Tanzania, watu 2,421 walipata ajali ambapo kati ya hao, 2,275 waliokolewa na watu 202 walifariki. Kwa muktadha huo, Mradi unakusudiwa kujenga miundombinu ya kuratibu utafutaji na uokoaji, pamoja na kununua vifaa vya zoezi hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kwa kuibua Mradi ambao utasaidia kuboresha usalama wa raia katika usafiri wa maji kwenye Ziwa Victoria. Hata hivyo, kwa kuzingatia kuchelewa kwa Mradi huu, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa mradi huo unakamilika kwa wakati.

### 2.6.5 **Mradi Na. 4227 - Uboreshaji wa Bandari ya Mwanza Kaskazini, katika Ziwa Victoria**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unahusisha ujenzi, upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya Bandari ya Mwanza Kaskazini (North Port), katika Ziwa Victoria na unatekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA). Mradi una thamani ya **Sh. 18,606,443,416.66** na ulianza kutekelezwa tarehe 03 Mei, 2023 kwa lengo la kukamilika tarehe 02 Novemba, 2024. Mkandarasi wa Mradi ni Kampuni ya M/S China Railway 15 Bureau Group Corporation (CR15G) ya China, na Mhandisi Mshauri ni Kampuni ya M/S Dar Al – Handasah Consultants ya Lebanoni inayoshirikiana na Kampuni ya M/S Inter-Consult ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa ziara ya ukaguzi Kamati ilijionea maendeleo mbalimbali ya mradi ikiwemo shughuli ya kuongeza kina cha maji *(dredging)* ili kuanza ujenzi wa gati. Kwa ujumla Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi kwa kuwa maendeleo ya

mradi huo yalikuwa ni **asilimia 30** ukilinganisha na matarajio ya **asilimia 46** kulingana na mpango wa utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zilizosababisha kusuasua kwa mradi. Moja ya changamoto hizo ni kuwepo kwa shughuli za ujenzi unaoingilia huduma za kila siku zitolewazo na bandari. Muingiliano huu sio tu unachelewesha mradi, lakini pia unasababisha usumbufu kwa watumiaji wengine wa huduma za bandari. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina ili kubuni namna bora ya kutekeleza mradi kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imebaini kuwepo na changamoto ya ufinyu wa eneo la mradi ambalo umeathiri usanifu wenye tija wa matumizi ya eneo la bandari. Ufinyu wa eneo umetokana na muingiliano wa kimipaka na kituo cha polisi linalomilikiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, Serikali imefanya jitihada na tayari mazungumzo yamefanyika ambapo Wizara imekubali kuachia sehemu ya eneo lake ili kuruhusu upanuzi wa mipaka ya eneo la Mamlaka ya Uendeshaji wa Bandari. Hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba, kuna umuhimu wa Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Wizara ya Ardhi na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, kufanya tathmini ya mahitaji ya eneo linalohitajika, ikiwemo kufanya uhakiki ili kubaini maeneo ambayo yanamilikiwa na Serikali ili kuboresha miundombinu ya bandari hii muhimu.

### 2.6.6 **Mradi Na. 4295 - Ujenzi na Ukarabati wa Meli katika Ziwa Victoria**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi unahusisha Ujenzi wa Meli Mpya ya MV Mwanza - Hapa Kazi Tu, Ujenzi wa Meli ya Kubeba Mizigo *(Ro-Ro & Wagon Ferry)*, Ukarabati wa Meli ya MT Ukerewe, na Ukarabati wa Meli ya MT Nyangumi. Utekelezaji wa ujenzi na ukarabati wa meli hizo uko katika hatua mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa ukaguzi wa mradi, Kamati ilipata fursa ya kujionea maendeleo ya Ujenzi wa Meli Mpya ya MV Mwanza – Hapa Kazi Tu ambayo ikikamilika itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200, mzigo wa tani 400, magari madogo 20 na malori 3. Wakandarasi wa Mradi huu ni Kampuni za GAS Entec Co. Ltd na Kangnam Corporation kutoka nchi ya Korea ya Kusini, wakishirikiana na SUMA JKT ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, gharama za utekelezaji wa mradi kuwa jumla ya D**ola za Kimarekani 49,322,365.40** (**Sh. 123,305,913,500**) ambapo hadi wakati Kamati inafanya ziara ya ukaguzi, Mkandarasi alikuwa ameshalipwa **asilimia 90.87** ya gharama zote za mradi na maendeleeo ya ujenzi kufikia **asilimia 93**. Inatarajiwa kwamba, mradi utakamilika ifikapo tarehe 31 Mei, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba kazi zinazoendelea ni kukamilisha mifumo ya uendeshaji wa meli kwa matarajio ya kufanya safari ya kwanza ya majaribio ya kiufundi ambayo ilifanyika tarehe 25 hadi 27 Machi, 2024. Safari hiyo ya majaribio ilifanyika kwa mafanikio.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya maendeleo ya mradi wa MV Mwanza – Hapa Kazi Tu, meli ambayo itahudumia wananchi walio wengi katika Ukanda wa Ziwa Victoria.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FUNGU 62 - WIZARA YA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 3.1 Vipaumbele vya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi inalenga kutekeleza vipaumbele mbalimbali vya kibajeti vikiwemo vifuatavyo: -

a) **Usafiri wa Reli**: Kuendeleza ujenzi na uendeshaji wa SGR na kuboresha miundombinu ya reli ya MGR na CGR, pamoja na ununuzi wa vifaa;

b) **Usafiri wa Anga**: Kuboresha uendeshaji wa ATCL, kuimairisha miundombinu ya viwanja vya ndege na kujenga viwanja vipya**;**

c) **Usafiri wa Majini**: Kuimarisha usafiri, usalama na mawasiliano katika Maziwa Makuu nchini;

d) **Usafiri Ardhini**: Kuimarisha usalama, udhibiti na utoaji wa huduma za usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo;

e) **Bandari**: Kuboresha miundombinu na uendeshaji wa bandari nchini ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa bandari kavu;

f) **Hali ya Hewa**: Kuimarisha miundombinu na huduma za hali ya hewa; na

g) **Vyuo vya Sekta ya Uchukuzi**: Kuimarisha mafunzo, miundombinu na vifaa vya kufundishia katika vyuo vya mafunzo.

3.2 Muundo wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Uchukuzi (Fungu 62) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 2,729,676,417,000** ambapo kati ya fedha inayoombwa, **Sh. 114,744,476,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Sh. 2,614,931,941,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, fedha inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa wastani wa **asilimia 30.65** ukilinganisha na Bajeti ya **Sh. 2,089,245,508,000** iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. Kielelezo Na. 5 kinafafanua kwa muhtsari ulinganisho kati ya

Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**KIELELEZO NA. 5 – ULINGANISHO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

| MAELEZO | BAJETI YA MWAKA 2023/2024 | BAJETI YA MWAKA 2024/2025 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | 118,215,599,000 | 114,744,476,000 | -3,471,123,000 | -2.93% |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | 1,971,029,909,000 | 2,614,931,941,000 | +643,902,032,000 | +32.67% |
| **JUMLA** | **2,089,245,508,000** | **2,729,676,417,000** | **640,430,909,000** | **+30.65%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 62 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, ongezo la Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni kutokana na Serikali kuongeza **Sh. 643,902,032,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, kama ambavyo Kielelezo Na. 5 kinavyoonesha, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepungua kwa **asilimia 2.93** ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha.

3.3 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Sh. 3,310,021,435,500** ambayo ni ongezeko la **Sh. 245,379,588,369** ikilinganishwa na malengo ya kukusanya **Sh. 3,064,641,847,131** katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Ongezeko hilo ni wastani wa **asilimia 8.01** kwa mchanganuo unaopatikana katika Kielelezo Na. 6.

**KIELELEZO NA. 6 – ULINGANISHO WA MAKADIRO YA MAKUSANYO KATIKA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MAKUSANYO 2023/2024 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO 2024/20245 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| ATCL | 482,205,391,833 | 717,967,025,000 | 235,761,633,167 | +48.89% |
| KADCO | 34,814,424,120 | 40,462,521,000 | 5,648,096,880 | +16.22% |
| TAA | 142,002,931,143 | 161,180,246,500 | 19,177,315,357 | +13.50% |
| DMI | 14,883,538,644 | 16,353,876,000 | 1,470,337,356 | +9.88% |
| LATRA | 40,100,000,000 | 43,890,000,000 | 3,790,000,000 | +9.45% |
| TASAC | 76,000,000,000 | 82,849,799,000 | 6,849,799,000 | +9.01% |
| NIT | 25,500,000,000 | 27,500,000,000 | 2,000,000,000 | +7.84% |
| TCAA | 92,000,000,000 | 98,701,888,000 | 6,701,888,000 | +7.28% |
| SINOTASHIP | 18,546,269,583 | 19,700,170,000 | 1,153,900,417 | +6.22% |
| MSCL | 17,306,085,200 | 17,646,048,000 | 339,962,800 | +1.96% |
| TPA | 1,858,000,000,000 | 1,837,781,845,000 | -20,218,155,000 | -1.08% |
| TRC | 125,118,407,863 | 118,894,300,000 | -6,224,107,863 | -4.97% |
| TAZARA | 120,000,000,000 | 111,113,717,000 | -8,886,283,000 | -7.41% |
| TMA | 18,164,798,745 | 15,980,000,000 | -2,184,798,745 | -12.03% |
| **JUMLA** | **3,064,641,847,131** | **3,310,021,435,500** | **245,379,588,369** | **+8.01%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 62 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa ujumla na hususan taasisi ambazo zimeongeza wigo wa makadirio ya makusanyo yake. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba, baadhi ya taasisi zimekadiria kukusanya maduhuli pungufu ukilinganisha na makadirio waliyojiwekea katika Mwaka wa Fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imefanya tathmini ya baadhi ya taasisi kupunguza makadirio ya makusanyo. Katika tathmini hiyo Kamati ina maoni kwamba, kupungua kwa makadirio ya

makusanyo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 hakuakisi malengo makuu ya uendeshaji wa taasisi hizo kutoa mchango stahiki katika Mfuko Mkuu wa Serikali, na kutekeleza kwa ufanisi malengo ambayo Wizara ya Uchukuzi imejiwekea.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mfano, makadirio ya makusanyo ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) yamepungua kwa **asilimia 12.03**. Hata hivyo, Kamati inatambua kwamba taasisi hiyo inaweza kuongeza vyanzo vyake vya mapato iwapo Serikali na wadau wote wa hali ya hewa nchini watachangia pesa kidogo katika huduma itolewayo na mamlaka hiyo muhimu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mfano, Shirika la Reli Tanzania (TRC) ambalo makadirio ya makusanyo yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 yamepungua kwa **asilimia 4.97**. Kamati ina maoni kwamba, iwapo TRC itafanya tathmini upya ya uwezo wake wa kukusanya maduhuli, hasa kwa kuongeza huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo na uendeshaji wenye ufanisi wa SGR kipande cha Dar es Salaam – Dodoma, makusanyo yanaweza kuongezeka. Pamoja na kwamba Kamati inatambua changamoto za uharibifu uliojitokeza katika miundombinu ya reli, Serikali ifanye tathmini itakayoboresha uendeshaji wa Shirika la Reli ili kuongeza mapato ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

3.4 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/205, **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi** inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 114,744,476,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Sh. 86,661,930,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 28,082,546,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepungua kwa **Sh. 3,471,123,000** sawa **asilimia 2.94** ukilinganisha na **Sh. 118,215,599,000** iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ambavyo Kielelezo Na. 7 kinaonesha.

**KIELELEZO NA. 7 – ULINGANISHO WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA KATI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA MWAKWA WA FEDHA 2024/2025**

| MATUMIZI YA KAWAIDA | BAJETI YA MWAKA 2023/2024 | BAJETI YA MWAKA 2024/2025 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| **MISHAHARA (P.E.)** | 89,291,108,000 | 86,661,930,000 | 2,629,178,000 | -0.94% |
| **MATUMIZI MENGINEYO (O.C.)** | 28,924,491,000 | 28,082,546,000 | 841,945,000 | -2.915 |
| **JUMLA** | **118,215,599,000** | **114,744,476,000** | **3,471,123,000** | **-2.94%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 62 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida imepungua kwa sababu ya kupungua kwa ukomo wa bajeti *(ceiling)* ambao umeathiri sehemu kubwa ya Bajeti ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na sababu zilizoainishwa hapo juu, Kamati haijaridhishwa na kupungua kwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida hasa kwa kuzingatia kwamba, Sekta ya Uchukuzi bado ina mahitaji mengi ya rasilimali watu, vitendea kazi pamoja na fedha za uendeshaji. Kwa muktadha huo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza fedha za Matumizi ya Kawaida kwa namna inayoakisi kuongezeka kwa fedha za Miradi ya Maendeleo.

3.5 Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 2,614,931,941,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, **Sh. 2,524,369,202,000** ni Fedha za Ndani, sawa na **asilimia 96.54** na **Sh. 90,562,739,000** ni Fedha za Nje, sawa na **asilimia 3.46** ya bajeti iliyotengwa.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa wastani wa **asilimia 32.67** ukilinganisha na Bajeti ya **Sh. 1,971,029,909,000** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ongezeko hilo linajionyesha katika Kielelezo Na. 8.

**KIELELEZO NA. 8 – ULINGANISHO WA BAJETI YA MIRADI YA MAENDELEO KATI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA MWAKWA WA FEDHA 2024/2025**

| MIRADI YA MAENDELEO | BAJETI YA MWAKA 2023/2024 | BAJETI YA MWAKA 2024/2025 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA NDANI** | 1,863,764,800,000 | 2,524,369,202,000 | 660,604,402,000 | **+**35.44% |
| **FEDHA ZA NJE** | 107,265,109,000 | 90,562,739,000 | 16,702,370,000 | **-**15.57% |
| **JUMLA** | **1,971,029,909,000** | **2,614,931,941,000** | **643,902,032,000** | **32.67%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 62 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, katika ongezeko la jumla ya Bajeti ya Maendeleo, Kamati imebaini kwamba Bajeti ya Fedha za Ndani imeongezeka kwa **asilimia 35.44** wakati Bajeti ya Fedha za Nje kutekeleza miradi hiyo imepungua kwa **asilimia 15.57**. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kubajeti utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutenga zaidi fedha za ndani na kupunguza utegemezi wa Fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba, Fedha za Ndani zilizotengwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo zinatokana na mchango wa wananchi kupitia kodi. Kwa muktada huo, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kwamba, inasimamia kikamilifu ubora wa miradi ili kuwepo na thamani ya fedha *(value for money)*, na kuwepo kwa huduma bora za usafirishaji ambazo zitachochea ukuaji wa uchumi.

**SEHEMU YA NNE**

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ambayo kwa ufanisi mkubwa imeendelea kutoa fedha za kutekeleza majukumu mbalimbali ya **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi**, hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha miaka mitatu, Kamati imeshuhudia sehemu kubwa bajeti ya Sekta ya Uchukuzi ikitolewa kwa kiwango kinachoridhisha. Aidha, Kamati imebaini kwamba, miradi yote ya kimkakati ambayo ilianza kutekelezwa katika Serikali ya Awamu ya Tano, Serikali ya Awamu ya Sita imeitekeleza kwa ufanisi mkubwa. Kwa mfano, zaidi ya **asilimia 70** ya uendelezaji wa Mradi wa SGR umefanyika katika Awamu ya Sita.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo, na kwa kuthamini mtaji wa fedha za maendeleo unaotokana na kodi za wananchi, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

a) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika utendaji kazi utakaochochea kuboresha huduma za Sekta ya Usafirishaji nchini, kwa kuwa sekta hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi;

b) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika kukusanya maduhuli kutokana na vyanzo vilivyopo, na kubaini vyanzo vipya ambavyo vitaongeza wigo wa makusanyo hayo.

   Sambamba na hilo, Serikali ihakikishe kwamba, huduma zitolewazo na taasisi zake, zinakuwa bora ili kukidhi matarajio ya wadau muhimu wa sekta ya uchukuzi ambao wanachangia mapato; na

c) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu *(sustainability)* na kuwepo kwa thamani ya fedha *(value for money)*.

**Mheshimiwa Spika**, aidha Kamati inaishauri Wizara kuzisimamia taasisi zake kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yake yote kwa ufanisi. Kamati inaamini kwamba, iwapo kutakuwepo na usimamizi madhubuti, taasisi hizo zitaweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na wakati huo huo zitaongeza tija na hatimaye kuboresha huduma za uchukuzi na kuongeza mapato ya Serikali.

4.2 Maoni Mahsusi

4.2.1 **Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR na Uendeshaji wa TRC**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua ambayo imefikiwa na Serikali kwa treni ya umeme kufanya majaribio kwa mafanikio kusafirisha abiria kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma katika Reli ya Kisasa ya SGR. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba huduma rasmi za usafiri wa treni katika reli ya SGR kati ya Dar es Salaam na Dodoma zinaanza haraka ili kutoa huduma kwa wananchi, na kuongeza pato la Serikali. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya kuandaa Mkakati wa Kuboresha Makusanyo katika Reli ya MGR na CGR. Mkakati huo, unapaswa kwenda sambamba na juhudi za makusudi za kuboresha miundombinu ikiwemo kutenga bajeti ya matengenezo ya mara kwa mara, na ya haraka pale miundombinu ya reli hizo zinapoathiriwa na majanga kama vile mvua kubwa.


4.2.2 **Maboresho ya Uendeshaji wa Bandari Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua marekebisho ya sheria yaliyofanyika mwaka 2017 katika Sheria ya Bandari Sura ya 166 ili kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikusanye mapato ya *wharfage* katika bandari na kupelekwa katika akaunti maalum iliyofunguliwa katika Benki Kuu ya Tanzania (BOT). Mabadiliko hayo, yameweka utaratibu unaoitaka TPA kuwasilisha maombi ya fedha hizo

kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya uendeshaji kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.[2]

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia njema ya Serikali, na ili kuboresha utendaji wa TPA, Kamati inashauri kwamba, Sheria ya Bandari ifanyiwe tena marekebisho ili kwamba mapato yatokanayo na *wharfage* yakusanywe na kubaki TPA.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, mapato yatokanayo na *wharfage* yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021. Inatarajiwa kwamba ifikapo Mwaka wa Fedha 2026/2027, mapato hayo yatakuwa **Shilingi Trilioni 1.4.** Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, makadirio ya makusanyo yalikuwa ni **Shilingi Bilioni 592**, na inakadiriwa kwamba mapato hayo yataongezeka kufikia **Shilingi Bilioni 792.489** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ambavyo **Kielelezo Na. 9** kinaonesha.





***Chanzo**: Kumbukumbu za Vikao vya Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Kamati katika jambo hili yamejengwa katika msingi kwamba, Mamlaka ya Bandari ni moja kati

[2] **Wharfage:** Tozo inayotozwa kwa matumizi ya miundombinu ya bandari kulingana na mzigo mahali unapokwenda.

ya nyenzo kuu za makusanyo ya Serikali *(revenue facilitator)*. Kwa utafiti mdogo ambao Kamati imeufanya, imebaini kwamba katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, makusanyo ya TRA yalikuwa jumla ya **Sh. Trilioni 22.611**. Kati ya Fedha hizo, makusanyo ya ushuru wa forodha, ambao kwa sehemu kubwa unachangiwa na huduma zitolewazo na bandari, yalikuwa ni **Sh. Trilioni 9.354** sawa na **asilimia 41** ya makusanyo yote. Kielelezo Na. 10 kinafafanua zaidi.




***Chanzo**: Kumbukumbu za Vikao vya Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, kwa tutafiti huo, mchango wa bandari ni dhahiri na Kamati inaamini kwamba, iwapo TPA itakusanya *wharfage* kwa mujibu wa Sheria, Mamlaka hiyo itakuwa na uwezo wa kuendeleza miundombinu ya bandari ikiwemo ujenzi wa gati mpya, na hivyo kuongeza idadi ya shehena na hatimaye kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuongeza mapato yatokanayo na kodi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuongezeka kwa shehena katika bandari zetu, usafirishaji wa mizigo kwa njia ya reli na barabara utaongezeka na hatimaye kukuza uchumi wa nchi yetu. Aidha, iwapo *wharfage* itakusanywa na kutumika kikamilifu na TPA, Mamlaka hiyo itakuwa na uwezo wa kutumia dhamana ya fedha hizo kukopa katika taasisi za kifedha kwa kuwa itakuwa na chanzo cha uhakika wa mapato yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Kamati inapongeza juhudi zinazofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) katika uwekezaji na uboreshaji wa bandari nchini. Kwa kutambua hilo, Kamati inaishauri Serikali kuisaidia TPA kubainisha na hatimaye kutwaa maeneo yote ya kimkakati ambayo yataiwezesha mamlaka hiyo kuboresha miundombinu ya bandari nchini kabla ya maeneo hayo kumilikishwa kwa mtu au taasisi nyingine yoyote.

**4.2.3** Mradi wa Ujenzi wa Meli katika Ziwa Tanganyika

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilibaini kwamba, suala la usafiri wa maji katika Ziwa Tanganyika bado halijapatiwa ufumbuzi pamoja na kwamba bajeti ilitengwa kwa ajili ya mradi huo. Pamoja na kwamba Kamati ilitaarifiwa kwamba hatua za awali za kumpata mkandarasi zimekamilika, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka ili kuhakikisha kwamba Mradi wa Usafiri wa Meli katika Ziwa Tanganyika unaanza mara moja. Aidha, Serikali iongeze fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ili kuhakikisha kwamba mradi huo unakamilika na kuanza kutoa huduma za usafiri katika Ziwa Tanganyika.

4.2.4 **Uendeshaji wa Shirika la Ndege (ATCL)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kununua ndege za abiria na mizigo. Hata hivyo, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati inaishauri Serikali kubuni njia bora zaidi zitakazoongeza ufanisi wa uendeshaji wa ATCL ili Shirika hilo liboreshe huduma zake kwa wasafiri, kujiendesha, kuzalisha faida na hatimaye kuongeza pato la Serikali.

4.2.5 **Maboresho ya Uendeshaji wa Reli ya TAZARA**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba wabia wa uendeshaji wa Reli ya TAZARA, kwa maana ya Nchi ya Tanzania na Zambia wanakaa meza moja ya majadiliano kuhusu maboresho ya reli hiyo. Pamoja na jitihada hizo,


Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba reli hiyo inapata mwekezaji ambaye ataitumia Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kuunganisha utendaji wenye tija kiuchumi kupitia bandari hiyo.

4.2.6 **Utendaji wa TAA**

**Mheshimiwa Spika,** kama ambavyo ilielezwa hapo awali, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kwa kufikia malengo ya makusanyo waliyojiwekea. Hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba, Mamlaka hiyo ina uwezo wa kuongeza vyanzo vyake vya mapato na kutoa huduma bora zaidi kwa abiria na mizigo iwapo tu watawezeshwa kisheria kubakiza fedha itokanayo na Tozo ya Huduma kwa Abiria *(Passenger Service Charges)*.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, Katika vipindi tofauti, Wizara iliyokuwa na dhamana na masuala ya uchukuzi iliwasilisha mapendekezo ya kupatiwa tozo ya huduma kwa abiria ili kuweza kumudu gharama za uendeshaji na ukarabati wa miundombinu katika viwanja vya ndege. Katika Mkutano wa Bunge la Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2005/2006, aliyekuwa Waziri mwenye dhamana wa Fedha alielekeza kuwa makusanyo yote yatokanayo na Tozo ya Huduma kwa Abiria yaelekezwe TAA.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia maelekezo hayo, Wizara ya Fedha ilikuwa ikiipatia TAA fedha zitokanazo na tozo ya huduma abiria kwa mfumo wa '*retention*'. Hata hivyo mnamo mwaka 2017, Serikali ilifuta utaratibu wa 'retention' kwa Taasisi za Umma kupitia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 kifungu Na. 58 (a-c). Kielelezo Na. 11 kinafafanua utofauti wa makusanyo na marejesho ya Tozo hiyo kati ya Mwaka wa Fedha 2013/2014 – 2022/2023.




***Chanzo:*** *Taarifa za Vikao vya Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo, kamati inaishauri Serikali iwasilishe marekebisho ya sheria yatakayoweka utaratibu wa kisheria kubakiza kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) walau **asilimia 40** ya fedha zitokanazo na kodi ya huduma za wasafiri *(retention of passengers' service charge)*, ili kuipunguzia taasisi hiyo utegemezi wake kwa Serikali kuu na kuiwezesha kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua jitihada ambazo TAA inafanya katika kuhakikisha kwamba viwanja vya ndege nchini vinakuwa na hatimiliki ya ardhi yake. Hata hivyo, Kamati inaishauri Mamlaka hiyo, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ishirikiane kikamilifu na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kuhakikisha kwamba maeneo yote ya TAA yanakuwa na hati ya umiliki wa ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** pendekezo hili linatokana na tathmini iliyofanywa na Kamati kuona kwamba kuendelea kumiliki maeneo ya viwanja vya ndege bila kuwa na hati, kunachochea uvamizi ambao unaweza kusababisha migogoro ya ardhi na kuwepo kwa gharama kubwa kwa Serikali kulipa fidia.

4.2.7 **Usalama wa Usafiri Majini**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Bajeti ya TASAC hususan katika Miradi ya Maendeleo, Kamati haikuridhishwa na mipango ya utekelezaji wa mradi wa usalama wa usafiri majini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kuisimamia TASAC ili Fedha za Maendeleo zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 zinatekeleza shughuli halisi zinazogusa usalama wa usafiri majini. Shughuli hizo ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya uokozi na huduma za dharura, na ujenzi wa vituo vya uratibu wa shughuli za uokozi katika maeneo ambayo itakuwa rahisi kutoa msaada wa haraka iwapo ajali zitatokea katika eneo lolote ndani ya maziwa na bahari.

4.2.8 **Utendaji wa LATRA**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kwamba, inashughulikia changamoto zote za mgongano wa kiuratibu na wa kisheria kuhusu masuala ya usalama barabarani ili LATRA iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo bila kuingiliana na majumuku ya Jeshi la Polisi. Sambamba na hilo, Kamati inashauri LATRA kujiendesha kisasa ili iwapo kuna ukiukwaji wa sheria za matumizi ya vyombo vya usafiri basi teknolojia ya kisasa itumike kubaini makosa hayo.

4.2.9 **Utoaji wa Huduma za Hali ya Hewa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua mchango mkubwa ambao Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) inatoa katika sekta mbalimbali, Kamati inashauri Serikali ifanye tathmini juu ya uwezo wa Mamlaka hiyo kuwa na vyanzo mbalimbali vya mapato ili kuongeza ufanisi wa makusanyo yake na hivyo kuboresha huduma zake katika mwaka wa Fedha 2024/2025.

4.2.10 **Maboresho ya Miundombinu ya Kiwanja cha Ndege Bukoba**

**Mheshimiwa Spika**, Uwanja wa Ndege Bukoba una historia ya kuwepo kwa changamoto za kiusalama kwa ndege zinazotumia uwanja huo

hasa kutokana na uoni hafifu unaosababishwa na hali ya hewa. Kamati inatambua kwamba, Serikali kupitia TAA na TCAA iko katika hatua za kujenga mnara wa kuongozea ndege *(control tower)*, pamoja na kuweka taa ili kuwarahisishia marubani kuona njia ya ndege *(runway)*.

**Mheshimiwa Spika**, wa upande mwingine, tayari kulikuwa na mapendekezo ndani ya Serikali ya kujenga uwanja mpya katika eneo la Mukajunguti, ingawa Serikali bado inasisitiza kwamba uwanja unaotumika sasa bado ni salama na unaweza kuendelea kutumika iwapo miundombinu itaboreshwa. Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina na kuliarifu Bunge lako mpango wa kudumu wa kutatua changamoto za usalama wa ndege Bukoba, Mkoa wa Kagera.

4.2.11 **Ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kwamba, ili kuhakikisha ujenzi wa miundombinu ya chuo hicho unaanza katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, utaratibu wa kubajeti miradi ya maendelo uzingatie kutenga fedha katika Bajeti ya Maendeleo ambapo mradi huo utakuwa na kifungu maalum pamoja na namba ya mradi. Aidha, Serikali ihakikishe kwamba, mradi huo unazingatia ubora ambao utavutia wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi na hatimaye kuongeza mapato ya Serikali.

## SEHEMU YA TANO

5.0 **HITIMISHO**

5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, namshukuru Naibu Spika, Mhe. Mussa Azzan

Zungu (Mb.) kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha Vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zilizo chini yake. Maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe hao ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Kapt. Abbas Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb.
5. Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb.
6. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb.
7. Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb.
8. Mhe. Amina Ali Mzee, Mb.
9. Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb.
10. Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb.
11. Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb.
12. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb.
13. Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb.
14. Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Mb.
15. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb.
16. Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb.
17. Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb.
18. Mhe. Mohammed Maulid Ali, Mb.
19. Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb.
20. Mhe. Mwantumu Dau Haji, Mb.
21. Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb.
22. Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, (Mb) kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb). Aidha niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius W. Kahyarara. Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya Sekta ya Uchukuzi, na inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidi.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

5.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu**
06 Mei, 2024

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumepokea wasilisho la Serikali lakini pia tumeshapokea wasilisho la Kamati ya Kudumu ya Miundombinu.

Tutajielekeza sasa kwenye kuchangia hotuba hizi. Kwenye orodha yangu nitaanza na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'azi Ulenge, atafuatatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile na Mheshimiwa Deus Clement Sangu, ajiandae.

Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mungu kwa neema na baraka zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, nakupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge letu. Naona koti hilo limekaa mahali pake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hatua mbalimbali inazozichukua ili kuhakikisha kwamba rasilimali zetu zinatumika vyema kuboresha uchumi wa Taifa letu. Kipekee pia naipongeza Kamati yangu ya miundombinu kwa taarifa nzuri yenye maoni yanayokidhi haja ya kuboresha sekta zilizo chini ya Wizara ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imepanga sekta ya bandari ichangie kwenye pato la Taifa kwa kiwango cha asilimia saba ifikapo mwaka 2025/2026. Pia Mamlaka ya Bandari inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa kuzingatia mpango kabambe wa mamlaka wa mwaka 2020 – 2045.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya miradi hiyo imeelezwa vizuri na mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri, kama vile upanuzi wa gati namba nane mpaka 11. Vilevile ujenzi wa matenki ya kupokea na kuhifadhi mafuta pamoja na ujenzi wa gati namba tatu ya kuhudumia makasha katika Bandari ya Tanga. Utekelezaji wa miradi hiyo yote unahitaji fedha za kutosha, ikizingatiwa kuwa washindani wetu miundombinu waliyonayo au gati walizonazo ni mara mbili ya gati zilizopo Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuzungumza hapa ni kwamba bila ya Mamlaka ya Bandari kuwa na vyanzo vya kutosha vya mapato kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii yote, hakika malengo tuliyojipangia kwa sekta hii ya bandari ya kuchangia asilimia saba katika pato la Taifa haiwezi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, popote pale duniani, mapato yatokanayo na *wharfage* ambayo ni mapato yanayotokana na mtumiaji wa meli katika kutumia miundombinu ya bandari, duniani kote fedha hizi zinatengwa kwa ajili ya kuboresha na kujenga miundombinu ya bandari. Vivyo hivyo nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Bandari Namba 17 ya Mwaka 2004 imekitaja chanzo hiki cha mapato *(wharfage)* kwamba ni chanzo cha mapato cha Mamlaka ya Bandari chenye lengo la kuboresha miundombinu ya bandari zetu. Kwa mujibu wa tamko lililotolewa mwezi wa Agosti, 2017, bandari ilisitisha kukusanya mapato yale. Kwa mujibu wa sheria ambayo ilikuja kuundwa mwaka 2019 Sheria Na. 7, iliipa Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya fedha zile zinazotokana na *wharfage* na kuziweka katika akaunti maalumu iliyoko *BOT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi kwa mujibu wa taarifa zilizopo, hazitumiki ipasavyo kwa uhitaji tulionao wa kuboresha miundombnu yetu, na ikizingatiwa kwamba tayari gati zilizokuwa zimekamilika sasa hivi zinatumika na *DP World*, ina maana Mamlaka ya Bandari Tanzania inahitaji kuongeza gati nyingine zaidi kwa ajili ya ufanisi na kuongeza shehena kwa ajili ya mustakabali mpana wa sekta ya Bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za *wharfage* ni *almost* 50% ya mapato yote ya Mamlaka ya Bandari Tanzania. Kwa sasa hivi bandari inatumia asilimia 50 ya mapato mengine yatokanayo na bandari ili kuendeleza miundombinu mbalimbali pamoja na kuiendesha Mamlaka ya Bandari Tanzania, fedha ambazo zimekuwa chache na hazitoshi kutimiza amza ya Serikali ya kuchangia katika pato la Taifa kwa takribani asilimia saba ifikapo mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa fedha hizi zimewekwa kwa mujibu wa sheria, kwamba ni mapato ya bandari kwa lengo la kuendeleza miundombinu yetu ya bandari, nasi sote ni mashahidi kwamba tunahitaji sekta ya bandari ifikie malengo yake ili nchi yetu iweze kunufaika na *advantage* ya kijiografia kwa kuwa na miundombinu bora ya bandari na meli kubwa ziweze kufika katika bandari zetu. Kwa hiyo, suala la kuboresha miundombinu ya bandari ni suala ambalo haliepukiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, nami ninashawishika, na ninaungana na maoni ya Kamati yangu, Kamati ya Miundombinu kubadilishwa kwa sheria ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ili kuiwezesha Mamlaka ya Bandari Nchini kuweza kukusanya mapato yale yatokanayo na *wharfage* ili iweze kuboresha miundombinu ya bandari zetu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba mapato haya yatokanayo na *wharfage*, kabla ya kupelekwa kule *BOT* yanaingia kwanza kwenye akaunti fulani za biashara halafu ndipo yanapelekwa kule *BOT*. Kwa taarifa zilizopo ni kwamba fedha hizi zinaanza kutumiwa na *TRA* kabla hazijafika kule kwenye akaunti maalumu iliyowekwa. Maana yake ni kwamba inakwenda kinyume na taratibu zilizowekwa kwa matumizi ya fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile utakuta fedha hizi labda zimekusanywa shilingi bilioni 500, lakini kabla hazijaingia kwenye akaunti iliyopangwa iliyoko *BOT*, fedha zile zinapunguzwa na utakuta zinaingizwa kwenye kiwango ambacho siyo halisi katika makusanyo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashawishika kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba sheria inabadilishwa na Mamlaka ya Bandari inakusanya fedha hizi kama ilivyokuwa kipindi cha nyuma ili kuboresha miundombinu ya bandari zetu nchini na ili kuongeza shehena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo naomba nizungumzie kuhusu *passenger service charge* ambayo kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa *ICAO (International Civil Aviation Authority)* inazitaka mamlaka zote za viwanja vya ndege kuwa na chanzo cha mapato, na *passenger service charge* ni miongoni mwa chanzo cha mapato ambapo tunalipia shilingi 10,000/= tunaposafiri ndani ya nchi na dola 40 tunaposafiri nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, chanzo hiki cha mapato kilibadilishwa kwa mujibu wa sheria na kinakusanywa na *TRA,* na kwamba mamlaka inayohusika na viwanja vya ndege mpaka iombe *TRA*. Tumeona hali halisi ya viwanja vyetu vya ndege nchini kuwa haikidhi haja kuendana na kasi ya ongezeko la watalii wetu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawiwa kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba kwa kuwa sheria zinabadilishwa, *passenger service charge* irudishwe na kukusanywa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania. Vivyo hivyo pamoja na *wharfage*, sheria ibadilishwe ili iweze kukusanywa na Mamlaka ya Bandari Tanzania ili kufikia azma ya Serikali ya kuchangia kwenye pato la Taifa asilimia saba na vilevile kuongeza shehena na kwenda na kasi ya ufanisi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Eng*. Mwanaisha Ulenge.

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo ya wageni, tunao wageni ambao wamekuja sasa hivi, kwanza tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Waziri wa Uchukuzi ambao ni Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Uchukuzi. Tunaomba wasimame tuwaone, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wawakilishi wa Benki ya *NMB, CRDB* na *AZANIA Bank*, mnaweza mkasimama, ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika msafara huo pia wapo wawakilishi kutoka Chama cha Wataalamu wa *Logistics* na Usafirishaji, na vilevile wapo marubani na *Cabin Crew* kutoka Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL)*. *(Makofi)*

Haya, ahsante, pokeeni pongezi hizo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Pili, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mbunge na Naibu Waziri wa Madini ambaye ni mwalimu kutoka Longido, Mkoa wa Arusha. Mwalimu karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki ambao ni wafanyabiashara wa Tarime Mji kutoka Mkoa wa Mara. Wafanyabiashara, karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni 35 wa Mheshimiwa Almasi Maige ambao ni wanafunzi kutoka Tabora Kaskazini, Uyui wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma, wasimame na karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 80 wa Mheshimiwa Salimu Alaudin Hasham ambao ni viongozi wa CCM Kata zote za Wilaya ya Ulanga, Mkoa wa Morogoro. Wasimame na karibuni sana. *(Makofi)*

Ahsanteni, tunaendelea na uchangiaji. Sasa anafuata Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Clement Sangu na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie kuhusu bajeti Wizara yetu ya Uchukuzi. Kipekee nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya kwenye Taifa letu. Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana ikiwemo kuhakikisha kwamba majimbo

yetu yanaendelea kupata fedha pamoja na kuzisimamia Wizara zetu tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Waziri wa Uchukuzi pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wake wote pamoja na Wakurugenzi mbalimbali wa taasisi zetu zote za Wizara ya Uchukuzi. Pia nakupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Tunaona unafanya kazi nzuri na uko *smart*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, nataka nichangie maeneo machache sana, kama maeneo mawili tu. Eneo la kwanza ni eneo ambalo pia dada yangu Mheshimiwa Mwanaisha hapa amejaribu kuchangia. Pia nitachangia sehemu ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa na katika taarifa ya Kamati imesemwa sana, wakati Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Miundombinu anahitimisha, amezungumza juu ya tozo ya *wharfage* ambayo inakusanywa na *TRA*. Labda tutafute kwanza nini maana ya tozo ya *Wharfage*. Tozo hii ni tozo inayotozwa kwa mizigo pale bandarini kwa ajili ya uendeshaji na kuboresha bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo hii ninajua mwaka 2017 ilibadilishwa kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati, na kukusanywa na *TRA*. Najua wazi kwamba enzi hizo mifumo ya bandari haikuwa mizuri na ndiyo maana ilisababisha kubadilisha na badala ya kukusanywa na *TPA*, basi ikaanza kukusanywa na *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uteuzi makini wa Mkurugenzi wa *TPA,* kaka yangu Mbossa. Ni Mkurugenzi makini, ni mchapakazi. Nina imani kubwa kwamba atakwenda kusimamia vizuri haya ambayo tunayazungumza. Kwa uteuzi huo unanishawishi sasa kuishauri Serikali kurudisha tozo hii iendelee kukusanywa na *TPA* ili ifanye kazi ambazo zimekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanaisha ametuambua hapa kwamba fedha hizi hazitumiki zote kama ilivyokusudiwa, kwamba kwenda kutumika katika uendelezaji wa bandari zetu. Tunaomba sasa, kama Mwenyekiti wa Kamati alivyoshauri, fedha hizi sasa watu wa Uchukuzi wakae na Waziri wa Fedha, wakae na watu wa Fedha ili wakubaliane kwamba fedha hizi zirudi zianze kukusanywa na watu wa *TPA* ili waweze kuendeleza bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuona makusanyo yanaongezeka, tunahitaji kuona Bandari ya Mwanza, Mtwara pamoja Tanga zikitengenezwa; na pia tunahitaji kuona gati zinaongezeka. Kwa nini? Inawezekana sasa hivi tunasema mizigo ni michache, ni kwa sababu tunakalisha meli muda mrefu, kwa sababu hatuna gati nyingi za kutosha kuweza kushusha mizigo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu wanaona bora waende Mombasa au sehemu nyingine kushusha mizigo yao kwa sababu ya uharaka, lakini tukiwa na magati mengi tutaenda kushusha mizigo kwa wakati na zaidi tutaenda kufanya pato la *TPA* liongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo *TPA* peke yake, kuna uhusiano mkubwa kati ya wingi wa mizigo itakayoshushwa pale *TPA* na makusanyo ya *TRA,* kwa sababu kama mizigo mingi itashushwa *TPA*, na kama mizigo mingi itapitia bandari yetu ya Dar es Salaam na bandari nyingine maana yake sasa *TRA* na wenyewe wanaenda kupata fedha nyingi watakazokusanya kulingana na mizigo utakayoenda kuipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wakati sasa wa kuendelea kutafakari ili tuwasaidie hawa watu wa bandari tuwarudishie hizi fedha waweze kufanya ukarabati, waweze kutafuta wakandarasi, waweze kuboresha miundombinu ya bandari ikiwemo gati namba 12 mpaka 15, imesemwa hapa, kina cha gati namba nane mpaka namba 11, Bandari ya Mwanza, Bandari ya Mtwara kama nilivyosema, na maziwa makuu yakiwemo Nyasa pamoja na ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *advantage* nyingine itakayo patikana maeneo haya baada ya fedha hizi kukusanywa na bandari yetu kwa maana ya *TPA*, watakapokusanya fedha hizi *advantage* watakapoingia mikataba ya uendelezaji wa bandari kwa maana ya wakandarasi watawalipa kwa wakati. Wakiwalipa kwa wakati, mantiki yetu sasa tunaenda ku-*solve* tatizo ambalo tumeendelea kuwa nalo la kulipa *interest* kwa wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sasa hivi tunalipa *interest* kubwa kwa wakandarasi kwa kucheleweshewa malipo kwa sababu ya mlolongo mrefu, kwa sababu ya fedha kuwa kidogo ambazo zinatokana na bandari, lakini sasa hivi tukiwaruhusu wakusanye, watumie vizuri tuwape *target*. Kazi yetu Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi ni kuwapa *target* hawa watu wa bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapeni *target* za nini kifanyike katika mwaka husika ili waweze kutimiza yale malengo, nasi tuwahoji baada ya muda husika ambao tutakuwa tumejipangia kuwahoji sasa, kwamba tulikubaliana hii fedha tumewapatia, mmekusanya ninyi wenyewe, tulikubaliana mjenge gati namba 12 mpaka 15, tulikubaliana mwendeleze Mwanza bado hamjaendeleza, tupeni sababu. Kwa sasa hivi hatutawahoji kwa sababu namna wanavyopata fedha, wanapata kidogo ikilinganishwa na uhalisia wa zile fedha za tozo ya *wharfage* zinavyokusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nishawishike sana kuishauri Wizara ya Fedha, kuishauri Wizara ya Uchukuzi sasa mkubaliane mapato haya sasa yaanze kukusanywa na *TPA* ili sasa *TPA* waweze kufanya kazi kubwa, ikizingatiwa kwamba sasa hivi mapato ya *wharfage* yalikuwa asilimia 50, yamesemwa kwenye taarifa na yote sasa yanakusanywa na *TRA*. Yale makusanyo ambayo yalikuwa yanakusanywa na *TPA* yalikuwa yanakusanywa asilimia 50 na sasa tayari *DP World* ameshaingia kwenye uwekezaji, anakusanya zaidi ya asilimia 35. Sasa *TPA* wanabakiwa na asilimia 15 ambazo hazitoshi kwenye kuendeleza bandari, hazitoshi kutengeneza miundombinu ya bandari ikiwemo hata na mawasiliano ya *TRC* pamoja na bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani sasa ile mizigo ikishashushwa iingie moja kwa moja kwenye treni ili iweze kusafirishwa. Bwana Kadogosa yupo hapa najua, watakuwa na mawasiliano ya karibu na watu wa bandari ili miundombinu ya reli iwasiliane pale bandarini iwe ni kushusha na kuweka kwenye treni na kusafirisha. Tutapata mapato aina mbili; tutapata mapato ya *TPA* na pia tutapata mapato ya reli na kusababisha nchi yetu kuendelea kupata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka nichangie ni ujenzi wa uwanja wa ndege pale Simiyu. Tumeshaachia eneo na wananchi tayari wameshapisha eneo la ujenzi, lakini mpaka sasa tunavyozungumza bado hawajalipwa fidia. Tunaomba sasa mweke kwenye mpango wa kulipa fidia wananchi ambao wamepisha maeneo yao kwa muda mrefu kupisha ujenzi wa uwanja wa ndege pale Bariadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa waweke kwenye mpango, tunatamani kuona ujenzi wa kiwanja cha ndege pale Simiyu unaanza mara moja. *Advantage* yake ni nini? Watalii watashuka pale Bariadi, na uchumi wa Bariadi utaongezeka, Simiyu kwa ujumla uchumi utaongezeka na pia pale Lamadi kwangu uchumi utaongezeka kwa sababu watalii watapita pale kuelekea lango la Serengeti na wananchi watazidi kupata kipato. Kwa hiyo, tunaomba sana iwekwe kwenye mpango ili tuweze kuwa na uwanja wa ndege pale Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba sasa Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi pamoja na Mkurugenzi wa *ATCL* nimemwona hapa, Bwana Matindi, ni aibu leo tunazungumza eti hakuna ndege ya kutoka Dodoma kwenda Mwanza. Haiwezekani! Hatuna ndege ya kutoka Mwanza kuja Dodoma! Hiyo ni aibu bwana. Tunatamani kuona tunapata ndege ya kutoka Mwanza kuja hapa Dodoma, tunatamani kuona ndege ya kutoka Dodoma kwenda Mwanza, hata kama ni siku tatu kwa wiki zinatosha. *(Makofi)*

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWEMYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Fyandomo.

**TAARIFA**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nataka kutoa taarifa kwa mchangiaji kwamba hata Mbeya tunahitaji ndege ya kutoka Mbeya - Dodoma, Dodoma - Mbeya kulingana na watu walivyo wengi wanaotokea Mbeya wanazunguka mpaka wafike Dar es Salaam na ndege ndiyo warudi Dodoma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Simon, unaipokea taarifa?

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa. Niongeze, na kutoka Dodoma kwenda Kilimanjaro. Kwa hiyo, haya maeneo ni ya kimkakati, Mkurugenzi Matindi naomba uyachukue haya. Natamani kuona wiki ijayo tunapata ndege kutoka Dodoma kwenda Mwanza, Dodoma kwenda Kilimanjaro, Dodoma kwenda Mbeya kama ilivyokwisha kusemwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Simon Songe. Mheshimiwa Deus Clement Sangu, atafuata Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, ajiandae.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia kwenye bajeti muhimu sana, bajeti ambayo ndiyo moyo wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja hii. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayofanya ya kusukuma fedha nyingi kwenda kwenye miradi mbalimbali hasa katika sekta hii ya uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mchango wangu utajikita sana kwenye uwekezaji kwenye sekta ya uchukuzi. Naendelea kutoa pongezi kabla sijasema hoja yangu kwa Mheshimiwa Waziri Prof. Mbarawa na Naibu Waziri na Menejimenti nzima ya Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya. Kwa kweli mimi nipo Kamati ya Uwekezaji. Tumetembelea miradi mingi, tumeona kazi kubwa inayofanyika. Katika ziara hiyo pia tumepata fursa ya kujifunza mambo mengi ambayo yanafanyika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli uwekezaji uliyofanyika, nitaanza kwenye Sekta ya Bandari, tulipata fursa ya kutembelea Bandari ya Tanga, Bandari ya Dar es Salaam na Bandari ya Mtwara. Serikali imewekeza fedha nyingi takribani shilingi trilioni 1.4 ambazo sisi kama Kamati ya Uwekezaji, na niendelee pia kuunga mkono hoja ya Kamati ya Miundombinu, wameeleza mambo ambayo yanashabihiana na yale sisi tuliyoyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na suala ambalo limefanyika kwenye Bandari ya Tanga, Dar es salaam na pale Mtwara limeleta *impact* gani katika pato la Taifa? Kupitia uwekezaji huu, umesababisha mabadiliko makubwa. *TRA* walikuwa wanapokea shilingi trilioni saba, zimepanda kufika shilingi trilioni tisa ambayo ni sawa na ongezeko la 42%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuliona uwekezaji huu umeleta tija kwa kiasi fulani, lakini tumeona shehena na alivyosema Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake, shehena imeongezeka kutoka asilimia hiyo 11.2 imeenda mpaka kufika shehena ya tani milioni 20. Ni *achievement* kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia makasha yaliyokuwa yanakusanywa mwaka ule uliyotangulia na mwaka huu yameongezeka kutoka 600,000 na sasa wanakimbilia makasha ya makontena 800,000. Huu ni uwekezaji wa shilingi trilioni 1.3 uliyofanyika katika bandari zetu zote hizi tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ninachotaka kusema? Kuna dhana imezungumzwa na Kamati ya Miundombinu, lakini kuna dhana imezungumzwa pia na wachangiaji walionitangulia juu ya hii tozo ya *wharfage*. Mimi na Kamati yangu tulipita tukaliangalia kwa upana wake kama Taifa tunatakiwa *concentration* yetu iwe wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *concertation* ni kuangalia ile *cash curve,* ile sekta inayotuzalishia fedha nyingi kuliko kui-*paralyse*. Kwa mfano, tuliona kwamba kuondolewa kwa hii *wharfage* kuchukuliwa na *TRA,* kunaenda ku-*paralyse* uboreshaji wa bandari zetu na hii *mileage* iliyotoka kwenye shilingi trilioni saba kuja kwenye shilingi trilioni tisa, *achievement* yake hatutaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niungane na Wabunge wenzangu na Kamati katika hoja yao hii. Kuna haja sasa ya Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Fedha warudishe hizi fedha ziendelee kwa utaratibu ule ule wa zamani, tuje tu-*amend* hapa sheria ili sasa tuweze kupata mapato ambayo *TPA* itachangia kwenye mapato ya Mfuko Mkuu wa Hazina, kupitia *TRA na* mapato yakue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlivyopeleka pale mmetoa *room*; *TRA* inaendeshwa na Sheria ya Kodi, ikitokea kuna mtu yeyote anasema nina madai nadaiwa, au nawadai *TPA* na hiyo ni *tax liability*, *TRA* hawachelewi, wanaikata hiyo *wharfage,* wanamalizana, mtajuana huko. Kwa hiyo, hii pesa badala ya kwenda ku-*invest*, na kutuletea fedha zaidi, inaishia sasa huku *TRA* ambapo inaweza ikatumiwa vile ambavyo sivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, kaeni na Wizara ya Fedha mrudishe hii *wharfage,* tukaboreshe miundombinu yetu ya bandari. Leo Kisiwa Mgao pale tunaenda kujenga bandari ya kupokea tani 100,000 za makaa ya mawe pamoja na *cement* inayozalishwa kule Mtwara; lakini pale pomba la *EACOP* linaenda kuanza hivi karibuni ambapo kwanza tu katika hatua za awali *TRA* ilikusanya shilingi bilioni 30 kupitia bomba la *EACOP,* tena katika *mobilization stage*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini mradi huu ukikamilika utaweza kuleta pato kubwa sana. Sasa *TPA* itafanyeje kazi yake kama tunai-*cripple*? Kwa hiyo, ni *high time* sasa tuanze kufikiria kiuwekezaji zaidi, tusiwe tunatamani zile fedha ambazo tunaziona, tukawekeze ili ile *return on investment* iweze kuleta tija katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hayo hayo yanazungumzwa kwenye mamlaka ya viwanja vya ndege. Haiwezekani Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, nitawapa mfano, *terminal three* ile ilijengwa kwa fedha takribani shilingi bilioni 560, lakini kwa *collection* inayofanyika pale, *return on investment* ya hiyo fedha shilingi bilioni 560 ni ndani ya miaka nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna uwekezaji mkubwa ambao unaweza ukalipwa ndani ya miaka nane. Maana yake ni nini? Tukiwarudishia hiyo *forty percent* kama Kamati ilivyopendekeza, hii itaenda kuwapa nguvu na *TRA* watakusanya sana. Kwa hiyo, tusiwe waoga, ile sheria tulikuwa na hofu kwamba hawana uwezo, sasa hivi naamini mkiwarudishia iwe *power* wataenda ku-*invest*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *terminal two* ile tulijenga mwaka 1984 imekuwa ya kizamani, *ATCL* inatakiwa kuwa na *hub* yake ambayo tukiwapa *terminal two* tutapata wageni wengi. Watapita pale kwa sababu *facility* zetu zitakuwa nzuri, tutaongeza mapato zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naombe Mheshimiwa Prof. Mbarawa, sisi tunafanya kazi pamoja na nashukuru Waziri wangu wa Uwekezaji na Mipango yupo hapa; kama Taifa lazima tuwe na *integrated planning*. Leo hii nitawapa mfano tumewekeza shilingi bilioni 421 kujenga Bandari ya Tanga, lakini Bandari ya Tanga itakuwa *underutilized* tu, kwa sababu hakuna miundombinu inayounganisha na nchi jirani kama Burundi na Rwanda ambapo ndipo mizigo mingi inahitaji kutumia Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umbali wa kutoka Bandari ya Mtwara kwenda kufikia nchi zile ni *less than* kilometa 300 ukitoka Dar es Salaam

kwenda Burundi na Rwanda. Kwa hiyo, wapo *interested* na kutumia Bandari ya Tanga na itakuwa *more effective* na tutawazidi *competitors* wetu ambao ni nchi jirani kama tutawekeza kwenye miundombinu ya Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara kutoka Tanga - Sengera inatakiwa iwe kipaumbele, lakini ile barabara ya kutoka Handeni kilometa 433, Handeni - Kiberashi kupitia Kiteto - Kondoa kilometa 433 zitawafanya na kuwavutia nchi jirani kama Burundi na Rwanda watumie Bandari ile ya Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajenga bandari ndogo pale, tumetangaza *tender* ya tani 100,000 ya makaa ya mawe, lakini kubeba makaa ya mawe kupitisha pale Kisiwa Mgao ni changamoto. Leo hii mmejenga Bandari ya Kalema, ile shilingi bilioni 47 hakuna barabara inayounganisha kuja kufika Mpanda, Bandari ya Kabwe mmeweka shilingi bilioni saba, pale hamna miundombinu ambayo inaunganisha. Kwa hiyo, ile imekuwa kama *white elephant*. Tumewekeza mabilioni ya fedha, lakini itabaki kuwa *white elephant*. Tutakuwa tumeweka fedha nyingi kwa kuwa hatuna *integrated planning* katika mipango yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sasa namshauri Mheshimiwa Waziri wa Mipango, mje, tuko pale Lagosa tumewekeza shilingi bilioni 15, miundombinu ya kuunganisha ili bandari ile iwe-*effective,* ifanye kazi na ili *return on investment* tuliyoiweka pale tuione hamna! Sisi kama watu wa uwekezaji tuliona jambo hili tuishauli Serikali mkae pamoja, kuna vipaumbele ambavyo mki-*invest, return on investment* itakuwa ndani ya muda mfupi, tutasonga mbele kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia leo hii nitaongea kuhusu Bandari ya Kasanga, Bandari ya Kalema, na Bandari ya Kabwe kwamba hamna meli. Mheshimiwa Profesa Mbarawa ni ndugu yangu, nakuheshimu sana na ni mtu unachapa kazi, lakini leo hii jioni kwenye mafungu ya shilingi tutapambana kuhusu meli katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyopita mlikuja na habari ya kutuletea meli ziwa Tanganyika. Kwenye meli hizo tulisema walau mbili ziamke; meli ile ya Mwongozo na Liemba, hizo imekuwa ni hadithi, na leo hapa nimeona unasoma. Sasa tunataka leo utuambie. Hizo meli kwenye ziwa hilo zina-*impact* kwa mikoa mitatu; Kigoma, Katavi na Rukwa, lakini sisi tunapakana na nchi tatu kule ambazo tuki-*trade* nazo tutapata faida za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapakana na Burundi, *DRC Congo* na Zambia, na wote wana *potential* ya *market* kwenye biashara. Kila bidhaa tunayouza upande wetu wa mikoa hii tukiwa na usafiri upande wa pili tutapata faida za kiuchumi. Kwanza tutainua uchumi wa watu wetu, lakini siyo kuinua tu uchumi wa watu wetu, Tanzania kama nchi itapata pato kubwa la kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika bajeti hii mambo ambayo hatutavumilia ni juu ya meli Ziwa Tanganyika. Jana tulivyokutana mahali, nilimwambia Mheshimiwa Waziri, na leo hii kwa kweli hili jambo tunakuja na msisitizo wake, tunataka lifike mwisho ili tukirudi, wananchi wasiseme mmezoea kuja kutuambia uwongo, kwamba meli inaanza mwaka huu, lakini mwaka unapita unakuja mwaka mwingine na unafuata mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Prof. Mbarawa anapokuja kuhitimisha aje na *commitment* ambayo itatu-*convince* Wabunge wa mikoa hii mitatu juu ya kurekebisha meli katika Ziwa Tanganyika, meli ya Liemba pamoja na meli ya Mwongozo wakati tukiendelea na mipango mingine mliyonayo kama Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ahsante sana pia kwa kutunza muda. Namwita sasa Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, ajiandae.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema ambaye ametupa zawadi hii ya uhai na uzima kuweza kusimama leo hapa katika kuendeleza majukumu yetu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya kulitumikia Taifa letu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalendo wa Dkt. Mama Samia, uchapaji kazi wake, utu wake unaonesha nia yake thabiti kabisa katika kuwatendea haki Watanzania na kuleta maendele makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Mbarawa, Waziri wa Uchukuzi kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya yeye na timu yake, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yao yote kwa utendaji mkubwa kuendelea kusimamia miradi mikubwa katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo inasimwamiwa na Wizara hii ni mikubwa na ya kimkakati, ambayo inagusa moja kwa moja maisha ya Watanzania hasa wa chini. Ukiangalia mradi wa *SGR*, ukiangalia mradi wa utengenezaji na uundaji wa meli na vivuko mbalimbali, ukiangalia mradi wa ufungaji na ununuzi wa rada mbalimbali, miradi hii yote na mingine ambayo sijaitaja ni miradi mikubwa ambayo inakwenda kugusa maisha ya Watanzania mmoja mmoja, hususan maisha ya Watanzania wa kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia, Taifa hili pamoja na dunia sasa hivi inavyoendelea, Mamlaka za Hali ya Hewa nchini pamoja na dunia kwa ujumla ni mamlaka ambazo zinafanya kazi nzuri sana. Tunaona mabadiliko mbalimbali ya hali ya hewa ambayo majanga yameendelea kuja katika maeneo mbalimbali ya dunia, lakini tunaona mvua kubwa, na upepo mkali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya kuwepo mamlaka kama hii ya hali ya hewa kuweza kutoa tabiri za kila siku, tabiri za siku kumi kumi na tabiri za misimu, kuweza kuonesha ni kitu gani kinatokea, kitu gani kitakuja kwenye masuala haya ya hali ya hewa, ni dhahiri kwamba na tunakubaliana kwamba kwa kweli maisha ya watu na mali zao yanaweza kuwa hatarini, lakini kwa sababu ya uwepo wa Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini na kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya, tunaona kwamba mali za wananchi zinaokolewa na maisha ya wananchi kwa kiasi kikubwa sana wanajitahidi katika kuokoa mamlaka hii ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kuhakikisha kwamba huduma hizi za hali ya hewa zinaendelea kuimarika ni lazima kuwepo na mikakati madhubuti kuhakikisha kwamba mamlaka hii inakuwa *sustainable* na huduma zake zinapatikana kila siku na zinakuwa endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma hizi za hali ya hewa haziwezi kuwa endelevu na haziwezi kuwa *sustainable* kama hakuna fedha za uendeshaji mamlaka hii. Tulipitisha hapa kwenye Bunge la Kumi na Moja, Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa, lakini Sheria ile imeunda kanuni mbalimbali ikiwemo Kanuni ya *Cost Recovery* ya huduma ambazo Mamlaka ya Hali ya Hewa inazitoa, lakini hadi leo Kanuni hizi za *Cost Recovery* bado hazijapitishwa rasmi na kuweza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wadau wengi ambao wanahitaji kutumia huduma hizi za hali ya hewa, lakini pia kama watahamasishwa naamini kwamba, wanaweza kulipia huduma hizi ambazo wanazitumia na kuifanya mamlaka yetu hii kuimarika na kutoa huduma bora zaidi. Bado hadi leo Kanuni hizi za *Cost Recovery* za Mamlaka ya Hali ya Hewa, hazijapitishwa rasmi kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba, utendaji wa Wizara hii kwenye jambo hili ni wa upande mmoja na upande mwingine ni Wizara ya Fedha, lakini tunatambua kwamba, Serikali ni moja na wanafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, jambo hili alisukume, aende akasimamie pale kwa

Waziri wa Fedha, ili liweze kufikia kikomo, mamlaka hii iweze kujiendesha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Chuo cha Hali ya Hewa pale Kigoma. Kila siku tunazungumza namna ya kuboresha chuo hiki ili kiweze kutoa huduma hasa kwa nchi ambazo zimetuzunguka. Huduma hizi za hali ya hewa ama taaluma hii nchi nyingi hawana, lakini sisi nchi yetu tunatoa taaluma kupitia Chuo kile cha Kigoma na *UDSM*. Bado huduma zinazotolewa pale zipo chini kabisa, hazina ubora na ndio maana nchi nyingi ambazo zimetuzunguka hawapendi kutumia kile chuo chetu kwa sababu, bado huduma ni duni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipata fedha hizi na Serikali ikawekeza zaidi pale kwenye Chuo cha Hali ya Hewa ni hakika kwamba, chuo kile kitapata wanafunzi wengi kutoka nchi mbalimbali za Afrika ambazo zinatuzunguka na kutoka duniani kwa ujumla kwa sababu, sasa hivi Mamlaka yetu ya Hali ya Hewa inaendelea kujitangaza na imeendelea kuaminika kidunia. Ndio maana Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania amechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Dunia kwenye lile Jopo la Kimataifa la Mabadiliko ya Tabianchi pamoja na hali ya hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi hii hakupewa tu kwa sababu, iligombaniwa na wagombea wengine kutoka nchi mbalimbali na tuliweza kuzishinda nchi kubwa ikiwemo Afrika Kusini, Urusi, *Seychelles* na nyinginezo. Hii ni kwa sababu, tayari Taifa letu linaaminika, mamlaka yetu inaaminika kwa huduma pamoja na kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie hizi Kanuni za *Cost Recovery* ni lini zitaweza kukamilishwa? Pia, ni upi mpango madhubuti ambao upo wa kuweza kukiboresha Chuo chetu cha Hali ya Hewa Tanzania ambacho kipo Kigoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la *ATCL*. Tunaipongeza sana *ATCL,* inafanya kazi nzuri katika kulitumikia Taifa

letu. Tunatambua kwamba, kuna vituo vimeongezeka na tangu mwaka juzi tumekuwa tunasikia mara nyingi tu hadithi na ahadi za kwamba, ndege za *ATCL* zitafika katika Uwanja wa Ndege wa Pemba na lakini hadi leo hii tunasikia matangazo mbalimbali yanatolewa, lakini hatujui ratiba hasa ya ndege hii kufika Pemba ni lini itaanza? Mwaka jana tuliahidiwa Mwezi Agosti itaanza, Mwezi Agosti umepita. Mwaka huu pia tumeahidiwa, lakini hadi leo hatujui ratiba ya ndege hii ya *ATCL* kufika pemba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kwamba, kufika kwa ndege kule Pemba kutanyanyua uchumi wa watu wa Pemba, kutainua uchumi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla na pia, itaboresha huduma za *ATCL.* Tunaomba sana na tunatamani sana ndege hii iweze kufika Pemba kutoa huduma mbalimbali ambazo zinapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo natamani kulizungumza, ikiwemo huduma ya meli katika ukanda wetu wa pwani. Sisi watu wa pwani uchumi wetu zaidi unategemea Bahari. Bila kuwa na usafiri wa meli zitakazoweza kuhudumia maeneo ya ukanda wote wa pwani, Pemba, Unguja, Lindi, Mtwara na Tanga kwa kweli, uchumi wetu utaendelea kudumaa. Ukituwekea meli ambayo itaweza kutoa huduma, basi itachangamsha na pia, itaongeza uchumi wa maeneo haya ambayo nimeyataja, hususani ukanda wetu wa pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na pia, ahsante kwa kuzingatia muda. Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, atafuatia Mheshimiwa Aida Joseph Khenani na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais. Katika miaka yake

mitatu tumeona amefanya mambo makubwa ya kimaendeleo kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie katika Wizara ya hii. Kwanza mchango wangu unaanzia katika jimbo langu, upande wa Kipunguni. Nimekuwa nikijiuliza mara nyingi, ni kwa nini Serikali inapenda migogoro na wananchi?  Kwa sababu, kuna wakati mwingine wananchi wanakuwa wamekaa tu wanaendelea na shughuli zao, Serikali ikiona wananchi wapo kimya inaanzisha mgogoro hapa hapa Bungeni. Mwaka jana, Mwezi Julai, alinitafuta hapa kwenye kiti change, Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi akaniambia, kwa sasa tuko tayari kuwalipa watu wa Kipunguni na akaniambia inabidi kwanza tukafanye mkutano kwenda kuwaelezea ni *process* gani tunataka kuzifanya ili waweze kulipwa pesa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia hawa watu wamekaa kwa muda wa takribani miaka 27 wakisubiri hizo pesa. Tukaondoka hapa tukaenda kufanya mkutano, watu wakaelezwa ni *process* gani zitatumika, ili waweze kulipwa. Baada ya Waziri kufanya mkutano wakaletwa watu wa kufanya tathmini akiwepo Mkurugenzi wa *Airport*. Namshukuru sana Mkurugenzi huyu kwa sababu, tumeshirikiana naye kwa kipindi chote. Hiyo ilikuwa mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wakaambiwa kwamba, mtakapolipwa mtapewa miezi mitatu, ili muweze kuondoka. Mwezi Julai Serikali ikafanya mkutano mwingine, wakasema wataanza kulipa tarehe moja Septemba, wananchi wakafukuza wapangaji, wananchi wakabomoa nyumba, wananchi wakasafisha maeneo, lakini mpaka leo hii Serikali haijawahi kwenda kulipa kitu chochote. Sasa najiuliza ni kwa nini Serikali inapenda mgogoro na wananchi ambao hawataki hata mgogoro na Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo hii hakuna kitu chochote ambacho kinaendelea. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa wananchi wameunda kamati na juzi wakaja hapa, ameongea nao ili wamuelezee matatizo yao ambayo yanaendelea huko Kipunguni.

Sasa hivi eneo hilo watu wanakufa, watu wanauawa, limekuwa kama ni eneo la wakimbizi, watu wamekuwa wakimbizi ndani ya nchi yao. Kwa nini, Serikali inawafanyia hivyo wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye bajeti hii kama Mheshimiwa Waziri hataniambia hawa wananchi watalipwa lini, nashika shilingi na siirudishi. Naomba sana jambo hili la watu wa Kipunguni lifikie mwisho, nimekuwa naongea hapa kwa miaka saba jambo la watu wa Kipunguni. Kila siku hawa wananchi wamekuwa wanasumbuliwa, yaani Waziri akijisikia tu anataka kufanya mkutano anaenda Kipunguni kuwadanganya, sasa hivi tupo tayari kulipa, sijui nini na nini, halafu akimaliza anapotea. Wanatutengenezea mazingira mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mimi Mheshimiwa Mbunge siwezi kufika huko, Diwani hawezi kufika huko, Mwenyekiti wa Mtaa kahama. Sasa sisi tutaendaje kuomba kura za Wenyeviti wa Mitaa? Hata chama hakiwezi kufika huko kwa sababu, hawa watu wanaishi katika mazingira magumu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atakaposimama kumaliza bajeti yako, azungumzie ni lini wananchi wa Kipunguni wanalipwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na *SGR*. Nawapongeza sana *SGR* kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Nampongeza sana Mkurugenzi pamoja na wengine, *SGR* pia, imepita katika Jimbo langu, imepita Kipawa, imepita Vingunguti na imepita Mnyamani, lakini maendeleo yasigeuke mateso kwa wananchi, hiyo Kampuni ya *Yapi Merkezi* imeenda imeziba barabara. Sasa hivi ni miaka miwili na nusu imepita, ni barabara gani zinazibwa kwa miaka miwili na nusu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna watu ambao wanaweza kutoka kwenda kufanya shughuli zao. Hata kama unakaa nyumba iko hapo tu, inabidi uzunguke uende mpaka Ukonga, ili uweze kufika nyumbani kwako. Walituambia wanafunga barabara kwa miezi sita, sasa hivi imekuwa ni miaka miwili na nusu barabara zimefungwa na halafu pia, kuna wagonjwa wanakaa maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, *flyover* walizojenga kuna mifereji ambayo maji yake wameyaelekeza kwa wananchi na ukiwaambia hawataki kusikia. Kuna barabara moja ambayo waliiweka kwa ajili ya kutumia wananchi kwa sababu, wenyewe wameshamaliza kazi zao ile barabara wameiacha imebaki pale pale haifanyi kazi yoyote. Barabara imekuwa na madimbwi makubwa, kila siku nawaambia jamani tuitengeneze hii barabara, hawataki kusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, awaambie watu wa *Yapi Merkezi* watufungulie barabara, hakuna barabara ambayo inafungwa kwa miaka miwili na nusu. Wamefunga Kipawa, wamefunga Vingunguti na wamefunga Mnyamani, hizo barabara zote kuna watu wanafanya biashara, kuna watu wana hoteli, kuna watu wana biashara zao. Watu hawawezi kwenda kwenye hoteli kwa sababu, barabara zimefungwa. Mtu anashuka *Airport* anataka achukue hoteli, atapita wapi? Naomba Mheshimiwa Waziri alishughulikie suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusiana na *Air Tanzania*. Naipongeza sana *Air Tanzania* kwa kazi kubwa ambayo inaifanya kwanza kwa kuimarisha *service* za ndani; imekuwa ikifanya vizuri sana na mimi binafsi nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka niishauri Serikali, kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu walivyosema kwamba, katika viwanja vyetu kuna tozo mbalimbali ambazo wanatoa. Mfano, tozo za abiria, abiria wa ndani wanatozwa 10,000/= na abiria wa nje 40,000/=. Hizi fedha za tozo zingebaki kwenye Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, ili ziweze kusaidia maboresho kwa sababu, kuna mambo mengi ambayo yanaendelea pale kwenye viwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo nyingine ambayo ningependa Serikali iwaachie ni hii ya *parking*, ili *Air Tanzania* waweze kuboresha *service* zao. *Air Tanzania* imefanya kazi nzuri sana ukizingatia kwa sasa imepunguza hasara. Kwa hiyo, napenda kuwapongeza, lakini Serikali hizi tozo ndogo ndogo za *parking* na nyingine, wawaachie kama nchi nyingine walivyofanya, mfano Rwanda pamoja na Kenya. Kwa hiyo,

namwomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kulishughulikia jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, wanaochangia kutoka CHADEMA, nimepewa maelekezo ya mgawanyo wa idadi ya wachangiaji kwa sababu, mmeleta wachangiaji wawili, hivyo mtachangia kwa dakika tano tano, mtagawana dakika 10.

Mheshimiwa Aida Joseph Khenani na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko baada ya kumaliza dakika 10 hizo ambazo mnazo, atafuatia Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira kwa dakika tano na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, ajiandae. Kwa hiyo, namwita sasa Mheshimiwa Aida Joseph Khenani kwa dakika tano, atafuatia Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, kwa dakika tano.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kulingana na dakika ambazo umeniambia, umeni-*pressurize* kidogo. Sasa Nitajikita kwenye eneo moja la usafiri wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Wizara kwa kutusoma mikoa mitatu kwenye vitabu kwa miaka nane mfululizo, juu ya usafiri wa Ziwa Tanganyika. Wakati tunazungumza kuhusu Ziwa Tanganyika wote tunajua kwamba, bidhaa zinazokwenda Congo zaidi ya 60% zinatoka Tanzania. Wakati tunazungumza kuhusu Ziwa Tanganyika sote tunajua Serikali imewekeza kwenye Bandari za Kigoma, Karema, Kabwe, Kipili pamoja na Kasanga. Tumewekeza kwenye bandari hizo fedha za Serikali halafu hatuna meli ya kusafirishia mizigo. Ukikaa unafikiri, kama Waziri wa Mipango yupo, Waziri wa Uchukuzi yupo na Waziri wa Fedha yupo, shida ipo wapi katika mipango yetu kwenye nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Waziri aliji-*commit* hapa akasema kuna mipango ya muda mrefu na mipango ya muda mfupi. Mpango wa muda mfupi alituambia ni kukarabati meli mbili, Meli ya *Mv Liemba* na *Mv Mwongozo*, lakini mpaka leo tunapozungumza huo mpango wa muda mfupi hakuna meli ambayo inatembea. Meli mpya bado na zinazohitaji ukarabati nazo bado, tunataka Serikali ikija hapa itueleze inatuwazia nini sisi watu wa mikoa mitatu ambayo tupo kwenye Ziwa Tanganyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajua tunapoteza ndugu zetu kila siku kwa sababu ya usafiri ambao siyo rasmi wa Ziwa Tanganyika. Kama tunaamini Ziwa Tanganyika linaweza kusaidia uchumi wa nchi hii, ni nini kimeshindikana kuwekeza kwenye usafiri wa Ziwa Tanganyika? Kama tumewekeza kwenye bandari ni nini ambacho kinasababisha kigugumizi kuweza kupata usafiri wa Ziwa Tanganyika? Naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri mambo mawili kwa sababu, ni dakika tano; cha kwanza, waliopata nafasi ya kumshauri Mheshimiwa Rais, basi wamshauri vyema kuhusu uchumi ambao tunaweza kuupata kupitia Ziwa Tanganyika. Naamini kama amekubali kutoa fedha kuwekeza kwenye bandari, hawezi kukataa kutoa fedha kwa ajili ya usafiri wa Ziwa Tanganyika, yaani haya mambo yanakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumza hapa, kama ukarabati umechukua zaidi ya miaka nane, meli mpya itachukua miaka mingapi? Hili jambo kama Watanzania tunaotoka kwenye hii mikoa mitatu halikubaliki. Naomba Mheshimiwa Waziri, tunaona jitihada ambazo anazionesha kwenye kutusoma kwenye vitabu, leo tunataka tusikie jibu lake kuhusu *Mv Liemba* na *Mv Mwongozo*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema aliyotuambia ya kutengeneza kiwanda kwa ajili ya meli, tumemsikia na tumeona ameandika, tunataka tuone utekelezaji wa hilo jambo na kwa sababu, hilo jambo ni la muda mrefu, basi tuone la muda mfupi linafanyikaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliposema hapa mwaka jana, niliondoka nikaenda kuwaambia wananchi mpigieni makofi Mheshimiwa Rais tunapata meli sasa, wakapiga makofi. Sasa Waziri aje yeye mwenyewe afute haya maneno kwa sababu, yeye ndiye alisema hapa na nikaamini maneno yake. Sasa wananchi wa hayo maeneo tunataka kujua, yaani sisi kila siku ni wa kusomwa tu kwenye vitabu au inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linahitaji dhamira tu, kwa nini maeneo mengine meli zipo? Ikiwa wanajua kabisa faida za hili Ziwa Tanganyika, kila siku tunaimba wimbo, ninapozungumza sasa ni miaka nane, kama ni dhamira basi tungeiona hata kwenye kutengeneza zilizopo. *Mv Liemba* mpaka leo imechukua miaka nane na vifo vingine sasa hivi wanaripoti, lakini vingine hawaripoti. Tumechoka kupoteza ndugu zetu kwa sababu ya kukosa dhamira ya dhati kwenye uwekezaji wa Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge ambao tunasema tutaondoka na shilingi ya Mheshimiwa Waziri asipotupatia jibu la kueleweka juu ya usafiri wa Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kidogo kwenye suala la *TPA*. Pamoja na uwekezaji ambao nauzungumza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa dakika zako zimeisha, tafadhali hitimisha.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aida Joseph Khenani. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, dakika tano tafadhali

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumekuwa tukizungumza sana umuhimu wa kuwa na Uwanja wa Ndege wa

Serengeti na Serikali imeahidi mara kadhaa. Mbuga ya Serengeti ni moja kati ya mbuga maarufu sana duniani na imekuwa ikichangia pato kubwa sana kwenye pato la Taifa, lakini napenda kukwambia wewe na Bunge lako Tukufu, wakati wa *high season* ndege ambazo zinatua kwa siku Hifadhi ya Serengeti ni takribani 200. Ndege hizi zinakuwa na *pollution* kwa maana ya *air pollution* na *noise pollution* ambazo zina-*affect* ekolojia ya Hifadhi ya Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inachagiza kuona umuhimu wa kujenga Uwanja wa Serengeti pale Mugumu. Nchi jirani tu wana miundombinu wezeshi ambayo wameweka, watalii wanatua Nchi jirani ya Kenya, wanatoka Nairobi wanakuja mpaka Migori wanachukuwa magari kuvuka kuja Mbuga ya Serengeti ambayo hata miundombinu ya barabara siyo rafiki na wale ambao walikuwa wametua *KIA* pia kutoka Kilimanjaro kule kuja mpaka Mbuga ya Serengeti, ni mbali na miundombinu ya barabara siyo rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoteza mapato mengi sana. Sasa nikataka nijue mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inajenga Uwanja wa Ndege wa Serengeti ambao utakuza uchumi, utakuza na kuendeleza uhifadhi kwa kutoku-*affect* wale wanyama na ndege kwa ekolojia hiyo ambayo nimeieleza. Pia utarahisisha usafirishaji na usafiri kwa watu ambao wanazunguka kwa upande wa Magharibi, kwa maana ya Mkoa wa Simiyu na Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Uwanja huu wa Ndege wa Serengeti ukikamilika na tukizingatia mipango ambayo tupo nayo sasa hivi, ambao tuna mpango mkakati wa kujenga mji wa kisasa wa Mugumu ambao utatoa huduma bora kabisa. Tunaomba Serikali kwa dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kukuza uchumi uwanja huu wa ndege uweze kukamilika lakini pia Uwanja wa Ndege wa Musoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara ndipo Baba wa Taifa anatoka. Uwanja wa Ndege wa Musoma kila wakati wanauweka kwenye bajeti, unaenda kwa kusuasua. Ulikuwa ukamilike mwaka jana Desemba 2023, hadi sasa hivi hata 60% hazijafika. Tunaomba

sana, ni aibu anapotoka Baba wa Taifa, pale kuna kaburi la Baba wa Taifa, watu wakienda kuzuru, inatakiwa wafike Mwanza ndiyo wa-*drive* kuja kwa Baba wa Taifa, haiwezekani, ni aibu sana. Tunaomba wampe heshima, uwanja huu ukamilike, tuwe na ndege zinazotua kila siku pale Musoma ili pia tuuenzi uwepo wa Baba yetu wa Taifa na kukuza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Musoma tuna mazalia ya Ziwa Victoria, hata ndege za mizigo zikifika pale zitasafirisha. Uchumi wa Mkoa wetu utakua, lakini sasa hivi hatuna ndege ambayo inatua pale. Pia Mkoa wa Mara tunalima mbogamboga na matunda na ndege wamenunua ambazo zinaweza kusafirisha kitu ambacho ni *perishable* kutoka kule kufika huku. Kwa hiyo tunaomba sana Serikali iweze kukamilisha. Wamemwongezea mkandarasi mwaka mmoja, tunahitaji ule Uwanja wa Ndege wa Musoma ukamilike *within time,* usiwe na *extension* nyingine yoyote ili tuweze kuwa na usafiri wa uhakika. Hata wananchi wanaokaa Mwanza ku-*drive* mpaka Mwanza ili waweze kupata usafiri si haki. Tuweze kukamilishiwa uwanja huu ili wananchi waweze kusafiri kirahisi na pia kwenda kuzuru pale kwa Baba wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuliomba hapa Kivuko cha *MV* Musoma, wametupatia ila tunaomba watujengee miundombinu ya abiria kukaa upande wa Kinesi ambao una tarafa mbili ambazo wanatumia usafiri wa maji. Wana Tarafa wa Suba ambayo ina kata tano na Tarafa ya Luo-Imbo ambayo ina kata tatu. Hawa wananchi wanapata adha, pale kuna kakibanda tu upande wa Kinesi. Tunaomba waanze ujenzi wa jengo la kusubiriaabiria, kama ambavyo wameanza Musoma Mjini ili sasa hiki Kivuko cha *MV* Musoma kiweze kuwa na maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia nimesema ndege zinatua Migori kule. Pale Tarime tuna *air strip* tu ambazo zipo chini ya halmashauri. Sasa Serikali iangalie kwa kushirikiana, *either* ipandishe ule uwanja maana sasa hivi zile *air strip* pamoja na kwamba zinatua ndege mbili, tatu, tano au kumi kwa siku, lakini zile za Migori wenyewe wameweka lami ndege zinatua. Wakati wanasubiria kujenga uwanja

wa Serengeti wapandishe hadhi ule Uwanja wa Tarime ili walau waweke lami zile *air strips* ili ndege ziweze kutua pale, kutoka Tarime kwenda Serengeti ni pafupi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna dhamira ya dhati ya kukuza Uchumi, lazima tuwekeze kwenye miundombinu ya hivyo viwanja ambavyo nimevitaja ili kuweza kusaidia utalii kukua Mara na kuweza kusaidia wananchi waweze kusafirisha mazao yao yatokanayo na samaki kuliko kuhangaika na kupunguza gharama ambazo zipo sasa hivi. Tukizingatia hayo yote kwa kweli tutaenda kukuza uchumi wetu na utalii wetu utakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia hapa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira kwa dakika tano, atafutia Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Bajeti ya Wizara hii ya Uchukuzi. Nami napenda kuanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa wa tija ambao umefanyika kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurejea tarehe 17 Novemba, 2022, niliiomba Serikali ichukulie kwa uzito mkubwa suala la uboreshaji wa *airport* yetu ya Bukoba Mjini ikiwemo na kutujengea *airport* mpya ya Kajunguti. Mnamo tarehe 19 Novemba, mwaka huo huo 2022 Serikali ilikiri kwamba *airport* yetu ya Bukoba Mjini ina mapungufu na itafanya uwekezaji kwa ajili ya kuboresha pamoja na kuanza taratibu za kujenga *airport* mpya ya Kajunguti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 24 Juni, 2023 kwa maana ya mwaka jana, nilisimama hapa Bungeni nikikumbushia lini *airport* yetu ya Bukoba Mjini itajengewa *control tower,* jambo ambalo nilipata ahadi kutoka Serikalini kwamba itafanya, lakini isivyo bahati kwenye

bajeti ya 2023/2024 haikufanyika hivyo. Halikadhalika tarehe 6 Februari, 2024 nilikumbushia tena hapa Bungeni kupata uhakika kutoka kwa Serikali, kwamba ni lini Serikali itaanza mpango wa kutujengea *Airport* mpya Kajunguti iliyopo Wilayani Missenyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 15 Mei, 2024, kupitia Ripoti ya *CAG* alikiri yeye mwenyewe kupitia tafiti aliyoifanya kwamba *airport* yetu ya Bukoba Mjini inahitaji uboreshaji wa haraka, kwa sababu ndege zinazotua Bukoba, rubani anapata maelekezo kwa kutumia simu kupitia *control tower* ya Mwanza na siyo ya Bukoba. Jambo ambalo ni kinyume na sheria na kuhatarisha maisha ya abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee sana naomba niishukuru Serikali chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Profesa Mbarawa; Mheshimiwa Naibu Waziri, Kihenzile pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Masuala ya Ndege *(TAA),* kaka yangu Mussa kwa kazi kubwa ambayo amefanya na kwa ushirikiano mkubwa ambao ameendelea kunipa kwa kipindi chote hiki tokea tarehe 17 Novemba, 2022 mpaka hivi leo ambapo nimekuwa nikiendelea kufuatilia uboreshaji wa *Airport* yetu ya Bukoba Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa furaha kubwa sana nimefarijika kuona katika Bajeti hii ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, *Airport* yetu ya Bukoba Mjini inakwenda kufanyiwa uboreshaji. Kupitia katika uboreshaji huo tunakwenda kujengewa *control tower Airport* ya Bukoba Mjini. Hali kadhalika tunakwenda kuwekewa taa za kuongoza ndege katika *Airport* yetu ya Bukoba Mjini kwa maana ya *Airport Ground Light (AGL).* Vilevile tunakwenda kuwekewa vifaa ambavyo vitamwezesha na kumwongoza rubani kuweza kutua katika *airport* yetu kwa maana ya *instrument landing system. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Bukoba pamoja na Mkoa mzima wa Kagera, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kuona namna ambavyo Serikali yetu sikivu chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, inapokea maoni ya

Wabunge na inayafanyia kazi kama ambavyo tunaona sasa kwenye Bajeti ya 2024/2025, jambo hili linakwenda kufanyiwa kazi na *airport* yetu inakwenda kuboreshwa. Kupitia uamuzi huo na namna ambavyo Serikali inafanyia kazi mawazo yetu Wabunge, inatupa sisi nguvu na kutuwezesha kuendelea kuishauri Serikali kwa tija, kwa maslahi mapana ya maendeleo ya maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi naomba pia kuishukuru sana Serikali, nimeona katika Taarifa hii ya Bajeti ya Wizara kwamba Wizara imetenga bajeti kwa ajili ya kufanya tathmini katika eneo la kujenga *airport* ya Kajunguti katika Bajeti hii ya Mwaka wa Fedha 2024/2025. Nimwombe sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa atakapohitimisha hoja yake, atueleze bayana hii bajeti iliyotengwa ni kwa ajili ya tathmini tu au pamoja na kuanza mchakato wa kulipa fidia? Maana miaka iliyopita tayari *airport* ilishafanyiwa tathmini na bajeti ilishajulikana kwamba ni takribani bilioni tisa za fidia. Hivyo nimwombe sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** …atakapohitimisha hoja yake atueleze kinagaubaga nini kinakwenda kufanyika kuhusu *airport* mpya, maana Mkoa wetu wa Kagera unaweza kuwa *economic hub* kwa ajili ya Afrika Mashariki. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Hotuba ya Wizara yetu ya Uchukuzi. Nami naanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kweli kwa kuona umuhimu wa Sekta ya Uchukuzi na kuitenganisha na Wizara ya Ujenzi. Hebu fikiria sasa mambo yote haya tunayoyajadili kama yangekuwa kwenye Wizara moja ingekuwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekuja leo mbele yetu anaomba karibu shilingi 2,700,000,000,000 ili aweze kwenda kutekeleza kwa kiasi kikubwa uwekezaji mkubwa ambao ukiangalia sekta ambazo anazisimamia na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, utaona wazi kwamba ndiyo zinashika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchukuzi; sisi katika Kamati ya Miundombinu tumepita katika meli, *TRC* tulipanda treni hapa mpaka Dar es Salaam, tumeshakagua Bandari *TPA*, tulienda kule tukaona Mamlaka ya Hali ya Hewa na rada. Hapa kwenye Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kweli niwapongeze sana wanafanya kazi nzuri. Juzi tumeona taarifa ya HIDAYA na kwa kweli watu wakazingatia kweli HIDAYA anakuja, HIDAYA anakuja; Wazee wa Mtwara na Lindi huko wakaomba dua, wakatambika. Naona kufika huko Kilwa sijui wapi HIDAYA akapotea, lakini kapotea wakati huo huo sisi wengine tumepata athari za upepo wa huyo HIDAYA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa pole kwa wananchi wangu wa Jimbo la Kilombero na Halmashauri ya Mji wa Ifakara. Jana tulipata hali ngumu sana, leo kidogo maji yameanza kupungua na mpaka sasa hivi Mlabani kuna watu 135, Katindiuka 35 na Ifakara 120. Tayari maombi yetu nimeshayawasilisha kwa viongozi wetu wa mkoa, wanayafanyia kazi, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, RAS na kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama ili kuona namna gani tunapata msaada wa nguvu zaidi na mimi Mbunge wao nipo pamoja nao, nitaelekea huko kwenda kuwapa pole. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa *DC*, Dunstan Kyobya, Kamati ya Usalama ya Wilaya kwa kazi kubwa ya uokoaji na mpaka sasa hivi hatujapata kifo chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchukuzi nashukuru Wizara ya Uchukuzi na mwaka jana nilisema hapa sana kuomba ufufuaji wa Reli ya Kilosa kwenda Kidatu. Naishukuru Serikali kwa sababu nimeona fedha angalau za *consultation* zimetengwa karibu shilingi bilioni nne ambapo reli ile itafufuliwa kutoka Kidatu kwenda Kilosa na kutakuwa kuna stesheni Kidatu, kutakuwa na stesheni pia Kilosa ya kubadilisha

kontena. Katika kujenga uchumi wa nchi yetu kwamba tunaweza tukaweka kontena katika Bandari ya Dar es Salaam ikafika Johannesburg, South Africa. Serikali sikivu hii naishukuru sana. Pamoja na hapo nilichomekea katika *TAZARA* kwamba, Ifakara ni Mjini na tuliomba kipande cha lami cha kutoka *TAZARA* kuunganisha katika Stendi ya Kibaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru pia Wizara kwa sababu nililalamika kidogo kuhusu *Airport* yangu ya Ifakara inajaa maji, *DG* wa *Airports* (Viwanja vya Ndege) akaniambia ananiletea wakandarasi. Ameleta wamechimba mitaro, wamepunguza kidogo hali ya maji kujaa na aliniahidi wanaweza kuweka lami kidogo na kujenga banda la kupumzikia abiria. Kutokana na hayo nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nichomekee tu kidogo kutokana na taarifa ya Mheshimiwa Waziri aliyoisema ya Idara zake zote za Wizara, inaonesha wazi kwamba nchi yetu inakwenda vizuri katika uwekezaji. Hapa katika bandari, kwa mfano amesema tuna bandari 693, bandari zilizosalimishwa ni 131, sasa hawa wanaopotosha kwamba kuna bandari zimeuzwa ni bandari gani? Nimesoma taarifa ya Waziri, nimerudia mara mbili, mara tatu sijaona mahali popote ambapo bandari imeuzwa au inawekezwa na mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema hivyo kwa sababu nimeona juzi, nimeona jana Morogoro, nimeona Iringa wapo viongozi wa kisiasa wanarudia kupotosha, kumharibia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wananchi. Natumia nafasi hii kumshukuru sana *Comrade* Abdulrahman Kinana kwa ufafanuzi wake wa jana kuhusu hoja zote zinazohusu uwekezaji wa Sekta ya Wizara yako. Katika kuharibu, yaani kuna mtu katika kila mkoa akienda anarudia, mama huyu kauza bandari, kila akienda na sasa hivi kashindwa hoja kaachana na Mama Samia ambaye anamsikiliza tu, kaenda hadi kwa watoto wake, siku hizi anamtaja na Abdul kila anapokwenda kwa uwongo tu ambao hauna maana yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo kwenye Ujumbe wa Kamati ya Miundombinu. Bandari ya Dar es Salaam ina magati 11 na magati

yote 11 hayajatolewa kwa mwekezaji mmoja na hawatoki nchi moja, wale wawekezaji wawili. Utasemaje Bandari ya Dar es Salaam imeuzwa kwa Waarabu, sijui kuna ardhi imeuzwa kwa Waarabu? Ni upotoshaji ambao kwa kweli hautusaidii chochote, tunaendelea kuchangia hapa kumpa moyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan afanye kazi kubwa. Kelele zilikuwa mwaka jana, halafu tunapowekeza katika mambo haya ya uchumi hii kusema sema kuna watu wamegoma, sijui kuna watumishi wataandamana, sijui nini, tunaharibu uwekezaji wa nchi yetu, tunajiharibia wenyewe tuachane na tabia hizi. Kama tunataka kura tuombe kura kwa busara siyo lazima kuzusha mambo ya uwongo uwongo, mtu unaongea maneno yamepinda na ukitembea hunyooki, tabu tupu. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia ametulia anajenga nchi yetu vizuri, kwa nini tusimuunge mkono? Tuseme tunaongea kwa maneno ambayo hayafai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili la msingi wenzangu wamesema hapa na kauli za Wabunge ni wazi kuwa zinathibitisha kwamba Wabunge wote wanataka hii *wharfage* irudi ikusanywe na *TPA*. Nataka kusisitiza hapa na nilivyokuwa naangalia *meaning* (maana) ya *wharfage* wanasema ni *accommodation provided at the wharf for the loading or storage of the goods*. Sasa kama *wharfage* maana yake ni hii, Wabunge wote wamesema hapa na mimi nataka kusisitiza sekta yoyote ukiangalia hapa makusanyo makubwa tunayopata tunapata katika bandari zetu tulizosema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Kamati ya Miundombinu tumezunguka wote huku tunakosoa bandari, uwekezaji ongezeni kasi, Dar es Salaam kuna foleni unganisheni na reli, kontena ziondoke mjini, foleni ipungue Dar es Salaam. Hawawezi kama hawana fedha, *50%* ya mapato ya *wharfage* haikusanywi na wao. Sasa hivi wameshafunga mfumo mzuri wa mapato ambao unaitwa *Real Time Revenue Collection Data*, warudishiwe hii. Wizara walete Sheria Na. 17 ya mwaka 2004 iliyoboreshwa mwaka 2019 kupitia Sheria Na. 7 Kifungu cha 67(1) ili Bunge hili lipitie libadilishe lipeleke fedha hizi. Shilingi bilioni 50 kila mwezi zinatolewa Bandarini Dar es Salaam zinapelekwa Hazina na huko wanaweza wakazipangia kazi nyingine yoyote na hazirudi kuboresha bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo tukiboresha bandari yetu kama sehemu inayotupa mapato makubwa; kauli ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba tukiwekeza vizuri katika bandari tutapata *50%* ya bajeti ya nchi yetu itaweza kufikika na kufikiwa. Kwa hiyo, naomba sana jambo hilo tulifanyie kazi kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, amesema Morogoro tuna Kiwanda cha Ndege na kweli kipo pale, matajiri ambao wapo humu waje wanunue ndege Morogoro, yaani kuna ndege za watu wawili wawili. Waje pale, walete *order,* waweze kununua ndege, tunatengeneza ndege kweli siyo uwongo. Waje pale waone kwa namna gani tunaweza kuboresha sekta yetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba kuzungumzia madeni; najua Mheshimiwa Waziri ulishasema mara kadhaa kwamba maendeleo ni mchakato, ni *process*. Mheshimiwa Waziri hata tukikukaba koo hapa huwezi kufanya yote kesho asubuhi, lakini kwenye madeni wajaribu katika Wizara yao kuweka vipaumbele. Kamati tulienda kule Mtwara tulikutana na kampuni iliyojenga *Airport* ya Mtwara na ma-*sub contractors* walikuja pale chini wanalia machozi zaidi ya karibu miaka miwili yule *Beijing Construction* hajalipwa na wao chini huku hawajalipwa na wana mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda huko Shinyanga, tumeenda Mwanza kuna wakandarasi wanalalamika kwamba hawajalipwa. Nafikiri hatuwezi kulipa wote, basi tuchague wachache ambao tunaweza tukapunguza madeni yao, tukalipa ili kuifanya sekta hii iweze kwenda vizuri, vinginevyo nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tumefika mwisho wa uchangiaji kwa asubuhi ya leo. Naomba niwasome wale ambao watachangia mchana kwa maana ya jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi na wengine

ambao watasomwa muda ule. Nimewasoma hawa ili wapate nafasi ya kujiandaa na kuwahi kwenye kikao tutakachoendelea nacho mchana.

Baada ya hayo, nasitisha Kikao cha Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.56 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa na Mheshimiwa Esther Edwin Malleko ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuwa mchangiaji wa kwanza mchana huu kwenye mjadala huu wa Wizara ya Uchukuzi. Natumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu anakwenda kuingia kwenye historia ya nchi hii kama Mheshimiwa Rais ambaye alifanya mapinduzi makubwa kwenye eneo la reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, inatarajia kutengeneza mtandao wa reli ya kisasa *(SGR)*, unaokaribia kilometa 4,572, hivi sasa mtandao huu wa *SGR* ambao tunaupambania kwenye *central corridor* kwa kazi zinazoendelea za kilometa takribani 2,102. Mradi wote huu utagharimu karibu trilioni 20 na sehemu na tayari Serikali ya CCM imekwishalipa trilioni 10 na zaidi kwa ajili ya kazi ambazo zimeshakamilika. Yapo mambo machache ambayo lazima tuyaboreshe wakati tukikaribia kuanza kwa *operations* za treni ya *SGR* kutokea Dar es Salaam mpaka Makutupora, wakati huohuo tukiendelea kukamilisha vipande vingine vilivyobaki, haya mambo lazima yaende sambamba na ujenzi wa reli kadri inavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza, lazima tuufanye usafiri huu kuwa usafiri wa kisasa, tufanye usafirishaji wa kisasa na njia pekee ya kufanya *SGR* kuwa usafiri wa kisasa na kufanya usafirishaji wa kisasa ni kuifungamanisha *SGR* na miundombinu mingine ya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo taasisi ambazo lazima zifanye kazi usiku na mchana na sisi kama Bunge hapa lazima tulione hili na kwenye bajeti zetu tujaribu kulipa majawabu. Kwa mfano, *TANROADS, TARURA,* Halmashauri za Miji, ambako reli inapita vilevile bandari, kwenye reli inakopita viko vituo vya *SGR* ambako ndiyo abiria watakuwa wanashuka na kupakiliwa, ambako ndiyo mizigo itakuwa inashushwa na kupakiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ambazo zinakwenda kwenye vituo hivi vya *SGR* lazima tuzijenge kwa kiwango hiki cha mradi huu mkubwa wa kitaifa ambao tunajivunia kuwa nao na ambao haupo Afrika Mashariki wala Nchi za Maziwa Makuu na Kusini mwa Afrika, lazima barabara hizi zikajengwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatolea mifano ya vituo kama vitatu hivi ambavyo viko *alongside*, ambavyo vinajengwa kwa ajili ya kushusha abiria. Kwa mfano, Kituo cha Morogoro, ni lazima kwenye kituo kile cha Morogoro, kwanza tuwe na barabara nzuri ya kufika kwenye kituo ijengwe kwa kiwango cha lami. Pia tujenge miundombinu ya mabasi

ili watu wanaoshuka waweze kupanda kwenye usafiri kutoka pale kwenda usafiri mwingine. Vivyo hivyo, kituo cha Kilosa na vituo vingine kama ilivyo pale Ngerengere. Kipande cha barabara kutoka Ngerengere kituo kilipo kwenda barabara kubwa kilometa 16 tupige lami pale, huu mradi lazima tuufananishe na thamani yake ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hauwezi ukawa na mradi kama huu halafu kesho tuje tukutane hapa tunajadili fedha za dharura za *TARURA* kwamba njia ya kwenda *SGR* haipitiki! Hilo ni jambo la msingi sana lazima tulifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, wenzetu wa sekta mbalimbali za uzalishaji, lazima *SGR* tuifungamanishe na Sekta za Uzalishaji kama Kilimo, Mifugo, Madini, Utalii na Viwanda. Tusijenge *SGR* hii tukitazama mizigo ya nchi jirani peke yake, lazima sisi wenyewe tuishibishe mzigo *alongside the way*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Waziri wa Madini na Wizara ya Utalii, lazima wakae chini na kuona wataifanyia nini *SGR* hii ambayo Watanzania tunaweka fedha nyingi. Kila mmoja kwa nafasi yake awaze na aweke mipango ya kuhakikisha kwamba treni yetu hii ya kisasa inapata mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwezo wa treni hii kwa mwaka *minimum* itakuwa na uwezo wa kusafirisha tani milioni 17 na ukibeba *maximum* itakuwa na uwezo wa kusafirisha tani milioni 25 kwa mwaka. Sasa kama hatukuweka mikakati katika maeneo ya uzalishaji kule inakopita, tutashindwa kuipatia mzigo wa kutosha treni hii na mradi wetu utaishia kuwa *a white elephant*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la kurekebisha na kuwekea mkazo ni uhusiano wa ujenzi wa *SGR* pamoja na utunzaji wa mazingira. Kwenye ujenzi kuna kitu kinaitwa *hard part engineering design*, ndiyo hiki ambacho tunaangalia *environment impact assessment* halafu watu wanajenga reli. Kitu muhimu katika miundombinu ya reli katika dunia ya leo ni *soft part engineering design*

ambayo inahusiana na namna gani tutayatunza mazingira na kuutunza huu mradi ili udumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitawatolea mfano, mwaka 2012 pale katikati ya Munisagara na Kilosa, kwenye reli yetu hii ya zamani ya *MGR* palijengwa daraja pale miaka kama 12 iliyopita. Wakati daraja lile likijengwa, kutoka pale daraja lilipo, kushuka maji ya mto yanapofika ilikuwa ni mita karibu 20. Leo ukienda pale kumefanyika *siltation*, udongo umetoka milimani, umeshuka kwenye mto, mto umejaa tope na *distance* ya maji pale imebakia kilometa tatu tu, *which means* ikinyesha mvua kubwa, lazima maji yata-*flood* pale, tusiruhusu hiyo ikatokea kwa *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tuweke sera madhubuti za kimazingira na tuweke mpango mzuri wa kulinda miundombinu hii ya *SGR*, ikiwezekana tuwe na asilimia fulani ambayo inakatwa kutokana na mapato ya *SGR* iende ikasimamie mazingira ili mradi wetu uweze kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa Reli ya Ruvu – Tanga na Tanga – Arusha. Reli hii ndiyo reli pekee ambayo iko kwenye Mikoa ya Kaskazini, kwa maana ya Tanga, Arusha, Manyara na Kilimanjaro. Pia, ni reli ambayo imebeba uchumi mkubwa. Ruvu – Tanga (kilometa 268) na Tanga – Arusha (kilometa 438) lakini Serikali haiifanyii ukarabati reli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna viwanda vya simenti Tanga na ambavyo ukitumia reli kusafirisha simenti, *you cut your cost of transportation* kwa karibu 40%. Tungeikarabati reli hii leo tusingekuwa tunalia na bei kubwa ya simenti. Ni jambo la ajabu sana, eti ikifika *Christmas* watu wanaanza kukarabati reli ya kaskazini. Hii ni reli ya mizigo, siyo ya kupeleka watu *Christmas*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya uwekezaji mkubwa Bandari ya Tanga na sasa tunajenga gati namba tatu pale kwa ajili ya makasha ya kontena, sasa tutayaondoaje haya kama hatukarabati reli hii? Vilevile, tukiikarabati hii reli, ndiyo itatumika kama *feeder* ya mzigo

kwenye *SGR*. Itakuwa rahisi mzigo kutoka Bandari ya Tanga na ukafika kwenye Bandari ya Kwala kwa urahisi kwa kutumia reli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa hapa ni tukayaimarishe madaraja yaweze kubeba mzigo mkubwa, vilevile, tukaondoe reli ambazo zimechakaa, yale mataluma na tuweke mengine. Kwa kufanya hivyo reli yetu itaweza kutembea angalau kwa *speed* ya 60 kilometa kwa saa. Hivi sasa inatembea kilometa 20 kwa saa, inatumia masaa 10 mpaka 12 kutoka Tanga kuja Dar es Salaam. Hiki ni kitu cha ajabu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho, bandari yetu kwa maana ya watu wetu wa *TPA* ni lazima tuwawezeshe. Iko sheria tulitunga hapa, inaitwa *The Treasurer Registrar Powers and Functions*, ambayo ni *Act, Cap.* 370. Sheria hii inawapa Hazina kupitia Msajili wa Mashirika, uwezo wa kutoza makusanyo kutoka kwenye mapato ghafi kwenye makampuni na mashirika ya umma 15%, kana kwamba haitoshi kwa mapato ya ziada anapewa Msajili wa Hazina kutoza tena 70%. Hii 15% ya mapato ghafi na 70% ya mapato ya ziada yalikuwa yanatosha kabisa kwa Serikali kuchukua mapato kutoka kwenye mashirika haya.

Mheshimiwa Spika, *wharfage* wawaachie watu wa bandari, wakusanye wenyewe, lengo watengeneze *balance sheet* zao vizuri, wakiwa na *balance sheet* nzuri wataweza kukopa na kuendeleza gati mbalimbali. Kwa kufanya hivyo watakuwa wanawapunguzia mzigo Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa. Atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mheshimiwa Haji Amour Haji, ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nami pia nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji katika hotuba hii ya Wizara ya Uchukuzi. Kipekee naungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika Sekta hii ya Uchukuzi, hasa uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanyika katika Shirika letu la Ndege la Air Tanzania, tunaona ndege ni nyingi kweli kweli, sasa hivi karibu *regional routes* hizi ndege zetu zinafika kwa sehemu kubwa kwa majirani zetu na tunafanya *routes* za hapa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *SGR* pia naungana na wenzangu ambao wametambua mchango mkubwa, huu ni uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Sita, chini ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia, uwekezaji mkubwa ambao umefanyika katika bandari, maana mwaka jana wakati wa bajeti gati Na.8 mpaka 11 bado yalikuwa na urefu wa kina cha mita 11 na kwa taarifa nilizonazo tuliposimama hapa leo tayari zile gati zimefika kina cha mita 15. Kwa hiyo, faida kubwa ambayo tunaiona vina hivi vilivyoongezwa, maana yake tumepunguza zile meli ndogo za kontena 2,500, sasa hivi tunapokea meli kubwa za kontena mpaka 6,000. Kwa hiyo ni *advantage* kubwa, nikimaanisha kwamba mizigo inakuwa mingi zaidi ambayo inapita katika bandari yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao wamebahatika kupita Dar es Salaam, naweza nikasema jinsi tulivyojitangaza na yale ambayo yanafanyika hasa kuvutia wenzetu wa nchi jirani wanaopitisha mizigo hapa na ndani pia biashara zinavyokuwa, naamini sasa hivi meli ni nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha nyuma ulikuwa unaweza ukakaa ukaona mzigo labda unafika ndani ya wiki mbili, kutakuwa na *delay,* lakini sasa hivi meli ni nyingi, nimejaribu kufuatilia, ni *low season* lakini meli zinafika mpaka 35 ambazo zipo kwenye foleni. Kwa hiyo, tunategemea tutakapofika *high season* kuanzia mwezi Agosti, Septemba mpaka mwezi Novemba, huenda inaweza ikawa *double* mpaka meli 70 na kuendelea. Kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa,

maana yake *revenue* yetu kupitia bandari inaenda kuongezeka hasa kwenye upande wa forodha, ukusanyaji wa kodi na mapato mengine yanayotokana na bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi tunayaona haya yote, mfanyabiashara *always* huwa ni mtu wa haraka kwa sababu ana *commitment* zake, anayo mikopo na kadhalika na anatakiwa ahudumie wateja, kwa hiyo, kila kimoja kinakuja na *advantage* yake na *disadvantage* pia.

Mheshimiwa Spika, tukijaribu kuangalia *conjunction* hii imesababisha *sometimes* meli zina-*delay* mpaka wiki tatu, nyingine huenda zinaenda zaidi kwa sababu muda wa kushusha meli moja sasa hivi ni siku tano, sasa tumesaini mikataba ya *DRC* kuanza kupitisha mizigo yao hapa kwenda nje.  Sasa ukipiga hesabu ya meli moja kushusha mzigo kwa siku tano, nyingine ije ipakie, huenda meli moja inaingia kwenye gati itakuja kutoka baada ya siku nane au siku tisa, kwa hiyo ni lazima, hatukwepi suala la uwekezaji kwenye habari ya bandari. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile ni lazima *TPA* awezeshwe, aongeze magati mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilivyofuatilia bei ya kujenga gati moja siyo kubwa, ni dola karibu laki moja au bilioni 250. Sasa ukipiga hesabu uwekezaji wa gati kama 10 ni *almost 2.5 trillion*. Sasa ukiwekeza 2.5 trillion kwenye gati 10 na gati moja kama utaangalia *average* ya mapato tofauti na yale mapato ya forodha tumekuwa tunaenda mpaka trilioni 13. Kwa hiyo, ukifanya *average* kwa gati 11 tuliyonayo ni *almost* kila gati inakuingizia trilioni moja. Ukijenga gati nyingine 10 una uhakika wa kupata siyo chini ya trilioni 10 kwa mwaka, maana yake mapato yataongezeka.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri yuko hapa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko hapa, Kamati imesema kwenye habari ya *wharfage,* tunaomba hili jambo liangaliwe na *TPA* wawezeshwe, kama inawezekana watafute mikopo katika mabenki, wafanye uwekezaji wa gati 10 kwa mara moja au hata zaidi ya 10 ili ziweze ku-*accommodate* ile mizigo, kwa sababu foleni inavyozidi

kuwa kubwa, mtu akaona anacheleweshewa mizigo maana yake ata-*opt* kwenda sehemu nyingine hatimaye tutapata hasara na hata yale mambo mazuri tunayoyatarajia hatutaweza kuyaona. Kwa hiyo, tunaomba jambo hilo walione, taarifa ya Kamati imesema, Mheshimiwa Waziri, alichukue ili waweze kwenda kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ukimwambia tena Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mwigulu akatafute tena pesa akope awape, kesho wakishindwa kulipa ni *commitment* nyingine tena, tutaanza kumhangaisha hapa. Maana atakuwa anakimbizana na barabara, reli na kila kitu kinamwangalia yeye, kwa hiyo, kama wanafanya biashara na wanao uwezo wa kujiendesha wenyewe, tuone kama tunaweza tukawarudishia hii pesa wakaingia kwenye *business* wakakopa, hatimaye wakaweza kufanya rejesho Serikalini na wakajiendesha wenyewe, *the way* ambavyo wanataka kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, nahama hapo naenda kwenye habari ya *SGR*. Nimeipongeza sana habari ya *SGR* lakini sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, sina shida na haya yanayofanyika, ni mazuri sana, lakini kitengo chenu cha mawasiliano aidha kupitia *TRC* au Wizarani hawako-*active* kwenye kupambana na haya mambo. Kipindi cha nyuma tuliona picha za ajabu ajabu zinatumwa, watu wanaambiwa mabehewa mabovu, wanaambiwa hiki na hiki, lakini ukiangalia picha ambazo Mheshimiwa Waziri ameweka kwenye *front page* ya hotuba yake ni picha za Kituo cha *SGR* cha Dodoma, huenda watu wanajua tu kile kioo cha Dar es Salaam hawajaona jengo la Dodoma lilivyojengwa, hawajaona mpishano wa zile reli ambavyo umefanywa kwenye picha kama hizi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali, vitengo vyao vinavyotoa taarifa, propaganda ni nyingi na hasa tunavyoelekea kwenye uchaguzi, watusaidie watu kwenda kwenye mtandao wa *twitter* wakaajiri vijana wenye uwezo wa kujibu mle, kunashindikana nini? Tunaomba Serikali waweze ku-*counter attack*. Kila upotoshaji unapotokea wawe na watu *active* wa kusaidia. Mambo makubwa yanafanyika, lakini bahati mbaya sana upande wa Serikali hawawahabarishi wananchi mpaka itokee taharuki ndiyo wanakuja.

Wafanye wananchi wajue uwekezaji mkubwa kwa kuona kwa picha, wajue pesa hii ya kodi yao inapokwenda, hatimaye hata wao waendelee kuiunga mkono Serikali. Hata Mheshimiwa Rais anaposemwa vibaya kwenye mambo mengine, wasimame naye kwa sababu wanaona na wanajua kinachofanyika. Naomba hilo nilisisitize ili muweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera hususani Wilaya ya Biharamulo, kwenye mpango ambao Mheshimiwa Waziri anajua p*lan* za *TRC* zipo, bado naendelea kusisitiza, reli ya kutoka Isaka kupitia Nyakanazi - Biharamulo, iende Rusumo na hatimaye iingie Kigali, tunaomba wazidi kuangalia *possibility* ya kutuunganisha na sisi pia, maana ndugu zetu wengi sana wamekufa huko, kwa sababu magari yanayotumika kuja mpaka Isaka kwenda sehemu nyingine ni *left hand*.

Mheshimiwa Spika, unakuta mtu anaye-*drive* gari kutokea Rusumo kupita Biharamulo mpaka afike Isaka kubeba makontena, nchini kwake anaendesha kwa *left hand*, sasa huyo mtu *sometimes* akishafika anaona barabara mita 500 mbele kuna nini, huwa wanahama wale watu. Sasa wewe ukimwona unajua labda amehama atarudi kumbe yeye ameshaingia kwenye *driving* ya nchi yake, hatimaye wanatusababishia ajali na vifo vingi sana kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakapozuia kwa kuhakikisha mizigo mpaka inavuka *border*; kwanza tuta-*facilitate CFR,* kama ni *CIF* iwasogelee kule na ni sehemu ya *SGR* kutumika. Pia, tunaokoa barabara na ajali nyingine nyingi ambazo zimekuwa zikitokea na kutusababishia vifo hasa watu wa Mkoa wa Kagera na maeneo ya jirani. Kwa hiyo, niombe Waziri aendelee kuliangalia kwa sababu, uchumi tunavyozidi kuujenga tukisambaza reli kila sehemu *advantage* yake unaiona, tutaenda kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, nimepongeza *Air Tanzania* na nikasema mambo mazuri ambayo wanafanya, uwekezaji ambao unafanywa na Mheshimiwa Rais. Wenzangu walisema hapa asubuhi, sisi watu wa

Kanda ya Ziwa tunajiuliza huwezi kuwa na *Capital City* kama hii ambayo shughuli zote za Serikali zinafanyika hapa, halafu *the only way* ya kuja Dodoma kwa ndege mpaka upite Dar es Salaam. Mtu wa Kagera au Mwanza, leo akitaka kuja Dodoma kwa ndege aende mpaka Dar es Salaam ndiyo arudi hapa, *not less than 1.4 million*. Hiyo ni nauli ya kwenda Dubai na kurudi, wewe utoke pale Kagera kuja hapa *this is not fair*.

Mheshimiwa Spika, sasa tuombe kwa Mheshimiwa Waziri yuko hapa, najua bado wanaweza wakapanga *route* nzuri maana ni *idea* kama watanyanyua ndege kubwa ikaamka asubuhi, ile ya Mwanza – Dar es Salaam iendelee kuwepo. Sasa hivi tuna *Boeing Max* nyingi tu, ikanyanyuka moja asubuhi ikaja Dodoma, ikatoka Dodoma ikabeba abiria ikapeleka Mwanza na *the same* ikatoka Mwanza ikarudi Dodoma, ikatoka Dodoma ikarudi Dar es Salaam. *It's a very easy route*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa kufanyika, Mheshimiwa Waziri ile ndege haiwezi kutua kwenye Uwanja wa Dodoma, *impact* yake na uzito wake ni mkubwa, huu uwanja utaharibika, ndiyo maana haiwezi kutua hapa. Waziri amesema kwenye taarifa Uwanja wa Msalato uko *fifty something percent*. Kama kweli uko hapo na *runway* iko sawa aweke ma-*tent* pale watu waanze kutua. *Tent* zimetumika Nairobi wakati wa adha, mtu anapita pale tu kwanza zitakuwa zinatumika asubuhi. Hatuna haja ya kukamilisha Jengo la Abiria, ndiyo tuanze kurusha ndege kubwa.

Mheshimiwa Spika, leo ninaposimama hapa, simu yangu hii hapa Wabunge wanaweza wakaangalia, huwezi kupata *booking* ya kwenda Bukoba leo. Asubuhi nilikuwa naangalia *booking* iliyokuwepo ni ya tarehe 12. Ndege za kwenda Kagera zimekuwa kama anasa kwa maana ndege ni moja inajaa haraka. Tunapoomba tujengewe Uwanja wa Kajunguti tuna maana. Sasa haiwezekani leo mtu anayetaka kwenda Bukoba kwa dharura inabidi utafute safari ya kwenda Mwanza, ukifika Mwanza ndiyo uanze kusafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi tena kwenda na ndege maana ndege *two weeks, one week* ndege inakuwa imeshajaa, ndege ni moja, lakini watu wa Kagera tunasafiri na ndege mara nyingi, kwa hiyo inatusababishia adha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba watusaidie, watujengee Uwanja wa Kajunguti maana Mheshimiwa Waziri, amesema wameona ni vyema uwanja ule uendelee kutumika. Nikwambie hata ukiweka ile rada, mvua Kagera zinavyoanza kunyesha hususan Bukoba hakuna rubani wa kutua na ile ndege pale. Tunajua sisi *the way* ambavyo tunakuja na ndege halafu tunakatishia safari Mwanza mpaka mvua iishe ndiyo tunaanza kwenda safari ya Bukoba. Tunaomba, tumeshapatwa na majanga mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ajali ya meli imetukumba wakati wa *MV Bukoba*, tumepata shida ya ndege na tumepata shida ya matetemeko. Kwa hiyo, hata sisi tunaposema tujengewe uwanja tuna maana abiria wapo Mkoa wa Kagera. Wakitujengea uwanja ile ndege haitarudi tupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yangu ndiyo hayo niliyotaka kuwasilisha, zaidi ya yote, naunga mkono hoja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, bajeti ipite, Uwanja wa Kajunguti ujengwe, hatimaye waone *flow* ya biashara kutoka Kagera. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Amour Haji na Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, ajiandae.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia jioni ya leo. Kipekee nimshukuru

sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuniwezesha kusimama hapa ili kuchangia katika Bajeti hii ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kipekee nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo ameweza kuweka mkazo na kipaumbele katika kuboresha na kuendeleza sekta hii ya uchukuzi. Ameboresha miundombinu, lakini pia huduma za uchukuzi zimeboreshwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisiache kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. Sekta ya Uchukuzi imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika kuleta maendeleo na kujenga huduma ya uchumi imara katika Taifa letu. Sisi wote ni mashahidi, miradi mikubwa ya kimkakati inaendelea katika Sekta hii ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianza na *SGR*. *SGR* inafanya kazi nzuri, tumeona tayari wameanza majaribio ya *SGR* kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma. Haya ni maendeleo makubwa sana kwa nchi yetu. Tukio hili ni la kihistoria kwa sababu na sisi tumevuka na tumekuwa katika Nchi za Afrika zenye *SGR,* lakini ambayo ni ndefu kuliko zote Barani Afrika ni *SGR* ya Tanzania ambayo ina kilometa 2,100. Sisi tunapaswa kujivunia na kumpongeza sana Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Nchi jirani kama Ethiopia mpaka sasa wana kilometa 700, Kenya wana kilometa 700. Kwa hiyo, sisi Tanzania tunamshukuru Mungu kwa hatua hii kubwa tuliyofanya. *SGR* hii imefanya majaribio, sasa iende ikaanze kazi na huduma zitolewe na wananchi waweze kufurahia *SGR* yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, nawaomba sana wanaohusika katika *SGR,* katika ujenzi wazingatie mabadiliko ya tabianchi kwa sababu wakati mwingine yanaenda kutukwamisha na sisi hatutaki *SGR* yetu ipate matatizo yoyote katika usafiri.

Mheshimiwa Spika, naendelea na bandari; katika uboreshaji wa huduma za bandari tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tumeona ni namna gani ameweza kuwekeza pia hapa kwenye bandari. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana kaka yangu Mbossa kwa kazi kubwa anayoifanya. Vijana hawa wameaminiwa na Mheshimiwa Rais na wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, tunaona gati zinajengwa, lakini si hivyo tu, wanapoenda kufanya hii kazi tunaomba tuishauri Serikali zile fedha za *wharfage* ambazo hata wenzangu wamesema sana ziweze kubaki pale *TPA* na ziweze kuboresha miundombinu. Miundombinu hiyo itasaidia *TRA* waweze kukusanya kodi yao kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia siku ya leo ni kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vya Tanzania. Niwapongeze sana *TAA*, sisi kwetu Kilimanjaro tunawapongeza sana kwa namna ambavyo waliona umuhimu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Waziri, Naibu Waziri na wote wanaofanya kazi katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kule Kilimanjaro tuwanapongeza sana kwa sababu, wameweza kuiondoa *KADCO* iende kukaa chini ya *TAA*. Hayo ni mapinduzi makubwa sana, tunawaongeza sana Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya. Ili hii Taasisi iweze kufanya kazi zake vizuri na kutoa huduma bora zaidi kwa abiria na mizigo. Nashauri waweze kuleta ile Sheria hapa, ifanyiwe marekebisho ili iweze kupata zile fedha zinazotokana na tozo ya huduma za abiria *(passenger service charges)* iweze kubaki katika taasisi hii ili iweze kujitegemea kwa sababu sasa inaitegemea sana Serikali. Kwa hiyo, naomba kushauri jambo hili lizingatiwe ili taasisi hii iweze kufanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea hapohapo, sisi kule kwetu Moshi tunaendelea kuwashukuru kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kiwanja chetu cha Moshi ili kiweze kupanuliuwa, tunaomba sasa Taasisi hii au Wizara iweze kuangalia ni namna gani inaweza kulipa fidia kwa wale watu wenye zile nyumba sita ambao wana hati pamoja na zile tatu

ambazo hazina hati ili sasa waweze kupanua *runway* na kuweka taa. Hapohapo iweze kuboreshwa kutoka, ndege ambayo inatua pale kwa sasa itakuwa ina abiria 40 tu, lakini pakiboreshwa kwa namna hiyo panaweza kutua ndege yenye watu zaidi ya 70. Tunaomba jambo hilo liweze kuzingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naenda kwenye *ATCL*. Naomba kwa kipekee sana nimpongeze sana *Engineer* Matindi kwa kazi nzuri anayoifanya. Sisi wote ni mashahidi, *ATCL* inafanya kazi nzuri na mpaka sasa tunaweza tukasema kwamba Tanzania tumepiga hatua kubwa sana kwenye usafiri wa anga. Leo tuna ndege 16 zikiwemo ndege za mizigo, hii ni hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunampongeza Mheshimiwa Rais katika uwekezaji unaoendelea katika Kampuni hii ya Ndege. Leo wakati wanatambulisha hapa tumeona Marubani wanawake. Naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Taasisi hii kwa namna ambavyo inaona umuhimu wa wanawake na kazi nzuri wanayoifanya wanawake. Tulimwona ndugu yetu, dada yetu Neema ameendesha ndege ile kwa masafa marefu na mpaka amefika Tanzania salama. Ni kiasi gani wanawake wanaendelea kuaminiwa na nampongeza sana *Engineer* Matindi kwa namna ambavyo anaona ni namna gani wanawake wanaweza kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona wahudumu wa ndani ya ndege, waliokuwa hapa leo wako katika viwango vya Kimataifa; ni bora sana, nawapongeza sana *ATCL*. Si hivyo tu, tunaona namna mtandao wa safari za *ATCL* unavyoendelea kukua hapa nchini na nje ya nchi, niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku hii yangu ya leo, nimesoma katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nimesilikiza pia Hotuba ya Kamati. Nimesikia wamesema maneno mengi sana mazuri, lakini kipekee niwapongeze kwa kazi nzuri sana waliyoifanya. Hata hivyo, nina jambo moja ambalo nataka kushauri. Naomba kuishauri *LATRA* kwa maana imesema katika vipaumbele vyake ni kudhibiti usafiri,

kuimarisha usalama, udhibiti na utoaji wa huduma za usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa niliyoisikia wamesema vizuri sana kuhusu mabasi na usafiri mwingine, lakini sikusikia wakisema kuhusu pikipiki. Naomba tujiulize sisi kama viongozi tulioko hapa ndani tunajua kabisa usafiri wa pikipiki ndiyo unaotumika sana kwa sasa hivi. Inaweza kuwa mtu asiseme lakini kiukweli pikipiki zinatuokoa sana. Niliwahi kuchelewa *airport,* kilichoniokoa ni bodaboda. Nasikitika sana katika taarifa hii sijaona ni namna gani wamejipanga kuwanusuru vijana wetu wanaoangamia kwa ajali za bodaboda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda *MOI*, asilimia kubwa ya vijana wako pale ambao wamepata ajali. Kuna Gazeti la Nipashe ambalo lilitoka Februari 7, lilikuwa limeandika *MOI* imezidiwa na wagonjwa ambao wanatokana na ajali za bodaboda. Hili ni jambo la Taifa kuliwekea macho, ni jambo ambalo wanatakiwa kuliangalia vizuri. Kipindi kilichopita sisi tulikwenda Rwanda kwenye michezo. Wote tuliokuwa pale tulijionea wenzetu wanavyofanya kazi nzuri ambapo bodaboda wamepewa elimu na wanafuata sheria za barabarani. Tunaomba sasa jambo hili liangaliwe na lizingatiwe vizuri ili kuokoa maisha ya vijana wetu na waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Amour Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kabudi na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii leo ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi. Kwanza kabla ya yote, nijumuike na wenzangu kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anatimiza ahadi na vilevile kuleta uwekezaji mkubwa sana katika nchi yetu hii hasa katika Wizara ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Makame Mbarawa pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara. Tatu, kwa kipekee kwa maana hizi ni pongezi za kipekee nampongeza Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi ambaye jana alitoa hotuba yake nzuri sana pale Jakaya Kikwete na kila ambaye hakuweza kwenda pale aitafute ile hotuba ya Makamu Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi kwa sababu kazungumza mambo ambayo ni mazuri sana pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo nije katika hali ya mashairi, kule kwetu Zanzibar kuna wimbo ambao mara nyingi huwa unaimbwa sana na ni wimbo wa kimapinduzi na wimbo huu ni maarufu sana. Leo sitoweza kuimba isipokuwa nitasema yale mashairi. Ni wimbo ambao ni maarufu sana, mashairi yale yanasema hivi: "*Walisema hatuwezi, waje watutazame*". Wakati huohuo kukawa na kibwagizo kingine, "*Walisema uongozi, kwetu hautosimama*". Sasa niingize shairi la tatu, "*Mama Samia kiongozi, imara amesimama.*" Hayo ndiyo mashairi ambayo kwa leo itakuwa kama ni kibwagizo kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika mtazamo wa Waswahili. Waswahili nao wana maneno yao ambayo ni maarufu sana huwa wanasema kwamba: "*Usimtake bubu kusema, ukimlazimisha kusema, siku atakayokuja kusema, maana yake utakuja kuadhirika. Usimlazimishe kipofu kusikia, siku utakapokuja kumlazimisha kusikia, utakuja kuadhirika au utakuja kwenda mbio*". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa la kuzungumza kwangu hapa ni kuchangia bajeti...

**SPIKA:** Mheshimiwa Amour, nadhani ulikusudia kusema kiziwi.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo kiziwi. Lengo kuu la kuchangia bajeti hii, kwanza kabla ya kusema lolote naunga mkono hoja ya Taarifa ya Bajeti ambayo imetolewa na Wizara ya Uchukuzi kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi iliyofanywa katika Bajeti ya Uchukuzi ni kazi ambazo ni kubwa sana. Hizi kazi zilizofanywa ni kazi za ahadi ambazo ameahidi Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siku ambayo ameapishwa. Kwa maneno ambayo aliyasema: *"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi Iendelee"*. Bahati nzuri Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia mtangulizi wake aliachiwa kazi nyingi sana ambazo hapo nyuma zilikuwa katika asilimia ndogo sana, lakini kwa sasa hivi kila mmoja anaona na mwenye macho haambiwi tazama. Kazi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kazi hizo zilizofanywa kupitia Wizara ya Uchukuzi kwanza, niangalie katika Taasisi yao moja ya *TRC*. *TRC* ambayo ina kazi iliyoachwa nadhani kwenye 30%, lakini kwa sasa hivi hakuna asiyeona kwamba Shirika la Reli *(TRC)* ambalo limefanya kazi kubwa sana ya kujenga ile Reli ya *Standard Gauge,* hatukutarajia kwamba ndani ya miaka miwili hii au mitatu ambayo kakaa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan; treni ile kwa sasa hivi itaweza kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma. Kwa kweli hiyo ni hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuangalie upande wa *TPA*, napo pamefanyika mapinduzi makubwa sana. Tukiangalia kwa namna ambavyo alivyoichukua kipindi chake kutoka kwa mtangulizi wake, mimi siyo mtu wa mahesabu lakini kila siku tunasikia kwamba mapato ya *TPA* sasa hivi yamekua kwa asilimia kubwa sana. Kwa wale Wabunge wenzangu ambao huita kwa mabilioni, nadhani mimi nitaita kwa matrilioni sitosema kwa mabilioni. Kwa hiyo, nawapa hongera sana *TPA*, *TRC* na *TASAC* kwa namna ambavyo wametimiza ahadi ya kuikamilisha ile Meli ya Hapa Kazi Tu. Pia, ile meli imeleta taswira nzuri sana kama ni moja ya maendeleo ambayo yatakuwa yamefanywa katika Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia suala la *TMA* kwa mujibu wa *radar* zilizowekwa pale maana yake napo kunastahiki sifa ambazo ni kubwa

sana na yote hayo yapo kutokana na uongozi bora, uongozi mzuri wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna mambo ambayo lazima tuyaseme. Kuwepo kwa miundombinu ya reli, ndege na meli ni moja ya mambo ambayo yataweza kuchangia kwa kiasi kikubwa sana katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, la pili, kwanza tufahamu wazi kwamba kutakuwa kuna zile fursa za kijamii kwa sababu kila kitu kitakuwa kimerahisishwa kwa namna yake. Kitu ambacho naiomba Serikali yangu Tukufu, haya mambo yote huko nyuma tulikuwa nayo, mashirika ya reli tulikuwa nayo, ndege tulikuwa nazo na mambo mengine mengi tulikuwa nayo, lakini kuna vitu vinaonekana kwamba labda pengine Watanzania tunakosea, tunakuwa na mambo mazuri sana, lakini hatimaye utaona kitu kimoja kimoja kinaanza kudondoka.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali yangu Tukufu, kuna mambo matatu ambayo ni mambo muhimu sana kwa kile ambacho tunakifanya. Kitu cha mwanzo tuwe na uongozi bora katika zile taasisi ambazo zinasimamia vitu vyetu vyote kama vile reli na ndege; ni lazima tuwe na uongozi ulio bora.

Mheshimiwa Spika, la pili ni *operation;* namna ya kuziendesha zile, maana yake tuwe na watu ambao wanaweza kusimamia katika hali nzuri sana. La tatu, linaloweza kugonga watu wote ni suala la *maintenance*. Tutakuwa na treni nzuri sana, tutakuwa na ndege nzuri sana, tutakuwa na mitambo mizuri sana lakini bila *maintenance* za kila wakati maana yake baada ya miaka mitano ama 10 tunaweza kuja kujihesabu tunarudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, siku zote hizo tumezungumzia suala la bajeti zetu hizi hapa na tunapitisha mafungu mengi sana. Kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa, maana tunapopitisha yale mafungu tunapitisha kwa pamoja, lakini wakati mwingine inakuwa ni vichekesho sana, Waheshimiwa Wabunge sote tunakuwepo hapa wakati Mafungu yanapitishwa sote tunasema ndiyo, lakini unakuja

baadaye kunakuwa na baadhi, wanakwenda kulaani huko nje kwamba lile fungu gani au kwamba kumefanyika kitu gani.

Mheshimiwa Spika, inavyotakiwa sisi viongozi ambao tupo hapa Waheshimiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunatakiwa tumsaidie Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kila kitu ambacho tunakipitisha hapa. Kama tunakipitisha hapa katika bajeti zetu maana yake tunakipitisha kwa umoja wetu. Kama tunakitenda ndani ya Bunge letu hili, tunakitenda kwa umoja wetu. Maana yake ni kwamba sisi tunakuwa kama ni wawakilishi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema kwamba, kama nilivyosema awali kwamba naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda ajiandae.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim wa ruzuku ya uhai, lakini na afya ambayo imetuwezesha kukutana leo kujadili bajeti hii ya Wizara ya Uchukuzi. Nami nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa ambao umefanyika katika mashirika mbalimbali yaliyo chini ya Wizara hii, lakini leo nitajikita zaidi katika suala la reli. Nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu Profesa Godius Kiharara na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Ally Possi na wafanyakazi wote kwa bajeti nzuri ambayo wametuletea.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika reli ni uwekezaji muhimu sana na uwekezaji ambao utadumu kwa muda mrefu, tukitilia maanani kwamba reli hii tunayoitumia sasa ilijengwa na Wajerumani takribani miaka zaidi ya 120 iliyopita na mpaka leo inafanya kazi. Kwa

hiyo tunawekeza kwa kizazi cha leo, lakini tunawekeza kwa miaka 100 mingine ijayo ambayo naamini wengi wetu katika chumba hiki tutakuwa ni sehemu ya makerubi na maserafi tukimwimbia Mungu bila mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze sana uwekezaji katika *SGR* ambao utatuunganisha na Burundi, *DRC*, Rwanda na Uganda, lakini pia kufufua reli hii ya *MGR* ambayo ni muhimu na sasa kuanza kukarabati reli ya *TAZARA*. Kwenye reli ya *TAZARA* ni muhimu sana tuikarabati ili tuweze kuiunganisha na reli ya Benguela inayotoka Zambia Kapiri Mposhi kwenda Lobito.

Mheshimiwa Spika, huu ni wakati wa kuanza kujiandaa kuunganisha Bahari ya *Atlantic* na Bahari ya Hindi kupitia Bandari ya Dar es Salaam na Bandari ya Lobito. Ningependa tuwe na mkakati wa kuifanya Bandari ya Lobito isiwe bandari shindani bali iwe bandari ya kusaidiana na Dar es Salaam ya kutoa mizigo Latin America na Caribbean kuja Afrika kwenda Asia na kwenda China, kwa sababu yapo madini kule Latin America, yapo madini kama vile *brockite* yanakwenda China leo. Kwa hiyo kuwe na mkakati wa kuigeuza Lobito kuwa bandari rafiki na si bandari shindani. Tuanze kuwekeza katika *TAZARA* na tayari wenzetu wanafufua reli ya Benguela inayokwenda Lobito.

Mheshimiwa Spika, reli ni kitu muhimu sana na niipongeze sana Serikali kwa kuwekeza katika kufufua reli ya *MGR*, yaani hii reli ambayo tunaitumia sasa iliyojengwa na Wajerumani. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri aje na maelezo ya kutosha kwamba kuna mikakati gani iliyopo ya kufufua yale mabwawa matano ambayo Wajerumani waliyajenga kati ya Kilosa na Gulwe ili kuilinda reli ya kati; Bwawa la Kidete, Bwawa la Kimagai, Bwawa la Msagali, Bwawa la Kibibo na Bwawa la Ikowa. Najua Bwawa la Msagali limeanza kujengwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, lakini tumeambiwa Bwawa la Kidete na mabwawa mengine Wizara ya Uchukuzi, kwa maana ya Shirika la Reli, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maji watashirikiana.

Mheshimiwa Spika, naomba tuanze haraka na Bwawa la Kidete kwa sababu Bwawa la Kidete si tu kwamba linatunza reli lakini ndilo linalozuia mafuriko katika Mji wa Kilosa; na liendane na ujenzi wa kingo za Mto Mkondoa eneo la Magomeni na eneo la Kisaki katika Mji wa Kilosa. Hii itatusaidia pia katika kilimo na uvuvi. Pale Kidete lile bwawa zamani lilikuwa lina samaki wengi sana ambao walilisha Miji ya Kilosa, Kimamba na Morogoro. Wakati huo tukiwa wadogo palikuwa na treni ambayo sijui kwa nini ilipewa jina hilo, ilikuwa inatoka Dodoma mpaka Morogoro iliitwa Malaya. Kazi yake moja ilikuwa ni kubeba mizigo hiyo ya samaki kutoka Kidete.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni la reli kati ya Kilosa na Kidatu. Fedha zimetengwa kwa ajili ya kukarabati na kufufua reli ya Kilosa na Kidatu. Hapa nina maombi mawili. Ombi la kwanza tufikirie hiki kipande cha Kilosa – Kidatu na chenyewe kiwe cha *cape gauge* ili treni ikitoka Kilosa isilazimike kubadili mzigo Kidatu na badala yake iende moja kwa moja mpaka Mlimba na Mlimba iweze kwenda mpaka Kapili Mposhi na Kapiri Mposhi mpaka Durban na Durban mpaka Walvis Bay. Kwa hiyo ningependekeza tuone uwezekano wa kipande hicho kijengwe kwa *cape gauge* badala ya *meter gauge*. Tujenge pia barabara ya lami kati ya Stesheni ya sasa ya Kilosa ya *SGR* pale Kondoa na Stesheni ya Kilosa ya *MGR* ili iwe rahisi kwa mizigo na watu kutoka kwenye stesheni ya *SGR* Kondoa na kuja kwenye stesheni ya *MGR* pale eneo la Uhindini.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho ningependa tufikirie sasa ni kwamba, reli itakayojengwa kwenda Mchuchuma isiishie Mchuchuma, iongezwe kutoka Mchuchuma kwenda Kidatu kwenda Kilosa; ndivyo hivyo Wajerumani walivyokuwa wamepanga kuijenga reli hiyo walipotaka kuliendeleza eneo la Ruhuhu *Valley* kuwa ni eneo la ujenzi wa viwanda. Wajerumani walikuwa wameamua eneo la Ruhuhu kuja Kidatu kuja Kilosa lifanane na Ruhr Valley ya kule Ujerumani ambayo ina Miji ya Dortmund, Essen, Dusseldorf, Bornholm na Kolon; wajenge viwanda. Kwa hiyo reli iongezwe iende mpaka Kidatu na Kilosa ili mzigo mkubwa huo wa madini ya chuma, makaa ya mawe, *vanadium, titanium, aluminium* na *rare earth* iweke kutoka

huko na kwenda Kahama kwenye *refinery* ya Tembo ili tuweze kuyeyusha na kupata *metal*. Kwa hiyo ningeomba hilo nalo lifikiriwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hilo hilo suala la hapo, Wajerumani walikuwa wamepanga bandari yao kubwa iwe Bandari ya Kilwa. Tuanze kufikiria kuifanya Bandari ya Kilwa kuwa *trans-shipment port* kama iliyo Salalah kule Oman. Tuanze kufikiria kujenga reli kutoka Kilwa iungane na Kidatu, iungane na Kilosa kutoka Kilwa iende Mbamba Bay; na wenyewe Wajerumani Mbamba Bay waliita Sphinx Hafen ili bandari hizo zifane.

Mheshimiwa Spika, katika suala hilo hilo la reli, ningependekeza pia tujenge reli kutoka Dumila – Dakawa kuja kuunganisha na stesheni ya Mkata ili kuunganisha viwanda vya sukari vya Kilombero, Kilosa na Mtibwa. Tuigeuze reli hii; kama ilivyosemwa; iweze kubeba mizigo ya ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda hautoshi, naiomba Wizara, Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu Profesa Kahyarara waje Kilosa tuone jinsi ya kufanya Kilosa kuwa ni mojawapo ya maeneo ya kuzalisha vitunguu na kuzalisha mbogamboga wanazoziona barabarani Dumila ili sasa treni iweze kuchukua mizigo hiyo ya nyanya, vitunguu na mbogamboga kwa ajili ya matumizi ya ndani, lakini pia kwa ajili ya matumizi ya nje.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la *Air* Tanzania na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Sote tunafahamu Shirika la Ndege la Afrika Mashariki lilivunjika tarehe 5 Februari, 1977 katika hali iliyokuwa ngumu sana na tukafanikiwa *pilot* mmoja kurusha ndege moja tu ambayo ndiyo ilikuja na baada ya hapo tukawa hatuna ndege. Hata hivyo, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere tarehe 31 Machi, 1977 akisaidiwa na Waziri wake aliyemwamini sana Mheshimiwa Amir Habib Jamal walianzisha Shirika la *Air Tanzania Corporation*., likawa na ndege mbili za boeing 737 Kilimanjaro na Serengeti, likawa na ndege nne za *Fokker Friendship* na ndege mbili za *twin water*.

Mheshimiwa Spika, shirika letu la ndege limepita katika vipindi mbalimbali, lakini sasa limefufuka tena na limeanza kukua. Tayari muamana, kwa maana ya *reliability* ya huduma za reli zimeongezeka, na hii imeweza kujenga itibari *(trust)* ya Shirika la Ndege.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu ni mwaka wa 60 tangu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iundwe, mwaka huu ni mwaka wa 25 tangu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipofariki dunia ingawa amegoma kufa. Napendekeza kwa Serikali kwamba ndege yetu kubwa ya *Dreamliner* ambayo haijaja tuipe jina la Julius Nyerere kazi iendelee kwa kuuenzi Muungano wa miaka 60, lakini pia kumpa heshima Baba wa Taifa ambaye miaka 25 iliyopita Mwenyezi Mungu alimchukua, lakini yu hai.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo hatutakuwa wa kwanza. Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini ndege yao kubwa kuliko zote ya *Air Bus A340–600* mwaka 2003 Mandela alipofikisha miaka 85 waliipa jina la Nelson Mandela. Kwa hiyo ndege hii ipewe jina la Julius Nyerere kazi iendelee miaka 60 ya Muungano ili kumuenzi Baba wa Taifa. Kwa namna hiyo tutakuwa tumeungana na wenzetu ambao pia wamempa Baba wa Taifa heshima kubwa, mojawapo ikiwa ni Nchi ya Guinea.

Mheshimiwa Spika, Nchi ya Guinea imekipa chuo kikuu katika mji wa Kankan Guinea jina la Julius Nyerere University; na sisi tuna vyuo viwili vya Julius Nyerere, tuna chuo cha Julius Nyerere Guinea lakini sasa tuwe na ndege ambayo itaruka katika anga ikibeba jina la mtu huyu ambaye miaka 60 aliunda Taifa ambalo leo ni Taifa na si mkusanyiko wa makabila na leo ni nchi yenye heshima, nchi inayojivunia na imeweza kumtoa Mheshimiwa Rais wa kwanza Mwanamke katika nchi hii. Katika utawala huu na uongozi wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ndege hiyo tuipe jina la Julius Nyerere Kazi iendelee.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja, lakini niombe kiwanja cha ndege katika mji wa Kilosa. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu ndani ya Bunge lako hili Tukufu. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Mama, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya kwenye Taifa letu. Pia nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa niaba ya wananchi ya Kata ya Mavanga, Mheshimiwa Rais aliona taarifa mtandaoni ya mtoto ambaye alikuwa amevimba sana tumbo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa alimchukua alimpeleka hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa ajili ya matibabu, akalipia gharama zote. Bahati mbaya mtoto yule alifariki na aliweza kugharamia kusafirisha mwili na mazishi. Napenda kutumia nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Ludewa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Kitendo alichokifanya kimetoa somo kubwa sana kwa Viongozi wa Ludewa na Viongozi wa Mkoa wa Njombe, kwa hiyo nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri na kwa hotuba nzuri. Nilijua kwamba Wizara imegawanywa kwa hiyo hotuba yake itakuwa na kurasa chache lakini cha ajabu nimeona ana kurasa 260. Hii ni ishara kwamba Wizara hii ni nyeti sana.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake ukisoma ukurasa wa 10 Mheshimiwa Waziri amelieleza Bunge lako, naomba kumnukuu, kwamba; "Sekta hii ni ya tatu kwa kuchangia fedha za kigeni kupitia mauzo ya huduma kwa mujibu wa taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)*. Katika kipindi cha kuishia mwezi Februari, 2024, Sekta ya Uchukuzi ilichangia Dola za Marekani bilioni 2.4 ya fedha za kigeni ikiwa nyuma ya mauzo ya dhahabu na biashara ya utalii. Kwa hiyo hii inaashiria kwamba Wizara hii ni Wizara nyeti sana." Kwa hiyo kwa kusoma hii na kutokana na umuhimu wa Wizara hii natamka kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, niende sasa kule jimboni kwangu. Nina kata nane ambazo zimezungukwa na Ziwa Nyasa, kuna Bandari pale Lumbila, Kilondo inaitwa Ifungu, Lupingu, Nsisi lakini vile vile kuna Bandari ya Manda na Lupingu.

Mheshimiwa Spika, meli hii ya *MV* Mbeya II inapokuwa inasafiri ikiwashusha wananchi wa pale Ifungu, wanatumia muda mrefu sana kufika Kijiji cha Nsele. Lakini vile vile ikishusha wananchi wa pale kituo cha Kata ya Lifuma, Kijiji cha Nsisi wanatumia muda mrefu, zaidi ya masaa mawili kutembea kufika makwao. Kwa hiyo kufuatia hili, nilipokwenda kwenye ziara wananchi wale waliomba sana Serikali iweze kutuma wataalam wakaangalie eneo lile la Nsele. Ni kijiji ambacho kina wananchi wengi na eneo lile la Lifuma ili waone kama wanaweza kuweka kituo cha kushusha abiria maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, vile vile sasa hivi tumeambiwa kwamba meli haifanyi safari zake kwa sababu ziwa limejaa sana. Yale maeneo ya kupita abiria pale Itungi na pale Kiwira hawawezi kusogea mpaka pale kuikuta meli ilipo. Kwa hiyo ningependa sana kuiomba Serikali iweze kufanya uchunguzi eneo la Matema *Beach* kwa sababu lile eneo lipo juu, ili ikiwezekana wakati wa dharura abiria na mizigo waweze kutumia eneo lile la Matema. Kwa sababu uwepo wa meli hii kwenye Ziwa Nyasa ulikuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa wananchi. Nina takwimu za mwaka 2022/2023, meli hii iliweza kusafirisha kwenye Ziwa Nyasa wananchi elfu 72.9, lakini vile vile mizigo tani 12,000 ziliweza kusafiri. Kwa hiyo hii ni ishara kwamba meli inapokuwa haipo wananchi wanapata adha kubwa sana. Niombe sana hilo liweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kuna ile meli ambayo ilikuwa inaitwa *MV Songea*, ilikuwa na uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 43 za mizigo. Meli ile inahitaji fedha chache sana ili iweze kukarabatiwa, kuwekwa zile mashine mpya lakini *furniture* mle ndani na kupaka rangi tu lile jumba lake. Meli hii inaweza ikasaidia kama mbadala wa ile meli ya MV Mbeya II. Zikiwa zinapishana tutaongeza huduma kwenye Ziwa Nyasa. Kwa hiyo ningeomba sana Wizara hii waweze kuiangalia ile meli kama wanaweza wakaikarabati iweze kusaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, aliweza kuwatuma wataalam kutoka *TPA* kwenda kukagua Bandari ya Manda na ikaonekana lile jengo la abiria, gati la kushushia mizigo na abiria pamoja na ofisi vinatakiwa vijengwe upya. Kwa hiyo ningeomba sana Wizara iweze kuharakisha. Katika hili watume wataalam pale Manda ili waweze kufanya uthamini ili wananchi ambao wanaondoka wajue na walipwe haki yao waweze kuachia eneo la bandari.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niende sasa kwenye eneo la reli. Ukanda ule wa Liganga na Mchuchuma una madini ambayo *logistics* za kuyatoa pale kuyapeleka bandarini ni changamoto kubwa kidogo. Tuliahidiwa kuwa kuna reli itajengwa kutoka Mtwara hadi *Bamba Bay* tawi Mchuchuma na Liganga. Nishukuru Serikali imeshatoa fedha na mkandarasi yuko pale *Bamba Bay* ameshaanza kujenga bandari. Tulikwenda pale na Mheshimiwa Naibu Waziri, tulishuhudia kazi inaendelea. Kwa hiyo, tunaomba na hii reli iweze kukamilika mapema ili sasa ule mzigo wa chuma na makaa ya mawe iwe rahisi kuweza kusafirisha na Mheshimiwa Profesa Kabudi amesema hapa nimemsikiliza kwa makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika ile reli ya *TAZARA* kuanzia pale Makambako waone uwezekano wa kulisogeza tawi liende kule Mchuchuma na Liganga na ikiwezekana iweze kuunganishwa hadi huku Ihumwa Dodoma, tuiangalie nchi hii kwa miaka mia moja au zaidi ijayo. Kwa hiyo, watumwe wataalam waangalie ni wapi reli hii inaweza ikaunganishwa kutoka pale Makambako mpaka Liganga na Mchuchuma, lakini vilevile ikiwezekana ije iunganishwe na *SGR* ili mizigo ya kule iweze kwenda katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kusafirishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru pia nimeona Uwanja wa Ndege wa Njombe umeingia kwenye bajeti.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao na Mheshimiwa Mohamed Said Issa ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na moja kwa moja namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutupa afya na uzima vinavyotuwezesha kuendelea kuwatumikia wananchi waliotuchagua.

Mheshimiwa Spika, nataka kuanza kwa kusema kwamba kuna kazi kubwa sana imefanywa na Wizara ya Uchukuzi ambayo sisi wote katika maeneo mbalimbali hapa nchini tumeiona na kwa kweli tunawapongeza sana kama Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kazi hiyo. Tunapozungumza habari ya Reli ya *SGR,* tunapozungumza habari ya bandari zetu, tunapozungumza habari ya viwanja vya ndege kikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Kigoma ambacho kinaendelea kukarabatiwa na kujengwa baadhi ya majengo, kazi inaendelea. Zaidi ya yote nishukuru sana kwa Wizara hii kutusaidia katika Chuo cha Hali ya Hewa wamefanya ukarabati mkubwa, wamekifanya kiwe cha kisasa zaidi, hongera sana na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kabla ya kusema yale ninayoyakusudia nataka Wizara iyatazame, ninukuu maneno ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyoyatoa mwaka 1976 wakati ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliagiza mchele kutoka nje. Mwalimu akaulizwa na waandishi wa habari, Mwalimu naona mmeagiza chakula, mmeagiza mchele ina maana Tanzania ina upungufu wa chakula? Mwalimu akasema hapana hatuna upungufu wa chakula bali tuna upungufu wa mchele kwa sababu wapo Watanzania hasa wakiwemo Wazaramo ambao kama hawakula wali hawajisikii kama wamekula, lakini wangetaka kula viazi,

wangetaka kula mihogo wangetaka vyakula tunavyo vingi ila tuna upungufu wa mchele.

Mheshimiwa Spika, ninachokusudia ni nini? Ni kwamba ninapozungumza mambo ambayo nataka Wizara iyatazame sikusudii kusema kwamba Wizara hii haijafanya mambo mengi na makubwa isipokuwa hayo ninayoyakusudia yana upungufu hayajafanyika kwa kiwango kinachotakiwa. Kwa hiyo, wamefanya kazi kubwa, lakini meli katika Ziwa Tanganyika bado ni msalaba wanaoendelea kuubeba. Ziwa kubwa kama Ziwa Tanganyika linalotuunganisha na Nchi ya Zambia, *DRC* Congo na Burundi mpaka sasa halina meli hata moja inayomilikiwa na Wakala wa Meli inayofanya kazi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Nchi ya *DRC* Congo, takwimu zilizotolewa na Baraza la Biashara la Jumuiya ya Afrika Mashariki inaonesha kwamba karibu 85% ya vitu vyote vinavyotumika katika nchi hiyo wana-*export* kutoka nje, lakini nchi ya kwanza inayofanya biashara kubwa na Congo ni China, inayofuata ni Afrika ya Kusini, inayofuata ni Zambia, inayofuata ni Kenya. Sisi ambao tuna mpaka na *DRC* Congo ni nchi ya saba kwa kufanya biashara na *DRC,* hii kwa kweli tumejipotezea nafasi kubwa ya kuinua nchi yetu kiuchumi kwa kukosa meli kwenye Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, najua Mheshimiwa Waziri tumekutana katika nyakati mbalimbali pamoja na Wakala wa Meli, wametupa maelezo hatua mnazokwenda nazo…

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Aida Khenani.

**TAARIFA**

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba pamoja na kwamba hatuna meli mpya hata

moja, hata zilizokuwa zinahitaji ukarabati sasa ni miaka nane hazijakarabatiwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa kwa mikono miwili na huko ndiko ninakoelekea kwamba wakati wanahangaika na meli ya mizigo na meli kubwa ya kisasa ya abiria 600, hebu waturudishie Meli ya *MV* Lihemba na Mwongozo kwa haraka. Najua hatua wanazozichukua kwa kuwa wametupitisha kwenye hatua wanazozichukua na tunajua wapi walipokwama. Leo sina mpango wa kushika shilingi ya Waziri kwa sababu najua wapi alipokwama na najua hatua anazozichukua, namwomba aongeze kasi katika hatua hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumze ni ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaotaka kupisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege Kigoma. Jambo hili nililizungumza kwenye Wizara ya Ardhi na sasa nalizungumza tena kwenye Wizara husika. Kwa kweli, jambo hili linatuletea mgogoro mkubwa sana, kama mnavyofahamu kipindi hiki kina mvua nyingi, wananchi wameharibikiwa maeneo yao lakini wanashindwa kuyaendeleza, hata choo kimevunjika, mtu anafikiria najenga choo inawezekana kesho nitaondolewa kwa sababu tayari *evaluation* ilikwishafanyika na inajulikana nitalipwa kiasi gani, nikianza tena kuingiza pesa huku, pesa zangu zitakuwa zinapotea.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, ni mtu makini na sisi tukisikia huko kwetu Profesa tunajua Profesa ndiye mbobezi wa mambo yote. Sasa nimwombe Profesa na bahati nzuri amepewa kijana chapakazi kumsaidia kufanya kazi, Naibu Waziri wake hebu wasaidie kuhakikisha hii kero ambayo iko kwa wananchi wetu inaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba leo sikusudii kusema mambo mengi kwenye Wizara hii, najua wapi walipokwama kwa Meli ya Lihemba na Mwongozo, itakapofika bajeti

ya Wizara ya Fedha nitasema mengi na hapo nafikiri patanisaidia zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Said Issa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Uchukuzi. Ni kwamba Wizara ya Uchukuzi na Ujenzi, wakati mwaka jana tunaleta ushauri kwamba igawanywe tulikuwa tuna maana kubwa sana na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kukubali mawazo ya Waheshimiwa Wabunge na kuigawa Wizara hii kuwa katika Wizara mbili ili kupunguza mzigo katika Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Wizara hii imebeba sehemu nyingi sana, imebeba idara nyingi sana za kiuwekezaji. Kuna uwekezaji, wafanyabiashara wanaosafirisha mizigo yao kwa njia ya magari, kwa njia ya bandari lakini kwa njia ya anga na kote huko ni sehemu kubwa sana kwa ajili ya kutengeneza uchumi wa nchi yetu. Sasa Mheshimiwa Rais baada ya kuigawa Wizara hii akatoa majukumu ya kazi ambazo Wizara imepangiwa kuzifanya. Nataka kuzungumza katika maeneo matatu; sehemu ya usafirishaji kwa barabara na sehemu ya usafirishaji kwa njia ya meli na ujenzi wa bandari lakini usafiri kwa ajili ya njia ya anga.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba uwanja wetu wa Dodoma sasa hivi pamoja na kuwa mdogo lakini bado hatujaufanya kuwa *busy* kwa ajili ya biashara. Kwa mfano, mpaka sasa hivi tulikuwa tuna ndege ya kutokea Dodoma kwenda Mwanza, hii ndege ikawa imeondolewa wakati ilikuwa inapata abiria. Na ni kama vile kuwazuia watu wa kanda ya ziwa wasikutane na wenzao watu wa Dodoma na kufanya shughuli zao za Dodoma kwa haraka. Waheshimiwa Wabunge, wote

wa kanda ya Ziwa tumelalamikia jambo hili, lakini Serikali haitaki kusikiliza kilio cha Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wanalalamika, watumishi wa Serikali wanalalamika, shughuli nyingi za Serikali ziko hapa, lakini ili uweze kufike Dodoma kwa haraka unatakiwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, unatakiwa katika Ofisi ya Waziri wa Fedha, unatakiwa Ofisi, Ofisi zote lazima uje Dodoma kutokea kanda ya ziwa. Sehemu ya karibu kwa anayetoka Simiyu, anayetoka Shinyanga, anayetoka Mara, anayetoka Kagera akitaka haraka aje Mwanza achukue ndege anawahi kufika Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri leo hii kama hatakuja na majibu ya ndege ya Kwenda Mwanza anairudisha lini, alitueleza kwamba tukipata ndege nyingine tutapata ndege ya Mwanza. Ndege imeshakuja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kapokea ndege, Wanamwanza tumeona hilo, sasa kama hutakuwa na majibu leo, nitashika shilingi japo ni ndugu yangu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la ndege kutokea Dodoma kwenda Zanzibar, Dodoma kwenda Arusha, Dodoma kwenda Mbeya, Dodoma kwenda Kigoma, kwa nini tunataka kuuvunja huu mji? Utakuwa lini Mji wa Dodoma? Leo mpaka mabasi yanatembea usiku, lakini sisi watu wa anga tunayo ndege yetu inayotokea Dar es Salaam - Dodoma. Wizara imetoa kipaumbele kwa ajili ya Dar es Salaam - Dodoma tu, mikoa mingine haina hadhi ya kupata ndege, hili jambo sio sawasawa, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la usafiri wa barabara, kumekuwa kuna matatizo makubwa sana hasa katika mizani zetu. Najua hii mizani iko Wizara ya Ujenzi na Waziri ana-*deal* na uchukuzi, lakini ni kwamba, lazima akae na Waziri mwenziwe kuhusiana na suala la mizani. Mizani imekuwa ni kero kubwa kwa madereva, mizani imekuwa ni kero kubwa kwa matajiri. Kwa mfano, gari linapakia lita 42,000 ya *petrol* au lita 37,000 ya *diesel* unaambiwa gari likifika Vigwaza limezidi kilo 50. Hao wa Congo watapitaje Bandari ya Dar es Salaam? Kwa hiyo, atakwenda anasumbuliwa kwa kilo 50 mpaka

anafika Tunduma, atakwenda anasumbuliwa analipa faini mpaka anafika Rusumo, mpaka anafika Kabanga au anafika Mtukura.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo lazima wakae waangalie na anaambiwa dereva ayapange mafuta vizuri mzigo umekaa vibaya, umezidi mbele kilo 120. Mzigo umefungwa *seal* na watu wa *TRA,* hawaoni kama wanasumbua hawa watu majirani zetu wanaotumia barabara hizi? Watumiaji wa ndani pia imekuwa ni kero, tunamwomba Mheshimiwa Waziri aje atupe majibu ya Serikali kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, suala la *Port* ya Kasanga, *Kasanga Port* kwenda Mlilo, *Kasanga Port* kwenda Kalemie, Kigoma kwenda Kalemie, Kigoma kwenda Uvira, Kigoma kwenda Bujumbura wanakwama wapi? Kwa mfano, kutokea Dar es Salaam mpaka Lubumbashi ni kilometa 1,870 na ukitoka Dar es Salaam mpaka *Kasanga Port* ni kilometa 1,200, kutokea *Kasanga Port* kwenda Lubumbashi kilometa 218, hawaoni kama sisi tunapoteza uchumi mkubwa?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kilumbe Nge'nda amezungumza hapa kuhusiana na suala la biashara ya Congo, kutokea Kigoma kwenda Bujumbura kilometa 300, Kigoma kwenda Uvira kilometa 300, Kigoma kwenda Kalemie kilometa 250. Hawaoni kama uchumi wa Congo tunaupoteza? Huu uwekezaji wa bandari utakuwa una manufaa gani kwa nchi yetu? Congo kuna mizigo ya mbao, Congo kuna mizigo ya madini, Congo wanahitaji chakula kutoka Tanzania, sisi tutafanyaje biashara zetu?

Mheshimiwa Spika, tunazalisha chakula Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Katavi na Kigoma, jamani Congo kuna biashara kubwa, sisi tunaofanya biashara na Congo ndio tunajua yaliyoko Congo. Congo wanataka mboga, dagaa na samaki lakini tutasafirishaje? Uwekezaji wa hizi bandari zote zilizojengwa kule, labda Mheshimiwa Waziri hajafanya ziara kwenye Ziwa Tanganyika aone uwekezaji uliowekezwa kule bandarini ni wa gharama kubwa hakuna mfano wake.

Mheshimiwa Spika, nakupa mfano mmoja kwa Bandari ya Mwanza, kutokea Mwanza kwenda *Port Bell* Kampala, Mwanza-Jinja, Mwanza – Kisumu, bandari ile tunavyozungumza haina hata *crane,* , hili jambo halikubaliki. Tumeenda pale na Mheshimiwa Waziri Mkuu amekwenda kuona kwanza hata hii meli ya Mwanza, MV Mwanza, Hapa Kazi tu haina gati. Nimekwenda pale na Naibu Waziri wa Uchukuzi tulikuwa naye hakuna gati pale Mwanza. Meli inatakiwa ikabidhiwe mwezi huu, je, itatumia gati lipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bandari yetu ya Mwanza tunaonewa, Bandari ile ya Mwanza hailingani na hadhi ya Mwanza. Tunaomba sana Waziri akija hapa atupe majibu lini ataboresha Bandari ya Mwanza. Hizi Bandari zetu zote zinatakiwa kufanya kazi, tunahitaji kutengeneza uchumi wa nchi hii kupitia kanda ya ziwa na sisi kanda ya ziwa ni wahanga tunapelekewa treni ya mwendokasi. Kama hatujajiandaa kutengeneza bandari, hii treni ya mwendokasi itafanya kazi vipi? Pia tuna meli ambayo mikataba yake ilisainiwa kwa ajili ya kubeba makontena ya kusafirisha kwenda Kisumu, Jinja na *Port Bell* Kampala, hatujui na yenyewe imekwama wapi. Sasa tunajua kwamba mipango mingi ya Serikali ni mizuri, lakini hawa wawekezaji wetu pia tunataka tujue ni namna gani wataweza kuboresha bandari yetu ya Mwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nataka pia nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kuhusu suala la *station* ya Fella. *Station* yetu ya Fella mpaka sasa hivi ni kwamba inatengenezwa, lakini eneo lile pale la Fella kuna hekta mia tano. Hekta mia tano zimewekwa pale, uwekezaji ambao ulikuwa unatakiwa pale ni zaidi ya dola bilioni tano kwa ajili ya uwekezaji wa Bandari ya Fella, lakini hatuoni kazi inayofanyika pale na sisi tunategemea itafanya kazi kwa ajili ya kupokea mizigo ya Mara, Kagera na Mwanza, mizigo inayokwenda katika Nchi nyingine za Kenya na Uganda. Kwa hali hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri, naona bado anaongea huko na mimi hapa namweleza suala la Mwanza sasa inakuwa haifai namna hii, inaonekana kama labda hanisikilizi sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, naam.

**SPIKA:** Mbunge ukiwa unachangia huongei na Waziri, unazungumza na Spika. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini Waziri anatakiwa anisikilize.

**SPIKA:** Ukiwa unaongea naye moja kwa moja hasikii, ukiongea na mimi ndio anasikia na kanuni zinakutaka hivyo, ndio maana unasema Mheshimiwa Spika. Ukimtaja Waziri mimi nahesabu kwamba umeteleza kidogo. Kwa hiyo, wewe ongea na Spika, yeye anasikia yote, ukitaja Spika tu yeye anasikia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, naongea na Spika, lakini suala la Bandari yetu ya Mwanza... *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam, sekunde thelathini malizia.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuboreshea uwanja wetu wa Mwanza, huu uwanja wa Mwanza ulikuwa umesahaulika sana, kwa hiyo tunaenda kupata *International Airport* kutoka Mwanza.

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Nampongeza Pia Mtendaji Mkuu wa Viwanja vya Ndege Wakili Musa, Mwenyezi Mungu amjalie sana kwa kukubali kutengeneza Uwanja wetu wa Mwanza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mwenyezi Mungu amjalie, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mohamed Said Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Wizara hii ya Uchukuzi. Kwanza leo nimefurahi upo hapo kwa sababu naamini dakika zangu nitazipata zote kwa sababu wewe ni mlezi wa wana kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukipongeza Chama changu cha ACT-Wazalendo kwa kutimiza miaka 10 toka kuanzishwa, lakini kutimiza miaka kumi bila migogoro, lakini kuwa ni chama ambacho kinakua kwa kasi sana, ni chama ambacho kitakuja kuiondoa CCM madarakani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia sasa. Kwanza naanza na suala la uwekezaji wa kampuni binafsi katika Bandari yetu ya Dar es Salaam. Ni jambo jema sana…

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohammed subiri kidogo, kuna Taarifa. Nani anasema Taarifa?

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Taletale.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale.

**TAARIFA**

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, nampa Taarifa muongeaji, inawezekana akawa anaota, aamke. Hakuna chama kinachoweza kukitoa Chama Cha Mapinduzi madarakani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed, umeipokea Taarifa hiyo? *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa yake siipokei kwa sababu, hata yeye aliota kuja kuwa Mbunge na leo ni Mbunge kwa hiyo, chama nacho ni hivyo hivyo. Siipokei. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naendelea na mchango wangu, tena sijui mnapata tabu ya nini, mimi nawapongeza. Ni *very rare* kumkuta mpinzani anapongeza, lakini kwa vile nimeona kuna jambo zuri, nawapongeza.

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala la uwekezaji wa kampuni binafsi katika Bandari yetu kutoka Gati Na.1 mpaka Na.7 pale. Kwa kweli, jambo hili nimekuwa nalifuatilia kwa ukaribu nimeona kwamba, hii kampuni ambayo imepewa, naamini itakuja kuiokoa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati tunaleta mijadala ya kumweka *DP World* Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema kuwa, hii inakuja kuchangia 62% ya bajeti yetu. Sasa Watanzania tunataka nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona hapa Mwaka 2023 makasha 600,000 ndiyo ambayo yalikuwa yanapata huduma, lakini sasa hivi yamefikia makasha 800,000. Ni jambo jema na ni jambo la kupongeza.

Mheshimiwa Spika, tuna imani kwamba, ikiingia kampuni binafsi haya mapato yatakuja kufikia kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, jambo hili ni jambo jema, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais ili awatumikie Watanzania. Pia, nasema kwamba, kwa sifa nilizoziona hawa *DP World* natamani wafike Zanzibar ili waende wakahudumie Bandari za Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naacha sehemu hiyo, nakuja kwenye mizigo inayotoka Zanzibar kuja Tanzania Bara. Jambo hili linawakwaza Wazanzibari ama wafanyabiashara wote kwenye upande wa *wharfage*. Utaratibu ambao una-*charge wharfage* kwenye mizigo inayotoka Zanzibar tunaona kwamba, siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru wenzetu wa *TRA* wao wana *differential tax.* Maana yake ni ukilipia *tax* kule Zanzibar ambako tunalipa *half of* ile *duty*, ukija hapa unalipa tofauti yake. Hata hivyo, hawa upande wa *wharfage* mpaka leo wameshindwa kuwasikiliza wafanyabiashara wanaotoka Zanzibar, kwa nini? Kwa hiyo naomba Wizara hii ilichukulie *serious* jambo hili ili hii *wharfage* ipungue kwa wale wenye mizigo inayotoka Zanzibar. Hata hivyo, pamoja na hayo sisi watu tunaotoka Zanzibar ambao tunaleta biashara zetu Tanzania Bara tuna jambo lingine ambalo linatusumbua, hili ni jambo la *storage*.

Mheshimiwa Spika, *storage* kwa mizigo inayotoka Zanzibar inapewa *24 hours*, lakini kwenye *charge* inakuwa *charged* sawasawa na ile *charge* iliyopo kwenye sheria. Jambo hili ni la kutungiwa Kanuni tu kwa sababu, hii mizigo ni *loose cargo.* Tunaweza tukapunguza *wharfage,* lakini wakati huo huo saa 24 hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza na Wabunge wengi humu, wakiwemo wa CCM, wamesema leo watanisaidia kushika shilingi kwa hiyo, nitashika shilingi, sawa eeh? Nitashika shilingi kwa hili kama Waziri hatatoa kauli ya kuwasaidia wafanyabiashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Hili jambo siyo sahihi. Haiwezekani watu wanaotoka nchi za jirani wanaopitisha hapa wanapewa siku saba, siku 14 hadi siku 21, halafu sisi watu wa Zanzibar, nchi ambayo tumeungana kwa Muungano wa mfano, leo tunaonekana mzigo ni saa 24 na *charge* ni ileile. Namwomba Mheshimiwa Waziri na timu yake waliangalie jambo hili ili kuwapa *comfort* Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea na suala la hizi meli za abiria. Sasa hivi meli za abiria zinafanya kazi nzuri sana hapa kwetu kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, lakini jambo la kushangaza na kusikitisha ni hizi meli zetu hazina afisa wa afya au daktari mle ndani. Tunabeba

abiria zaidi ya 600 kwa muda wa saa tatu, wanaingia wagonjwa na wazazi, lakini hakuna daktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja imenitokea ambapo alitokea mzazi anataka kujifungua na ndani ya boti hakuna daktari, bahati nzuri nilikuwa nimefuatana na ndugu ambaye ni daktari nikamwomba aende akasaidie. Kama asingekuwepo ingekuwaje? Kwa hiyo, jambo hili namwomba Waziri alichukue ili kila boti au meli ya abiria, kuwe na afisa afya.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la ma-*container* yetu ya biashara ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kipindi cha nyuma ma-*container* yalikuwa yanapitia Kenya yanakuja Zanzibar. Sasa hivi tumekuwa tunaleta ma-*container* hapa Dar es Salaam, tunafanya *transshipment* kule, ili kupeleka Zanzibar. Jambo la kushangaza ni kwa nchi nyingine *transshipment* gharama zinakuwa chini, lakini kwa sisi Wazanzibari gharama ziko juu, sijui ni kwa nini?

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, ukishafanya *assessment* ya yale ma-*container* kwamba, yanakwenda Zanzibar yanapangiwa kwenda *ICD* ili kuongezewa gharama na muda, mwisho wake unakutana na vikwazo vingi. Jambo hili siyo sahihi. Tunaiomba Wizara ya Uchukuzi kwa upande wa *TPA* waliangalie hilo na wasiyapangie haya ma-*container* yanayokwenda Zanzibar kuyapeleka *ICD*. Hii ni kero kwetu sisi na biashara zinakwama.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia pia suala la usafiri na upepo huu uliotokea juzi. Huu upepo umeleta janga kwa sisi wasafiri wa kutoka Tanga kwenda Pemba na pia, nataka kuwapa pole wananchi wangu wa Jimbo la Konde. Boti ambayo walikuwa wameweka mizigo yao ilipotea mpaka Nchi ya Kenya na ile mizigo ikapotea. Hivi sasa hawana mtaji tena. Kwa nini Serikali mpaka leo inashindwa kuunda meli ambayo itatoa usafiri wa uhakika kati ya Zanzibar na Tanzania Bara ili kuepusha jambo hili? Hili jambo kwa kweli, linatakiwa lizingatiwe. Kuna wakati fulani nilisema na wananchi wa Tanga walinipongeza sana, siyo jambo la Zanzibar peke yake, ni jambo la nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, naenda kwenye suala la kuwapa maisha rahisi wananchi, kwanza narudi kwenye *TASAC*. Hii *TASAC* nimeona kwenye Taarifa ya Kamati wamesema kwamba, haifanyi kazi vizuri, pia naunga mkono kwa sababu, hivi vyombo vyetu vilivyosajiliwa kati ya Bara na Zanzibar, kule Zanzibar kuna *ZDMA* na hapa kuna *TASAC*. Ukienda upande wa Zanzibar kuna sheria ambazo wanazisimamia vizuri, lakini ukija huku bara *TASAC* wamefanya ni chanzo cha uchumi, kila wakienda kwenye meli wanaikagua na kuitoza faini. Kwa nini wakati mwingine wasiweze tu kutoa maelekezo kwamba, boresha hiki na hiki? Wao wakishakagua wanatoza faini. Jambo hili siyo zuri. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri hizi faini zipungue, wawe wanatoa maelekezo. Wao ni walezi na wazazi, sisi tuko tayari kushirikiana na wao kufanya biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Shabiby, atafuatiwa na Mheshimiwa David Kihenzile na mtoa hoja ajiandae.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa eneo hili la Wizara yetu ya Uchukuzi. Kwanza na-*declare interest* kwamba, mimi ni mfanyabiashara wa usafirishaji kwa hiyo, leo nitajikita sana kwenye usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, nimeona Wabunge wengi wanazungumzia habari ya ndege, reli na viwanja vya ndege, nataka niseme kwamba, hivi vyote tunavyovizungumza kwa sasa tunaweza tukaviona kwa kuwa, tuko kwenye wakati mzuri na tunaenda vizuri, lakini vinaweza visichukue muda vikawa historia. Ndege zikawa *history*, treni zikawa *history* na kila kitu kikawa *history*. Nimewahi kuzungumza kwamba, Shirika la Ndege na Shirika la Reli yaachiwe uhuru yajiendeshe kibiashara, ili yaweze kujiendesha, lakini naona hilo halipo.

Mheshimiwa Spika, niko kwenye Kamati ya Miundombinu. Shirika la Reli kwenye upande wa abiria kwa miaka mitatu limepata hasara ya shilingi bilioni 25. Ukiangalia hiyo hasara yenyewe siyo kwamba, limeipata kwa sababu kuna uongozi mbaya, hapana, ni *simple* tu,

kuna mamlaka nyingine na Serikali yenyewe inachangia kuingilia uendeshaji wa shirika. Kwa hiyo, ukiangalia kwa mtazamo wa juu au wa nje unaweza ukajua labda waliomo mle siyo wafanyakazi wazuri, lakini ni kwa sababu ya uingiliaji, hawajipangii mambo yao, mambo mengine wanapangiwa kwa hiyo, mwisho wake wanapata hasara.

Mheshimiwa Spika, naona Wabunge wengi wanaongelea viwanja vya ndege. Morogoro kuna Mikumi sasa hivi wazungu wengi wanatua. Yule ndugu yangu Mussa Mbura, Mkurugenzi wa Viwanja vya Ndege, anafanya kazi nzuri sana. Ni kijana mchapakazi na anafanya kazi nzuri sana. Naomba aangalie pale Morogoro, sasa hivi wana-*assemble* ndege, hata Wabunge wakitaka ndege pale zinauzwa za watu wawili, watapakiana na mkewe, wanakaa huku nyuma, ziko pale *Airport* ya Morogoro. Kwa hiyo, tunaomba uwanja wa ndege, siyo tu wanapeleka Njombe, maana nimesikia Njombe unakwenda uwanja. Sasa jamani Morogoro hakuna uwanja, naomba uwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa najikita kwenye eneo la usafirishaji. Juzi bodaboda wamekuja kwangu wanalalamika, najua Mkurugenzi wa *LATRA* pamoja na wafanyakazi wengi ni wapya, lakini naomba wasichukue mawazo yaliyopita ya wale waliowatangulia. Wakichukua mawazo ya waliotangulia wanaleta mizozo, kazi ya *LATRA* ni kusimamia udhibiti wa nchi kavu. Tukizungumza hivyo ina maana tuna maguta, bodaboda, magari, treni na kila kitu.

Mheshimiwa Spika, leo hii nimeona pale Gairo *LATRA* wanachukua kwa bodaboda shilingi 17,000 kwa mwaka. Hata hivyo, ukiangalia hawawapangii *route, route* anatafuta mwenyewe, usiku kucha anahangaika yeye mwenyewe, wao wanachukua shilingi 17,000 tena pamoja na polisi, lakini ukiangalia hawawasaidii chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi ngoja niwaulize, wao wameshindwa kuiambia Serikali na kuitetea taasisi yao kwamba, leseni ya bodaboda ya kuendesha pikipiki ni shilingi 70,000 ili apate leseni ni lazima aende chuo akasome kwa shilingi 50,000 kwa hiyo, bodaboda alipe shilingi

110,000 ndiyo apate leseni? Halafu dereva wa basi na dereva wa lori naye hivyo hivyo, kwa hiyo, gari la miguu minne na ile pikipiki ya miguu miwili thamani ya leseni yake ni moja shilingi 70,000, inawezekana wapi hii? Hiki ni kitu ambacho hakiwezekani. Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko hapa, hivi ni kweli wanachukua shilingi 70,000 kwa dereva wa basi, dereva wa lori na kwenye bodaboda?

Mheshimiwa Spika, mpaka leo 95% ya madereva wa bodaboda hawana leseni, kwa hiyo, wanakosa mapato kwa sababu, wanatunga sheria na utaratibu ambao hautekelezeki. Bodaboda alitakiwa leseni yake isizidi shilingi 25,000 au shilingi 30,000. Ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge waliona hapa na wakaishauri Wizara ya Mambo ya Ndani ikakubali kwamba, faini ya gari ni shilingi 30,000, lakini faini ya bodaboda ni shilingi 10,000. Leo wanafurahia kumgonga bodaboda leseni shilingi 70,000 na aende akasome kwa shilingi 50,000, lakini wamesahau kwamba, wanakosa mapato, wanawapa tu shida polisi ya kuwakamata kila siku. 95% ya bodaboda hawana leseni, kwa hiyo, naomba walifikirie hilo, washushe, wasiweke sheria ambayo watu wataivunja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiweka kiasi kikubwa mtu anavunja sheria kwa sababu, hana hicho kiasi halafu unamwambia mpaka akasome. Nasema hapa kama kuna asilimia tano ya bodaboda wamesoma, wenye vyeti, najiuzulu Ubunge. Wanaenda wanawahonga wale wenye vyuo wanawapa shilingi 50,000 anaandika cheti na jamaa hajasoma chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna polisi kata, ma-*inspector, IGP* amewaweka kila kata. Kwa nini wasiwatumie hawa watoe semina na vibali watu wapewe leseni, kuliko kwenda kusumbua watu kwa kutumia hizo shilingi 50,000? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, *LATRA* wasiwe *TRA*. Wasiwe wanapanga mbinu za kupata pesa tu, kwenye bodaboda wachukue shilingi 17000, kwenye mabasi wanakataa wapiga debe wa stendi, halafu *LATRA* wanaingia wanakuwa wapiga debe wa mtandao. Sasa sielewi hapa, maana wameongeza nauli shilingi 3000, halafu gari

likitoka Bukoba mpaka Dar es Salaam wanachukua shilingi 3000, tena wanapiga juu kwa juu kwenye ile tiketi mtandao. Wanakata hela wanasema huyu *agent* wa tiketi mtandao *(vender)* amechukua, lakini yule *vender* hana shida ya aina yoyote. Basi, wamuunganishe *vender* na *TRA*, lakini *vender* hana shida kwa sababu, anachukua shilingi 200 tu. Unakuta kwenye basi abiria mmoja anachukuliwa shilingi 3000 na inakatwa juu kwa juu kwenye tiketi mtandao, sasa hawa wamekuwa *TRA* badala ya kudhibiti watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waangalie bodaboda, kuna dada yangu mmoja pale amesema wawaangalie bodaboda wawape semina. Sasa wao wamekuwa wakusanya mapato tu. Kitu kama hicho hakiwezekani! Ni lazima wajitafakari, hasa Mkurugenzi mpya, asije akaleta mzozo wa watu wenye mabasi wakagoma halafu baadaye akaanza, maana siku hizi kuna tabia ambayo imeanza hasa kwa wenzetu wa huko mbele, watu wakigoma unasikia wanampinga mama, wanawapakazia, wanampinga mama. Wao ndiyo wanaoleta sheria na vitu ambavyo havitekelezeki, watu wakigoma au wakifanya hivi kwenye haki zao za msingi unasikia hawa wanampinga mama. Wao ndiyo wanaompinga mama, wanaweka mavitu ya hovyo hovyo. Wao ni wapingaji wa mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka hata mama anisikie huko aliko kwamba, wapingaji wako kwake na taasisi zake. Hawa ndiyo wapingaji wakuu, wanaweka vitu ambavyo havitekelezeki. Huo ndio ukweli, maana sasa hivi kila mtu anataka akusanye pesa ili azitwange. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, semeni tu leo, Bunge tuamue hapa, pesa zote, taasisi zote na hizi *authority* zote, mamlaka zote zinazokusanya pesa ziingie kwanza Benki Kuu halafu wapewe kidogo kidogo, kama tutaona hizi sheria zinakuja. Sasa hivi si anakusanya halafu anapanga *plan* za kutandika. Sisi Wabunge hapa ndio tukipata vimshahara kidogo watu wanapiga kelele eeh! eeh! Eeh! hela yenyewe iko wapi? Watu wanatangwa huku hela siyo mchezo. Huo ndio ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, hizi sheria zote zinazoletwa zilikuja mwaka 2019 kwenye Awamu ya Tano. Watu walitaka kugoma, tumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, aliwaita wasafirishaji wote na haya yote yakafutwa, yakatulia. Sasa wamemwona mama amekuja wanaanza, ukiangalia kila taasisi wanaanza kuleta vichokonoko-chokonoko. Labda sijui ni kwa sababu, wanamwona mama ni mpole au mama hajui, mama anafahamu. Sisi ndiyo tunamwambia hapa kwenye spika ili atusikie.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu aliliondoa watu wakatulia. Walikuwa wanataka kugoma, Waziri Mkuu akatuliza mgomo. Sasa tena wameyarudisha yale yale ambayo Waziri Mkuu aliyamaliza. Sasa, sijui ni nani mkubwa kati ya Waziri Mkuu na wao? Naomba wajitafakari kwa kina.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia basi, maana mimi ni mfanyabiashara wa mabasi na nisipozungumza mambo ya mabasi halafu nimo humu ndani, basi nitakuwa mwendawazimu. Kwenye basi *LATRA* wanatoa *license* kwa shilingi 180,000 halafu kwenye tiketi wana-*charge* tena pesa kwa kila abiria. Ukija kwenye malori ni shilingi 180,000, lakini kwenye mzigo hawa-*charge* pesa kwa sababu, ule mzigo wakati mwingine si unalipwa baada ya mwezi, ila huku kuna *cash* wanaipata *chap chap* ndiyo maana kila siku wanatamani wakusanye ile pesa. Sasa hiyo siyo haki.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia lori linapewa *exemption*. Unaweza ukaingiza lori ukalipa shilingi milioni 15, ukiingiza basi moja jipya, ushuru wa *TRA* peke yake bila *wharfage* na bila *port charge* ni shilingi shilingi milioni 102. Ushuru peke yake kwa basi moja ni shilingi milioni 102, halipati *exemption* wala halipati chochote. Sasa wajitafakari kwenye hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine wajitafakari kwenye *school bus*. Mabasi ya shule ni mabovu, madereva ni wabovu, wao wameng'ang'ania tu kwenye pesa. Juzi hapa Arusha yameua, sasa ni mara ya pili, Dar es Salaam huko ni kila siku, kila sehemu.

Mheshimiwa Spika, ukipishana na vile vibasi kinaenda upande, dereva mwenyewe kasuka rasta, yaani yule dereva hata haeleweki anatoka wapi, lakini sijawahi kusikia *LATRA* wanasimamia habari ya abiria wa *school bus,* wameng'ang'ania tu kwenye sehemu wanazopata pesa. Kule kwenye sehemu ambazo hakuna pesa wao hawapo. Dereva wa basi haendeshi mpaka apimwe kama amelewa na aweke *fingerprint* kwamba ametambulika, kwenye mabasi wanafanyaje?

Mheshimiwa Spika, kwanza, Sheria ya Mabasi yanayosafirisha duniani watoto wadogo wa chekechea ni haya? Sheria ya Mabasi yoyote inayosafirisha watoto wadogo wa chekechekea lazima iwe na pua mbele *engine* inakaa mbele dereva anakaa nyuma ili hata ikitokea kugonga inaumia ile *engine* kule mbele, abiria huku wanakuwa salama lakini sasa hivi dereva yupo hapa na mtoto naye chezacheza anachungulia nje hata akigonga ng'ombe mtoto anaumia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa…

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, hata mkiingia kwenye *google* hapo…

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabiby, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, mimi si ndio mtu wa mwisho au bado? Mama inatosha. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Wewe siyo Mbunge wa mwisho kuchangia, Mbunge wa mwisho kuchangia ni Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kabla hajachangia Mheshimiwa Naibu Waziri, tunao wageni kutoka Baraza la Wawakilishi.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao wamekaa Jukwaa la Spika na hawa ni wageni kutoka Baraza la Wawakilishi, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, hawa ni Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano.

Waheshimiwa Wabunge mnaongea sana na nimesimama, nikaamua kuendelea kusoma nikajua mtajua nimesimama sasa kumbe hamnioni pamoja na huu urefu. Sasa nimesimama mtulie kwanza nimalizie kilichonisimamisha.

Tunao wageni kutoka Baraza la Wawakilishi na hawa Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano Ardhi na Nishati, hawa ni wageni wa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David na hawa ni Mheshimiwa Aza January Joseph ambaye ni Makamu Mwenyekiti, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Fatma Ramadhani Mohamed ambaye ni Mjumbe; Mheshimiwa Hassan Hamad Omar ambaye pia ni Mjumbe; Mheshimiwa Ameir Abdulla Ameir ambaye ni Mjumbe; Mheshimiwa Mwanajuma Khassim Makame, Mjumbe, Mheshimiwa Hudhaima Mbarak Tahir, Mjumbe, Ndugu Masoud Ally Hamad, Afisa Habari; Ndugu Salma Muhsin Hajj, Katibu wa Kamati; Ndugu Himid Hajj Choko, Katibu Kamati na Ndugu Saad Othman Said, Katibu Kamati, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Uchukuzi, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Uchukuzi kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha uendelezaji wa miradi ya kimkakati na pia utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi kumi ya bajeti inayoishia Juni, 2024 Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi imetekeleza miradi mingi ya miundombinu ya reli, bandari na uimarishaji wa safari za anga ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege. Napongeza Serikali kwa hatua nzuri za utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* pamoja na uboreshaji wa bandari utaimarisha kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu. Reli ya *SGR, TAZARA* na Bandari ni nguzo imara ya kiuchumi na kiushindani katika biashara ya usafirishaji wa ndani na nchi za maziwa makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati. Bandari za Tanzania ni lango la usafirishaji kwa Zambia, Malawi, DR Congo, Uganda, Burundi, Rwanda, Sudan ya Kusini na hata Zimbabwe na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea kwa ufanisi mkubwa ambapo kipande cha Dar es Salaam – Morogoro na Morogoro – Makutopora umekamilika kwa asilimia karibu zote na huduma ya treni imepangwa kuanza hivi karibuni. Pia napongeza jitihada za Serikali za kuendelea kutafuta vyanzo vya fedha vya masharti nafuu kugharamia ujenzi wa vipande vilivyobaki. Pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, Serikali imefanya maboresho makubwa ya miundombinu na huduma katika bandari zetu hususan Bandari ya Dar es Salaam ili kukabiliana na ushindani mkubwa wa bandari zingine za ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Dar es Salaam inakumbana na ushindani mkubwa toka bandari za Mombasa (Kenya), Beira (Msumbiji), Nacala (Msumbiji), Durban (Africa Kusini), Lobito (Angola) na Walvis Bay (Namibia). Maboresho ya bandari zetu iendane na kuondoa changamoto zingine ambazo zinasabisha gharama kubwa za usafirishaji kwa bandari zetu na kusababisha kupoteza biashara ya usafirishaji kwa bandari shindani. Ufanisi wa bandari unategemea pia maboresho ya barabara, Reli ya Kati *(TRL),* Reli ya *TAZARA,* utendaji wenye tija wa wadau wote wa bandari na hata watumishi ili kupunguza gharama za usafirishaji kwa wateja wa bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maboresho ya miundombinu hususan Bandari ya Dar es Salaam, kwa mwaka 2022/2023 mchango wa mapato yanayokusanywa na *TRA* kutokana na huduma za kibandari kwenda Mfuko wa Serikali umeendelea kuongezeka hadi kufikia shilingi trilioni 9.354 ambayo ni asilimia 41.37 ya mapato yote yanayokusanywa na *TRA*.

Mheshimiwa Spika, katika ushuhuda wa mchango huu mkubwa, Serikali inashauriwa kuongeza uwekezaji zaidi katika kuboresha miundombinu ya bandari zetu ikiwemo mifumo ya TEHAMA. Mamlaka ya Bandari *(TPA)* inapaswa kuhimili ushindani, kwa kutoa huduma za uhakika, zenye ubora wa hali ya juu kuliko washindani wake. Katika kipindi hiki cha mahitaji makubwa ya kuboresha miundombinu ya bandari zetu, napendekeza mapato ya *wharfage* yakusanywe na *TPA* badala ya *TRA*. Katika utaratibu wa sasa, *TPA* itashindwa kujiendesha kibiashara kwa kusoma fursa ya kutumia karibu shilingi bilioni 700 za mapato ya *wharfage* ambayo ni zaidi ya asilimia 50 ya mapato ya shughuli za bandari. Utaratibu huu hautakuwa mgeni kwa vile duniani kote, mapato ya *wharfage* yanakusanywa na bandari kama chanzo cha kuboresha miundombinu ili kuboresha huduma za kibandari.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa karibu asilimia 70 ya mzigo wote wa nchi za nje unasafirishwa kwa kupitia *Dar es Salaam Corridor* ambapo DR Congo ni asilimia 36, Zambia asilimia 31 na Malawi asilimia tano. Pamoja na fursa za kijiografia ya bandari zetu, mzigo unaopita sasa kwenye Bandari ya Dar es Salaam ni chini ya fursa ya

asilimia 50 ya biashara yote ambayo kwa sasa sehemu kubwa inashikiliwa na bandari shindani.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa za kiushindani zinatokana na ufanisi usiokidhi ushindani na gharama kubwa za bandari na watoa huduma wa Bandari ya Dar es Salaam. Pia kuna changamoto za kiutendaji kwa mashirika ya reli ya *TAZARA* na hata reli ya kati *(TRL)* inayopelekea gharama kubwa ambazo siyo za kiutendaji. Kwa ajili ya kunusuru biashara hii inayopotea kwa bandari shindani, Serikali ichukue hatua za haraka kuboresha huduma za *TAZARA* ikiwa ni pamoja ya maboresho ya miundombinu ya reli, ununuzi wa vichwa vya reli, mabehewa, na vitendea kazi vingine.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali kwa haraka ishughulikie maboresho ya Mkataba wa *TAZARA* ili kuwezesha kutafuta mkandarasi mwenye uwezo wa uendeshaji na menejimenti. Katika kipindi hiki cha ushindani mkubwa na hata mfumuko wa bei wa mafuta ya petroli, mbolea na bidhaa mbalimbali, usafirishaji wa reli ni mojawapo ya suluhisho kubwa kupunguza mzigo wa bei kubwa kwa wateja wa bandari zetu na hata wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maboresha ya reli ya *TAZARA*, napendekeza kuendelea na ujenzi wa bandari kavu Mbeya ambayo ina fursa kubwa katika kipindi hiki katika kuwezesha kupunguza gharama za kusafirisha kwa wateja wa bandari na hata kupunguza bei za mafuta ya petroli, pembejeo na mazao ya kilimo. Bandari kavu ya Mbeya ni njia panda kwa wateja wa nchi za Malawi, Zambia, DRC Lubumbashi na hata kwa Zimbabwe na Msumbiji. Serikali ichukue hatua za haraka kuinusuru reli ya *TAZARA* hata ikibidi kurekebisha mikataba ya umiliki na uongozi ili mradi iendeshwe kwa tija. Kuna kuchukua hatua za makusudi kwa kutumia zaidi *TAZARA* kusafirisha mizigo ambayo imeelemea hata uwezo wa barabara zetu. Usafirishaji wa mizigo kwa kutumia *TAZARA* ilenge kupunguza gharama za mafuta ya petroli, pembejeo kwa wakulima na wakati huo kupunguza gharama za kusafirisha mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuboresha *TAZARA*, napendekeza kukamilisha taratibu za ujenzi wa bandari kavu ya Mbeya, ambapo Serikali ya Mkoa imetenga maeneo makubwa mkabala na uwanja wa ndege wa Songwe na pia kuna njia ya reli ya *TAZARA* na barabara ya TANZAM. Eneo hili ni la kimkakati zaidi kutokana na kuwa ni njia panda ya nchi zote za Kusini mwa Afrika ikiwemo DRC. Pia eneo la kiusalama zaidi kutokana na kuwepo vikosi vyetu vya majeshi, pia Mamlaka ya Bandari kwa kipindi kirefu wamewahakikishia wananchi wa Inyala, Mbeya kulipa fidia ya eneo lao wanalolichukua.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Bandari ya Dar es Salaam kuingia makubaliano na *TAZARA* na *TRL* ili iweze kumiliki mabehewa yake kwa lengo la kuongeza ufanisi na kupunguza gharama ambazo sio za kiushindani. Pamoja na hatua hiyo, kuna fursa kubwa ya kutafuta mwekezaji mwenye uzoefu mkubwa katika uendeshaji wa reli kwa lengo la kuboresha utendaji hasa kwenye upande wa makontena. Serikali ifanye jitihada ya kupata mwekezaji ikiwemo kwa mfumo wa *PPP* kwa lengo la kuongeza biashara ikiwemo kurudisha biashara iliopotea kwa bandari shindani.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iendelee na mkakati wa kutafuta mwekezaji wa Bandari ya Mbegani – Bagamoyo ambayo ina lango lenye kina asili cha mita 18 na haina kikomo cha upana wa meli ambazo zinaweza kuingia na kutoka bandarini hapo. Kutokuwepo kwa ukomo katika lango, bandari hiyo inaweza kuhudumia meli ambazo zinahudumiwa kwenye bandari kubwa duniani zenye urefu wa mita 400 na uwezo wa kubeba makasha hadi *TEUs 22,000*. Aidha, uwezo huu ni mkubwa katika eneo la Afrika Mashariki na Kati kwani kwa sasa hakuna bandari yenye uwezo kama huo. Hivyo, uendelezaji wa Bandari ya Mbegani, Bagamoyo utasaidia kupunguza msongamano wa shehena katika Bandari ya Dar es Salaam na kupelekea bandari zote kuwa shindani.

Mheshimiwa Spika, napongeza Serikali kwa uwekezaji kwenye viwanja vya ndege na pia kufufua shirika letu la ndege la *ATCL*. Kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao na madini, napendekeza

Serikali iongeze ndege za mizigo na kuboresha viwanja vyetu kwa kujenga maghala yanayokidhi viwango vya kimataifa. Pia *ATCL* ianzishe safari za Mbeya - Dodoma na pia Mbeya na nchi za *SADC* ikiwemo DRC, Lubumbashi, Zambia na Malawi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ikamilishe kulipa fidia za wananchi waliopisha ujenzi wa viwanja vya ndege kikiwemo kiwanja cha ndege cha Songwe, Mbeya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa na Naibu wake Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, watumishi wote wa Wizara na taasisi zake kwa kazi kubwa wanazofanya kwenye kusimamia Wizara ya Uchukuzi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa leo utahusu changamoto za mdau muhimu wa uchukuzi hapa nchini ya bodaboda na ushauri wa nini kifanyike kuwasaidia. Kundi hili ni muhimu, lakini limesahaulika sana.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa pikipiki maarufu bodaboda sasa ni kimbilio la Watanzania walio wengi bila kujali ukubwa wa kipato chao. Kwa kutumia bodaboda mtumiaji hutumia muda mfupi kufika anapoenda. Kwenye miji mikubwa yenye misongamano, bodaboda hutumika ili kuokoa muda wa kusafiri. Sehemu nyingi vijijini huwa hakuna magari na barabara za kupitisha magari, hivyo basi bodaboda hutegemewa sana.

Mheshimiwa Spika, biashara ya bodaboada ni biashara inayokua kwa kasi sana hapa nchini Tanzania. Hii ni kwa sababu vijana wengi kutokana na ukosefu wa ajira wameamua kuingia kwenye biashara ya bodaboda. Hivyo basi, kazi ya uchukuzi kwa kutumia bodaboda imekuwa ni fursa kwa vijana kutokana na ukosefu wa usafiri wa magari kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Ni

muhimu kundi hili liangaliwe kwa jicho la pekee ili wasaidiwe kuboresha huduma zao kwa raia.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu karibu zote nchini Tanzania, usafiri kwa kutumia huduma ya bodaboda imekuwa kitu cha kawaida. Kutokana na changamoto ya barabara, kwenye maeneo mengine ya makazi hii ndiyo njia pekee ya watu kufika makwao. Bodaboda hutumika pia kwenye shughuli za kisiasa, zimekuwa zikinogesha misafara ya wanasiasa wetu wakiwa katika majukumu yao ya kutembelea maeneo mbalimbali, lakini pia bodaboda zimekuwa usafiri mbadala ikiwa mtu ana haraka na hataki kukwama katika changamoto ya msafara wa magari barabarani. Vilevile wafanyabiashara pia wanatumia bodaboda kuwachukulia wateja wao bidhaa za aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu huu wa bodaboda, waendeshaji wa vyombo hivi hukabiliana na changamoto nyingi. Hivyo basi Wizara ya Uchukuzi ikishirikiana na wadau wengine wa uchukuzi wanahitaji kuja na mikakati ya kitaifa ili kukabiliana nazo. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

Kwanza, baadhi ya waendesha magari huwadharau sana bodaboda. Utakuta bodaboda ipo barabarani gari inaipigia honi kwa fujo itoke au utakuta gari inataka kuingia barabara kuu wakiona bodaboda hawasubiri wanaingia tu na kusababisha ajali. Ikumbukwe vyote ni vyombo vya moto, vina haki ya kutumia barabara na vinalipia mapato ya Serikali. Aidha, bodaboda inakuwa imebeba roho za watu pia. Hilo nalo linahitaji kuangaliwa, kwani vitendo hivi husababisha ajali na vifo.

Pili, waajiri walio wengi hawawapi mikataba madereva wa bodaboda inayowapa haki zao kimkataba. Wale wenye mikataba, sehemu kubwa haina haki ya kupata bima za afya na kuweza kujiwekea akiba. Mikataba inaonesha kulinda maslahi ya mwenye chombo badala ya maslahi ya dereva wa bodaboda.

Tatu, hapa nchini hakuna mfumo rasmi na rafiki wa kuwakagua madereva wa bodaboda kama wamekidhi vigezo vya kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Spika, nne, baadhi ya abiria wanaowapa huduma huwa wanakuwa wezi na sio abiria wa kweli. Katika maeneo mengi hapa nchini waendesha bodaboda wengi wameibiwa na kuporwa pikipiki na watu wanaojifanya kuwa abiria, lakini baadaye wanawageuka na kuwapora kwa kuwatishia kuwafanyia mambo mabaya ikiwa ni pamoja na kuwatoa uhai.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ya tano ni ajali kuongezeka; hii inasababishwa na vijana wengi kutokujua sheria za barabara. Kuna vijana wanaamini ukishajua kuendesha bodaboda mtaani unaweza pia kuendesha barabarani. Hii hupelekea waendeshe pikipiki barabarani bila kuwa na uelewa kuhusu sheria za barabara. Ajali nyingi zimepelekea vifo na ulemavu wa kudumu kuongezeka. Taarifa zinaonesha kwamba asilimia 70 wa majeruhi wa ajali za barabarani wanaopokelewa *MOI* wanatokana na ajali za bodaboda.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ya sita ni ya waendesha bodaboda kupata vishawishi vya ngono. Kuna abiria ambao ni wanawake wakipanda pikipiki hawataki kulipa na kuwaambia waendesha bodaboda kuwa wanaweza kulipa kwa kufanya ngono hasa abiria ambao wanawachukua usiku kutoka sehemu za starehe.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya saba ni kwamba waendesha bodaboda wanaugua ugonjwa wa *pneumonia* kutokana na upepo mkali na baridi kwa wale wasiovaa kinga za baridi.

Mheshimiwa Spika, nane ni kuhusu faini za barabarani; waendesha bodaboda wengi huwa wanakamatwa na polisi na kuandikiwa faini kwa kutofuata sheria za usalama barabarani na kuhatarisha maisha yao na ya watumia njia kwa miguu na hata kusabaisha mtafaruku na usumbufu kwa waendesha magari.

Mheshimwa Spika, kutokana na changamoto zilizotajwa hapo juu, ni vyema Wizara ya Uchukuzi ikaweka umuhimu mkubwa kwenye sekta hii ambayo kwa mawazo yangu ndiyo inayosafirisha watu wengi kuliko vyombo vingine vyote vya usafiri hapa nchini na kutoa ajira za vijana wetu wengi na huchangia kwenye pato letu la Taifa.

Mheshimia Spika, ili kukabiliana na changamoto ya bodaboda hapa chini, ninaishauri Serikali ifanye tafuatayo:-

Kwanza kuwe na usajili wa vituo rasmi vya bodaboda katika maeneo yote nchini (vijijini na mijini). Kwenye hivi vituo kuwe na ukaguzi wa madereva pamoja na pikipiki mara kwa mara na kwa yule asiyekidhi vigezo asiruhusiwe kupakia abiria hadi pale atakaporekebisha kasoro zake. Ni vyema madereva wa bodaboda waende kupata mafunzo maalumu ya uendeshaji salama.

Pili, nguvu na uwezo wa pikipiki uangaliwe; pikipiki nyingi za bodaboda kwa sasa zina *cc125-150.* Pikipiki hizi hukimbia sana na hiki ndicho chanzo cha ajali nyingi. Napendekeza Serikali iweke sheria kwa pikipiki za kusafirishia abiria zisiwe na nguvu zaidi ya *cc100.*

Tatu, sheria iweke adhabu kali kwa waendeshaji wanaopakia abiria zaidi ya mmoja (mishikaki); nan ne, Serikali ihamasishe raia kukataa kupanda abiria zaidi ya mmoja (mishikaki) kwa sababu udhibiti wa chombo *(control)* hupungua kwa dereva akipakia abiria zaidi ya mmoja, hivyo ni rahisi kupata ajali ukiwa uko kwenye mshikaki endapo itatokea dharura yoyote.

Mheshimiwa Spika, katika barabara zote kuu za nchi, kuwe na eneo muhimu la waendesha pikipiki kama ilivyo kwa watembea kwa miguu na waendesha baiskeli.

Aidha, bodaboda hufika katika maeneo yote ya vijijini na mijini. Kama kuna sera yoyote itakayotungwa kuzuia bodaboda zisifike maeneo fulani, hili inabidi liangaliwe kwa umakini mkubwa kwani inaweza kuathiri kwa kiwango kikubwa kuyafikia maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo pikipiki zinahitajika sana, sera zizingatie kwenye kutoa kipaumbele kwa usafiri wa bodaboda dhidi ya magari binafsi kwa kuboresha usafiri wa umma.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naishauri Serikali pia ifanye yafuatayo ili kuwasaidia watoa huduma katika sekta hii kukabiliana na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na wadau wengine ianzishe *clinics* za kutoa elimu na katika *clinics* hizo, yafuatayo yapewe kipaumbele:-

(i) *Clinic* hizi zitoe elimu mara kwa mara kwa waendesha bodaboda kuhusu usalama barabarani;

(ii) *Clinic* kwa wamiliki wa bodaboda ziwaelekeze kwamba mtu wanayempa chombo cha usafiri awe ana leseni;

(iii) Waendesha bodaboda wazingatie sheria za barabarani na kutotumia kilevi chochote muda wa kazi;

(iv) Vijana wafundishwe kujihami ili wasiambukizwe au kuambukiza *VVU;*

(v) Kwa kuwa changamoto kubwa ya kazi ya bodaboda ni ajali, *clinic* hizi ziwafundishe umuhimu na namna ya kupata bima za afya na kujiunga na mifuko ya pensheni ili akiba hizi zije kuwasaidia uzeeni. Bima za afya zitakuwa msaada mkubwa katika usalama wao pale inapotokea changamoto ya ajali au kuugua; na

(vi) *Clinic* hizi zitoe elimu kwa madereva bodaboda ili waweze kuepukana na kundi la kulaumiwa. Bodaboda linafahamika kama kundi linalovunja sheria za barabarani na kufanya vurugu, hasa pale mwenzao anapopata ajali. Wengi hujichukulia sheria mkononi ikiwa ni pamoja na kuua watu na kuchoma magari hata kama kosa ni la bodaboda.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara ya Uchukuzi na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kuridhia uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam. Tunaimani kubwa uwekezaji wa bandari utakuwa wenye tija na utapunguza matumizi makubwa yaliyokuwa yanafanywa na bandari na kutupelekea sasa tupate faida.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Serikali na taasisi zake zote kwa kazi nzuri wanayaoifanya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa kuiomba Serikali waboreshe miundombinu ya Bandari ya Mbweni kwa kweli hali ya Bandari ya Mbweni haipendezi, ni vyema Serikali iangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali kuimarisha usafiri wa treni ya Jiji la Dar es Salaam kuwe na vituo vyenye ubora, lakini napongeza pia *TRC* kuwezesha kuanza kwa safari kwa kutumia reli ya *Standard Gauge*. Nampenda kumpongeza sana sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kutafuta fedha ambazo zimewezesha treni hiyo kuanza kazi kipande cha *Dar es Salaam to Dodoma.*

Mheshimiwa Spika, angalizo langu naomba wataalam wetu wakae na wafanye usanifu wa bei za abiria, tusije kufanya makosa ya kuweka bei ambazo zitafanya mradi huo ushindwe kujiendesha na kuingia hasara. Kwa kuwa treni ya kawaida bado ipo basi abiria wa *SGR* wawepo na wale wengine watakuwepo, hongereni sana *TRC*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa mabasi tunashukuru mabasi yanaenda usiku, lakini changamoto ni vizuizi vya Serikali ambavyo vinawekwa msituni na usiku hawana taa, wanasababisha

hatari kubwa sana. Kama ni vizuizi vile bayana siyo vya siri na viwekwe taa kwenye vile vyuma wanavyoviweka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya gharama za ndege zinakuwa kubwa siku hadi siku kwa *Dar es Salaam to Dodoma* kuliko maeneo mengine, tatizo ni nini? Naomba nipewe maelezo ya kina kwa nini Dar es Salaam kwenda Kigoma ni nafuu kuliko Dar es Salaam kwente Dodoma?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha safari za majini (baharini) kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwa mfano boti ya kutoka Mbweni mpaka bandarini au Pembamnazi, Kimbiji mpaka Bandarini? Naomba tuzingatie usafiri mbadala, tumeona mvua zilivyoharibu barabara ya Kigamboni, wananchi wangekuwa na usafiri mbadala angalau hekaheka zingepunua.

Mheshimiwa Spika, nashauri Mamlaka ya Bandari kwa kushirikiana na Wizara ya Utalii wanunue meli za utalii ambazo wananchi watazitumia kwenye utalii na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia 100 na ahsante sana.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nimepitia bajeti yote lakini sijaona *commitment* ya Serikali kwenye maombi ya Wananjombe kuhusu kuanza ujenzi wa *airport* ya kisasa. Mkoa wa Njombe ni mkoa wa kimkakati kwa maana ya uzalishaji wa mazao ya *horticulture*. *Horticulture* ndio *sub-sector* inayokuwa kwa kasi zaidi kuliko sekta zote za Wizara ya Kilimo. Njombe ina *packhouse* 12 za mazao ya parachichi na mazao yote ni kwa ajili ya *export*.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana mwezi Oktoba Makamu wa Rais alitembelea Njombe kikazi na akatoa ahadi kuwa Serikali itajenga upya uwanja huo, lakini bajeti hiii haioneshi dalila yoyote kuhusu kuanza kwa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata taarifa za uhakika nini mpango wa Serikali?

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii kwa kazi nzuri mnayofanya. Aidha, namshukuru sana Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha nyingi kwenye Wizara hii kwani tunaona mambo mengi yanatekelezwa yakiwemo reli ya kisasa ya kati *(SGR),* ndege zinazonunuliwa, ujenzi wa meli kubwa kwenye Ziwa Victoria, uboreshaji wa bandari na ujenzi wa viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, dunia nzima imeathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi, kila mahali athari zinaonekana kama mafuriko, ukame ulokithiri, vimbunga na milipuko ya magonjwa. Nawashukuru kwa kuona mbali, mkaiwezesha Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kuwawezesha na kuwapatia mitambo ya kisasa, wanafanya kazi nzuri sana, kuwapa Watanzania taarifa mapema ili wajiandae kukabiliana na matatizo kama kimbunga, mvua z*a El-Nino* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nilikwishachangia na kuomba mkaufungue Mkoa wa Kagera kwa kujengewa kiwanja kikubwa cha ndege pale Omukajunguti Missenyi. Huu ni mradi wa miaka mingi, lakini huwa hauanzi. Kagera wanalima ndizi, *vanila*, matunda na mbogamboga, vinaweza kusafirishwa hadi nje ya nchi. Mradi huu utafungua mkoa kiuchumi. Ni lini uwanja wa ndege wa Omukajunguti utaanza kujengwa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa juhudi kubwa zinazofanyika katika uwekezaji kwenye miradi ya kimkakati, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna anavyotekeleza

majukumu yake, huu ni uwekezaji mkubwa sana ambao kukamilika kwake utaifanya nchi yetu kuongeza kasi ya ukuzaji uchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri kuhusu utwaaji wa maeneo katika mitaa mitano ya Manispaa ya Ilemela yaani Myaa wa Kihili, Mhonze, Nyamwilolelwa, Shibula na Bulyanhulu ambapo mpaka sasa idadi ya wananchi imefikia 3,700 waliofanyiwa uthamini mpaka sasa katika mitaa miwili, je, itakapokamilika, ulikilinganisha na idadi ya watu 1,404 iliyokuwa imetajwa awali.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni vyema uamuzi wa awali wa kutwaa eneo la mita 700 kutoka eneo la njia ya kurukia ndege ulikuwa muafaka sana kwa sababu zifuatazo, kwanza kupunguzwa kwa eneo linalotwaliwa ingepunguza gharama kwa Serikali na idadi ya wananchi wanaotakiwa kuhama wangepungua sana. Mpaka sasa idadi iliyofikiwa ni zaidi ya mara mbili hata kabla mitaa yote haijakamilika kufanyiwa uthamini. Mtaa iliyofanyiwa uthamini mpaka sasa ni miwili bado mitaa mitatu idadi inaweza kuzidi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuomba *route* ya ndege Mwanza – Dodoma na Dodoma hadi Arusha, na Dodoma - Mbeya - Dodoma ni vyema ikaanzishwa ili kuwapunguzia gharama wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa fursa anayotujalia ya uhai pamoja na afya njema. Nitumie nafasi hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye bajeti kama hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu kwa imani yake kubwa ya kuniteua na kuniamini kwa nafasi ya Naibu Waziri. Ahadi yangu wakati wote ni unyenyekevu, utii na kumsaidia kwa kadiri ya maelekezo yake. Pia nimshukuru Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kama viongozi wetu wakubwa kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Waziri wangu, Profesa Makame Mbarawa, Mheshimiwa Waziri amekuwa ni baba, amekuwa ni mlezi, amenipokea, ananifundisha na ananivumilia. Kiongozi huyu mnyenyekevu, mpole na msomi wa daraja la juu ameendelea kuwa mwalimu wetu sote katika Wizara yetu kwa kutupa miongozo na maelekezo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana wewe umekuwa kiongozi wangu mkuu nilipokuwa Mwenyekiti wako wa Kamati na Mwenyekiti wa Bunge, umenifundisha wakati wote na kunielekeza.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Kamati yangu niliyofanya nayo kazi kwa muda mrefu ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo pamoja na Mwenyekiti wake mpya. Naishukuru Kamati yangu inayotusimamia Kamati ya Miundombinu, Kamati ya *PAC* na *PIC* na viongozi wake pamoja na watendaji wote Wizarani: kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wenyeviti wa Bodi, Watendaji wa Wizarani pamoja na Watendaji wa Taasisi. Aidha, naishukuru familia yangu kwa kuwa nami wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kipekee kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini, kwa kunichagua na kunileta niwe mwakilishi wao katika Bunge hili. Aidha, kama kiongozi mkuu kule *Redcross* niwashukuru *volunteer* wenzangu ambao wakati wote wamekuwa wakiniamini na kunisaidia majukumu yangu. Pia, kwa unyenyekevu mkubwa niwashukuru Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimesikiliza hoja, michango na ushauri, kwa hakika nimejifunza mengi, tunawashukuru sana sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango ya leo kwa haraka haraka ina taswira tatu; la kwanza inathibitisha nia, dhamira, ushupavu, vipawa na maono ya Rais wetu aliyonayo kwa Taifa letu. Michango hii inadhihirisha kiwango cha juu cha upeo wa Bunge letu (Bunge la Kumi na Mbili) katika kufuatilia, kusimamia lakini zaidi kushauri na kuelekeza Serikali yao. Wametimiza jukumu lao la kikanuni kama Kanuni inavyosema kuanzia 118 mpaka 129 ya kusimamia mchakato mzima wa kibajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya Wabunge mbalimbali leo imetoa uhakika na usalama wa Taifa letu, leo kesho na hata miaka 100 ijayo chini ya kiongozi wetu shupavu Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini imedhihirisha kwamba kumbe CCM ina uwezo wa kuendelea kuongoza miaka mingine 100 ijayo, kwa sababu mambo inayosimamia ni yanayogusa watu leo, kesho na hata kesho kutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, nitagusia maeneo machache kama ambavyo tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri. Zimejengwa hoja nyingi kuhusiana na uwekezaji kwenye reli, nataka niseme mambo mawili au matatu kwenye reli; nambari moja ni upekee wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Bara la Afrika anajidhihirisha kwenye reli. Kama alivyosema mchangiaji mmojawapo, ndiye Rais anayejenga reli ndefu kuliko zote Barani Afrika. Reli yetu ina urefu wa zaidi ya kilometa 2,100, ndiye Rais amedhihirisha utekelezaji wa ajenda ya 2023 ya kuunganisha Bara zima na Majiji kwenye Reli ya Kisasa. Nchi inayotufuatia kwa mbali ni Nchi ya Ethiopia yanye urefu wa kilometa 756 na ndugu zetu wa Kenya wana reli ya 592 inayokwenda mpaka Naivasha. Hili ni jambo la kutembea kifua mbele tukijidai na kujivuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata kwenye gharama ama uwekezaji ambao Taifa limefanya wakati Tanzania imewekeza Dola za Kimarekani bilioni 10 mpaka sasa, sawa na shilingi trilioni 25, wenzetu majirani zetu wanatufuata kwa mbali sana. Nikisoma hapa takwimu, wenzetu wa Nigeria wamewekeza dola bilioni sita, wenzetu wa Kenya dola bilioni tano na hawa wengine wa Ethiopia dola bilioni nne, tuko mbali sana. Hii inadhihirisha umadhubuti wa Rais wetu, inadhihirisha dhamira ya dhati ya CCM pamoja na uongozi wake uliopo madarakani kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia reli yetu hii ya Tanzania; kwa sababu ni vyema tukafafanua kwa wananchi wakaifahamu gharama tunazojenga kwa kilometa moja ni dola milioni nne, wenzetu wa Kenya ni dola milioni sita kwa kilometa moja, wakati wenzetu wa Ethiopia ni dola milioni 6.5, lakini reli yetu ni ya umeme yenye uwezo

wa kubeba mzigo wa tani 35 kwa *excel* wakati wenzetu wa Kenya ni ya *diesel* yenye uwezo wa kubeba mzigo tano 25 kwa *excel*. Sasa hayo ndiyo mambo ambayo ndiyo upekee wa reli yetu, upekee wa maono ya Rais wetu, ni vyema watu wakalifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini dhamira yetu kama Wizara kwenye bajeti hii? Nini maono ya Rais wetu? Moja…

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, moja ni kunufaika na uchumi wa kijiografia, lakini pili…

**SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka kumpa sifa nyingine ya reli yetu ni kwamba ina mifumo ya Ulaya ambayo ina milimeta 1,435 ukubwa na upana wake. Kwa hiyo ni *standard* ile ya Ulaya tumejenga siyo ya Kiafrika.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile, unaipokea taarifa hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo naipokea na namtuma aenende akayaambie mataifa habari hizi njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika reli yetu hii tunayoizungumzia dhamira ya Rais wetu ni nini? Ni kuifanya Tanzania kuwa kituo kikubwa cha biashara na huduma katika ukanda wetu wa *East Africa* na *SADC*. Yuko mtu mmoja amechangia Mheshimiwa mmoja kwamba nchi yetu ni ya saba katika ufanyaji biashara na Congo, ni kweli kabisa kwa sasa hali yetu ni mbaya lakini tunarekebisha changamoto zilizopo siyo tu tukawe namba moja, tukawe namba moja kwa mbali dhidi ya wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye reli naomba nizungumzie jambo lingine dogo la *open access* kwa sababu ni hoja ambayo inazungumziwa sana. *Open access* ni nini? Ina faida gani? Kwa nini tunafanya? Huu ni mfumo ambao tunautumia wa Shirika la Reli kuruhusu wawekezaji binafsi kuleta vitendea kazi na mtu mwingine atauliza kwa nini? Ukiangalia reli yetu sisi tuliyoijenga ina uwezo wa chini kabisa wa kubeba mzigo tani milioni 17, uzito wa juu kabisa tani milioni 25.

Mheshimiwa Spika, tumewekeza zaidi ya dola bilioni 10 ili tukatengeneze vitendea kazi, mabehewa na vichwa tunahitaji 10% mpaka 15% tuiwekeze huko. Maana yake leo Bunge lako hapo lipitishe karibu trilioni tatu ili twende tukanunue mabehewa na mabehewa tunayoyahitaji ni zaidi, vichwa vya treni tunavyovihitaji ni zaidi ya vichwa 160; wakati huo kuna mafuriko barabara zinahitajika zikajengwe, tunahitaji vituo vya afya, elimu ya juu na kadhalika. Serikali imeamua ita-*control* reli itaruhusu watu binafsi kuweka vitendea kazi na jambo hili siyo geni duniani.

Mheshimiwa Spika, wenzetu nchi zifuatazo wanafanya: Cameroon wanafanya; Afrika ya Kusini wanafanya; Japan, Korea, Norway, Sweden, Uingereza, Ufaransa, Canada na nchi nyingine nyingi duniani. Sisi siyo wa kwanza na ni maono mema ya Rais wetu kuona kwamba miundombinu tunayoijenga haibaki bure, itumike kama tunavyojenga Barabara, tunaruhusu malori ya watu binafsi kutumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumepata uzoefu kwenye *TAZARA* kuanzia mwaka 2018/2019 mpaka mwaka jana tumeweza kusafirisha tani 944,000, hizi ni *TAZARA* peke yao, lakini tuliporuhusu *open access* tumeongeza tani 909,000 zingine, jumla 1,800,000 maana yake ni nini? Tusingeruhusu mfumo huu maana yake tusingefika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha nimalizie hoja ya Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi amezungumzia kuhusu Reli ya Kidatu. Huko nyuma tulikuwa tunasafirisha kahawa kutoka Uganda tunaipeleka *South Africa*, wakati wa Mwalimu Nyerere. Rais Dkt.

Samia Suluhu Hassan ameamua kufufua maono ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere. Anatengeneza reli na zaidi ya bilioni moja tumeiwekeza kuunganisha Reli ya Kidatu ambayo alikuwa anaizungumza ili iunganishwe kutoka Uganda ije kwenye meli, ije *TRC,* iende *TAZARA* ielekee mpaka *South Africa.* Haya yanakwenda sambamba na mengine tunayosema ya kuunganisha *Atlantic* pamoja vitu vingine. Kwa hiyo nimtoe mashaka, tayari maono yameshaanza kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha kuhusu Waziri kutembelea eneo lake tutatembelea, ameshanipa maelekezo hapa. Mwisho mabwawa matatu aliyozungumza Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi. Wizara ya Kilimo wapo hatua za mwishoni kuhakikisha kwamba yanajengwa mabwawa matatu ili tukahakikishe kwamba wananchi hao wananufaika na kilimo, uvuvi lakini tuna-*control* mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Reli ya Mtwara ambayo wote mnaifahamu kwa umuhimu wake Liganga na Mchuchuma inayotoa mzigo Mtwara inaupeleka mpaka *Mbamba Bay*. Inatoa mzigo Liganga na Mchuchuma kupeleka mpaka Mtwara kuunganika na Kilosa, tutachukua ushauri huo, wataalam watafanyia kazi na kadri itakavyoonekana inafaa tutakwenda kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi aje ahitimishe hoja yake. Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika Bunge letu hili Tukufu la bajeti ili kukamilisha kazi tuliyoanza leo asubuhi ambapo niliwasilisha hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Bunge kwa jinsi walivyotuongoza na kusimamia majadiliano ya hoja hii pamoja na hoja nyingine zilizotangulia. Aidha, nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa wawazi na kutoa michango yao ya kina wakati wa majadiliano haya. Niwathibitishie kwamba michango yao yote tumeichukua kwa uzito mkubwa na kwenda kuyafanyia kazi ili kuendelea kuleta ufanisi na utekelezaji mzuri kwenye sekta ya uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kipekee nimshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa hoja nzuri walizozitoa kwenye Kamati yetu. Nikiri kwamba hoja zao ni muhimu sana kwa maendeleo na ukuaji wa miundombinu na huduma za usafiri na usafirishaji hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wabunge wote waliochangia katika bajeti hii. Waheshimiwa Wabunge 26 wamechangia wakati wa majadiliano ya hoja hii ambapo Wabunge 20 wamechangia kwa kuongea na Waheshimiwa Wabunge sita wamechangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda mchache uliopita Mheshimiwa Naibu Waziri amemalizia kuchangia na kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa ufasaha na weledi mkubwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa jinsi ambavyo amejibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na nitajibu baadhi ya hoja zilizobaki. Aidha, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara itajibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi na kuziwasilisha hapa Bungeni kabla ya kuhitimishwa kwa Mkutano wa Bunge hili la bajeti unaoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kuhitimisha hoja yangu kwa kutoa ufafanuzi wa kijumla wa baadhi ya hoja zilizojitokeza kwenye maeneo makubwa yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema asubuhi hii leo kwamba Sekta ya Uchukuzi imeendelea kutoa mchango mkubwa wa ukuaji wa uchumi wetu na Taifa kwa ujumla na kuwa sekta hii ni sekta wezeshi hasa kwa Sekta ya Kilimo, Madini, Utalii, Viwanda na Biashara. Kama nilivyosema mwaka 2022, Sekta hii ya Uchukuzi ilikua kwa 3.8% na ilichangia pato la Taifa kwa takribani 6.7%. Kwa upande wa fedha za kigeni kama nilivyosema asubuhi, pato la kigeni ambalo linachangiwa na sekta hii limeongezeka kutoka Dola za Kimarekani bilioni 1.6 mwaka 2022 hadi kufikia Dola za Kimarekani bilioni 2.4 mwaka 2024 ambayo limeongezeka kwa 50% na mchango huu mkubwa kwa kiasi kikubwa umetokana na Sekta ya Uchukuzi hasa eneo la bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli huo ndiyo uliosababisha au uliosukuma Waheshimiwa Wabunge takribani 85% leo wamejikita zaidi kwenye eneo la bandari wengine wamejikita kwenye w*harfage*.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia na wamefanya hivyo pia kwa sababu bandari ndio lango kuu la uchumi wa nchi yetu na takribani 37% ya makusanyo ya kiforodha ya *TRA* yanakusanywa kupitia hasa kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu changamoto mbalimbali za Bandari ya Dar es Salaam, kama tulivyojua kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa la meli kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Leo ukipita na ndege ama ukipita na boti kwenda Zanzibar au kwenda maeneo mengine kwenye nanga, utakuta takribani meli kati ya 20 mpaka 25. Kuna baadhi ya siku zinafika mpaka meli 30 na meli hizi zinakaa pale nangani kwa siku kuanzia kumi mpaka siku 15 na kila siku mwenye mzigo analipa takribani dola 25 ambayo hiyo kwa ufupi ni takribani shilingi milioni 50, 52 au 53.

Mheshimiwa Spika, tunazo changamoto kubwa hasa kwenye eneo la gati. Gati tulizonazo Bandari ya Dar es Salaam hazitoshi, hivi

leo ninavyozungumza Bandari ya Dar es Salaam kuna gati 13. Tuna gati namba *zero* mpaka gati namba 11, halafu tuna gati namba 12 kwa ajili ya mafuta - *KOJ,* tuna gati 13. Wakati bandari za wenzetu hasa tunazoshindana nazo kwa mfano Bandari ya Mombasa wana gati 19. Gati 13 ni gati za kawaida na gati 6 ni kwa ajili ya kontena. Pia, wana gati maalumu kwa ajili ya kushushia nafaka.

Mheshimiwa Spika, mshindani wetu mkubwa mwingine ni Bandari ya Durban. Bandari ya Durban ina gati 50, gati 31 ni za mizigo ya kawaida na gati 10 ni kwa ajili ya makontena na magati 9 ni kwa ajili ya bidhaa chafu. Hivyo, lazima tufanye maamuzi sahihi ya kujenga bandari wakati huu, lazima tujenge gati mpya kuanzia leo *otherwise* tukifanya kesho tutakuwa tumechelewa. Tunao ushindani mkubwa hasa kwa wateja wetu wa kutoka Zambia, *DRC,* Malawi, Zimbabwe pamoja na Kenya. Kwa hivyo, Serikali tumeamua kuanza uwekezaji mkubwa kwenye Bandari ya Dar es Salaam kuhakikisha kwamba hatuendi kuwapoteza wateja wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali tumeamua sasa kama nilivyosema asubuhi, tunajenga matanki 15 ya mafuta kwa ajili ya kuhifadhia mafuta mita za ujazo 420,000 kwa siku kwa wakati mmoja ambapo mradi huo una gharama ya shilingi bilioni 578.6. Serikali imeanza kutoa pesa hizo.

Mheshimiwa Spika, pia tunajenga Bandari ya Mbamba *Bay* ambayo gharama yake ni takribani shilingi bilioni 75, bandari hii ni muhimu sana hasa kwa ndugu zetu wa Malawi na Zambia. Pia, tunafanya ukarabati wa Bandari ya Kemondo na Bukoba Mjini kwa gharama takribani shilingi bilioni 40. Tumenunua vifaa vya kisasa *SSG (Ship to Shore Gantry Cranes)* ambazo zimegharimu takribani shilingi bilioni 250.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea na uwekezaji wa ujenzi wa Bandari Chafu huko Mtwara ambayo itajengwa kule Kisiwa Mgao, tayari Mkandarasi ameshapatikana. Tunaendelea na ujenzi wa gati pale Dar es Salaam ambayo itakuwa na urefu wa mita 500 ambapo kwa ufupi hizo zitakuwa ni gati mbili, pale tunapopaita *marine wharf*,

sasa hivi tuko kwenye hatua ya mwisho ya kumpata mkandarasi. Tunaendelea kufanya ukarabati wa Bandari ya Mwanza *South* kwa shilingi bilioni 20.

Mheshimiwa Spika, haya yote yanafanywa kupitia Serikali pia tunaendelea kuhimiza sekta binafsi kuwekeza na kufanya kazi na Serikali kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Kama nyote mnavyojua bandari namba nne mpaka namba saba tayari sasa hivi iko *private sector,* gati namba nane mpaka 11 tuko katika hatua ya mwisho ya kumpata mwekezaji mwingine. Vilevile, Serikali tuko katika hatua nyingine ya kutafuta mjenzi kwa njia ya *private sector* au kwa kutumia taratibu yoyote kwa ajili ya gati namba 13 mpaka namba 15.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Waheshimiwa Wabunge wengi 85% leo wamechangia kuhusu *wharfage,* kwamba malipo ya *wharfage* yanayokusanywa yabaki *TPA,* suala hili ni muhimu; tumelipokea na tutalifanyia kazi. Tunaenda kulifanyia kazi kwa sababu ni muhimu kwa maslahi ya bandari na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na suala lingine la *Air* Tanzania kuja Dodoma, kutoka Dodoma kwenda Mbeya, kutoka Dodoma kwenda Mtwara na maeneo mengine. Tunatamani kwamba *Air* Tanzania isambae Tanzania nzima, lakini changamoto inayotukabili hatuna ndege za kutosha. Kila mwaka Serikali tunaendelea kununua ndege, kama nilivyosema mwaka huu tumepokea ndege tatu na mwakani naamini tutaanza kupokea ndege nyingine. Naomba niwapatie habari njema kuhusu hapa Dodoma, kuanzia mwezi Oktoba tutaleta ndege kubwa ya *Max 737* ambayo itaanza kuja Dodoma, kwa sababu Dodoma wasafiri ni wengi na ukweli wenyewe ndege tuliyonayo haiwezi kutimiza mahitaji ya Dodoma. Kwa hiyo uwanja wetu wa Dodoma sasa hivi hauwezi kuruhusu ndege kubwa ya Boeing *737 Max.*

Mheshimiwa Spika, tunategemea mwezi Oktoba na Novemba uwanja wetu wa Msalato utakuwa tayati na tutaanza kufanya kazi hiyo, ingawaje jengo la abiria na *control tower* itakuwa havijakamilika

lakini ndege ile itaweza kutua kwa sababu tutajenga *temporary* pale kama alivyosema Mheshimiwa Ezra na tutairuhusu ndege ile ku-*control* kwa kutumia *temporary control tower* ambayo tutaijenga pale kwa muda mfupi, lakini ni muhimu kwa sasa na wakati umefika kuleta ndege kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa siku moja hapa tunaleta ndege nne, hazitoshi lakini tunaamini tukileta ndege kubwa mbili zitaweza kuhimili mahitaji ya Dodoma. Vilevile, tutaleta ndege nyingine itaanzia Dar es Salaam hapa Dodoma mpaka Mwanza, hii ni habari njema sana kwa wananchi wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuangalia soko linasemaje, tunaamini huko mbele pengine tutatoka hapa kwenda Mbeya, Kilimanjaro na maeneo mengine, safari ni hatua tumejipanga na tunaamini tutafika vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la *Air* Tanzania kwenda Pemba. Mimi natoka Pemba nitahakikisha kwamba ndege ya *Air* Tanzania itakwenda Pemba bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ambayo pia imechangiwa kwa mtazamo au kwa hisia kali ya malipo ya *passenger service charges* yabaki *TAA*. Hili suala ni muhimu na tunalijua na sisi kama Serikali tumelichukua tunakwenda kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ambayo Wabunge wa Kigoma, Rukwa na Katavi wamelichangia sana suala hili, nakubaliana na hawa Waheshimiwa Wabunge, ni kweli wananchi wa mikoa ile wanapata tabu sana kwa ajili ya usafiri wa majini. Jana tulikaa sana kulizungumza jambo hili na sisi kama Serikali tumeamua kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wa muda mfupi au kwa kutatua tatizo hili kwa muda mfupi kwanza tumeamua kuikarabati meli ya *MV Liemba*. Tayari tumeshampata mkandarasi na mkataba ulisainiwa tarehe 11 Novemba, 2023 na tayari Serikali imeshatoa shilingi

bilioni tano za *advance payment* kwa ajili ya malipo ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatukuangalia hivyo, kama tulivyokubaliana na wananchi wa kule kupitia Wabunge wao, tumekubaliana tufanye ukarabati wa *MV Mwongozo*. *MV Mwongozo* ni meli ambayo ilikuwa inafanya kazi zamani, ni meli nzuri, lakini baada ya kutokea ajali ya *MV Victoria* meli hiyo ilisimamishwa kwa sababu wataalam walisema kulikuwa na shida ya *stability* ya meli hiyo. Sasa tumepeleka timu ya wataalam wamefanya uchunguzi wa kutosha na wametushauri nini cha kufanya ili meli ile iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, tayari wametupa gharama za meli hiyo ambayo kuitengeneza ili iweze kufanya kazi vizuri itagharimu dola za Kimarekani milioni 2.77 ambapo Serikali nayo imetoa shilingi bilioni tano kwa ajili ya ukarabati wa meli hiyo. Huu ni mpango wa muda mfupi, tunaamini meli ya *MV Mwongozo* itakapofika mwisho wa mwaka huu itakuwa tayari. Ni kazi ambayo naamini kunako baina ya miezi sita mpaka saba itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, tuna mpango pia wa muda mrefu. Kwanza, tunakwenda kujenga meli mpya ya mizigo ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua tani 3,500 ambayo itagharimu shilingi bilioni 158 na mkandarasi tumeshampata. Kitu cha muhimu tunachokwenda kukifanya kule kwanza ni kujenga *shipyard,* kiwanda cha kutengenezea meli kwa ajili ya Ziwa Tanganyika. Ni mara ya kwanza katika nchi yetu katika maziwa yote haya tuliyonayo Tanzania hakuna kiwanda cha kutengenezea meli.

Mheshimiwa Spika, gharama ya kiwanda hicho ni takribani shilingi bilioni 313 na mkandarasi tumeshampata. Mwisho wa mwezi huu tutamlipa mkandarasi huyo pesa za *advance payment* hasa kwa utengenezaji wa kiwanda hicho, kwa sababu kwanza unatakiwa utengeneze kiwanda halafu ndiyo unaenda kutengeneza meli. Tunaamini mipango hii ya Serikali kuanzia ya muda mfupi na ya muda mrefu itaweza kutatua tatizo lote la usafiri wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2024/2025, tumepanga takribani shilingi bilioni 190 kwa ajili ya ujenzi wa meli. Kati ya pesa hizo shilingi bilioni 116 tumeelekeza Ziwa Tanganyika, ambazo hizi ni pesa nyingi ukilinganisha na eneo hilo lote, shilingi bilioni 100 tumeelekeza katika maeneo mengine kwa vile hili ni jambo kubwa sana na nawaomba Waheshimiwa Wabunge wa Katavi, Kigoma na Rukwa watuamini, tunakwenda kufanya kazi hii. Watuamini tutahakikisha kwamba kazi hii itafanyika kwa umakini mkubwa na kwa wakati tuliopanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya hoja ambazo zimewasilishwa hapa na Kamati ya Kudumu ya Miundombinu. Hoja ya kwanza inasema, hakikisha kwamba Wizara inasimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kukidhi viwango bora endelevu *(sustainability)* na kuwepo kwa thamani ya fedha. Majibu ya hoja hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ushauri umepokelewa, Serikali imeendelea kuweka mifumo mbalimbali ya kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuanzisha kitengo maalumu kinachojitegemea cha kufuatilia na kufanya tathmini ya miradi mbalimbali yote inayosimamiwa na Wizara ili kuangalia *value for money*. Tunaamini Mradi wa *SGR* tulioutekeleza una viwango vya juu, watu wengi wamekuja kujifunza kwenye Mradi wetu huu wa *SGR*. Watu wametoka Uganda, *DRC,* Burundi na nchi nyingine nyingi wamekuja kujifunza.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya pili kutoka Kamati inasema kwamba, ujenzi wa reli ya kisasa *(SGR)* na uendeshaji wa *TRC,* Kamati imetoa pongezi kwanza kwa kazi hiyo, kufanya majaribio ni jambo jema, lakini kazi hiyo imalizike kwa haraka. Kwa niaba ya *TRC* na wadau wote tumepokea pongezi na ushauri uliotolewa na Kamati. Wizara inapenda kujibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TRC* inaendelea na maandalizi ya uendeshaji ili kuanza kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria ifikapo Julai, 2024, kama ilivyoelekezwa na Mheshimiwa Rais. Kwa kipande

cha kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma. Kuhusu ujenzi wa kipande hicho kutoka Dar es Salaam - Morogoro kama nilivyosema asubuhi, umekamilika kwa asilimia 98.93, kazi zilizobaki ni kukamilisha ujenzi wa reli kuelekea bandarini ambako mradi umefikia asilimia 46.12.

Mheshimiwa Spika, vivuko vya juu vya Vingunguti, *Airport* na Njia panda ya Segerea umefikia asilimia 99.3. Mheshimiwa Mbunge hapa amesema kwamba barabara zake zimefungwa kwa muda mrefu, lakini tunamwambia itakapofika mwezi Juni tutakuwa tumemaliza kuweka lami barabara hizo na tutazifungua rasmi.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika ujenzi wa kipande cha kutoka Morogoro – Makutupora, kilometa 422 umekamilika kwa kiasi cha asilimia 96.61. Kazi zilizobaki ni kukamilisha ujenzi wa vivuko vya juu ambao umefikia asilimia 98.52 na kazi ya uzio imefikia asilimia 86.02. Reli yetu yote ina uzio wa kuzuia wanyama na watu wengine kukatiza wakati reli hii itakapokuwa inafanya kazi. Aidha, *TRC* inaendelea na majaribio ya njia pamoja na vitendea kazi ikiwemo mabehewa na vichwa vya treni kabla ya kuanza kazi rasmi. Naomba niwahakikishie Watanzania kwamba itakapofika mwezi Julai wataweza kufaidika na reli hiyo na bei za reli hiyo zitakuwa ni bei nzuri hasa kwa lile daraja la tatu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ya Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kuboresha makusanyo katika reli ya *MGR,* mkakati huu unapaswa kwenda sambamba na juhudi za makusudi za kuboresha miundombinu ikiwemo kutenga bajeti ya matengenezo ya mara kwa mara na ya haraka pale miundombinu ya reli hiyo inapoathiriwa na majanga kama vile mvua.

Mheshimiwa Spika, kwanza, tumeupokea ushauri, lakini Serikali inaendelea na mpango wa ukarabati wa reli hii ya *meter gauge* ambayo ina urefu wa kilometa 2,707. Mradi huu umegawanyika kwa awamu mbili, awamu ya kwanza ulianza kutoka Dar es Salaam mpaka Tabora, kwa kuongeza uwezo wa kubeba mizigo kwa reli hiyo kutoka tani 13 kwa *excel* hadi kufikia tani 18.5 kwa *excel* pamoja na kuweka reli nzito za ratili 80 kwa yadi.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika *TRC* imesaini mikataba ya ukarabati wa njia ya reli kati ya Tabora na Kigoma yenye urefu wa kilometa 411 na Kaliua – Mpanda yenye urefu wa kilometa 210 na kazi za ukarabati zinaendelea. Sambamba na hilo, *TRC* imesaini mkataba wa ununuzi wa malighafi ya ukarabati kwa ajili ya ukarabati wa njia ya reli ya kaskazini ikijumuisha kipande cha Ruvu na Mruazi *Junction,* kazi hii itaanza mara moja. Aidha, kupitia bajeti ya mwaka huu ambao tumeiomba 2024/2025, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 312.0 kugharamia matengenezo ya miundombinu ya reli, *MGR*.

Mheshimiwa Spika, hoja namba nne iliyowasilishwa na Kamati yetu ni uendeshwaji wa Shirika la Ndege, Kamati imeendelea kuipongeza Serikali kwa ununuzi wa ndege za abiria na mizigo. Hata hivyo, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inakuwa na ubunifu wa kuboresha usafiri wa anga kupitia *ATCL* na hatimaye kuzalisha faida ili kuongeza mapato au pato la Serikali. Tunaomba kujibu hoja hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia na kuiwezesha *ATCL* katika ufunguzi wa vituo vipya ikiwemo kituo cha Dubai kilichofunguliwa tarehe 29 Machi, 2024, kuendelea na taratibu za kurejeshwa kwa Kituo cha Johannesburg huko *South* Afrika na maandalizi ya kufungua Kituo cha London. Kama nilivyosema na kwa vituo vya ndani tutaanza na kituo cha kutoka hapa Dodoma kwenda Mwanza na maeneo mengine kuhakikisha kwamba tunaweka *network* yetu vizuri na hata hapa ndani.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja namba tano kuhusu maboresho ya uendeshaji wa reli ya *TAZARA*. Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuhakikisha kwamba wabia wa uendeshaji wa reli ya *TAZARA* kwa maana ya Tanzania na Nchi ya Zambia wanakaa meza moja kwa majdiliano kuhusu *TAZARA*. Serikali zetu mbili Serikali ya Zambia na Serikali ya Tanzania zimeamua kutafuta mbia wa kuwekeza kwenye reli ya *TAZARA,* hivi tunavyozungumza mazungumzo yanaendelea vizuri kati ya Zambia, Tanzania na Serikali ya China kwa ajili ya kumpata mwekezaji kutoka China.

Mheshimiwa Spika, timu hiyo ambayo inafanya majadiliano inaongozwa na ndugu Mussa Mbura, Mkurugenzi Mkuu wa *TAA* ambaye ndiye Mwenyekiti wa timu upande wa Tanzania na Zambia. Tunaamini utakapofika mwezi Juni, jambo hili litakuwa limeshafika mwisho na tutahakikisha kwamba *TAZARA* inasimama vizuri na inaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunafanya haya yote kwa ajili ya kuifungua Bandari yetu ya Dar es Salaam, huko Zambia na *DRC* kuna mzigo mkubwa wa madini na makampuni yote yanayochimba madini huko ni Makampuni ya Kichina, tunaamini tukimpa *TAZARA* Kampuni ya Kichina tunavutia makampuni mengi ya madini kuitumia *TAZARA* na tukiitumia *TAZARA* maana yake tunaitumia Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine kuhusu usafiri wa majini kama ilivyoulizwa na Kamati yetu. Kamati inapenda kuikumbusha Serikali kwamba isimamie kwa bidii miradi ile ya kusimamia utafutaji na uokoaji kwenye kituo cha Mwanza. Hili tumelichukua na tunaenda kulisimamia kuhakikisha kwamba mradi huo unamalizika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *LATRA*. Utendaji wa *LATRA,* Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kwamba inashughulikia changamoto zote za mgongano wa kiuratibu na kisheria kuhusu masuala ya usalama barabarani ili *LATRA* iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo bila kuingiliana na majukumu ya Jeshi la Polisi. Majibu ya hoja hii ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha utendaji wa *LATRA* unaratibiwa bila mgongano hususan na Jeshi la Polisi, *LATRA* ilikutana na Tume ya Haki Jinai na Jeshi la Polisi na kujadiliana kwa kina namna ya kuondoa changamoto hiyo. Sasa inaandaa rasimu ya mapendekezo ya mabadiliko ya kisheria kwa ajili ya kupata maoni ya wadau kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mwisho kuhusu Uwanja wa Ndege wa Serengeti. Uwanja wa Ndege wa Serengeti ni muhimu hasa kwa Sekta ya Utalii. Serikali tumeamua, tunakwenda kuujenga uwanja huo kwa kushirikiana na Sekta Binafsi. Uwanja huo ni muhimu sana kwa sababu kwa sasa wakati wa *peak season* kunakuwa na ndege ndogo nyingi zinaingia kwenye mbuga kule ambapo siyo jambo zuri. Tunaamini tukijenga uwanja huu utachangia sana kwenye Sekta ya Utalii pamoja na uchumi wa nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza, naomba kuzungumzia suala moja hapa la mwisho ambalo Mheshimiwa Bonnah amezungumza sana kuhusu kulipa fidia. Tunajua kwamba wananchi wake wanadai Serikali fidia takriban shilingi bilioni 129. Kwenye bajeti hii ambayo tumeomba leo tumeweka fedha kwa ajili ya kuwalipa wananchi hao. Naomba Mheshimiwa Mbunge awe mvumilivu, kuanzia mapema mwezi Julai fedha hizo zitatolewa kwa ajili ya kuwalipa wananchi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Mwisho kabisa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Ahsanteni sana, tutaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*………..................................Sh. 3,387,329,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kifungu hiki kina mshahara wa Waziri. Kuna Waheshimiwa Wabunge ambao wanataka ufafanuzi wa mambo ambayo yanaruhusiwa kikanuni kwa Kifungu hiki.

Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niseme kabisa kwamba nisiporidhishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mwenendo usiokua mzuri kwenye taasisi za Serikali kuchukua maeneo ya wananchi na kuanza kuyafanyia kazi bila kulipa fidia kwa wananchi. Mojawapo ya taasisi ambazo zimekuwa zikifanya hivyo ni Taasisi ya Mamlaka ya *Airport*. Sehemu ambazo kuna matatizo hayo ni Geita, Simiyu, Masasi, Ukerewe, Nachingwea pamoja na Segerea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipopata maelezo mazuri nakusudia kushika shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuwa nasikiliza hoja ya Mheshimiwa Mbunge. Hayo uliyoyataja yako na majimbo mengine au ni Jimbo la Segerea pekee?

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo na majimbo mengine ndiyo maana nimesema Simiyu, Geita, Ukerewe, Nachingwea pamoja na Jimbo la Segerea.

**MWENYEKITI:** Sawa, baada ya kutaja jimbo ndiyo nikawa natafakari hapa kwenye kanuni zetu kama hilo jambo; maana sasa kanuni zetu zinataka jambo hapa liwe la namna fulani hivi lakini sasa imetajwa na mikoa mingine Mheshimiwa Waziri japokuwa mifano yote inatoka Segerea, kwenye jimbo la Mheshimiwa Mbunge.

Kanuni zetu huwa zinataka kwenye mshahara wa Waziri ni jambo la kisera. Sasa kisera maana yake hakuna sera ambayo inashughulika na eneo moja kwa maana ya jimbo moja. Yametajwa maeneo mengi Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo tafsiri yangu hapa mbele inaniambia huenda yanatokea na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama nilivyosema nilipokuwa najibu hoja. Tulichukua, wananchi hao walitakiwa kuhamishwa kwa ajili ya kupisha uboreshaji wa kiwanja cha ndege cha eneo lile pale. Tumeshafanya tathmini na kwenye bajeti hii kama nilivyosema; tunakubali na tumetenga shilingi bilioni 129 kwa ajili ya kulipa fidia hiyo. Tunamhakikishia na tutaweza kuifanya bila wasiwasi wowote.

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa kwa sababu anakusudia kushika shilingi asiporidhika na majibu yako, jibu lako tusaidie kwa sababu likishughulika na jambo la Segerea tu itakuwa hofu yangu ile ya mwanzo ilikuwa halisi kwamba hoja yake inahusu jimbo lake pekee.

Wewe tujibu kama vile unazungumzia fidia za viwanja vilivyopo hapa nchini. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kweli kuna maeneo mbalimbali nchini tumechukua kwa sababu tunataka kufanya uendelezaji wa miundombinu ambayo ni ya msingi. Kwenye bajeti hii tumepanga kila tulipochukua tunakwenda kulipa fidia, ikiwemo hilo eneo lake ambalo amelizungumza Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo yamekuwa ni majibu ya Waheshimiwa Mawaziri tofauti tofauti kwa muda wa kipindi cha miaka saba mpaka kufikia kwenda kwenye jimbo langu. Kwa hiyo, mimi naomba Wabunge waniunge mkono tuweze kuchangia jambo hili.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja yake haijaungwa mkono, mliosimama hamjafika kumi. *(Minong'ono)*

Waheshimiwa Wabunge, ngoja kwanza; Mheshimiwa Mbunge ameshasema jambo lake kwamba Waheshimiwa Wabunge nawaomba mniunge mkono tuweze kulijadili jambo hili; amesimama Mheshimiwa jirani yake pale, Mheshimiwa Lucy Mayenga na Wabunge watatu huku. Wengine mkawa sasa mnajiuliza tusimame au tusisimame?

Tusikilizane vizuri, mpaka mimi niliposema hoja haijaungwa mkono ndiyo mmeanza kuamka. Kwa hiyo, utaratibu wa kikanuni mnaufahamu, ni watu 10 ndiyo wanaounga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbunge mwenzao na nyinyi hamkusimama. Kwa sababu mimi natazama, nimegeuka huku nimeona watatu wamesimama, huku alisimama Mheshimiwa mwenye hoja na jirani yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo hoja haijaungwa mkono, ndiyo utaratibu. Huu jamani ni mwaka wa nne tuko hapa kwa hiyo hakuna kanuni mpya

inayofundishwa sasa, wote tunafahamu. Mbunge ameomba kuungwa mkono, hamjamuunga mkono tunasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Bonnah Kamoli, hoja yako haijaungwa mkono.

Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kuhusu soko la *DRC,* sisi kama nchi bado hatujalitendea haki kabisa soko la *DRC* kama ambavyo Wabunge wengine ambao wametangulia kupita wakachangia. Pamoja na sisi kupakana moja kwa moja kijiografia na *DRC,* bado hatuko hata *top three* kwenye kuhudumia Nchi ya Congo katika kupata fedha kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo kikubwa ambacho kimefanya tusiweze kufika Nchi ya *DRC* moja kwa moja ni pamoja na Wizara ya Uchukuzi. Nikirejea kwenye mchango wa Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda na Mheshimiwa Hamis Tabasam na nikiongezea kidogo kutoka kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, Sura ya Saba, ukurasa wa 184 unasema: *"Kulinda uchumi na maslahi mapana ya Taifa kwa kutumia jiografia ya nchi kimkakati na ushawishi wa kihistoria hususan kwenye ukanda wa kusini." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hatujaweza kuifikia Nchi ya *DRC* moja kwa moja pamoja na nchi yetu kujenga bandari nyingi. Bandari ya Kibirizi, Kabwe, Kipili, Kirando, Kigoma na Bandari kubwa ya zaidi ya shilingi bilioni tisa za Kitanzania, bado hatuwezi kuifikia Nchi ya *DRC* hususan kwenye majimbo makubwa yenye fedha kama Haut-Katanga, Mji wa Lubumbashi, Lualaba, Kolwezi, Moba pamoja na Kivira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022 tumeshawahi kumpa Mheshimiwa Waziri, ushauri kwamba yeye aende na timu yake Kutoka Karema kwenda upande wa pili Jimbo la Tanganyika, Kalemi; namna gani tunaweza tukafika Jimbo la Haut-Katanga, Lubumbashi pamoja

na Kolwezi. Akasema kwamba tumpe muda yeye na Wizara yake waweze kuchakata na ni Waziri huyu huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipopata ufafanuzi wa kina kuhusu maslahi mapana ya nchi kuhusiana na soko la *DRC* nimekusudia kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu tunapoteza fedha nyingi za kigeni. Tumepoteza ajira na tumepoteza fedha nyingi za kigeni kwa kuliachilia soko la *DRC*. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hebu husianisha hilo soko linahusikaje na uchukuzi? Linahusikaje yaani? Umetaja zaidi soko kuliko uchukuzi na leo tuko hapa na uchukuzi.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye Wizara ya Uchukuzi, bandari zote ambazo ziko kwenye Mwambao wa Ziwa Tanganyika zinasimamiwa na uchukuzi. Ili tuweze kufika Nchi ya *DRC* moja kwa moja ni lazima tutahitaji bandari zetu ziweze kufanya kazi na tuweze kuwa na meli. Pia, kujengwa kwa Bandari ya Karema ya zaidi ya shilingi bilioni 49…

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana, umeshaeleweka sasa. Haya, Mheshimiwa Waziri ufafanuzi, nadhani hoja yake umeielewa kwa nini masoko yanakuja chini yako.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi. Kwanza, naomba nimsahihishe Mheshimiwa Mbunge, mimi mwenyewe nimekwenda kote; nimekwenda Lubumbashi na nimekwenda Kalemi. Timu yetu ya Wizara, imetoka timu kutoka *TANROADS* nilipokuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, *TPA*, *TRC*, wote tumekwenda na tumefanya *survey* ya Barabara kutoka Lubumbashi mpaka Kalemi, kilometa 2,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wetu wametumia takriban siku nane kwa sababu gari kule inakwenda kilometa nane, kilometa sita kwa saa, siyo kama hapa unaenda kwa kilometa 120. Hakuna barabara, hakuna gati, hakuna bandari. Tumekwenda na tumekaa

na tuko katika mpango wa kushirikiana na wenzetu ili tuweze kutekeleza kazi hiyo ya kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Mbunge amekaa kuashiria; haya, Mheshimiwa Condester Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuwa hujaniita.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, akimaliza akiketi ukiwa na hoja ni kama swali la nyongeza tu, unasimama ili nikuone kwamba hujaridhika. Ndiyo utaratibu.

Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Majibu ya Mheshimiwa Waziri hayajitoshelezi. Lengo la kujenga bandari zote hizo kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika kama nchi ni kwa sababu gani? Baada ya yeye kwenda kutembea na watu wake amekuja na suluhisho gani?

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa kwa sababu kikanuni hana nafasi tena ya kutoa ufafanuzi, ukisimama unasema kama umeelewa alichosema au unataka kutoa hoja Wabunge wakuunge mkono.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sijaridhika, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuweze kuwashauri Wizara njia bora na namna bora ya kufikia soko la *DRC*. Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono tuweze kujadili jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Haya, hoja haijaungwa mkono. Mmewaona waliosimama, moja, mbili, tatu, wewe hapo katikati ulisimama, nne.

Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, wa kumi anatoka wapi? *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hoja haijaungwa mkono na kwa kweli si kosa la Mwenyekiti maana wamesimama na nyinyi mmehesabu. Maana mlitaka kuniletea mimi kesi. Haya, hoja haijaungwa mkono Mheshimiwa Condester Sichalwe, kwa hivyo tunasonga mbele.

Haya, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi sikusudii kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri, namuazima imani isipokuwa nataka *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na adha kwa wananchi ambao wanatumia usafiri wa majini upande wa Bahari Kuu, Maziwa Makuu pamoja na mito mikubwa. Maeneo hayo tumepoteza ndugu zetu wengi sana, lakini watu wetu wamekuwa maskini, wanapozama na mizigo yao inazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maelezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri, maelezo mazuri sana. Tuliahidiwa mwaka juzi tukaambiwa na bajeti tukapangiwa, mwaka jana na mwaka huu tena. Ninachotaka ni kupata *commitment* ya Serikali; ni kipi cha tofauti watakachoenda kukifanya tujue kama wataenda kutekeleza hayo waliyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa kwa kukubali *commitment* ya Serikali. Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri hapa alipokuwa anazungumza, ameeleza kwa kina hatua mbili ambazo tumezifanya. Moja; tuliposaini mikataba ya zile meli za upande wa Ziwa Tanganyika

pamoja na ujenzi unaoendelea kwenye Ziwa Victoria na usanifu unaoendelea kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; ameeleza hapa Mheshimiwa Waziri kwamba tayari imeshatoka shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuanza ukarabati wa *MV* Liemba pamoja na shilingi bilioni tano nyingine kwa ajili ya *MV* Mwongozo. Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa atupe muda kidogo kwa sababu baada ya hapo tunakwenda hatua ya pili ya kulipa fedha kwa ajili ya Kiwanda cha Kutengeneza Meli kinachojengwa Mwambao wa Ziwa Tanganyika ambapo na yeye Mheshimiwa Mbunge nafikiri ni mnufaika mkubwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge yalikuwa ni hayo majina matatu na Mheshimiwa Aida Khenani alishasema hakusudii kushika shilingi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……….…….Sh. 798,232,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……………......Sh. 1,637,569,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*…….…Sh. 342,617,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*……….…Sh. 654,228,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*…………………..............Sh. 505,600,000
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*…………………………..Sh. 536,364,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*………………………………Sh. 624,465,000
Kifungu *1009* – *Monitoring and Evaluation Unit*………….....Sh. 702,061,000
Kifungu 2005 – *Transport Infrastructure Division*………….Sh. 1,418,916,000
Kifungu 2006 – *Transport Services Division*……………..Sh. 103,013,307,000
Kifungu 5002 – *Transport Safety and Environment Division*……………………………………….Sh. 1,123,788,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*………………Sh. 193,762,900,000
Kifungu 2005 – *Transport Infrastructure Division*……Sh. 1,823,035,861,000
Kifungu 2006 – *Transport Services Division*…………….Sh. 598,133,180,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Mtoa Hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Wote wameafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwahoji na ninyi kuikubali kwa asilimia mia moja bajeti hii, nitumie fursa hii kutangaza kwamba, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yamepitishwa rasmi na Bunge.

Pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote chini ya Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa ambao mmeutoa kwa Kamati mpaka kufikia mahali ambapo Wabunge wameafikiana na hayo makadirio na kuwapitishia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawapongeza sana na tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa yale yote ambayo mmeahidi kupitia hotuba hii ya Wizara kwamba mnaenda kuyafanya, tunaamini kwamba mtayatekeleza. Yale ambayo hayakuandikwa humu kwenye hii taarifa yenu, lakini mmeyasema wakati mkihitimisha kuashiria kwamba mmeisikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge wote, tunaamini kwamba mmeichukua michango hiyo na mtaitazama huko mbele mtakapokuwa mnaleta makadirio mengine. Pia, mtatumia mawazo ya Waheshimiwa Wabunge kwenye utekelezaji wa haya ambayo wameyapitisha leo. Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Pia, Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Miundombinu, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati hii tunawashukuru sana kwa kazi

nzuri ambayo mmeifanya ya kulishauri Bunge kupitia taarifa ambayo mmeitoa na sasa Bunge limeweza kufanya maamuzi. Kwa hiyo, tunawapongeza kwa kazi nzuri na tunawashukuru sana kwa kufanya kazi nzuri kwa niaba ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge wengine ambao siyo Wajumbe wa Kamati hii, lakini mmeweza na ninyi kuchangia mawazo yenu, naamini yataisaidia Wizara kwenye kuboresha utendaji kazi wake na kuona maeneo ambayo pengine hawakuyagusa safari hii kuweza kuona namna ambavyo wanaweza kujipanga na kuyagusa safari zinazokuja huko mbele. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge maadam Waziri amesema hapa kwamba wameyasikia yale yote mliyoyasema, basi tuamini utekelezaji utakuwa bora kabisa kwa mawazo yenu ambayo mmeyatoa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.44 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 7 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*